*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

**BUNGE LA TANZANIA**

____________

**MAJADILIANO YA BUNGE**

_____________

**MKUTANO WA TATU**

**Kikao cha Thelathini na Saba – Tarehe 26 Mei, 2021**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu

**NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:**

Randama ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

**MHE. ASIA A. HALAMGA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu utekelezaji wa majukumu na Bajeti

ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya makazi kwa mwaka wa fedha 2020/2021 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio, Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2021/2022. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, makofi hayo nadhani anapigiwa msomaji, lakini pia Mwenyekiti kwa kulea vizuri vijana waliopo kwenye Kamati yake. *(Makofi)*

Tunaendelea, Katibu.

**NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali, tunaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Jonas William Mbunda, Mbunge wa Mbinga Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 305

### Kujenga kwa Kiwango cha Changarawe Barabara ya Kijiji cha Uzena Njomlole – Mbinga Mjini

**MHE. JONAS W. MBUNDA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanza kujenga Barabara ya Kijiji cha Uzena kwenda Kijiji cha Njomlole katika Jimbo la Mbinga Mjini kwa kiwango cha changarawe ili iweze kupitika kwa wakati wote?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa David Ernest Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali

la Mheshimiwa Jonas William Mbunda, Mbunge wa Jimbo la Mbinga Mjini, kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara inayounganisha Vijiji vya Uzena na Njomlole inayojulikana kama barabara ya Masimeli – Njomlole na ina urefu wa kilomita 5.5, katika mwaka wa fedha 2021/2022 *TARURA,* Halmashauri ya Mji Mbinga imetenga Shilingi milioni 10 kwa ajili ya matengenezo ya barabara hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/ 2022, Wakala wa Barabara za Vijijni na Mijini umepanga kufanya tathmini ya miundombinu ya barabara na madaraja nchini kote ikiwemo Jimbo la Mbinga Mjini ili kuandaa mpango wa namna bora ya kutoa kipaumbele cha ujenzi na matengenezo ya miundombinu ya barabara na madaraja.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jonas William Mbunda, swali la nyongeza.

**MHE. JONAS W. MBUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu ya Serikali, lakini nina swali moja la nyongeza. Barabara hiyo ili iweze kukamilika inatakiwa yajengwe madaraja mawili; je, Serikali haioni kwamba kiasi cha fedha cha shilingi milioni 10 kilichotengwa hakitatosheleza kukamilisha ujenzi wa barabara hiyo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Jonas William Mbunda, Mbunge wa Jimbo la Mbinga Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge ameuliza, kwa nini Serikali isijenge pamoja na daraja lingine

kwa sababu hiyo barabara ina madaraja mawili na fedha tuliyotenga ni ndogo kukamilisha hiyo barabara. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tutakwenda kufanya tathmini na baada ya hiyo tathmini tutatafuta fedha ili tuweze kumalizia na hilo daraja lingine ili liweze kukamilika. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Rehema Juma Migilla, Mbunge wa Ulyankulu, sasa aulize swali lake.

Na. 306

**Kumalizia Ujenzi wa Vituo vya Afya Mwangozo na Uyowa**

**MHE. REHEMA J. MIGILLA** aliuliza:-

Je, Serikali ipo tayari kutenga fedha kwa ajili ya kumalizia ujenzi wa Vituo vya Afya vya Mwangozo na Uyowa katika Jimbo la Ulyankulu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Dugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rehema Juma Migilla, Mbunge wa Jimbo la Ulyankulu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali katika mwaka wa fedha 2020/2021 imeipatia Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua kiasi cha Shilingi milioni 600 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Afya cha Uyowa na ujenzi unaendelea. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na wananchi inaendelea na ujenzi wa Kituo cha Afya Mwangozo. Hadi Aprili 2021, shilingi milioni 158.69 zinazotokana na michango ya wananchi na mapato ya ndani ya halmashauri zimetumika kujenga jengo la

wagonjwa wa nje na wodi ya wazazi ambapo ujenzi unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2020/2021, halmashauri imetenga shilingi milioni 25 na katika mwaka wa fedha 2021/2022, Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua imetenga shilingi milioni 140 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Rehema Juma Migilla, swali la nyongeza.

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza niipongeze Serikali na kuishukuru pia kwa kuweza kutupatia fedha hizi ambazo nina uhakika zinakwenda kumaliza Kituo cha Afya cha Uyowa, lakini niendelee kuiomba Serikali basi hiki Kituo cha Mwangozo na chenyewe kiweze kufikiriwa ili kiweze kuendelea kutoa huduma. Hata hivyo, nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; kwa taaluma mimi ni Mwalimu na tunajua vigezo ambavyo vinatumika kuanzisha hizi shule zetu, lakini ningeomba kujua, je, wataalam wa Afya na TAMISEMI huwa wanatumia vigezo gani wanapoamua kujenga hizi zahanati zetu, kwani tunaona baadhi tu ya majengo ndiyo yanajengwa pasipokuwa na maabara ambapo tunajua maabara ndiyo kigezo kimojawapo ili Daktari aweze kutoa huduma vizuri. Je, kwa nini zahanati nyingi huko vijijini hazina maabara?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kama vigezo hivyo vinazingatiwa, je, Serikali sasa haioni umuhimu wa kutujengea hizi maabara katika zahanati zetu ili kuweza kuwapunguzia mzigo hawa wananchi wetu ambao wanatembea umbali mrefu kwenda kufuata huduma za maabara? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)**: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Rehema Juma Migilla, Mbunge wa Ulyankulu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, napokea pongezi zake kwa Serikali kwa kupeleka fedha shilingi milioni 600 kwa ajili ya kujenga Kituo cha Afya cha Uyowa. Pili, vigezo ambavyo vinatumika kujenga zahanati zetu ni michoro ambayo imepitiwa kitaalam na ambayo kimsingi kwa ramani zetu kwa sasa za Ofisi ya Rais, TAMISEMI za zahanati zina *provision* ya maabara. Kwa hiyo, ramani zote za vituo vya afya, zahanati na Hospitali za Halmashauri zina maabara. Hivyo, tutaendelea kuhakikisha tunatenga fedha kwa awamu kukamilisha yale majengo ya zahanati lakini pia na vyumba vya maabara kwa ajili ya kuhakikisha kwamba wananchi wetu wanapata huduma bora za afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, tunaona *of course* umuhimu wa kuhakikisha kwamba tunaendelea kujenga maabara na ndiyo maana kwenye swali la msingi nimeeleza ambavyo Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kujenga vituo hivyo zikiwemo maabara katika maeneo hayo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa George Mwenisongole, swali la nyongeza.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa niaba ya wananchi wa Mbozi napenda kuuliza swali langu kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Hayati Rais Magufuli akiwa kwenye kampeni aliahidi wananchi wa Mji Mdogo wa Mlowo kwamba kutajengwa kituo cha afya kikubwa cha kisasa pale. Tayari wananchi wameshapeleka *site* matofali 150,000 na tayari heka 10 zimeshatengwa. Sasa ni lini Serikali itapeleka fedha kuanza ujenzi wa kituo hicho cha afya katika Mji Mdogo wa Mlowo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)**: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa George Mwenisongole, Mbunge wa Mbozi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ahadi za Viongozi wetu wa Kitaifa ni ahadi ambazo lazima Serikali tutakwenda kuzitekeleza na hivyo tumeandaa mpango kabambe wa kuhakikisha kwamba tunaratibu utekelezaji wa ahadi zote zilizotolewa na Viongozi wetu wa Kitaifa ikiwemo Kituo cha Afya cha Mlowo katika Jimbo la Mbozi. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaendelea kuweka mpango na kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Kituo cha Afya cha Mlowo, Mbozi.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Waheshimiwa Wabunge niwakumbushe tena kwenda moja kwa moja kwenye swali; muda wa maswali sio muda wa kuchangia.

Mheshimiwa Lusengekile, swali la nyongeza.

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Serikali katika Jimbo la Busega imeanzisha vituo vya afya viwili ambavyo mpaka sasa vimeshaanza lakini bado vinakosa wodi ya wazazi, wanaume pamoja na wodi ya wanawake. Nini kauli ya Serikali ili kupeleka fedha kwa ajili ya kumalizia vituo vya afya hivyo kwa maana ya Lukungu pamoja na Sanza…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa umeshamaliza swali yaani ukisimama uwe umeandaa swali lako, usirudie tena maana mwanzoni umeanza na swali unataka tena kurudia hicho hicho mwishoni.

Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais (TAMISEMI) majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)**: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Lusengekile, Mbunge wa Busega, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Serikali imejenga vituo vya afya viwili katika Jimbo la Busega na ujenzi ule unaendelea kwa awamu. Tumejenga awamu ya kwanza lakini tunafahamu kwamba kunakosekana wodi ya wazazi, lakini pia wodi ya wanaume na baadhi ya miundombinu mingine ambayo bajeti ijayo tutatenga fedha kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunakamilisha ujenzi wa miundombinu hiyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mohamed Lujuo Moni, Mbunge wa Chemba, sasa aulize swali lake.

Na. 307

**Barabara ya Kwamtoro – Sanzawa - Mpendo**

**MHE. MOHAMED L. MONNI** aliuliza:-

Je, ni lini Barabara ya Kwamtoro – Sanzawa – Mpendo yenye kilomita 58.2 itajengwa kwa kiwango cha kupitika msimu mzima kwani kwa sasa imekatika kutokana na mvua kubwa na kutojengwa kwa muda mrefu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali

la Mheshimiwa Mohamed Lujuo Monni, Mbunge wa Jimbo la Chemba, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/ 2021, *TARURA* Halmashauri ya Wilaya ya Chemba imetenga shilingi milioni 84.04 kwa ajili ya matengenezo ya Barabara ya Kwamtoro – Sanzawa – Mpendo yenye urefu wa kilomita 23. Ujenzi wa barabara hii unaendelea ambapo matengenezo ya barabara yenye urefu wa kilomita 10, makalvati mawili na *drift* moja umekamilika. Katika mwaka wa fedha 2021/2022, jumla ya shilingi milioni 42 zimetengwa kwa ajili ya matengenezo ya barabara yenye urefu wa kilomita 10 na ujenzi wa makalavati matatu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022 pamoja na kazi nyingine Wakala wa barabara za Vijijini na Mijini, umepanga kufanya tathmini ya miundombinu ya barabara zake zote ikiwemo za Halmashauri ya Wilaya ya Chemba ili kuandaa mpango wa namna bora ya kutoa vipaumbele vya ujenzi na matengenezo ya barabara na madaraja. Serikali itaendelea kuboresha miundombinu ya barabara ikiwemo ya barabara ya Kwamtoro – Sanzawa – Mpendo kwa kadri ya upatikanaji wa fedha ili kuimarisha usafiri na usafirishaji.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mohamed Lujuo Monni, swali la nyongeza.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nasikitika sana swali langu halijajibiwa, swali limeuliza juu ya kilometa 58.2, nimejibiwa juu ya kilometa 23 tu. Naomba nirudi tena, ni lini Serikali itajenga barabara yote ya kilometa 58.2 kwa sababu sehemu kubwa ya barabara hiyo tayari imekatika kwa sababu ya mvua?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; barabara pia ya Larta – Lahoda – Handa imekatika kabisa hakuna namna watu wanaweza kupita. Naomba kupata majibu ya Serikali barabara hizi ni lini pia zitajengwa ili watu wapiti? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Monni kwanza niliwakumbusha Waheshimiwa Wabunge kuhusu Kanuni zetu ukisema swali halijajibiwa inamaanisha nini, nadhani nilishawakumbusha; tuwe tunasoma Kanuni zetu. Swali unalosema halijajibiwa hii sehemu ya mwisho kabisa anaeleza barabara utengenezaji utakuwaje. Ukisema halijajibiwa ni kwamba usingependa kusikia majibu hayo, lakini Serikali ndiyo imejibu hivyo, lakini sio kwamba haijajibu.

Mheshimiwa Naibu Waziri kwa ajili ya swali la nyongeza la pili la Mheshimiwa Mbunge.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)**: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mohamed Monni, Mbunge wa Jimbo la Chemba, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge ameuliza kwamba ni lini barabara inayopitia Lahoda na maeneo ambayo ameyaainisha kwamba itajengwa. Kama nilivyoeleza katika jibu la msingi kwamba katika mwaka huu wa fedha 2021/2022, *TARURA* kwa maana ya Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini umepanga kufanya tathmini ya barabara zote nchini pamoja na madaraja ili tuweze kuwa na *database* ya kutosha kuangalia zile barabara ambazo zinaharibika sana tuzipe kipaumbele katika mipango yetu inayokuja. Ndiyo maana nimeahidi kwamba moja ya barabara ambayo tutaipa kipaumbele ni hizi barabara ambazo ameitaja ikiwemo hii barabara ya Kwa Mtoro - Sanzawa – Mpendo ambayo tulikuwa tunaijenga kwa awamu kulingana na fedha inavyopatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge awe na Subira, Serikali ipo kazini na hatupo hapa kwa ajili ya kumdanganya mtu yeyote, lengo la Serikali ni kuwahudumia wananchi ili waweze kupata huduma bora kabisa ya usafiri na usafirishaji. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Engineer Ezra John Chiwelesa, Mbunge wa Biharamulo Magharibi aulize swali lake.

Na. 308

**Ujenzi wa Barabara ya Nyamirembe – Chato mpaka Katoke Biharamulo**

**MHE. EZRA J. CHIWELESA** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara ya Nyamirembe – Chato mpaka Katoke Biharamulo ya kilomita 50 kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Engineer Msongwe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ezra John Chiwelesa, Mbunge wa Biharamulo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Nyamirembe Port – Katoke yenye urefu wa kilometa 50 ni barabara ya Mkoa inayounganisha Bandari ya Nyamirembe ambayo ipo Mkoa wa Geita na Mji Mdogo wa Katoke ambao upo Mkoa wa Kagera kupitia vijiji mbalimbali na Hifadhi ya Burigi Chato. Barabara hii inahudumiwa na Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara nchini *(TANROADS).*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeshaanza taratibu za kuijenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami kwa kuifanyia upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa gharama ya Shilingi milioni 861.046 kwa kutumia fedha za ndani. Katika mwaka wa fedha ujao 2021/2022, fedha zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa Nyamirembe Port – Katoke, urefu wa kilomita 50.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kutambua umuhimu wa barabara hii inaendelea kuiimarisha kwa kuifanyia matengenezo ya aina mbalimbali kila mwaka kabla ya ujenzi kwa kiwango cha lami kuanza ili barabara hiyo ipitike katika vipindi vyote vya mwaka. Katika mwaka huu wa fedha 2020/2021, jumla ya Shilingi milioni 447.771 zilitengwa kwa ajili ya matengenezo mbalimbali na kwa sasa barabara hiyo ipo katika hali nzuri. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ezra John Chiwelesa, swali la nyongeza.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naishukuru Serikali kwa majibu mazuri. Hata hivyo, nina maswali mawili ya nyongeza ambayo ningependa kupata majibu yake. Swali la kwanza; kwa kuwa barabara hii ni kiunganishi muhimu ambacho kinaunga Chato na Biharamulo kuelekea katika Hifadhi ya Taifa ya Burigi Chato, ningependa kujua sasa kwamba *construction period* ya barabara hii itakuwa ni miezi mingapi ili nijue na wananchi wale waweze kujipanga kwa ajili ya kuchukua fursa za pale?

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuzingatia umuhimu wa Hifadhi ya Chato Burigi na *location* ya Uwanja wa Ndege wa Geita Chato ulipo, sasa ningependa kujua je, Serikali haioni ni wakati muhimu sasa wa kuijenga barabara hii sambamba na barabara ya Mkingo – Chato kupitia Kaswezibakaya ili iweze kuunganisha Kabindi pale watu wanaokuja waweze kutoka vizuri? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Msongwe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Ezra Chiwelesa, Mbunge wa Biharamulo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwenye jibu la msingi ni kwamba barabara hii imetengewa fedha

kwenye bajeti hii na yeye Mheshimiwa Mbunge ni shahidi. Kipindi cha matengenezo kitategemea na hali halisi, lakini cha msingi tu ni kwamba mara bajeti itakapoanza barabara hii itaanza kujengwa, lakini kipindi kitakachotumika itategemea na taratibu za manunuzi zitakavyokamilika, lakini pia na hali ya hewa itakayokuwepo. Kwa hiyo, ni ngumu kusema itachukua muda gani, lakini tutaanza kujenga mara tu bajeti itakavyoanza kutolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara nyingine aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge ni kwamba, barabara hii itaendelea kukarabatiwa katika kiwango cha changarawe. Hata hivyo, azma ya Serikali ni kuijenga kwa kiwango cha lami kadri fedha itakavyopatikana ili watalii na watu mbalimbali waweze kupita kwenye hizo mbuga za wanyama na kufika kwenye Uwanja wa Ndege wa Chato. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Sasa tunaendelea na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mheshimiwa Taska Restuta Mbogo, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 309

**Ujenzi wa Hospitali wa Mkoa wa Katavi**

**MHE. TASKA R. MBOGO** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itamaliza ujenzi wa Hospitali ya Mkoa wa Katavi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mheshimiwa Dkt. Mollel, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO (MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa hospitali ya Mkoa wa Katavi umekamilika kwa wastani wa asilimia 70, ambapo ujenzi kwa upande wa maabara umefikia asilimia 98 na jengo kuu la hospitali umefikia asilimia 42. Mradi huu unagharimu jumla ya shilingi bilioni 9.82 ambapo hadi sasa kiasi cha shilingi bilioni 3.97 zimetumika na bilioni 5.85 zimetengwa katika bajeti ya mwaka 2021/2022 na zitatumika kukamilisha ujenzi huu ifikapo Januari, 2022. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Taska Mbogo, swali la nyongeza.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, ninayo maswali mawili ya nyongeza. Kwanza, napenda kuishukuru Serikali kwa ujenzi na swali langu la nyongeza ni kwamba, kwa kuwa ujenzi huu umechukua muda mrefu na kwa kuwa wananchi wa Mkoa wa Katavi bado wanaisubiri kwa hamu sana hiyo Hospitali ya Mkoa. Je, Serikali inatoa *commitment* gani kutoa pesa zilizobaki bilioni 5.8 kwa ajili ya kumaliza ujenzi wa hii hospitali? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili; kwa kuwa Mkoa wa Katavi tumejenga vituo vingi sana vya afya, lakini pia tunazo hospitali tatu tumejenga kwenye Wilaya zetu tatu za Mkoa wa Katavi pamoja na zahanati. Je, Serikali ina mkakati gani wa kutuletea vifaa tiba kama vile vifaa vya upasuaji, *ultrasound* na kadhalika kwa ajili wananchi wakati wakiwa wanasubiri hiyo hospitali iishe waweze kuhudumiwa kwenye vituo vya afya pamoja na hizo hospitali? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Naibu Waziri swali lake la kwanza limejibiwa kwenye swali la msingi, bajeti inayokuja inayo hiyo bilioni 5.85, jibu swali la pili la nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO (MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niwapongeze Wabunge wote wa Mkoa wa Katavi, kwa kweli wamekuwa wakifuatilia suala la afya kwenye mkoa wao kwa kina sana na nawaelewa sana kwa sababu ni mojawapo ya mikoa ambayo ni migumu kufikika.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili ni kwamba ni lini sasa Serikali kwenye hospitali ambazo zimejengwa itapeleka vifaa tiba. Kama ambavyo Wabunge wanajua Rais wetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan ametoa bilioni 80 kwa ajili ya ununuzi wa dawa na vifaa tiba. Kwenye hizo bilioni 80 mojawapo ya vipaumbele ambavyo tayari tumeviweka ni hospitali ambazo Mheshimiwa Mbunge amezitaja hapa. Kwa hiyo, kwa uhakika kabisa tutafanya hivyo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Aysharose Mattembe, swali la nyongeza.

**MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Singida imechukua muda mrefu sana kukamilika. Je, ni lini sasa Serikali itakamilisha ujenzi wa hospitali hiyo ili wananchi waweze kupata huduma nzuri za afya? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO (MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL):** Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo tumeeleza kwenye Hospitali ya Mkoa ya Katavi, kwa ujumla kwenye Hospitali zetu za Mikoa kwa ajili ya umaliziaji wa ujenzi, Serikali kwenye bajeti ya mwaka huu imetengwa bilioni 57 ambapo kwenye bajeti hiyo mojawapo ya hospitali ambayo imetengewa bajeti ni Hospitali ya Mkoa wa Singida.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge baada tu ya bajeti hii sasa tunaenda kuanza kazi hiyo. Naomba mimi na yeye tupange kwenda kwenye Hospitali ya Mkoa wa Singida tuangalie mambo mengi kwa sababu vilevile kuna suala la wao kutoka kwenye ile hospitali ya mjini kuhamia kwenye hiyo hospitali inayojengwa. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hasunga, swali la nyongeza.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi. Ningependa kujua ni lini Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Songwe iliyopo Vwawa Ilembo itakamilika kwa sababu ilikuwa ianze kufanya kazi mwaka 2020? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO (MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL):** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge anakumbuka yeye alikuja akanieleza suala hilo na nilikwenda kwenye ile hospitali. Ninachotaka kumwambia jengo la *OPD* na maabara limeshakwisha lakini sasa jengo ambalo liko kwenye *level* ya msingi linajengwa ni jengo la wazazi ambalo nalo linaendelea na Waziri Mkuu alikuwa amepanga ziara ya kwenda kuzindua hayo majengo mawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwenye bilioni 80 iko kwenye bajeti ya kuweka vifaa kwenye hilo jengo la wagonjwa wa nje. Kwa hiyo, mara tu baada ya Bunge hili ratiba ile ya Waziri Mkuu ya kwenda kulizindua itakamilika na kazi itaanza kwenye hospitali wakati majengo mengine yanaendelea kuingizwa kwenye bajeti. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Stella Simon Fiyao, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 310

**Hitaji la Pembejeo za Kilimo- Songwe**

**MHE. STELLA S. FIYAO** aliuliza: -

Asilimia 70 ya wakazi wa Mkoa wa Songwe wanategemea kilimo.

Je, ni lini Serikali italeta pembejeo za kilimo kwa bei nafuu ambayo wakulima wengi wataweza kumudu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Hussein Mohammed Bashe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Stella Simon Fiyao, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali tumeanza kuboresha mifumo ya upatikanaji wa pembejeo kwa maana ya mbegu, mbolea na viuwatilifu, kuratibu mahitaji ya pembejeo kutoka katika mikoa na kuweka mazingira wezeshi kwa ajili ya makampuni kupeleka na kuuza. Majukumu hayo yanatekelezwa kwa kutumia mfumo wa *bulk purchase* hasa katika eneo la mbolea.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha miaka minne tangu kuanzishwa kwa mfumo huu wa ununuzi bei za ununuzi kwa maana ya *Free on Board* zimepungua. Changamoto kubwa tunayokabiliana nayo ni gharama za usafiri na bima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kutekeleza mikakati ya kuongeza upatikanaji wa pembejeo kwa kuvutia wawekezaji wa kampuni binafsi hasa katika eneo la mbegu, mikataba maalum kwa ajili ya kupunguza gharama.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikakati mingine ni kuanzisha mifumo ya ugharamiaji wa sekta ikiwemo uanzishwaji wa Mfuko wa Pembejeo *(Credit Guarantee Scheme)* pia kupunguza au kufuta baadhi ya tozo na ada. Kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita Serikali imepitia na kufuta tozo 12 katika mbegu na tozo nne za mbolea ili kupunguza bei na gharama za pembejeo hizo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Stella Simon Fiyao, swali la nyongeza.

**MHE. STELLA S. FIAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kutokana na changamoto kubwa ya upungufu wa mafuta iliyopo katika nchi yetu, nataka kujua Serikali imejipanga vipi kuhakikisha inaleta mbegu bora ya alizeti kwa bei ndogo na ya chini ambayo kila mkulima ataweza kuimudu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kutokana na changamoto kubwa ya upatikanaji wa mbegu ya mahindi na mbolea katika Mkoa wa Songwe, je, Serikali iko tayari kuwaruhusu wananchi wa Mkoa wa Songwe kununua mbegu ya mahindi na mbolea katika Nchi jirani ya Zambia pasipo kuwabughudhi? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Bashe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Stella, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba wananchi wamekuwa wakinunua mbegu hasa waliopo mipakani katika maeneo ya Mkoa wa Rukwa na Mkoa wa Songwe kupitia mbegu zinazoingia kwa njia ambazo si halali. Vilevile tunajiridhisha na naweza nikamtolea mfano Mheshimiwa Hasunga akiwa mkulima katika Mkoa wa Rukwa aliwahi

kununua mbegu za njia hizo na matokeo yake mahindi hayakuweza kukua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niahidi tu mbele ya Bunge lako kwamba hii changamoto tunaifanyia kazi na tutakaa na wadau wa maeneo hayo ili tutathmini njia nzuri ya kuingiza mbegu kihalali ambazo tuna upungufu nazo na kwa gharama nafuu kwa wakulima wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la alizeti ni kweli kama nchi tuna upungufu wa karibu *metric tons* laki nne za mafuta ya kula. Hatua ambayo tunachukua mwaka huu, jana Waheshimiwa Wabunge wametupitishia bajeti, tumekaa na sekta binafsi na taasisi yetu ya *ASA;* mahitaji yetu ya mbegu ni kati ya *metric tons* 5,000 – 6,000 ambazo tutaenda kutumia kuzalisha kwenye eneo la hekari milioni 1.3 ambalo hili litatupatia zaidi ya tani milioni 1.2 za mbegu kwa ajili ya kwenda viwandani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua tunayoichukua uzalishaji wa ndani utazalisha tani 2,000, tunakaa na *ASA* na waagizaji kutoka nje tutaagiza *deficit* ya mbegu kwa mwaka huu na tutaipeleka kwa wakulima *at subsidized rate* kwa sababu tumetenga fedha katika bajeti ili kupunguza bei ya *hybrid* kutoka Sh.30,000 kwa kilo moja angalau ifike kati ya Sh.7,000 hadi Sh.10,000 na Wizara ita-*subsidize* mbegu hizo ili wakulima waweze kupata kwa bei rahisi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Sasa ni Wizara ya Maji, Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 311

**Mradi wa Maji Kabwe – Nkasi**

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA** aliuliza:-

Je, ni lini Mradi mkubwa wa Maji wa Kabwe katika Wilaya ya Nkasi utakamilika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa *Eng*. Mahundi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakangata, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji Kabwe una miundombinu yote kwa ajili ya kutoa huduma ya maji. Miundombinu hiyo ni matanki matatu yenye ujazo wa lita 50,000, lita 10,000 na lita 135,000, vituo vya kuchotea maji 29, nyumba ya pampu ya kusukuma maji na mabomba ya kilometa 10.9. Changamoto iliyojitokeza kwenye mradi huu ni uwezo wa nishati ya umemejua kushindwa kusukuma maji ipasavyo kwenda kwenye matanki hayo, hivyo, kusababisha huduma ya maji kusimama kwa wananchi hususan kipindi cha usiku.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha huduma ya maji kwa wananchi wa Kabwe inapatikana muda wote, Serikali imeamua kubadili mfumo wa umemejua kwa kufunga umeme toka kwenye gridi kupitia *REA* na kazi hiyo inatarajiwa kukamilika kabla ya mwishoni mwa mwezi Juni, 2021.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata, swali la nyongeza.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwanza kabisa naishukuru Serikali imeweza kuingiza kiasi cha shilingi bilioni 1.3 kwenye mradi huu. Mradi huu ulifanya kazi miezi mitatu tu na watu wakaihujumu ile miundombinu kwa kuiba vifaa kama *solar,* betri na pampu. Sasa swali langu linakuja, ni lini sasa Serikali itarudisha vifaa hivi ili wananchi waweze kuendelea kupata maji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa wezi wapo wanajulikana kabisa kwenye Kata ile, Serikali ina mpango gani sasa wa kuwachukulia hatua kazi za kinidhamu? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa *Eng*. Maryprisca Mahundi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake namba moja lini vifaa vile vitarudishiwa pale kama nilivyojibu kwenye jibu langu la msingi na kadiri ambavyo tumekuwa tukiongea naye kuhusu suala hili na nimpongeze kwa namna ambavyo amekuwa mfuatiliaji mzuri. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba suala hili hatutazingatia zaidi kwenye vile vifaa vya *solar,* tutazingatia kuleta umeme kwa kupitia *REA* ili tuwe na umeme wa uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na wale wezi kuchukuliwa hatua, kwanza niombe ushirikiano Zaidi, tuendelee kuwasiliana, hawa wezi Mbunge akiwa kama mwakilishi wa akinamama wa eneo lile, aende akaripoti polisi, lakini tumekuwa tukimsikia mara nyingi Mheshimiwa Waziri wetu kwamba mwisho wa kuchezea miradi ya maji ni sasa. Kama una mambo ya kutaka kuchezea, kachezee kitambi chako. Kwa hiyo, tutaendelea kuhakikisha kwamba miradi ya maji mwisho kuchezewa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Haya hapa sasa kuna swali la asiyekuwa na kitambi, nadhani atatafuta yeye cha kuchezea. Mheshimiwa Aida Khenani swali fupi la nyongeza.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na nishukuru majibu ya Naibu Waziri. Waziri Mheshimiwa Mbarawa akiwa Waziri wa Maji alipofika kwenye mradi huu aligundua shida ni mfumo ambao ni umeme wa kutumia jua na kwa sababu huo mradi wa *REA* bado

haujaanza kufanya kazi Kata ya Kabwe, ni lini watashirikiana na Wizara ya Nishati ili wananchi wa Kijiji cha Odachi, Kabwe *Camp* pamoja na Kabwe Asilia waweze kupata maji? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji, Mheshimiwa Aweso, majibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikushukuru, lakini nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri wangu kwa namna nzuri anavyojibu maswali. Sisi Mawaziri viongozi wetu wametuelekeza kufanya kazi kwa pamoja na tumeshafanya mawasiliano na Mheshimiwa Waziri wa Nishati kuainisha maeneo yote yenye miradi yenye mfumo wa jua kuhakikisha kwamba tunafanya mageuzi kuweka mfumo wa *REA* kwa maana ya nishati ya umeme ili kuhakikisha kwamba tunapunguza gharama ya uendeshaji ili wananchi waweze kupata huduma ya majisafi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nataka nimhakikishie Mheshimiwa Aida hili jambo tumeshakaa na tumeshaainisha kwa hiyo wenzetu wa nishati watatupa nguvu kuhakikisha maeneo yote yenye *solar* tunafanya mabadiliko kuhakikisha kwamba tunaweka nishati ya umeme. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga, Mbunge wa Mbinga Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 312

**Kuongeza Upatikanaji wa Maji – Ruanda - Mbinga**

**MHE. BENAYA L. KAPINGA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza upatikanaji wa maji katika Mji wa Ruanda Wilayani Mbinga?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji *Engineer* Maryprisca Mahundi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Liuka Kapinga Benaya, Mbunge wa Mbinga Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mji wa Ruanda unakua kwa kasi hivyo kuongezeka kwa mahitaji ya maji kufikia wastani wa ujazo wa lita 210,100 kwa siku ikilinganishwa na uzalishaji wa sasa wa ujazo wa lita 162,000 kwa siku. Serikali katika mwaka 2021/2022 imepanga kukarabati Mradi wa Maji Ruanda ambapo kazi zitakazofanyika ni pamoja na kujenga vituo 15 vya kuchotea maji, kujenga chemba moja ya kugawa kwenda kwenye njia kuu, kufanya ukarabati wa chanzo, kulaza bomba njia kuu na njia ya usambazaji umbali wa kilometa 22.9 pamoja na ukarabati wa matanki mawili ya kuhifadhia maji ya ujazo wa lita 50,000 na 75,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022, Serikali imetenga kiasi cha Shilingi bilioni 1.39 kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maji Wilayani Mbinga ukiwemo ukarabati wa Mradi wa Ruanda kwa ajili ya kuboresha upatikanaji wa maji katika Mji wa Ruanda.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Benaya Kapinga, swali la nyongeza.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naishukuru Serikali kwa majibu mazuri, lakini nina swali moja dogo la nyongeza. Mradi wa Maji wa Litembo una uchakavu mkubwa wa miundombinu hali iliyopelekea Kijiji cha Langandondo kukosa maji kwa miaka minne mvululizo, lini mradi huu unaenda kukarabitiwa na wananchi wale wa Langandondo waweze kupata maji Kata ya Litembo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu kwa swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Liuka Benaya, Mbunge wa Mbinga Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, uchakavu wa Mradi wa Litembo kama Wizara tunautambua na tayari tumetoa maagizo kwa Meneja wa *RUWASA* tayari na yeye anaendelea kujipanga ili kuhakikisha kwamba mwaka ujao wa fedha nao tuweze kutupia jicho la utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nipende kumpongeza Mheshimiwa Liuka amekuwa ni mfuatiliaji mzuri, tumeondoka hapa wakati wa *weekend* tumekwenda Mbinga Vijijini tumefanya kazi nzuri na miradi hii yote ya uchakavu pale anafahamu tulishakubaliana utekelezaji wake utafanyika kwa haraka.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Sasa tunaendelea na Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Flatei Gregory Massay Mbunge wa Mbulu Vijijini sasa aulize swali lake.

Na. 313

**Ujenzi wa Mahakama – Hydom**

**MHE. FLATEI G. MASSAY** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake ya kujenga Mahakama Hydom katika Jimbo la Mbulu Vijijini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Geophrey Pinda, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Flatei Gregory Massay, Mbunge wa Mbulu Vijijini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Ujenzi wa Mahakama ya Hydom ni moja ya miradi ambayo Mahakama imesaini mkataba Machi, 2021 na tayari Mkandarasi ameanza kazi. Mradi huu utakamilika ifikapo mwezi Agosti, 2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha miaka mitano 2016/2017 – 2020/2021, Mahakama inafanya maboresho makubwa ili kukabiliana na changamoto ya uhaba na uchakavu wa majengo. Maboresho hayo ni pamoja na ujenzi na ukarabati wa majengo katika maeneo mbalimbali kwa ngazi zote za Mahakama. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Flatei Massay, swali la nyongeza.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwanza nionyeshe furaha yangu kwa Serikali kwa kukubali kujenga hii Mahakama ya Mwanzo ya Hydom. Swali, Mahakama ya Wilaya bahati mbaya eneo lake limepitiwa na barabara, je, Wizara ina mpango gani wa kuingiza kwenye bajeti zao ili Mahakama ile ipate kujengwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; Waziri amesema Mahakama imeanza kujengwa, je, yupo tayari sasa kwenda Hydom kuona ule ujenzi unaendeleaje ndani ya Jimbo la Mbulu Vijijini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Flatei sasa hilo la pili wewe unamwambia kama ujenzi umeanza ama haujaanza, kweli Mheshimiwa Waziri aje tu kuangalia kama ujenzi umeanza, kama umeanza yeye yaani anakuja pale kufanya nini? Hebu fafanua, kama ujenzi haujaanza mwambie ulichosema ujenzi umeanza haujaanza, kama umeanza yeye unamtaka wa nini huko kwako. *(Kicheko)*

**MHE: FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Ni kweli ujenzi umeanza ila mwezi Agosti ni mapema sana, sasa ndiyo tufuatane na yeye mwenyewe...

**NAIBU SPIKA:** Sawa, umeshaeleweka Mheshimiwa.

Mheshimiwa Naibu Waziri nadhani huyu anataka kutembelewa ukimaliza ziara zingine unaweza kwenda kumtembelea Mheshimiwa Massay. Jibu swali lake la pili.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimtoe wasiwasi kwenye mfumo huu wa Mahakama asicheze ile sarakasi aliyokuwa ameiahidi kwenye Wizara ya Kilimo. Kwa hiyo nipende tu kumuhakikishia kwamba kwenye swali lake la kwanza la nyongeza kuhusu ile Mahakama ya Wilaya kupitiwa na barabara hilo tutalifanyia kazi na kwa kushirikiana naye tutajua namna ya kufanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili la kutembelea Mahakama inayoendelea kwenye ujenzi, nipo kwenye ratiba leo ninapomaliza kujibu swali hili nakwenda huko Hydom. Kwa hiyo nimualike tu Mheshimiwa Mbunge tufuatane naye kwa sababu tunahakiki yale majengo yanayoendelea kujengwa. Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI:** Ahsante sana. Sasa tunakwenda Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Atupele Fredy Mwakibete Mbunge wa Busokelo, sasa aulize swali lake.

Na. 314

**Ujenzi wa Mradi wa Umeme wa Maji Mto Rumakali – Busokelo**

**MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE** aliuliza:-

Je, ni lini ujenzi wa Mradi wa Umeme wa Maji kutoka Mto Rumakali katika Kata ya Lufilyo utaanza?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Stephen Byabato Lujwahuka, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Atupele Fredy Mwakibete, Mbunge wa Busokelo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Shirika la Umeme nchini *(TANESCO)* inatekeleza Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa kutumia maporomoko ya maji ya Mto Rumakali, Mkoani Njombe.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu unahusu ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme cha *megawati* 222 na njia ya kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 220 yenye urefu wa kilomita 150 kutoka Rumakali hadi Kituo cha Kupoza Umeme cha Iganjo, Mkoani Mbeya. Gharama za mradi ni takriban shilingi bilioni 913.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua iliyofikiwa sasa ni kukamilisha taratibu za manunuzi ya Mkandarasi wa ujenzi wa mradi. Kazi za ujenzi zinatarajiwa kuanza mwezi Oktoba, 2021 na kukamilika mwezi Juni, 2024.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete, swali la nyongeza.

**MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kabla sijauliza maswali mawili ya nyongeza naomba kwanza nikushukuru sana pamoja na Serikali kwa changamoto ambazo tulizipata Jimbo la Busokelo kwa mafuriko ambayo yalisababisha nyumba zaidi ya 30 pamoja na mtu mmoja kufariki, lakini wewe pamoja na timu yako mlikuja kutoa msaada. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa niulize maswali mawili ya nyongeza, pamoja na majibu ya Serikali, huu Mradi wa Mto Rumakali upo katika halmashauri mbili kati ya Halmashauri ya Busokelo pamoja na Mkoa wa Njombe, lakini mradi huu katika utekelezaji wake inaonyesha kwamba licha ya kwamba megawati hizo zitazalishwa tunahitaji kujua wananchi wa Busokelo, je, ni kwa kiwango gani kupitia *Corporate Social Responsibility* ya mradi huu

watanufaika wananchi wa Busokelo pamoja na Kata hii ya Lufilyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa mradi huu utaanza kuzalishwa hivi karibuni na tunafahamu kwamba Halmashauri ya Busokelo ni halmashauri changa, je, ni kwa kiwango gani Serikali imejipanga kuboresha miundombinu kufikia sehemu ya uzalishaji wa mradi huu kupitia Halmashauri ya Busokelo hususani madaraja ya Mto Lufilyo pamoja na madaraja ya Mto Malisi? Ahsante.*(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Nilikuwa naangalia Naibu Waziri TAMISEMI yupo wapi kwa ajili ya hayo madaraja. Mheshimiwa Naibu wa Nishati, Mheshimiwa Lujwahuka, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Atupele, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapotekeleza miradi mikubwa ya namna hii kipande cha *Corporate Social Responsibility* kwa maana ya manufaa ya mradi kwa umma ni kipande ambacho kinaongozwa na sheria tuliyokuwa nayo kwetu Tanzania na tunakiweka kwenye mkataba kwa ajili ya kukubaliana kwamba katika mapato na kazi utakayoifanya kiasi hiki basi kirudi kurudisha huduma katika jamii husika. Tunakwenda afya, tunakwenda kwenye maji, tunakwenda kwenye elimu na kwenye miundombinu kama hiyo ya barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mzuri ni katika mradi wetu wa Mwalimu Nyerere, katika mradi wetu ule tunazo trilioni sita, lakini asilimia nne zimeenda kwenye *CSR* kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutakapokuwa tumeingia mkataba na mkandarasi wa kujenga mradi ule, lazima tuwe na kifungu cha *Corporate Social Responsibility* ambacho kitawanufaisha wananchi wa Busokelo, lakini pia na Makete ambapo ndiyo bwawa linapoanzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye swali la pili, umuhimu wa kufikia ile miundombinu itakayotengenezwa ndiyo itakayofanya miundombinu ya barabara iwepo, kwa sababu mradi kama mradi kwa maana ya ujenzi wa bwawa, lakini pia ujenzi wa ile *power house,* sehemu ambayo umeme utazalishwa, lazima tuwe tuna barabara nzuri zinazopitika kwa sababu tunayo mizigo mikubwa ambayo tunatakiwa kuisafirisha kuifikisha katika maeneo yale. Kwa hiyo tutajenga barabara hizo ikiwa ni faida kwa kuhudumia mradi, lakini pia na kuhudumia wananchi wa maeneo hayo kwa ajili ya kufikika katika maeneo yote.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Festo Sanga, swali la nyongeza.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana, kwanza niipongeze Wizara ya Nishati kwa sababu mradi huu wa Bwawa la Rumakali, bwawa linajengwa Wilaya ya Makete, lakini *power plant* inajengwa Busokelo kwa ndugu yangu Mwakibete.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu dogo la nyongeza lilikuwa Waziri alipokuja Makete mwezi wa kwanza aliahidi kwamba mradi huu utaanza mwezi Machi kwa maana ya *demarcation* kuweka alama, lakini hadi sasa haujaanza. Je, ni lini Serikali itaanza kuweka alama *(demarcation)* kwenye mradi huu ili wananchi waendelee na shughuli za kijamii, waachane na hii changamoto waliyonayo sasa wanashindwa kuendelea na shughuli za kijamii kwa sababu, hawajui bwawa mipaka itaishia wapi? Naomba pia kujua kuhusu mambo ya fidia. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Festo Sanga, Mbunge wa Makete, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli mwezi Januari Mheshimiwa Waziri alitembelea mradi ule kuona maandalizi yake yamefikia wapi na sisi kama Serikali tumejipanga kuanzia tarehe Mosi, mwezi Juni, wataalam wa Wizara na *TANESCO* wataenda katika eneo la mradi kwa ajili ya kuhakiki mipaka na kuweka *demarcation* na kufanya maandalizi ya kulipa fidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, fidia italipwa katika maeneo makubwa matatu. Fidia kwenye eneo ambapo litajengwa bwawa, lakini fidia katika eneo ambalo litaenda kuweka hiyo *power house,* sehemu ya kuzalisha umeme kwa sababu kutoka kwenye bwawa kushuka mpaka sehemu ya kuzalisha umeme kuna kilometa kama saba. Vile vile fidia italipwa kutoka kwenye njia ya kuzalisha umeme mpaka kwenye kituo chetu cha Iganjo ambapo kuna kilometa kama mia moja hamsini kutoka kwenye lile eneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo maeneo yote hayo kuanzia tarehe Mosi mwezi Juni yataanza kufanyiwa kazi ikiwa ni pamoja na kufanya tathmini kwa ajili ya kuweza kulipa fidia na mradi uweze kuendelea kama ilivyosemwa kufikia mwezi Oktoba.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, aya ya tatu ya jibu lako, kuna sehemu inasomeka hadi kituo cha kupooza umeme cha Iganjo Mkoani Mbeya. Sasa hiki kituo cha kupooza umeme hii Kata hii inayoitwa Iganjo mlipoweka kituo hiki cha kupooza umeme, Mtaa wa Igodima hauna umeme, sasa mmeweka kituo cha kupooza umeme, lakini mtaa hauna umeme. Huo mtaa utapata lini umeme? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na kama tulivyokuwa tukieleza hapo awali ni nia ya Serikali kuhakikisha kila mwananchi wa nchi hii anapata umeme katika eneo lake. Katika eneo hili sasa ni eneo la kipaumbele kwa sababu siyo vema kumpelekea mtu shughuli ambayo wananufaika nayo wengine. Kwa hiyo, nitoe ahadi ya Serikali kwamba, tutahakikisha hicho kituo kinapowekwa

pale basi tunaweza kupata umeme wa kuhudumia yale maeneo yote ya jirani kama ambavyo tumefanya hivi karibuni katika Bwawa la Mtera kwa kuongeza pale *transformer* ya kuhudumiwa wale wananchi wanaoishi katika maeneo yale kwa haraka kabisa.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Bado tuko Wizara hiyo hiyo ya Madini, Mheshimiwa Ghati Zephania Chomete, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 315

**Teknolojia Mbadala ambayo Itaepusha Kutumia Magogo kwenye Migodi**

**MHE. GHATI Z. CHOMETE** aliuliza:-

Je, Serikali ina teknolojia gani mbadala ambayo itaepusha kutumia magogo kama matimba kwenye mashimo ya migodi hasa maeneo ya Nyamongo, Tarime, Buhemba na Butiama?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini, Mheshimiwa Profesa Shukrani Manya.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ghati Zephania Chomete, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa wachimbaji wengi wadogo nchini na katika maeneo yote yenye shughuli za uchimbaji wa dhahabu yakiwemo maeneo ya Nyamongo, Tarime, Buhemba na Butiama wamekuwa wakitumia magogo na kwa lugha yetu ya kichimbaji yanaitwa matimba na yanatumiwa kama mihimili ulalo pamoja na wima kwenye mashimo ya migodi ili kuweka *support*. Pamoja na teknolojia hiyo kuonekana kuwa ya

gharama nafuu, imekuwa ikisababisha uharibifu mkubwa wa mazingira licha ya kuwa si salama na si ya kudumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, teknolojia mbadala inayotumika kwa sasa ni ujenzi wa mashimo ya migodi kwa kutumia zege pamoja na nondo. Teknolojia hii ni salama na haina athari kubwa za kimazingira ukilinganisha na ile inayotumia magogo. Miongoni mwa sababu zinazopelekea wachimbaji wadogo kutotumia teknolojia hii ni ufinyu wa mitaji, lakini pia, kutokuwa na maeneo ya kudumu ya uchimbaji na baadhi yao kutokuwa na leseni za uchimbaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kuwarasimisha wachimbaji wadogo kwa kuwapatia leseni za madini ili waweze kutambulika kisheria na kwa jinsi hiyo kuwawezesha kuaminika katika taasisi mbalimbali za fedha. Aidha, Serikali kupitia *STAMICO* inaendelea kutoa elimu kwao kuhusu uchimbaji wa kitaalam na wenye tija unaozingatia masuala ya afya, usalama na utunzaji mazingira.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ghati Chomete, swali la nyongeza.

**MHE. GHATI Z. CHOMETE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali machache ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa Serikali imesema kwenye majibu yake ya msingi kuwa teknolojia mbadala itakayotumika sasa ni ujenzi wa zege kwa kutumia nondo. Je, ni lini teknolojia hii itawafikia wachimbaji wale wadogo wa Nyamongo, Butiama, Tarime na Buhemba ili waweze kufanya uchimbaji wenye tija kwao na kwa Taifa letu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; Serikali imekiri kuwa kinachopelekea kutumia miti, mitimba na magogo kwenye mashimo ni ufinyu wa mitaji waliyonayo wale wachimbaji. Je, ni lini Serikali itawawezesha kwa kuwapa mitaji wachimbaji hao ili waweze kukidhi mahitaji hayo? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini, Mheshimiwa Profesa Manya, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tena niweze kujibu maswali ya nyongeza mawili ya Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la kwanza linazungumza juu ya lini teknolojia hii itafikishwa kwa wachimbaji wadogo. Nimpe taarifa tu, Mheshimiwa Mbunge kwamba katika mojawapo ya Migodi ya Wachimbaji Wadogo ya Kalende katika eneo la Tarime tayari mgodi mmojawapo wa Mara *Mine* umekwishaanza kutumia teknolojia hii kuashiria kwamba kumbe teknolojia imefika. Kwa sababu inahitaji kusambazwa kwa wengi nitumie nafasi hii, kumuagiza Afisa Madini Mkaazi wa Mkoa wa Mara, Ofisi yetu ya Musoma, aanzishe mafunzo kwa wachimbaji wote wa maeneo hayo ili waweze kuipokea teknolojia hii.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, ni kuhusu uwezeshaji. Itakumbukwa hapa kwamba, mwaka jana 2020 Tume ya Madini ilianza kutoa semina kwa mabenki yetu nchini ili kujenga *awareness* ya kwamba, uchimbaji madini ni biashara inayolipa kama biashara nyingine. Tulipokuwa tukisoma bajeti yetu hapa, tulithibitisha jinsi ambavyo mabenki yamepokea kwamba, biashara ya madini inawezekana na ni kweli kwamba tayari mabenki yameanza kuwezesha wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tutakachokifanya ni kuendelea kutoa elimu hii kwa mabenki ili kwamba, watambue maeneo ambayo yanapata tija katika uchimbaji na kwa jinsi hiyo waweze kuelekeza fedha katika kuwezesha wachimbaji wadogo. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali na majibu kutoka upande wa Serikali.

Sasa nilete matangazo niliyonayo hapa mbele, tutaanza na tangazo la wageni. Kwanza ni wageni wangu watano ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma, wakiongozwa na Ndugu Ngao Godliving Petro na hawa ni Ndugu Lema Kamao, Shoo Anamwikira, Mustapha Ahmad na Shoo Eliudi. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni 34 wa Mheshimiwa William Lukuvi, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ambao ni Watendaji Wakuu wa Wizara na Taasisi zilizo chini ya Wizara hiyo. Tutaanza na Ndugu Mary Makondo ambaye ni Katibu Mkuu. Karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye pia, Ndugu Nicholas Mkapa ambaye ni Naibu Katibu Mkuu. Tunaye pia Ndugu Mathew Muhonge ambaye ni Kamishna wa Ardhi, sijui amekaa upande gani. Tunaye pia, Ndugu Eveline Ngasha ambaye ni Mthamini Mkuu wa Serikali. Tunaye pia, Ndugu Dkt. Maulid Banyani ambaye ni Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Taifa la Nyumba. Karibuni sana. *(Makofi)*

Vile vile tunaye Profesa Wakuru Magigi, ambaye ni Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Taifa ya Matumizi ya Ardhi. Tunaye pia Ndugu Stella Tulo ambaye ni Msajili Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya, huyu kama nakumbuka vizuri mwanafunzi wangu huyu, hebu simama. Waheshimiwa Wabunge nikiwaambia umri umesonga huyu ni Msajili wa Mabaraza ya Ardhi na mimi ni Mwalimu wake, kwa hiyo, karibu sana Stella Tulo, nimefurahi kukuona. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia siku ya leo Mheshimiwa Lukuvi anaye mgeni mwingine ambaye ni mke wake, Ndugu Germina Lukuvi, karibu sana, karibu sana mama, Mheshimiwa Lukuvi yuko salama kabisa humu ndani usiwe na wasiwasi. *(Makofi)*

Wageni wengine 26 wa Mheshimiwa Lukuvi, hawa ni Makamishna wa Ardhi kutoka Mikoa yote ya Tanzania, wakiongozwa na Kamishina wa Ardhi wa Mkoa wa Arusha Ndugu Leo Komba. Makamishna wa Ardhi, karibuni sana. *(Makofi)*

Hapo kwa sababu mmesema mikoa yote naamini na wa kwangu yupo, Siambumi Mwaipopo yupo jamani? Karibu sana, jamani huyo ni Kamishna wa Ardhi anatoka Mkoa wa Mbeya, anafanya kazi nzuri sana hapa nimesikia na eneo lingine wanasema sana, kwa hiyo naamini mambo mazuri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge wapo pia wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge wengine na tunao wageni 21 wa Mheshimiwa Jenista Joachim Mhagama, ambaye ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu, ambao ni WAWATA Parokia ya Kiwanja cha Ndege na Veyula, Jijini Dodoma wakiongozwa na Ndugu Rosalia Mwanga, karibuni sana WAWATA. *(Makofi)*

Yupo pia mgeni wa Innocent Bashungwa ambaye ni Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, ambaye ni mshindi pekee wa Kiafrika wa Mashindano ya Dunia kuhusu Amani na Vijana. Pia ni mwandishi wa habari kutoka Redio *Kings FM* ya Jijini Dar es Salaam na huyu ni Ndugu Iman Luvanga, karibu sana. Huyu anasema ni mshindi pekee wa Kiafrika wa mashindano ya Dunia kuhusu amani na vijana, sijui mashindano yanafanywaje, lakini yeye ndio mshindi wetu jamani wa Kiafrika. Karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tunao pia wageni 22 wa Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula, ambao ni wapiga kura wake kutoka Ilemela Jijini Mwanza wakiongozwa na Ndugu Renatus Mlunga, sijui wamekaa upande gani ni Madiwani? Haya, hapa nimeambiwa wapiga kura nikawa nawaza nitaona sijui watu wangapi hapo, lakini sasa naambiwa hawa ni Waheshimiwa Madiwani kutoka Ilemela. Karibuni sana Waheshimiwa Madiwani, naamini mnamlindia vizuri Jimbo Mheshimiwa hapa akiwa kwenye harakati za kusaidia nchi nzima nyie mnamtunzia Jimbo huko Ilemela, karibuni sana. *(Makofi)*

Leo pia, wapo wageni tisa wa Mheshimiwa Omar Kipanga, ambaye ni Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia ambao ni viongozi na watendaji wa Baraza la

Taifa la Elimu ya Ufundi *(NACTE),* wakiongozwa na Mwenyekiti wa Baraza Profesa John Kondoro, karibuni sana, karibuni sana. *(Makofi)*

Kabla hamjakaa Waheshimiwa Wabunge jana mlitangaziwa tangazo hapa kuhusu, maonesho ya elimu na mafunzo ya ufundi ambayo yataanza tarehe 27 Mei hadi 2 Juni, 2021, katika Uwanja wa Jamhuri. Waheshimiwa Wabunge mnakaribishwa mwende kuona hayo maonesho ya elimu na mafunzo ya ufundi, ili na nyie yumkini mtoe ushauri kule ufundi gani wawe wanatoa, ili vijana wetu kule Majimboni waweze kujiajiri.

Ahsanteni sana mnaweza kukaa na kwa wale wanaofanya fanya mazoezi pale Jamhuri nadhani mtakuwa mmeona maandalizi ya hatari kabisa. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge kuanzia kesho mnakaribishwa huko, mkaone mambo mazuri wanayoyafanya hawa ndugu zetu wa *NACTE*. *(Makofi)*

Tunao pia, wageni wanne wa Mheshimiwa Mrisho Gambo ambao ni Madiwani kutoka Jijini Arusha, wakiongozwa na Naibu Meya, Mheshimiwa Veronica Mwelange, karibuni sana Waheshimiwa. Naibu Meya ni yupi hapo kati yenu? Naibu Meya mwana mama, ahsante sana, karibuni sana. *(Makofi/Vigelegele)*

Tunao pia wageni 10 wa Mheshimiwa Mhandisi Ezra Chiwelesa, ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma kutoka Biharamulo, Mkoani Kagera wakiongozwa na Ndugu Elis Pastory. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni 10 wa Mheshimiwa Vita Kawawa, ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma kutoka Jimboni Namtumbo, wakiongozwa na Ndugu Saidi Amir, sijui wamekaa upande gani hawa ama hawakupata fursa ya kuingia.

Tunao pia wageni 20 wa Mheshimiwa Dkt. Pius Chaya ambao ni wajasiriamali wa Kikundi cha Manyoni *Vision* kutoka

Mkoani Singida, wakiongozwa na Madiwani Mheshimiwa Ally Minja na Mheshimiwa Kodman Mpondo, karibuni sana, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Stanslaus Mabula ambaye ni mwanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Mzumbe, Mkoani Morogoro, Ndugu Rehema Mwemkala, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni 23 wa Mheshimiwa Magreth Simwanza Sitta, kutoka Taasisi ya *Patriotic Youth Association* iliyopo Urambo, Mkoa wa Tabora, wakiongozwa na Ndugu Marko Nusur, karibuni sana. *(Makofi/Vigelegele)*

Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Ighondo Ramadhan ambaye ni mpiga kura wake kutoka Jimbo la Singida Kaskazini Ndugu, John Hasi. Karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 11 wa Mheshimiwa Japhet Hasunga ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma wanaotokea Mbozi, Mkoa wa Songwe, wakiongozwa na Ndugu Jacob Mdalauma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni watano wa Mheshimiwa Zaytun Swai ambao ni wadau wa maendeleo wa elimu *TED* kutoka Jijini Arusha, wakiongozwa na Mkurugenzi wao Ndugu Gloria Anderson. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Oran Njeza kutoka Jijini Mbeya, ambaye ni Mkurugenzi na mdau wa zao la pareto, Ndugu Daniel Kapusi. Karibu sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni 20 wa Mheshimiwa Venant Protas, ambao ni wanafunzi wanaosoma Chuo Kikuu cha Dodoma wanaotokea Jimboni Igalula Mkoa wa Tabora, wakiongozwa na Ndugu Naila Marko. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Fred Mwakibete, ambaye ni mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha *Saint* John's

anayetokea Jimboni Busokelo Mkoani Mbeya na huyu ni Ndugu Emmanuel Mwasamwile. Karibu sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni 35 wa Mheshimiwa Riziki Lulida, ambao ni Wanachama wa Chama cha Mapinduzi tawi maalum la Chuo Kikuu cha Waislam Morogoro wakiongozwa na Ndugu Rashid Mtagaluka. Karibuni sana vijana wetu. *(Makofi)*

Tunao pia wageni 23 wa Mheshimiwa Keneth Nollo, ambao ni Makatibu Wenezi Kata kutoka Mkoani Dodoma, wakiongozwa na Katibu Mwenezi Wilaya ya Bahi Ndugu Nason Kachinda. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni 35 wa Mheshimiwa Mohamed Monni, ambao ni Maafisa Tarafa na Maafisa Kata wa Wilaya ya Chemba Mkoa wa Dodoma, wakiongozwa na Afisa Tarafa, Kata ya Kwamtoro, ambaye ni Ndugu Prosper Sanga. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni wawili wa Mheshimiwa Masache Kasaka ambao ni wafanyakazi kutoka Geita *Gold Mine* na hawa ni Ndugu David Kasaka na Ndugu Upendo Mwakyusa. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni wawili wa Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, ambao ni mtoto wake Ndugu Titus Mwakagenda na rafiki yake Ndugu Kelvin Mtui kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana. *(Makofi)*

Mtoto wa Mheshimiwa Mwakagenda ndio yupi? Karibu sana, nilitaka tukuone ili tujue unafuata nyayo za mama kwenye masumbwi au wewe umechukua njia nyingine? *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, hayo ndio matangazo ya wageni tuliyonayo hapa na pia mnatangaziwa Waheshimiwa Wabunge kwamba, kuna mabadiliko kidogo ya ratiba yetu ya Bunge na Mheshimiwa Spika alisoma jana mabadiliko namna yatakavyokuwa. Sasa yale marekebisho

yameshawekwa kwenye vishikwambi vyenu. Kwa hiyo, mpitie ili muweze kujiandaa vizuri kwa ajili ya michango ya bajeti zinazokuja. Kwa hiyo, mtazame vizuri ili mfahamu ni bajeti gani zimepelekwa siku zipi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo tunaendelea na ratiba iliyo mbele yetu. Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU - KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

## MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 - WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge nimwite Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi, awasilishe hoja yake. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii na namshukuru Mwenyezi Mungu kwamba ametuweka hai, ili tuweze kufanya kazi hii muhimu ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii iliyochambua Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Fungu Na. 48 na Fungu Na. 3 mnamo tarehe 29 Machi, 2021 Jijini Dodoma, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kujadili taarifa za utekelezaji wa bajeti ya Wizara Fungu 48 na Fungu Na.3 kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Aidha, naomba Bunge lako Tukufu lijadili na kupitisha makadirio ya mapato na matumizi ya Fungu 48 na Fungu Na.3.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaendelea na hotuba yangu kwa heshima kubwa naomba kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye aliapishwa tarehe 19 Machi, 2021 kuwa Rais wa Awamu ya Sita. Aidha, tunampongeza kwa hotuba yake aliyoitoa Bungeni tarehe 22 Aprili, 2022 ambayo ilitoa mwelekeo wa Serikali katika kusimamia utekelezaji wa ajenda za Kitaifa kama zilivyoainishwa katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 - 2025 yenye kurasa 308. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa miaka mitano yaani 2021/2022 - 2025/2026 na Dira ya Maendeleo 2020 - 2025. Sisi wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi tunamuahidi tutaendeleza kazi kwa kasi na uadilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango, kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambaye alithibitishwa na Bunge lako Tukufu kwa kura za kishindo na kuapishwa tarehe 31 Machi, 2021. Tunapenda kumhakikishia kwamba tutatekeleza ipasavyo maelekezo na ushauri wake katika kuboresha na kuimarisha huduma za sekta ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naungana na Watanzania wenzangu kutoa pole kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mjane mama Janeth Magufuli, familia, pamoja na wananchi wote, kutokana na msiba wa Hayati Dkt. John Pombe Magufuli, aliyekuwa Rais wa Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi katika Sekta ya Ardhi, tutaendelea kumkumbuka Hayati Dkt. John Pombe Magufuli, kutokana na kuwezesha na kusimamia baadhi ya mambo makubwa yaliyoacha alama ambayo ni pamoja na kuridhia maboresho ya sekta ya ardhi, kwa kuanzisha Ofisi za Ardhi za Mikoa na kuweka wataalam wote wa sekta ya ardhi chini ya usimamizi wa Wizara na kuwezesha utatuzi wa migogoro ya matumizi ya ardhi, hasa katika vijiji 975 kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta, ambayo ilikuwa ni kero kubwa kwa wananchi na kuimarisha usalama wa miliki za ardhi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, uongozi wake thabiti na makini katika kusimamia rasilimali za nchi, kupambana na rushwa, ubadhirifu wa mali za umma, dawa za kulevya pamoja na kurejesha nidhamu katika utumishi wa umma, umekuwa ni chachu ya maendeleo ya haraka na umeacha alama itakayodumu katika kipindi kirefu. Nasi tuliobaki tutaendelea kumkumbuka na kumuenzi kwa kutekeleza malengo na maono yake ili kuijenga Tanzania mpya iliyo imara kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa natoa pole pia kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kufuatia kifo cha Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu Hayati Benjamin William Mkapa kilichotokea tarehe 24 Julai, 2020. Pamoja na kifo cha Hayati Balozi Mhandisi John William Kijazi, aliyekuwa Katibu Mkuu Kiongozi kilichotokea tarehe 21 Februari, 2021. Hakika tutaendelea kuwaenzi kwa michango yao katika maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile natoa pole kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, pamoja na Watanzania wote kufuatia kifo cha Hayati Maalim Seif Sharif Hamad, aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kilichotokea tarehe 17 Februari, 2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, kadhalika natoa pole kwako binafsi, pamoja na Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kufuatia vifo vya Waheshimiwa, Mhandisi Atashasta Nditiye, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Muhambwe kilichotokea tarehe 12 Februari, 2021. Mheshimiwa Martha Umbulla, aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Manyara kilichotokea tarehe 20 Januari, 2021 na Mheshimiwa Khatib Said Haji, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Konde kilichotokea tarehe 20 Mei, 2021. Vile vile, natoa pole kwa wananchi wote waliopatwa na misiba na kuondokewa wapendwa wao. Tunawaombea marehemu wote Mwenyezi Mungu azilaze roho zao mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, kwa kuchaguliwa na wananchi wa Zanzibar kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika Uchaguzi Mkuu uliofanyika mwezi Oktoba, 2020. Aidha, nawapongeza Mheshimiwa Othman Masoud kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdula kuwa Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, natumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuaminiwa na kuteuliwa tena katika wadhifa huo. Napenda kumshukuru kwa ushauri na ushirikiano na maelekezo ambayo amekuwa akinipa katika utekelezaji wa majukumu yanayohusu Wizara yangu ikiwemo maelekezo yaliyotolewa kwenye hotuba yake. Daima maelekezo yake yamekuwa ni dira ya kuongoza utekelezaji wa majukumu ya Sekta ya Ardhi kwa maendeleo ya Taifa letu. Vile vile, nawapongeza Mawaziri na Naibu Mawaziri wote walioteuliwa kuongoza Wizara mbalimbali na nawashukuru kwa ushirikiano wao kwangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee nimpongeze Mheshimiwa Job Ndugai, Mbunge wa Kongwa kwa kuchaguliwa tena kushika wadhifa wa Uspika na kuendesha shughuli za Bunge kwa ufanisi mkubwa. Aidha, nikupongeze wewe kwanza kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Mbeya Mjini, lakini pia kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge letu Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Niwapongeze pia Wenyeviti wote waliochaguliwa. Nawapongeza pia Wabunge wote tuliomo humu ndani kwa kuchaguliwa au kuteuliwa katika uchaguzi huu uliopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nawapongeza Wabunge wapya walioapishwa Mheshimiwa Dkt. Florence Samizi, Mbunge wa Muhambwe na Mheshimiwa Kavejuru

Felix, Mbunge wa Buhigwe. Pia nampongeza Bi. Nenelwa Joyce Mwihambwi kwa kuteuliwa kuwa Katibu wa Bunge. Nawaombea kwa Mwenyezi Mungu aendelee kuwajaalia afya njema na hekima katika kuwatumikia wananchi kupitia Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii chini ya uongozi wa Mwenyekiti shupavu Mheshimiwa Aloyce Andrew Kwezi Mbunge wa Jimbo la Kaliua kwa ushirikiano pamoja na ushauri waliotupatia katika kuboresha utendaji kazi na kutekeleza majukumu ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, nawapongeza Wajumbe wote wa Kamati hiyo kwa uchambuzi makini sana na ushauri waliotoa wakati wa kupitia Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya mwaka 2020/2021 pamoja na makadirio ya matumizi ya Fungu 48 na Fungu Na.3. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba tutaendelea kuzingatia maoni na ushauri, maelekezo ya Kamati katika kuboresha utendaji na kuongeza tija katika huduma za Sekta ya Ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile namshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Utawala na Serikali za Mitaa kwa kufanikisha kikao cha pamoja kilichofanyika tarehe 7 na 8 mwezi huu kujadili masuala mbalimbali yanayohusu Sekta ya Ardhi. Kikao hicho kimetupa nguvu na msukumo wa pekee katika kutekeleza majukumu ya Sekta ya Ardhi kwa mujibu wa sheria na kimekuwa na mafanikio makubwa. Nawashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee napenda kutumia fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kunipa nafasi ya kuendelea kuiongoza Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Namshukuru pia kwa kuendelea kumwamini Mheshimiwa Dkt. Angelina Mabula kuendelea na

nafasi yake kama Naibu Waziri. Kadhalika, namshukuru kwa kuendelea kumuamini Bi. Maria Makondo kuendelea kuwa Katibu Mkuu wa Wizara yangu. Pia, namshukuru sana kuendelea kumuamini ndugu Nicholas Mkapa, Naibu Katibu Mkuu kuendelea na nafasi zao. Tunamwahidi kuwa tutafanya kazi kwa bidi, weledi, ubunifu, uaminifu na utiifu kwake na kwa nchi yetu katika kumsaidia kusimamia shughuli za Sekta ya Ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa wananchi wa Jimbo la Isimani kwa imani yao kubwa waliyoionesha kwangu kwa kunichagua tena kwa kishindo kuwa mwakilishi wao hapa Bungeni. Naahidi kuwapa ushirikiano katika jitihada zao za kuleta maendeleo na utatuzi wa changamoto mbalimbali zinazowakabili za kijamii na kiuchumi kadri inavyowezekana. Nafahamu ahadi iliyoko kwenye Ilani yao na ahadi yangu ni kuhakikisha kazi zilizobaki za ujenzi wa lami kwenda Ruaha *National Park* pamoja na uwekaji wa maji ya kutosheleza wananchi wa Isimani, pamoja na mfereji wa mkombozi, hizi ni ahadi kubwa za Jimbo la Isimani ambazo niko hapa kuzisimamia na kuhakikisha zinafanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kufikia malengo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano na Ilani ya Chama Cha Mapinduzi katika miaka mitano ijayo Wizara itatekeleza maeneo ya kipaumbele yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, kutambua, kupanga, kupima na kumilikisha vipande vya ardhi milioni 2.5 mijini na kutoa hatimiliki za kimila milioni 2.6 vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbili; kuandaa mipango kabambe ya matumizi ya ardhi, kuendeleza miji, maeneo tengefu, visiwa ukanda wa Pwani na kutenga ardhi ya kutosha hazina ya ardhi kwa ajili ya uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, kuimarisha uwekezaji katika ujenzi wa nyumba za gharama nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, kuboresha mfumo wa usimamizi wa taarifa za ardhi kwa kutumia TEHAMA.

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, kuwianisha mifumo ya usimamizi wa ardhi na mipango ya maendeleo ya Sekta nyingine katika matumizi ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sita, kuhamasisha matumizi ya TEHAMA katika upimaji wa ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka huu wa Fedha 2021/2022, Wizara imepanga kukusanya shilingi bilioni 200 kutokana na vyanzo mbalimbali vya mapato ya kodi, ada na tozo mbalimbali za ardhi. Hadi kufikia tarehe 15 mwezi huu, Wizara imekusanya shilingi bilioni 110 sawa na asilimia 55 ya lengo. Jedwali Na.1 linaonesha ukusanyaji ulivyo ndani ya mikoa. Wizara inaendelea kutekeleza mikakati ya ukusanyaji maduhuli ili kufikia lengo lililokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia fursa hii kuwapongeza wamiliki wote wa ardhi wakiwemo humu ndani Waheshimiwa Wabunge ambao wamelipa kodi zao za pango la ardhi kwa wakati. Aidha, Wizara itaendelea kuchukua hatua dhidi ya wadaiwa sugu wa kodi ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, Wizara yangu imepanga kukusanya shilingi bilioni 260 kutokana na kodi ya pango la ardhi, ada na tozo mbalimbali zinazohusiana na Sekta ya Ardhi. Lengo hilo linatarajiwa kufikiwa kwa kutekeleza mikakati ifuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, bajeti ya Serikali iliyotolewa itasaidia uwezeshaji katika halmashauri ambazo ndiyo mamlaka za upangaji ili ziweze kushiriki katika kupanga na kupima viwanja vipya vitakavyowezesha kulipa kodi mpya kutoka kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbili, kuimarisha miundombinu ya TEHAMA katika Ofisi za Ardhi za Mikoa na Halmashauri itakayosaidia ukusanyaji wa mapato kwa urahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, kuboresha kanzidata ya wamiliki wa ardhi kwa kutumia mfumo unganishi wa kielektroniki utakaosaidia kuhifadhi kumbukumbu za ardhi na kuwasiliana na wamiliki kwa kutumia ujumbe mfupi wa baruapepe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, kuhakiki majina ya wamiliki wa ardhi katika hati zilizosajiliwa ili kuoanisha na taarifa zilizopo katika mifumo mingine ya Serikali ili kuwabaini wamiliki hewa na ambao hawalipi kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, kufanya uhakiki wa viwanja na mashamba ili kubaini wamiliki waliobadili matumizi ili waweze kulipa kodi stahiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, kushirikiana na Serikali za Mitaa kusambaza hati za madai kufuatia malipo ya madeni na kuwafikisha Mahakamani wadaiwa sugu wa kodi ya pango ya ardhi kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, sita, kuongeza wigo wa makusanyo kwa kuhamasisha wananchi kumilikishwa viwanja vilivyopimwa ambavyo ni vingi pamoja na kutambua na kusajili wamiliki wa kila kipande cha ardhi katika maeneo ambayo hayajapangwa na kupimwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, saba, kupima na kumilikisha maeneo ya uchimbaji wa madini, na kutoza kodi stahiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, nane, kuhakiki matumizi ya ardhi iliyomilikishwa yakiwemo maeneo ya taasisi za umma na za dini ili sehemu ya ardhi katika maeneo hayo inayotumiwa kibiashara iweze kutoza kodi stahiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, tisa, kuongeza kasi ya kutambua, kupanga, kupima na kumilikisha ardhi kwa kushirikiana na mamlaka za upangaji ambazo ni Halmashauri za Wilaya na Sekta Binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumi, kuendesha elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa wamiliki ardhi kulipa kodi kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa matumizi; katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, Wizara iliidhinishiwa shilingi bilioni 129.5 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 19.4 zilikuwa kwa ajili ya mishahara. Shilingi bilioni 27.4 kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha, shilingi bilioni 82.6 zilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambapo shilingi 16.3 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 66.3 ni fedha za nje. Vile vile, katika kipindi hiki Wizara iliongezewa shilingi bilioni 13.5 kwa ajili ya kulipa mishahara, madeni ya wazabuni na watumishi. Hii ni kwa sababu, watumishi wa Halmashauri wamehamishwa rasmi kwenda Wizara ya Ardhi ndiyo maana mishahara hii imehamia huku.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia tarehe 15 Mei, Wizara imepokea na kutumia jumla ya shilingi bilioni 55.6 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo, sawa na asilimia 38.9 ya bajeti ya shilingi bilioni 143.1 baada ya uhamisho wa fedha kufanyika. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 25.2 sawa na asilimia 81.2 ni mishahara na shilingi bilioni 24.9 sawa na asilimia 89.3 ni matumizi mengineyo. Shilingi bilioni 5.4 sawa na asilimia 30.9 ni kwa ajili ya maendeleo zilizotolewa kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye mapato katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, Tume ya Taifa ya Matumizi Bora ya Ardhi ilitarajiwa kupata shilingi milioni 906. Kati ya fedha hizo shilingi milioni 900 ni kutoka kwa wadau wa kimkakati na shilingi milioni sita ni kutokana na makusanyo ya kodi ya pango la nyumba. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, Tume imepokea shilingi milioni 305.9, sawa na asilimia 33.8 ya lengo. Kati ya fedha hizo, shilingi milioni 298.6 ni fedha kutoka kwa wadau wa kimkakati na shilingi milioni 7.35 ni mapato ya kodi ya nyumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, Tume imeidhinishiwa shilingi bilioni 4.67 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 1.5 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi bilioni 1.66 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, usimamizi wa Sekta ya Ardhi; Wizara imeendelea kuboresha utoaji wa huduma ya Sekta ya Ardhi kwa wananchi kwa kuboresha Ofisi za Ardhi katika Mikoa yote 26 nchini na ndiyo maana mnaona wakubwa wa ofisi hizo 26 leo wamefika hapa ili muwatambue na ndani ya kitabu hiki mtakuta namba zao za simu ili iwe rahisi kwenu kuwatafuta na kuwajua ili waweze kushughulikia kero za wananchi huko mikoani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuanzisha ofisi hizi kumekuwepo na ongezeko katika huduma. Kwa mfano, upimaji wa viwanja umeongezeka kutoka viwanja 222,849 mwaka 2019/2020 hadi kufikia 409,150 mwezi Mei mwaka huu. Hii imesababishwa na utendaji mzuri unaofanywa na ofisi hizi kusogezwa karibu na wananchi. Hati zilizosajiliwa zimeongezeka kutoka 37,870 mwaka 2019/2020 hadi 56,390. Aidha, Wizara imeendelea kuziwezesha Ofisi ya Ardhi na Mikoa kwa kuzipatia vitendea kazi muhimu, rasilimalifedha, watumishi pamoja na kusimia mifumo unganishi ya TEHAMA ili kuongeza ufanisi katika utoaji huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2021 Wizara yangu imefanya yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, Vyeti vya Ardhi za Kijiji 195 vimeandaliwa kwa kushirikiana na mamlaka za upangaji. Hii inafanya kuwa na jumla ya vijiji 10,762 vilivyopimwa na kupewa vyeti vya ardhi na Kamishna za Vijiji kati ya vijiji 12,319 vilivyopo, kazi inaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbili, hatimiliki za kimila 34,869 zimetolewa kwa wananchi na baadhi ya hati

zimetumika kama rehani kwa kupatia mikopo kutoka taasisi mbalimbali za fedha kutumia hizi hati za kimila.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, hatimiliki 56,390 na nyaraka za kisheria 84,658 na hati za umiliki wa sehemu ya jengo *(unit title)* 632 zimesajiliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, taarifa ya uthamini 56,257 zimeidhinishwa ambapo kati ya hizo taarifa za uthamini wa kawaida ni elfu 21.5 na uthamini wa fidia elfu 32.7.

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, viwango vya bei ya soko la ardhi katika mikoa yote 26 vimehuishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sita, Wajumbe wa Kamati za Kugawa Ardhi wa Wilaya 127 wameteuliwa kati ya halmashauri 184 zilizopo nchini. Naziagiza halmashauri 54 zilizobaki kuwasilisha mapendekezo ya majina ya Wajumbe wa Kamati za Kugawa Ardhi kwa kuzingatia uwiano wa jinsia kama sheria inavyoelekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, saba, Kamati ya Taifa ya Ugawaji wa Ardhi imeidhinisha maombi ya ardhi 130 yenye ukubwa wa hekta 110,084.6 kati ya maombi 131 yaliyoidhinishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nane, alama za msingi za upimaji 36 zimesimikwa katika Mikoa ya Kigoma - nne, Dodoma - sita, Shinyanga - tatu, Morogoro - mbili, Arusha - sita, Mbeya - kumi na Mwanza - tano na kufanya jumla ya alama za upimaji nchini kuwa 881. Alama hizi zinarahisisha kazi za upimaji na kupunguza muda na gharama za upimaji ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tisa, ramani za msingi za mikoa 26 zimehuishwa. Ramani hizo zitasaidia kuongeza kasi ya upangaji na upimaji ardhi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumi, ramani za upimaji zenye jumla ya viwanja 409,150 na mashamba 442 zimeidhinishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumi na moja, migogoro 50 ya mipaka ya vijiji, hifadhi na wilaya imetatuliwa kwa kutafsiri matangazo ya Serikali *(GN)* na kurejesha alama za mipaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumi na mbili, tumetangaza maeneo yaliyoiva kimpango miji 117 tuliyoyapokea kutoka Mamlaka za Upangaji 19 na kuandaliwa rasimu za matangazo ya Serikali *GN.* Jedwali Na.8 linaonesha vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumi na tatu, Wizara imeidhinisha mipango kabambe mitano kwa ajili ya Majiji ya Mbeya, Tanga na Halmashauri za Manispaa ya Mpanda, Lindi na Morogoro. Aidha, mipango kabambe ya miji mitano ya Manispaa ya Moshi, Kahama na Halmashauri za Miji Mafinga na Makambako, Halmashauri za Wilaya ya Bagamoyo iko katika hatua mbalimbali za uandaaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumi na nne, Sheria ya Mahakama ya Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi, Sura 216 imerekebishwa kuwezesha matumizi ya lugha ya Kiswahili katika uendeshaji wa mashauri ya utoaji wa maamuzi katika Mabaraza ya Ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumi na tano, Wizara imekamilisha maboresho ya mfumo katika miamala ya msingi ambapo kwa sasa iko katika hatua za majaribio kwa kutumia Taarifa za Jiji la Dodoma kabla ya kuanza kutoa hati za kielektroniki.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha ujao moja, tunatarajia kusajili na kutoa vyeti vya ardhi kwa vijiji 100, hati za kimila 520,000, hatimiliki 500,000, miamala ya nyaraka za kisheria 100,000 na hati za umiliki wa sehemu ya jengo *(unit title)* 1,000. Napenda kutoa msisitizo kwa halmashauri zote nchini ambazo ndiyo mamlaka za upangaji

kuongeza kasi ya upangaji, upimaji na umilikishaji ardhi ili kuongeza usalama wa milki ya ardhi kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbili, kuongeza idadi ya mabaraza au kutoa ajira kwa Wenyeviti, watumishi wa kada saidizi na kuanza kutumia mfumo wa kielektroniki katika utoaji wa huduma za Mabaraza ya Ardhi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, Wizara itaendelea kuboresha huduma kwa wateja kwa kutumia teknolojia ya habari na mawasiliano. Uboreshaji utahusisha kusimika vifaa vipya vya TEHAMA katika Kituo cha Huduma kwa Wateja kilichopo Ofisi Kuu ya Dar es Salaam pamoja na kuimarisha Kituo cha Mawasiliano kwa Wateja *(call centre)* kilichopo Makao Makuu hapa Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, Wizara inaendelea kuimarisha na kusimamia Kituo cha Taifa cha Taarifa za Ardhi kilichopo Mkoa wa Dar es Salaam na kuunganisha kituo hiki na Ofisi za Ardhi zote za Mikoa. Vile vile miundombinu ya TEHAMA na miundombinu wezeshi itaendelea kujengwa na kusimikwa kwa awamu katika Ofisi za Ardhi za Mikoa yote Nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, Wizara itaanza kutoa hati za kielektroniki baada ya kukamilisha Mkoa wa Dar es Salaam sasa wataalam wa ndani wazalendo wameweza kutengeneza mfumo wa *ILMIS* kwa kutumia uwezo tulionao wa kutumia wataalam tulionao wa Kitanzania na kuanzia mwezi Julai mwaka huu Dodoma itaanza kutoa hati za elektroniki. Wizara itaendelea kushirikiana na mamlaka za upangaji katika kutambua, kupokea na kutangaza maeneo yaliyoiva kimipango miji ili kudhibiti ukuaji holela wa vijiji na miji ya kibiashara nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa rai kwa mamlaka za upangaji kuendelea kutambua na kuwasilisha mapendekezo ya vijiji na miji ya kibiashara inayokua na kukidhi vigezo vya kutangazwa kuwa maeneo ya upangaji kwa ajili ya kuyaendeleza. Kwenye jedwali mtaona

halmashauri zetu ngapi ambazo vijiji fulani fulani vinavyokua kibiashara tumevitangaza ili viweze kupangwa kimji.

Mheshimiwa Naibu Spika, utatuzi wa migogoro; katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, Wizara ilipanga kutatua migogoro 1,000 ya wamilikaji wa ardhi kiutawala. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, jumla ya migogoro 1,838 kati ya migogoro 2,378 imepokelewa, ikatatuliwa kwa njia za kiutawala katika Ofisi za Ardhi za Mikoa na halmashauri mbalimbali nchini. Aidha, jumla ya migogoro ya ardhi 3,171 ilipokelewa kwa kutumia programu ya Funguka kwa Waziri ambapo hadi kufikia tarehe 15 Mei, jumla ya migogoro 1,144 ilishughulikiwa. Kati ya hiyo, asilimia 39 inahusu masuala ya fidia. Migogoro mingi sasa inahusika zaidi na masuala ya fidia. Aidha, mashauri 23,927 yalifunguliwa katika Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya kufanya mashauri yote sasa kuwa 49,638, lakini kati ya hayo mashauri 22,711 yaliamuliwa na mashauri 26,927 yanaendelea kusikilizwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tatizo la fidia limekuwa sugu sana, kuanzia sasa hakuna halmashauri, taasisi au idara ya Serikali au yeyote anayeruhusiwa kuchukua ardhi ya wananchi bila kulipa fidia. Wizara yangu inawataka wote wanaodaiwa fidia walipe mara moja. Aidha, nimemwelekeza Mthamini Mkuu wa Serikali *(Chief Valuer)* kuanzia sasa ni marufuku kuidhinisha majedwali ya fidia ya ardhi bila wahusika kuthibitisha uwezo wa bajeti wa kulipa fidia hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Halmashauri, idara, taasisi haina fedha ya fidia isichukue ardhi ya wananchi na wale wote ambao wamechukua maeneo ya watu na hawana fedha za fidia wayarudishe bila kujali ni Taasisi ya Serikali. Nimewaagiza Makamishna wa Mikoa waandae orodha ya wadaiwa wa fidia wote ndani ya mikoa yao ili nimwombe Mheshimiwa Waziri Mkuu aingilie kati ili wananchi wapate haki yao na kazi iendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo mengine yenye manung'uniko ya wananchi ni kwenye mazoezi ya uhakiki

wa mipaka ya utawala na maeneo ya hifadhi. Natoa wito kwa Wizara na Mamlaka na Taasisi mbalimbali zinazomiliki ardhi nchi hii, zenye migogoro inayotokana na muingiliano wa mipaka ya ardhi na wanaohitaji kutafsiriwa *GN* wawasiliane na Wizara yangu, ili kuweza kutafsiri ardhini maelezo ya Matangazo ya Serikali *(GN).*

Mheshimiwa Naibu Spika, iwe ni marufuku kwa Idara au Taasisi yenye migogoro kwenda yenyewe uwandani kutafsiri *GN* zao bila uwepo wa Mkurugenzi wa Upimaji na Ramani ambaye ndiye mhusika mkuu. Aidha, Viongozi wa Mikoa na Wilaya lazima washirikishwe wakati wote mipaka ya watumiaji wa ardhi mbalimbali inapohakikiwa. Aidha, natoa rai kwa viongozi wa ngazi mbalimbali wa Serikali wajihusishe kikamilifu katika utatuzi wa migogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi za Ardhi zitoe usaidizi wa kitaalam kwa viongozi wa ngazi zote ili kuondoa migogoro ya ardhi. Nitumie fursa hii pia kuwaomba Waheshimiwa Wabunge wenye migogoro mikubwa tuendelee kama tulivyoanza, wengi wanaleta watu wao hapa, lakini kama hawawezi kuwaleta hapa tuwasiliane, ili niweze kupanga ratiba kwenda *site.* yale yaliyoshindikana huko waniambie hapa ili niende hukohuko mikoani tuweze kumaliza mambo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, Wizara itaendeleza kwa kasi sana programu hii ya Funguka kwa Waziri kwa kutembelea mikoa yote kutatua migogoro ambayo wananchi wameshaiwasilisha kwetu. Natoa wito kwa wananchi na wadau wote wenye kero waje kuwasilisha malalamiko yao kwenye Ofisi zetu za Halmashauri au Mikoani au Wizarani ili tuweze kuzitatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuboresha huduma za wateja kupunguza kero kwa wananchi, Wizara imeanza ujenzi wa Kituo cha Mawasiliano kwa Wateja *(Call Centre).*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha miaka mitano Wizara inalenga kupinga takribani asilimia 37 ya ardhi

kwa ajili ya uwekezaji, makazi, biashara na matumizi mengine ya ardhi. Lengo hilo litafikiwa kwa kutekeleza miradi mbalimbali katika mamlaka za upangaji kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa na wadau wengine chini ya uratibu wa Wizara. Natoa rai kwa halmashauri zote nchini kuhakikisha kuwa zinatenga fedha kwa ajili ya upangaji, upimaji, umilikishaji wa ardhi pamoja na ununuzi wa vifaa, usimikaji wa mifumo ya TEHAMA na uwekaji wa miundombinu, hususan barabara katika maeneo yao, kwani halmashauri ndio wenye ardhi na pia ndio mamlaka za upangaji wa ardhi zao kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuimarisha usalama wa miliki na kuiwezesha Serikali kuongeza wigo wa mapato yanayotokana na sekta ya ardhi, Wizara inaendelea kutekeleza program ya kupanga na kupima, kumilikisha kila kipande cha ardhi nchini. Program hii inatekelezwa kwa kushirikiana na mamlaka za upangaji ambazo ni Halmashauri za Wilaya. Katika mwaka wa fedha 2018/2019 Wizara iliziwezesha halmashauri 24 kiasi cha shilingi bilioni 6.2 katika kutekeleza majukumu yao na jumla ya viwanja 41,733 vilipimwa. Aidha, jumla ya shilingi bilioni 4.1 zimerejeshwa Serikalini kutokana na mauzo ya viwanja hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nazipongeza halmashauri saba zilizokamilisha marejesho ya fedha kwa asilimia 100, nazo ni Jiji la Mbeya, Manispaa ya Ilemela, Kahama, Shinyanga, Mji wa Bariadi, Misungwi na Geita. Kuna jedwali linaloonesha hivyo. Natoa rai kwa halmashauri zilizopatiwa fedha za upimaji na umilikishwaji ardhi kurejesha fedha ambazo zinatakiwa kurejeshwa bila riba yoyote ili halmashauri nyingine waweze kupata kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia tarehe 15 Mei, Wizara ilizipatia Ofisi za Ardhi za Mikoa 17 shilingi bilioni 3.5 kwa ajili ya kupanga na kupima kwa mwaka huu. Halmashauri 22 zimepokea fedha hizo na viwanja 64,227 vimepimwa na hatua za umilikishaji zinaendelea. Program hii inaonesha mafanikio kwa kuziwezesha mamlaka za

upangaji na kuongeza kasi ya kupanga, kupima na kumilikishwa kila kipande cha ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka huu wa fedha tumeongeza fedha za kukopesha halmashauri bila riba ili ziweze kupanga viwanja vingi sana na maeneo yao katika halmashauri bila riba yoyote, lakini kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI ambapo vitawekwa vigezo vya kuzingatia katika kuziongezea halmashauri uwezo wa kifedha ili kutekeleza majukumu yao. Halmashauri zimekuwa zinapata *own source* kutokana na fedha hizi ambazo tunaziwezesha, wakishapanga na kuuza viwanja vyao, lakini Kamati zetu mbili za Ardhi zimetusaidia na kutushauri tuunde timu ya pamoja ambayo itaratibu shughuli hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, Wizara itaendelea kuratibu zoezi la urasimishaji kwa njia rahisi ya kuyaondoa makampuni binafsi walio wababaishaji ambao wanaingia mikataba na Viongozi wa Mitaa kuchukua fedha za wananchi bila kukamilisha kazi. Vilevile Wizara ina dhamira ya kupunguza gharama ambazo wananchi wanatakiwa kuchangia. Hivi sasa wanachangia 150,000/=, tutazipunguza *this time* na hili tangazo litatokea mwezi Julai, lazima ipungue iwe chini ya 150,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutaweka utaratibu pia ambao utawafanya wapima binafsi wawe kama kampuni za ujenzi, waingie mikataba na wahusika na halmashauri ili wapime kwa gharama zao na wananchi walipie baada ya upimaji kukamilika. Aidha, wale wote waliochukua fedha za wananchi na hawajakamilisha kazi zao, mikoa na halmashauri zihakikishe wanakamilisha na watakaokaidi hatua za kisheria zichukuliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la rasilimali watu. Tunaendelea kuratibu utendaji bora uliotukuka wa watendaji wetu waliopo kwenye halmashauri, lakini nataka niwaahidi Waheshimiwa Wabunge, tunajua baadhi ya halmashauri zetu hazina watumishi kabisa wa fani ya ardhi ambao wanatakiwa wawe watano wa fani hizi; Mthamini, Mpima,

Afisa Mipangomiji, Afisa Ardhi na *Technician.* Kuna wengine hawana, tumepata vibali juzi na tumemwomba Waziri wa Utumishi, tunataka kuwahakikishia mwaka huu tutahakikisha kila wilaya inakuwa angalau na watendaji wa fani zote za Sekta ya Ardhi ili kazi ya kupanga na kupima iende kutekelezwa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, Shirika la Nyumba la Taifa liliahidi kuanza utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa nyumba 400 za gharama nafuu kati ya nyumba 1,000 Dodoma. Nataka kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba, nyumba 400 zinajengwa, 300 Iyumbu hapa na 100 ziko kule Chamwino. Nyumba hizi zinajengwa kwa utaratibu mpya, nawaalika Waheshimiwa Wabunge wote waende kutembelea na bila shaka hata siku ya uzinduzi tutawakaribisha, tunawaalika vilevile wakope.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara ya kwanza tutakopesha, tutawasaidia wanunuzi wa nyumba hizi waweze kukopeshwa na benki na zitalipwa gharama *single digit,* mikopo hii itakuwa ya *single digit.* Maana yake ni kwamba, itakuwa ni mikopo ya chini ya asilimia 10 kwa nyumba hizi. Kwa hiyo, nyumba hizi zinajengwa pale, hazina mgogoro, kila mtu anaweza akakopa, lakini tunaendelea na program ya ujenzi mpaka zikamilike nyumba 1,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, zoezi hili ni endelevu kwa sababu, Serikali imeshatupa hizi fedha. Tutaendelea kujenga, mtakapoona kwenye jedwali letu, tutaendelea kujenga mikoa yote yenye uhitaji wa nyumba hizi. Tumeanza na Dodoma kwa sababu ndio tumepata fedha na hii program itatuwezesha kwa mara ya kwanza mnunuzi wa nyumba hii atakapolipa siku ile tutakapomwezesha atapata funguo ya nyumba na hati ya nyumba siku moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika pia litatekeleza miradi yote ya Kawe mwaka huu na kukamilisha kwa sababu, kibali cha kukopa tutakipata, lakini pamoja na miradi mingine ambayo imeorodheshwa katika majedwali mbalimbali yaliyopo kwenye kitabu chetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo mengi na majedwali yako humo kwenye kitabu. Naomba nitoe shukrani kwa kumaliza hotuba yangu kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa maelekezo kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara yangu na Serikali kwa ujumla. Aidha, namshukuru Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango kwa maelekezo aliyotoa kuhusu namna ya kuongeza ufanisi katika usimamizi wa shughuli za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile namshukuru Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa miongozo na maelekezo yaliyowezesha kuboresha utendaji wa kazi ya Wizara yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara nyingine tena nakushukuru sana wewe Naibu Spika na Mheshimiwa Spika na Wenyeviti wote wa Bunge hili kwa kazi kubwa mliyoifanya. Pia namshukuru sana Mwenyekiti wangu wa Kamati na Kamati yangu ya Ardhi na Maliasili kwa usimamizi thabiti wa Wizara yetu na kutushauri vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nawashukuru Waheshimiwa Mawaziri, Naibu Waziri na Makatibu Wakuu kutoka katika Wizara mbalimbali zilizoshirikiana katika utekelezaji wa majukumu yetu. Napenda kuwashukuru Wenyeviti wa Kamati mbalimbali nyingine za Bunge, lakini na Wabunge wote kwa ujumla kwa ushauri wao ambao wamekuwa wanatuambia huko nje, *informaly,* kwa muda wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutambua mchango mkubwa wa viongozi wenzangu katika kutekeleza majukumu haya. Napenda kipekee nimshukuru Naibu Waziri Dkt. Angeline Mabula, Mbunge wa Jimbo la Ilemela, kwa kunisaidia katika kutekeleza majukumu ya kazi hii. Aidha, natoa shukrani kwa Katibu Mkuu Mama Makondo, Naibu Katibu Mkuu Nicholous Benjamin Mkapa, Kaimu Mkurugenzi

Mkuu wa Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Nyumba, Wakuu wa Vyuo vya Morogoro na Tabora na Wakuu wa Idara wote na wafanyakazi wote wa Wizara yangu pamoja na wale wa Halmashauri wa Sekta yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nazishukuru Halmashauri za Wilaya ambao ndio wadau wakuu na ndio wasimamizi wa ardhi katika wilaya zetu na wakuu wa vitengo wengine. Vilevile napenda kushukuru wadau wote wa sekta ya ardhi, wakijumuisha mamlaka za upangaji, sekta binafsi, mashirika ya maendeleo ya ndani na nje pamoja na michango yao katika utekelezaji wa majukumu. Tunatambua na kuthamini michango iliyotolewa na wadau hawa katika kuwezesha utekelezaji wa majukumu yetu kwa maslahi ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya kwa kuendelea kutoa ushirikiano katika kuimarisha ofisi zetu za mikoa. Aidha, natoa pongezi sana kwa Waheshimiwa Wabunge katika jitihada zao za kusikiliza na kutatua kero za wananchi katika majimbo yao. Najua kila mmoja ametenga muda wake, atake asitake atafanya kazi hiyo. Najua wengi wamejihusisha sana katika utatuzi wa migogoro, nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa pia nitoe shukrani zangu kwa familia yangu inayoongozwa na mke wangu Bi. Germina Lukuvi, yuko pale mmemuona na wototo wangu Norbert, Brown na Anne ambao bahati mbaya hawakuja kutokana na majukumu. Mnajua kukaa Dodoma muda mrefu kuna shida, lakini wale jamaa wanavumilia kule Dar-es-Salaam, Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa hayo maelezo naomba niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge, kitabu hiki kina kurasa nyingi sana, taarifa ni nyingi kwenye kitabu, majedwali ni mengi, mjue ni Bunge la kwanza na wengi ni wageni. Najua muda ni mdogo, lakini tumejitahidi

kutoa taarifa mbalimbali, lakini tuendelee kushirikiana, ili angalau kila mmoja ajue sheria zinazosimamia ardhi zinasemaje, tunaweza tukashirikiana namna gani ili kuhakikisha kwamba, wananchi wetu wanatawala ardhi yao kwa mujibu wa sheria, hawanyanyaswi na wanapata haki yao ya kisheria. Tuendelee kuwasiliana hata baada ya bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya, Wizara yangu inaomba jumla ya matumizi, jumla kuu ya fedha zinazoombwa kwa Wizara yangu, Fungu 48 na Fungu Na.3, ni Sh.101,525,586,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho natoa shukrani zangu za dhati, tena kwako binafsi. Baada ya maelezo haya naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**HOTUBA YA WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI, MHESHIMIWA WILLIAM V. LUKUVI (MB.), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/22 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**1.0 UTANGULIZI**

**1.** ***Mheshimiwa Spika*****,** kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii iliyochambua Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (Fungu **48**) na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu **3**) mnamo tarehe 29 Machi, 2021 Jijini Dodoma, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kujadili taarifa za utekelezaji wa Bajeti ya Wizara (Fungu **48**) na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu **3**) kwa mwaka wa fedha 2020/21. Aidha, naomba Bunge lako Tukufu lijadili na kupitisha makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara (Fungu **48**) na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu **3**) kwa mwaka wa fedha 2021/22.

***2.*** ***Mheshimiwa Spika*****,** mkutano huu wa Bunge la **12** la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni wa tatu (**3**) kufanyika

baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwezi Oktoba, 2020 ambapo viongozi wa kitaifa pamoja na waheshimiwa wabunge walichaguliwa na wananchi kwa wingi wa kura kwa zaidi ya asilimia **84**.

***3. Mheshimiwa Spika*****,** kabla sijaendelea na hotuba yangu kwa heshima kubwa naomba kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye aliapishwa tarehe 19 Machi, 2021 kuwa Rais wa Awamu ya Sita. Aidha, tunampongeza kwa hotuba yake aliyoitoa Bungeni tarehe 22 Aprili, 2021 ambayo imetoa mwelekeo wa Serikali katika kusimamia utekelezaji wa ajenda za kitaifa kama zilivyoainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020 – 2025 yenye kurasa 308, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26 na Dira ya Taifa ya Maendeleo (2025). Sisi Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi tunamwahidi tutaendeleza kazi kwa kasi na uadilifu.

***4. Mheshimiwa Spika*****,** napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye alithibitishwa na Bunge kwa kura za kishindo na kuapishwa tarehe 31 Machi, 2021. Tunapenda kumhakikishia kwamba tutatekeleza ipasavyo maelekezo na ushauri wake katika kuboresha na kuimarisha huduma za Sekta ya Ardhi.

***5. Mheshimiwa Spika***, naungana na watanzania wenzangu kutoa pole kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mjane Mama Janeth Magufuli, familia pamoja na wananchi wote kutokana na msiba wa Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, aliyekuwa Rais wa Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania uliotokea tarehe 17 Machi, 2021.

***6. Mheshimiwa Spika,*** sauti ya mwanamapinduzi, kiongozi jasiri, mchapakazi, mzalendo wa kweli kwa nchi yake na mtetezi wa wanyonge, Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli imetoweka ghafla. Hakika Taifa letu limeondokewa na kiongozi shupavu, mahiri na aliyependa kuona vitendo

vinafanyika kwa haraka na vyenye matokeo chanya kupitia kaulimbiu ya Hapa Kazi Tu. Alikuwa na uthubutu wa kufanya maamuzi magumu yenye maslahi kwa Watanzania.

**7.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Sekta ya Ardhi tutaendelea kumkumbuka Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kutokana na kuwezesha na kusimamia baadhi ya mambo makubwa yaliyoacha alama ambayo ni pamoja na kuridhia maboresho ya Sekta ya Ardhi kwa kuanzisha Ofisi za Ardhi za Mikoa na kuweka wataalam wote wa Sekta ya Ardhi chini ya usimamizi wa Wizara, kuwezesha utatuzi wa migogoro ya matumizi ya ardhi ya vijiji 975 kwa kushirikiana na wizara za kisekta ambayo ilikuwa ni kero kubwa kwa wananchi na kuimarisha usalama wa milki za ardhi nchini. Aidha, masuala mengine muhimu ya kitaifa aliyoyasimamia ni pamoja na kuhamisha Makao Makuu ya nchi kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma, ujenzi wa Reli ya Kisasa (Standard Gauge Railway), ujenzi wa Bwawa la Kufua Umeme la Julius Nyerere (MW 2,115), kuboresha Shirika la Ndege la Tanzania, usambazaji wa umeme vijijini, elimu bila malipo, uboreshaji wa huduma za afya na ujenzi wa miundombinu ikiwemo barabara na madaraja makubwa.

**8.** ***Mheshimiwa Spika,*** uongozi wake thabiti na makini katika kusimamia rasilimali za nchi, kupambana na rushwa, ubadhirifu wa mali za umma, dawa za kulevya pamoja na kurejesha nidhamu katika utumishi wa umma, umekuwa ni chachu ya maendeleo ya haraka na umeacha alama itakayodumu kwa kipindi kirefu. Nasi tuliobaki tutaendelea kumkumbuka na kumuenzi kwa kutekeleza malengo na maono yake ili kuijenga Tanzania mpya iliyo imara kiuchumi na kijamii.

**9.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa masikitiko makubwa natoa pole pia kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan kufuatia kifo cha Rais mstaafu wa Serikali ya Awamu ya Tatu, Hayati Benjamin William Mkapa kilichotokea tarehe 24 Julai, 2020 pamoja na kifo cha Hayati Balozi Mhandisi John William Kijazi, aliyekuwa Katibu Mkuu Kiongozi,

kilichotokea tarehe 21 Februari, 2021. Hakika tutaendelea kuwaenzi kwa michango yao katika maendeleo ya Taifa letu.

***10. Mheshimiwa Spika*,** vilevile, natoa pole kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi pamoja na watanzania wote kufuatia kifo cha Hayati Maalim Seif Sharrif Hamad, aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kilichotokea tarehe17 Februari 2021.

***11. Mheshimiwa Spika,*** kadhalika, natoa pole kwako binafsi pamoja na wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kufuatia vifo vya Waheshimiwa Mhandisi Atashasta Justus Nditiye, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Muhambwe kilichotokea tarehe 12 Februari, 2021, Martha Jachi Umbulla aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Manyara kilichotokea tarehe 20 Januari, 2021 na Khatib Said Haji aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Konde kilichotokea tarehe 20 Mei 2021. Vilevile, natoa pole kwa wananchi wote waliopatwa na misiba ya kuondokewa na wapendwa wao. Tunawaombea marehemu wote Mwenyezi Mungu azilaze roho zao mahala pema peponi, Amina.

***12. Mheshimiwa Spika***, napenda kutumia fursa hii kumpongeza Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuchaguliwa na wananchi wa Zanzibar kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika Uchaguzi Mkuu uliofanyika mwezi Oktoba, 2020. Aidha, nawapongeza Mhe. Othman Masoud kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Mhe. Hemed Suleiman Abdulla kuwa Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

***13. Mheshimiwa Spika,*** natumia fursa hii kumpongeza Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuaminiwa na kuteuliwa tena katika wadhifa huo. Napenda kumshukuru kwa ushauri, ushirikiano na maelekezo ambayo amekuwa akinipa katika utekelezaji wa majukumu yanayohusu Wizara ikiwemo

maelekezo yaliyotolewa kwenye hotuba yake. Daima maelekezo yake yamekuwa ni dira ya kuongoza utekelezaji wa majukumu ya sekta ya ardhi kwa maendeleo ya Taifa letu. Vilevile, nawapongeza mawaziri na naibu mawaziri wote walioteuliwa kuongoza wizara mbalimbali.

***14. Mheshimiwa Spika,*** kipekee nakupongeza wewe binafsi Mhe. Job Yustino Ndugai Mbunge wa Kongwa kwa kuchaguliwa tena kushika wadhifa wa uspika na kuendesha shughuli za Bunge kwa ufanisi mkubwa. Aidha, nampongeza Naibu Spika Mhe. Dkt. Tulia Ackson Mwansasu Mbunge wa Mbeya Mjini pamoja na wenyeviti wote wa Bunge lako Tukufu kwa uendeshaji mzuri wa Bunge. Vilevile, nawapongeza wabunge wapya Mhe. Dkt Florence George Samizi Mbunge wa Muhambwe na Mhe. Kavejuru Eliedory Felix Mbunge wa Buhigwe kwa kuchaguliwa kuwa Wabunge na kuapishwa tarehe 24 Mei, 2021. Pia nampongeza Bi, Nenelwa Joyce Mwihambi kwa kuteuliwa kuwa Katibu wa Bunge. Tunawaombea kwa Mwenyezi Mungu aendelee kuwajalia afya njema na hekima katika kuwatumikia wananchi kupitia Bunge hili.

***15. Mheshimiwa Spika,*** napenda pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii chini ya uongozi wa Mwenyekiti Mhe. Aloyce Andrew Kwezi Mbunge wa Jimbo la Kaliua kwa ushirikiano pamoja na ushauri wanaotupatia katika kuboresha utendaji kazi na kutekeleza majukumu ya Wizara. Aidha, nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati kwa uchambuzi makini na ushauri waliotoa wakati wa kupitia Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka wa fedha 2020/21 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara (Fungu **48)** na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu **3)** kwa mwaka wa fedha 2021/22. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba tutaendelea kuzingatia maoni, ushauri na maelekezo ya Kamati katika kuboresha utendaji na kuongeza tija katika huduma za Sekta ya Ardhi.

***16.*** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, namshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa kwa kufanikisha kikao cha pamoja kilichofanyika tarehe 7 – 8 Mei, 2021 kujadili masuala mbalimbali yanayohusu sekta ya ardhi. Kikao hicho kimetupa nguvu na msukumo wa kipekee katika kutekeleza majukumu ya sekta ya ardhi kwa mujibu wa sheria na kimekuwa na mafanikio makubwa.

***17.*** ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuniamini na kunipa fursa ya kuendelea kuiongoza Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Ninamshukuru pia kwa kuendelea kumwamini Mhe. Dkt. Angeline S. Mabula (Mb.) kuendelea na nafasi yake ya Naibu Waziri. Kadhalika ninamshukuru kwa kuendelea kumwamini Bibi Mary G. Makondo, Katibu Mkuu na Bw. Nicholas B. Mkapa, Naibu Katibu Mkuu kuendelea na nafasi zao. Tunamuahidi kuwa tutafanya kazi kwa bidii, weledi, ubunifu, uaminifu na utiifu kwake na kwa nchi yetu katika kumsaidia kusimamia shughuli za Sekta ya Ardhi.

***18.*** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa wananchi wa Jimbo la Isimani kwa imani kubwa waliyoionesha kwangu kwa kunichagua tena kwa kishindo kuwa mwakilishi wao hapa Bungeni. Naahidi kuwapa ushirikiano katika juhudi za kuleta maendeleo na utatuzi wa changamoto mbalimbali zinazowakabili kijamii na kiuchumi kadri itakavyowezekana.

***19.*** ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya maelezo hayo ya utangulizi, sasa napenda kutoa ufafanuzi kuhusu majukumu ya Wizara, hali halisi ya Sekta ya Ardhi pamoja na mwelekeo na utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2020/21 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara pamoja na taasisi zilizo chini ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2021/22.

## 2.0 MAJUKUMU YA WIZARA

***20. Mheshimiwa Spika,*** Wizara inao wajibu wa kutekeleza majukumu yafuatayo: -

i) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995;

ii) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000;

iii) Kusimamia utawala wa ardhi;

iv) Kusimamia upangaji na uendelezaji wa miji na vijiji;

v) Kusimamia na kuwezesha upimaji wa ardhi na kutayarisha ramani;

vi) Kumilikisha ardhi na kuwezesha utoaji wa hati za hakimiliki ya kimila;

vii) Kusajili hatimiliki za ardhi, miamala na nyaraka za kisheria;

viii) Kusimamia uthamini wa mali nchini;

ix) Kuhamasisha na kuwezesha ujenzi wa nyumba bora;

x) Kusimamia uendelezaji milki;

xi) Kusimamia utunzaji wa kumbukumbu za ardhi;

xii) Kusimamia ukusanyaji wa maduhuli yatokanayo na huduma za Sekta ya Ardhi;

xiii) Kuwezesha uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi na kufuatilia utekelezaji wake;

xiv) Kusimamia taasisi zilizo chini ya Wizara ambazo ni Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi; Shirika la Nyumba la Taifa na Vyuo vya Ardhi vya Tabora na Morogoro; na

xv) Kusimamia maslahi, utendaji kazi na maendeleo ya watumishi wa Wizara.

***21. Mheshimiwa Spika,*** Wizara inatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia sera na sheria zifuatazo:-

i) Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995 na Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000;

ii) Sheria ya Ardhi, Sura ya 113;

iii) Sheria ya Ardhi ya Vijiji, Sura ya114;

iv) Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini Sura ya 138;

v) Sheria ya Mahakama za Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi, Sura ya 216;

vi) Sheria ya Upimaji Ardhi, Sura ya 324;

vii) Sheria ya Usajili Wapima Ardhi, Sura ya 270;

viii) Sheria ya Utwaaji Ardhi, Sura ya 118;

ix) Sheria ya Upangaji wa Matumizi ya Ardhi, Sura ya 116;

x) Sheria ya Usajili wa Maafisa Mipangomiji, Sura ya 426;

xi) Sheria ya Mipangomiji, Sura ya 355;

xii) Sheria ya Usajili wa Ardhi, Sura ya 334;

xiii) Sheria ya Usajili wa Nyaraka, Sura ya 117;

xiv) Sheria ya Umiliki wa Sehemu ya Jengo, Sura ya 416

xv) Sheria ya Usajili wa Rehani za Mali Zinazohamishika, Sura ya 210; na

xvi) Sheria ya Shirika la Nyumba la Taifa, Sura ya 295.

## 3.0 HALI YA SEKTA YA ARDHI NCHINI

***22. Mheshimiwa Spika,*** Sekta ya Ardhi imeendelea kuimarika na kuwa mhimili na sekta wezeshi kwa uwekezaji na uzalishaji katika sekta za kilimo, viwanda, ujenzi, mifugo, uvuvi, maliasili, nishati, madini na miundombinu; hivyo, kuchangia katika kuongeza ajira kwa wananchi, pato la mwananchi mmoja mmoja, mapato ya Serikali na kukuza pato la Taifa kwa ujumla.

***23. Mheshimiwa Spika,*** katika kuendelea kuboresha huduma za sekta ya ardhi nchini, Wizara inatekeleza Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha kila kipande cha ardhi. Programu hii inatekelezwa kwa kushirikiana na mamlaka za upangaji, sekta binafsi na washirika wa maendeleo. Vilevile, Wizara imeendelea kuandaa na kusimamia utekelezaji wa miongozo ya uthamini na ulipaji fidia, upangaji, upimaji, urasimishaji, umilikishaji, usajili wa ardhi, na ujenzi wa nyumba bora za gharama nafuu.

***24. Mheshimiwa Spika,*** jukumu la kupanga miji kwa mujibu wa Sheria ya Mipangomiji Na. 8 ya mwaka 2007 ni la Halmashauri. Hivyo, Wizara yangu imeendelea kuzijengea uwezo Halmashauri kwa kuzipatia vifaa vya kisasa vya upimaji ardhi, magari, kompyuta, samani za ofisi na vitendea kazi vingine kwa ajili ya kufanya kazi za kupanga, kupima na kumilikisha ardhi, ukusanyaji wa maduhuli na utatuzi wa migogoro ya ardhi. Hatua hii inalenga kuwahakikishia wananchi usalama wa milki, kuwawezesha wananchi

kutumia ardhi yao kama mtaji, kuongeza thamani ya ardhi, kudhibiti migogoro ya matumizi ya ardhi na kuongeza wigo wa mapato ya Serikali.

***25. Mheshimiwa Spika*****,** upangaji na upimaji ardhi unapaswa kujielekeza zaidi katika kupanga miji, kudhibiti na kusimamia uendelezaji wa ardhi na miji katika maeneo ya kiutawala, utoaji wa huduma za ardhi na kuwezesha upatikanaji wa viwanja na mashamba kwa gharama nafuu. **Natoa rai kwa Halmashauri zote nchini kuhakikisha kuwa zinatenga fedha kwa ajili ya upangaji, upimaji, umilikishaji wa ardhi pamoja na ununuzi wa vifaa, usimikaji wa mifumo ya TEHAMA na uwekaji wa miundombinu hususan barabara katika maeneo yao kwani Halmashauri ndio wenye ardhi na pia ni Mamlaka za Upangaji wa ardhi zao kwa mujibu wa sheria.**

***26. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imebaini uwepo wa madalali wasio rasmi zikiwemo pia kampuni zinazofanya shughuli mbalimbali zinazohusiana na sekta ya ardhi kama vile kusimamia na kuratibu mauziano ya viwanja, mashamba na nyumba. Hali hii isiyoratibiwa imekuwa ikisababisha migogoro ya ardhi, upandishaji holela wa bei, kutolipa kodi za Serikali na kuikosesha Serikali mapato yatokanayo na miamala inayofanyika baina ya wadau. Hivyo, imefika wakati sasa wa kuwatambua madalali wanaofanya shughuli hizo ili kuwawekea utaratibu maalum/mahsusi. Wizara imeandaa rejista pamoja na vigezo vitakavyozingatiwa katika kuwatambua madalali wote wanaojihusisha na shughuli za sekta ya ardhi. Katika mwaka wa fedha 2021/22 Wizara itaandaa mwongozo/kanuni utakaoweka utaratibu wa kuratibu kazi za madalali hao ili wasiendelee kuwaumiza wananchi, kukwepa kodi na waweze kufanya kazi kwa mujibu wa sheria.

***27. Mheshimiwa Spika,*** Wizara yangu pia inashiriki katika uwezeshaji na utekelezaji wa Miradi ya Kimkakati ya Kitaifa ikiwemo Mradi wa Ujenzi wa Bwawa la Kuzalisha Umeme la Julius Nyerere, Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki

linaloanzia Hoima nchini Uganda hadi Chongoleani jijini Tanga, na ujenzi wa Reli ya Kisasa. Katika miradi hii, Wizara imeshiriki katika utwaaji ardhi, ulipaji wa fidia, upangaji, upimaji na umilikishaji ardhi. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na mamlaka za upangaji itatoa kipaumbele katika kupanga, kupima na kumilikisha ardhi kulingana na Kanda za Kiuchumi hususan maeneo yanayolima mazao ya kimkakati kama vile pamba, korosho, alizeti na mengineyo ili kuongeza tija katika uzalishaji na kukuza pato la Taifa.

## 4.0 MWELEKEO WA SEKTA YA ARDHI NCHINI

***28. Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2021/22 - 2025/26); Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020; Hotuba ya aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli wakati wa kuzindua Bunge la 12 mwezi Novemba, 2020; Hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan alipolihutubia Bunge tarehe 22 Aprili, 2021; Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030; Mpango wa Taifa wa Matumizi ya Ardhi (2013-2033); Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995; Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000; pamoja na sheria, kanuni na miongozo inayosimamia sekta ya ardhi.

***29. Mheshimiwa Spika,*** Wizara yangu itaendelea kutekeleza kwa makini masuala yaliyomo kwenye nyaraka na miongozo yanayohusu Sekta ya Ardhi mwaka hadi mwaka ili kutimiza malengo yaliyokusudiwa na Serikali. Mwelekeo wa Wizara ni kuleta mageuzi katika utoaji wa huduma karibu na maeneo ya wananchi kwa kuimarisha na kuongeza matumizi ya TEHAMA katika sekta ya ardhi, kutambua vipande vya ardhi kwa njia rahisi na shirikishi; kufanya uhakiki wa milki; kujenga mifumo na miundombinu imara ya upimaji ardhi; na kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali.

***30.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha ukusanyaji, uchakataji na utunzaji wa kumbukumbu za ardhi, Wizara itasimika kwa awamu Mfumo Unganishi wa Taarifa za Ardhi (ILMIS) katika Ofisi zote za Ardhi za Mikoa na kuendelea kuimarisha Mfumo huo katika Ofisi za Ardhi za Halmashauri. Aidha, Wizara itaongeza juhudi katika kuhuisha mifumo ya ukusanyaji maduhuli, uhakiki wa Nyaraka za Umiliki ardhi ili zilingane na taarifa za NIDA, uandaaji wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Vijiji na kuimarisha miundombinu.

***31.*** ***Mheshimiwa Spika,*** ardhi ni rasilimali kuu kwa jamii na matumizi yake ni mtambuka hivyo maendeleo katika sekta mbalimbali nchini yanategemea ardhi. Wizara itaendelea kutambua, kupanga, kupima na kumilikisha ardhi hatua ambayo ni suluhisho la kupunguza migogoro ya matumizi ya ardhi. Serikali itaendelea kutambua na kuhakiki uwekezaji katika ardhi ili kutambua mchango wake katika uchumi wa nchi. Katika muda wa kati wa miaka mitano Wizara inalenga kupima takribani asilimia **37** ya ardhi kwa ajili ya uwekezaji, makazi, biashara na matumizi mengine ya ardhi. Lengo hilo litafikiwa kwa kutekeleza miradi mbalimbali katika mamlaka za upangaji kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa na wadau wengine chini ya uratibu wa Wizara.

***32.*** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kufikia malengo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22-2025/26 na Ilani ya Chama Cha Mapinduzi 2020-25, katika miaka mitano ijayo Wizara itatekeleza maeneo ya kipaumbele yafuatayo:-

i) Kutambua, kupanga, kupima na kumilikisha vipande vya ardhi **2,500,000** mijini na kutoa hatimiliki za kimila **2,600,000** vijijini;

ii) Kuandaa mipango kabambe ya matumizi ya ardhi, kuendeleza miji, maeneo tengefu, visiwa, ukanda wa pwani na kutenga ardhi ya kutosha (hazina ya ardhi) kwa ajili ya uwekezaji;

iii) Kuimarisha uwekezaji katika ujenzi wa nyumba za gharama nafuu;

iv) Kuboresha Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa za Ardhi kwa kutumia TEHAMA;

v) Kuwianisha mifumo ya usimamizi wa ardhi na mipango ya maendeleo ya sekta zingine katika matumizi ya ardhi; na

vi) Kuhamasisha matumizi ya TEHAMA katika upimaji wa ardhi.

***33. Mheshimiwa Spika,*** baada ya maelezo hayo ya utangulizi kuhusu majukumu, hali ya Sekta ya Ardhi na mwelekeo wa Sekta ya Ardhi, naomba sasa nitoe ufafanuzi kuhusu Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (Fungu **48**), pamoja na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu **3**) kwa mwaka wa fedha 2020/21 pamoja na makadirio ya mapato na matumizi ya mafungu haya kwa mwaka wa fedha 2021/22. Takwimu zinazohusu utekelezaji wa bajeti ya Wizara yangu kwa mwaka wa fedha 2020/21 zilizopo katika hotuba hii zinaishia tarehe 15 Mei, 2021.

## 5.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2020/21 NA MALENGO YA MWAKA WA FEDHA 2021/22

### Mapato na Matumizi ya Fedha: Fungu 48 *Mapato*

***34. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2020/21, Wizara ilipanga kukusanya shilingi bilioni **200** kutokana na vyanzo vya mapato ya kodi, ada na tozo mbalimbali za ardhi. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2021, Wizara imekusanya shilingi bilioni **110** sawa na asilimia **55** ya lengo chini ya uratibu wa Ofisi za Ardhi za Mikoa kama inavyoonesha katika Jedwali **Na. 1**.

**Jedwali Na. 1 Ukusanyaji wa Maduhuli ya Serikali kimkoa hadi 15 Mei, 2021.**

| Na. | Mkoa | Lengo la Mwaka 2020/21 | Makusanyo Halisi | % |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Arusha | 8,890,910,720 | 7,234,299,031 | 81 |
| 2 | Dar Es Salaam | 62,787,363,738 | 34,231,014,459 | 55 |
| 3 | Dodoma | 10,096,544,316 | 10,394,744,608 | 103 |
| 4 | Geita | 3,508,350,614 | 1,136,948,273 | 32 |
| 5 | Iringa | 4,218,732,002 | 2,757,153,298 | 65 |
| 6 | Kagera | 3,508,350,614 | 1,613,185,222 | 46 |
| 7 | Katavi | 3,097,790,239 | 450,720,903 | 15 |
| 8 | Kigoma | 3,127,148,340 | 1,528,443,475 | 49 |
| 9 | Kilimanjaro | 3,834,544,242 | 3,848,830,060 | 100 |
| 10 | Lindi | 1,717,127,379 | 3,150,996,555 | 184 |
| 11 | Manyara | 2,988,966,345 | 1,360,986,165 | 46 |
| 12 | Mara | 3,862,953,778 | 1,654,728,771 | 43 |
| 13 | Mbeya | 11,573,519,795 | 3,608,782,865 | 31 |
| 14 | Morogoro | 11,362,162,934 | 3,988,323,897 | 35 |
| 15 | Mtwara | 2,833,673,058 | 5,281,280,592 | 186 |
| 16 | Mwanza | 15,229,503,770 | 7,326,718,534 | 48 |
| 17 | Njombe | 5,257,500,540 | 1,209,986,880 | 23 |
| 18 | Pwani | 10,779,730,377 | 6,485,559,278 | 60 |
| 19 | Rukwa | 2,209,889,940 | 625,938,219 | 28 |
| 20 | Ruvuma | 4,644,685,026 | 1,066,212,559 | 23 |
| 21 | Shinyanga | 6,316,084,637 | 2,556,634,319 | 40 |
| 22 | Simiyu | 2,022,009,127 | 809,899,913 | 40 |
| 23 | Singida | 1,959,228,308 | 1,005,527,491 | 51 |
| 24 | Songwe | 2,469,582,076 | 894,369,182 | 36 |
| 25 | Tabora | 6,010,744,021 | 1,203,432,458 | 20 |
| 26 | Tanga | 5,692,904,064 | 5,012,066,975 | 88 |
| | JUMLA | 200,000,000,000 | 110,436,783,982 | 55 |

***35. Mheshimiwa Spika,*** napenda kutumia fursa hii kuwapongeza wamiliki wa ardhi waliolipa kodi ya pango la ardhi kwa wakati. Aidha, Wizara inaendelea kutekeleza mikakati ya ukusanyaji maduhuli ili kufikia lengo lililokusudiwa ikiwemo:-

i) Kushirikiana na Serikali za Mitaa katika ngazi zote kusambaza hati za madai, kufuatilia malipo ya madeni na kuwafikisha Mahakamani wadaiwa sugu ili kulipa kodi ya pango la ardhi kwa mujibu wa sheria;

ii) Kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kulipa kodi ya pango la ardhi kwa wakati na kutuma ujumbe mfupi kupitia simu za mkononi pamoja na kutenga siku maalum ya mlipakodi;

iii) Kuhimiza wananchi waliopimiwa viwanja kulipia gharama za umilikishaji na kuandaliwa hatimiliki; na

iv) Kuendelea kuhuisha kumbukumbu za ardhi na kubainishwa viwanja na mashamba ambayo hayajamilikishwa kwa kutumia Mifumo ya TEHAMA kwa ajili ya kurahisisha ulipaji kodi.

***36. Mheshimiwa Spika,*** pamoja na juhudi hizo za ukusanyaji wa maduhuli, Wizara bado inazidai taasisi za umma malimbikizo ya kodi ya pango la ardhi yanayofikia shilingi bilioni **82**. Jitihada zinaendelea kufanyika kuhakikisha madeni hayo yanalipwa. **Natoa rai kwa wananchi ambao ardhi yao imetambuliwa, imepimwa au kumilikishwa, kulipa kodi ya pango la ardhi kwa wakati ili kuepuka tozo ya adhabu au kuchukuliwa hatua za kisheria.**

***37. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, Wizara yangu imepanga kukusanya shilingi bilioni **260** kutokana na kodi ya pango la ardhi, ada na tozo mbalimbali zinazohusiana na Sekta ya Ardhi. Lengo hilo linatarajiwa kufikiwa kwa kutekeleza mikakati ifuatayo:-

i) Kuimarisha miundombinu ya TEHAMA katika Ofisi za Ardhi za Mikoa na Halmashauri itakayosaidia ukusanyaji wa mapato kwa urahisi;

ii) Kuboresha kanzidata ya wamiliki wa ardhi kwa kutumia mfumo unganishi wa kielektroniki utakaosaidia kuhifadhi kumbukumbu za ardhi na kuwasiliana na wamiliki kwa kutuma ujumbe mfupi na barua pepe;

iii) Kuhakiki majina ya wamiliki wa ardhi katika hati zilizosajiliwa ili kuoanisha na taarifa zilizoko katika mifumo mingine ya Serikali ili kuwabaini wamiliki hewa na ambao hawalipi kodi;

iv) Kufanya uhakiki wa viwanja na mashamba ili kubaini wamiliki waliobadili matumizi ili waweze kulipa kodi stahiki;

v) Kushirikiana na Serikali za Mitaa kusambaza hati za madai, kufuatilia malipo ya madeni na kuwafikisha mahakamani wadaiwa sugu wa kodi ya pango la ardhi kwa mujibu wa sheria;

vi) Kuongeza wigo wa makusanyo kwa kuwahamasisha wananchi kumilikishwa viwanja vilivyopimwa pamoja na kutambua na kusajili wamiliki wa kila kipande cha ardhi katika maeneo ambayo hayajapangwa na kupimwa;

vii) Kupima maeneo ya uchimbaji wa madini na kutoza kodi stahiki;

viii) Kuhakiki matumizi ya ardhi iliyomilikishwa yakiwemo maeneo ya taasisi za umma na za kidini ili sehemu ya ardhi inayotumiwa kibiashara iweze kutozwa kodi stahiki;

ix) Kuongeza kasi ya kutambua, kupanga, kupima na kumilikisha ardhi kwa kushirikiana na mamlaka za upangaji; na

x) Kuongeza kasi ya utoaji elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa wamiliki wa ardhi kulipa kodi kwa wakati.

***Matumizi***

***38. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2020/21, Wizara iliidhinishiwa shilingi **129,579,479,000** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi **19,496,335,000** zilikuwa kwa ajili ya mishahara; shilingi **27,482,305,000** kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha, shilingi **82,600,839,000** zilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambapo shilingi **16,300,000,000** ni fedha za ndani na shilingi **66,300,839,000** ni fedha za nje. Vilevile, katika kipindi hiki Wizara iliongezewa shilingi **13,536,734,474.01** kwa ajili ya kulipa mishahara, madeni ya wazabuni na watumishi. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2021, Wizara imepokea na kutumia jumla ya shilingi **55,664,838,472.51 (Jedwali Na. 2)** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo, sawa na asilimia **38.9** ya bajeti ya shilingi **143,116,213,474.01** baada ya uhamisho wa fedha kufanyika. Kati ya fedha hizo, shilingi **25,232,121,713.56** (sawa na asilimia **81.2** ya bajeti ya mishahara) ni kwa ajili ya mishahara na shilingi **24,944,169,083.15** (sawa na asilimia **89.3** ya bajeti ya matumizi mengineyo) ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi **5,488,547,675.80** (sawa na asilimia **30.9** ya bajeti ya maendeleo) zilitolewa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo.

**Mapato na Matumizi ya Fedha: Fungu 3**

***Mapato***

***39. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2020/21, Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi ilitarajia kupata shilingi milioni **906**. Kati ya fedha hizo, shilingi milioni **900** ni kutoka kwa wadau wa kimkakati na shilingi milioni **6** ni kutokana na makusanyo ya kodi ya pango la nyumba. Hadi tarehe 15 Mei, 2021, Tume imepokea shilingi milioni **305.9** sawa na asilimia **33.8** ya lengo. Kati ya fedha hizo, shilingi milioni

**298.6** ni fedha kutoka kwa wadau wa kimkakati na shilingi milioni **7.35** ni mapato ya kodi ya pango la nyumba.

***Matumizi***

***40. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2020/21, Tume iliidhinishiwa shilingi bilioni **4.67** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni **1.51** ni kwa ajili ya mishahara, shilingi bilioni **1.66** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi bilioni **1.5** ni kwa ajili ya mradi wa maendeleo. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2021 Tume ilipokea kiasi cha shilingi bilioni **2.92** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo, sawa na asilimia **62.53** ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni **1.04** ni za mishahara na shilingi bilioni **1.29** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi milioni **592.1** ni kwa ajili ya maendeleo.

## 5.1 UTAWALA WA ARDHI

### Baraza la Taifa la Ushauri wa Ardhi

**41. Mheshimiwa Spika,** Baraza la Taifa la Ushauri wa Ardhi ni chombo kilichoundwa kwa mujibu wa Fungu la 17 (4) la Sheria ya Ardhi (Sura 113) na Kanuni zake za mwaka 2001. Majukumu ya Baraza ni pamoja na kufanya mapitio na kumshauri Waziri mwenye dhamana na masuala ya ardhi kuhusu masuala ya sera, sheria, kanuni pamoja na kufanya mapitio ya mfumo wa kitaasisi na kupendekeza namna bora ya kutekeleza masuala ya sekta ya ardhi. Tangu kuundwa kwa chombo hiki mwaka 2018, Wizara imeendelea kuliwezesha kutekeleza majukumu yake. Katika mwaka wa fedha 2020/21, Wizara imeliwezesha Baraza kufanya vikao na kutekeleza majukumu yake kwa kutoa ushauri na mapendekezo mbalimbali ambayo yamechangia kuleta ufanisi katika kutekeleza majukumu ya Wizara. Katika mwaka wa fedha 2021/22, Wizara itaendelea kuliwezesha Baraza kufanya vikao vya kisheria na kuchambua taarifa na mapendekezo mbalimbali yanayohusu sekta ya ardhi.

***Usimamizi wa sekta ya ardhi***

***42. Mheshimiwa Spika,*** Utawala wa Ardhi unalenga kuhakikisha ardhi yote nchini inatambuliwa, inapangwa,

inapimwa na kumilikishwa kwa lengo la kuboresha huduma za makazi, uwekezaji, milki salama, kuongeza mapato ya Serikali na hivyo kukuza pato la Taifa. Katika kufanikisha azma hiyo, Wizara imeendelea kuboresha utoaji huduma za Sekta ya Ardhi kwa wananchi kwa kuboresha Ofisi za Ardhi katika Mikoa yote **26** nchini. Ofisi za Ardhi za Mikoa zinaongozwa na Kamishna wa Ardhi Wasaidizi kama inavyooneshwa katika jedwali lifuatalo.

| NA. | JINA | MKOA | ANUANI | NA. YA SIMU |
|---|---|---|---|---|
| 1. | LEO MEINRAD KOMBA | ARUSHA | 3194, ARUSHA | 0713455388 |
| 2. | IDRISA JUMA KAYERA | DAR ES SALAAM | 9132, DAR ES SALAAM | 0754400913 |
| 3. | THADEI ALDO KABONGE | DODOMA | 1062, DODOMA | 0754422437 |
| 4. | RUGAMBWA J. BANYIKILA | GEITA | 484, GEITA | 0767086174 |
| 5. | WANCELAUS IGNACE MTUI | IRINGA | 1191 & 785, IRINGA | 0784426485 |
| 6. | ERICK PETER MAKUNDI | KAGERA | 38, BUKOBA | 0768212980 |
| 7. | GEOFREY MARTIN MGISHA | KATAVI | 488, MPANDA | 0754425786 |
| 8. | CHEDIEL ELIFADHILI MRUTU | KIGOMA | 1322, KIGOMA | 0783654683 |
| 9. | JEREMIAH NURUELI MINJA | KILIMANJARO | 1186, MOSHI | 0754594515 |
| 10. | SAID JUMA KIJIJI | LINDI | 1084,LINDI | 0789083643 |
| 11. | LEORNARD MELCHIOR MSAFIRI | MANYARA | 621, BABATI | 0755889020 |
| 12. | HAPPY MTUTWA | MARA | 63, MUSOMA | 0717001514 |
| 13. | SYABUMI MWAIPOPO | MBEYA | 485, MBEYA | 0754366665 |
| 14. | FRANK MINZIKUNTWE | MOROGORO | 587, MOROGORO | 0752565665 |
| 15. | REHEMA G. MWINUKA | MTWARA | 877, MTWARA | 0713656361 |
| 16. | ELIA KAMIHANDA | MWANZA | 668, MWANZA | 0713168705 |
| 17. | FLUGENCE KIMARIO KANUTI | NJOMBE | 776, NJOMBE | 0754522610 |
| 18. | LUCY DOMINICO KABYEMERA | PWANI | 9132, DAR ES SALAAM | 0713278040 |
| 19. | SWAGILE MSANANGA | RUKWA | 76, SUMBAWANGA | 0715731717 |
| 20. | ILDEFONCE LUNILI NDEMELA | RUVUMA | 707, SONGEA | 0784232352 |
| 21. | HEZEKIEL UFOROSIA KITILYA | SHINYANGA | 29, SHINYANGA | 0713330750 |
| 22. | ESSAU BERNARD MWAKATUMBULA | SIMIYU | 247, BARIADI | 0787075471 |
| 23. | SHAMIMU SHABANI HOZA | SINGIDA | 1511, SINGIDA | 0714444197 |
| 24. | SUMA TUMPALE MWAKASITU | SONGWE | 23, SONGWE | 0754304648 |
| 25. | JABIR M. SINGANO | TABORA | 342, TABORA | 0652507350 |
| 26. | TUMAINI RIGHTON GWAKISA | TANGA | 5058,TANGA | 0782222124 |

***43. Mheshimiwa Spika,*** uanzishwaji wa Ofisi za Ardhi za Mikoa kwa muda mfupi umewezesha kutoa huduma zote za upangaji, upimaji na ramani, umilikishaji, uthamini, usajili wa Hati na Nyaraka. Wananchi wameweza kupata hati kwa wakati, kupunguza gharama za usafiri kufuata huduma na utatuzi wa migogoro. Kwa kuanzishwa Ofisi hizi kumekuwepo na ongezeko katika huduma kwa mfano upimaji wa viwanja umeongezeka kutoka **222,849** mwaka 2019/20 hadi **409,150** Mei, 2021, hati zilizosajiliwa zimeongezeka kutoka **37,870** mwaka 2019/20 hadi **56,390** Mei, 2021. Aidha, Wizara imeendelea kuziwezesha Ofisi za Ardhi za Mikoa kwa kuzipatia vitendea kazi muhimu, rasilimali fedha, watumishi pamoja na kusimika mifumo unganishi ya TEHAMA ili kuongeza ufanisi katika utoaji huduma. Katika mwaka wa fedha 2021/22, Wizara itaendelea kuimarisha ofisi hizo ikiwemo kuwapanga wataalam wa sekta ya ardhi kwa uwiano ili kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma za ardhi kwa wananchi.

### Uandaaji na Usajili wa Hati na Nyaraka za Kisheria

**44.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza Sera na Sheria za Ardhi, Wizara inaratibu uandaaji na usajili wa Vyeti vya Ardhi ya Kijiji, Hati za Hakimiliki ya Kimila na Hatimiliki za Ardhi. Azma hii inalenga kuimarisha usalama wa milki za ardhi kwa wananchi. Katika mwaka wa fedha 2020/21, Wizara yangu kwa kushirikiana na mamlaka za upangaji iliahidi kuandaa na kusajili Vyeti vya Ardhi ya Kijiji **100.** Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2021, jumla ya Vyeti vya Ardhi ya Kijiji **195** vimeandaliwa na kusajiliwa. Hii inaifanya nchi kuwa na jumla ya vijiji **10,762** vilivyopimwa na kupewa Vyeti vya Ardhi ya Kijiji kati ya vijiji **12,319** vilivyopo.

***45. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2020/21 Wizara iliahidi kuratibu uandaaji na utoaji wa Hati za Hakimiliki za Kimila **520,000**. Hadi kufikia tarehe 15 Mei 2021, jumla ya Hati za Hakimiliki ya Kimila **34,869** zimetolewa kwa wananchi na baadhi ya hati zimetumika kama rehani za kupatiwa mikopo kutoka katika taasisi za fedha (**Jedwali Na. 3A**).

***46.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2020/21, Wizara iliahidi kusajili Hatimiliki **200,000,** Miamala na Nyaraka za Kisheria **100,000** na hati za umiliki wa sehemu ya jengo **1,000.** Hadi tarehe 15 Mei, 2021, jumla ya Hatimiliki **56,390**, Miamala na Nyaraka za Kisheria **84,651** na hati za umiliki wa Sehemu ya Jengo **632** zimetolewa (**Jedwali Na. 3B**). **Natoa rai kwa wananchi kuona umuhimu wa kumiliki ardhi kisheria na kutumia nyaraka za umiliki kama dhamana ya kupata mikopo katika taasisi za fedha.**

***47.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, Wizara inakusudia kusajili na kutoa Vyeti vya Ardhi ya Kijiji **100**, Hati za Hakimiliki ya Kimila **520,000**, Hatimiliki **500,000**, Miamala na Nyaraka za kisheria **100,000** na Hati za umiliki wa sehemu ya jengo **1,000**. **Napenda kutoa msisitizo kwa Halmashauri zote nchini ambazo ndio Mamlaka za Upangaji kuongeza kasi ya upangaji, upimaji na umilikishaji ardhi ili kuongeza usalama wa milki ya ardhi kwa wananchi.**

### *Usimamizi wa Masharti ya Umiliki*

***48.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Sheria za Ardhi zinamtaka kila mmiliki kuendeleza ardhi aliyomilikishwa. Katika mwaka wa fedha 2020/21 Wizara iliahidi kuendelea kufanya utambuzi na ukaguzi wa mashamba makubwa ili kubaini wamiliki wasiozingatia masharti ya umiliki na kuwachukulia hatua za kisheria. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2021 jumla ya mashamba **384** yalitambuliwa na kukaguliwa ambapo wamiliki **26** walibainika kukiuka masharti ya umiliki na hatua mbalimbali zinaendelea kuchukuliwa dhidi yao ikiwemo kufutiwa milki. Mashamba yaliyofutiwa milki yatapangwa na kupimwa upya kwa kushirikiana na Mamlaka za Upangaji na kuwa sehemu ya hazina ya ardhi kwa ajili ya uwekezaji, matumizi ya umma pamoja na kuwapatia wananchi wenye mahitaji. **Natoa rai kwa wamiliki wa mashamba kuyaendeleza kwa mujibu wa masharti ya umiliki ili kuepuka kuchukuliwa hatua za kisheria.**

***Uthamini wa Mali***

***49. Mheshimiwa Spika,*** uthamini wa mali zinazohamishika na zisizohamishika, na uidhinishaji wa taarifa za uthamini ni miongoni mwa majukumu yanayotekelezwa na Wizara. Uthamini hufanyika ili kuwezesha ulipaji wa fidia, utozaji wa ushuru wa Serikali unaotokana na mauzo au uhamisho wa umiliki wa mali, utozaji wa malipo ya awali (*premium*) wakati wa kutoa milki, mizania ya hesabu, kuweka mali rehani kwa ajili ya kupata mikopo, mirathi, kinga ya bima na utozaji kodi ya pango la ardhi.

***50. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2020/21 Wizara iliahidi kuratibu uandaaji na uidhinishaji wa taarifa za uthamini **29,000** ambazo kati ya hizo uthamini wa kawaida ni **10,000** na uthamini wa fidia ni **19,000**. Kadhalika, Wizara iliahidi kuendelea kushughulikia malalamiko **120** ya uthamini wa fidia, kuendelea kufanya utafiti na kuandaa viwango vya thamani ya ardhi katika mikoa yote **26**. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2021 Wizara imeidhinisha Taarifa za Uthamini **54,257** ambapo kati ya hizo taarifa za uthamini wa kawaida ni **21,541** na uthamini wa fidia **32,716.** Ongezeko la taarifa za uthamini linatokana na utekelezaji wa miradi ya kimkakati. Aidha, jumla ya malalamiko
**65** ya uthamini wa fidia yalipokelewa na kushughulikiwa. Vilevile, kazi ya kuhuisha viwango vya bei ya soko la ardhi katika Mikoa yote **26** imekamilika.

***51. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22 Wizara itaratibu uandaaji wa taarifa za uthamini **50,000.** Kati ya hizo, taarifa za uthamini wa kawaida ni **20,000** na za uthamini wa fidia ni **30,000**. Aidha, Wizara inatarajia kushughulikia malalamiko **100** yatokanayo na uthamini wa fidia na kufanya uhakiki wa uthamini wa fidia katika maeneo **20**.

***Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi nchini***

***52. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kushughulikia migogoro ya ardhi kwa kutekeleza mikakati mbalimbali kwa

kushirikiana na Wizara za Kisekta. Mikakati hiyo ni pamoja na kufanya ukaguzi wa milki, kuongeza kasi ya upangaji na umilikishaji ardhi, vikao na wadau mbalimbali kuhusu usimamizi bora wa ardhi, kudhibiti uvamizi na kuchukua hatua za kisheria dhidi ya wavamizi, kutoa elimu kwa umma kuhusu utatuzi wa migogoro kwa kushirikiana na viongozi wa Serikali za Mitaa, kuwajengea uwezo watumishi ili kuimarisha huduma zitolewazo kwa jamii, kuimarisha madawati ya malalamiko katika ofisi za ardhi za Halmashauri nchini. **Natoa wito kwa viongozi wa ngazi mbalimbali wa Serikali kujihusisha kikamilifu katika utatuzi wa migogoro ya ardhi.**

***53. Mheshimiwa Spika,*** vilevile utatuzi wa migogoro ya ardhi kiutawala unafanyika kupitia programu ya '**Funguka kwa Waziri'.** Katika mwaka wa fedha 2020/21 Wizara ilipanga kutatua migogoro **1,000** ya umilikaji ardhi kiutawala. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2021 jumla ya migogoro **1,838** kati ya migogoro **2,378** iliyopokelewa (**Jedwali Na.4**) ilitatuliwa kwa njia za kiutawala katika Ofisi za Ardhi za Mikoa na halmashauri mbalimbali nchini. Aidha, jumla ya migogoro ya ardhi **3,171** ilipokelewa kupitia programu ya Funguka kwa Waziri ambapo hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2021 jumla ya migogoro **1,144** ilishughulikiwa, kati ya hiyo **asilimia 39 inahusu masuala ya fidia**. **Natoa wito kwa wizara, taasisi na mamlaka mbalimbali kuhakikisha zinatenga bajeti kwa ajili ya kulipa fidia kabla ya kutwaa ardhi kutoka kwa wananchi.** Vilevile, milki za mashamba **11** yenye ukubwa wa hekta **24,119** zimebatilishwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa.Wizara kwa kushirikiana na Mkoa wa Morogoro inaandaa mpango wa matumizi ya ardhi hiyo ili kuwanufaisha wananchi.

***54. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22 Wizara itaendeleza programu ya "**Funguka Kwa Waziri"** Awamu ya Pili ambapo wananchi wenye kero au malalamiko watayawasilisha kwa njia ya simu/barua na utatuzi wake utafanyika kwa haraka. **Natoa wito kwa wananchi na wadau wote wenye kero za ardhi kuwasilisha malalamiko yao katika ofisi za Halmashauri na Makamishna Wasaidizi wa Ardhi wa Mikoa kwa ajili ya utatuzi.**

### *Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya*

***55. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kusimamia na kuhudumia Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya yanayofanya kazi ya kupokea, kusikiliza na kuamua mashauri yanayohusu migogoro ya ardhi. Katika mwaka wa fedha 2020/21, Wizara ilipanga kushughulikia mashauri **25,711** yaliyokuwepo na yatakayofunguliwa. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2021 mashauri mapya **23,927** yalifunguliwa na kufanya jumla ya mashauri yote kuwa **49,638**. Kati ya hayo, mashauri **22,711** yaliamuliwa na mashauri **26,927** yanaendelea kusikilizwa. Katika mwaka wa fedha 2021/22 Wizara itashughulikia mashauri **27, 801** yaliyobaki pamoja na yatakayofunguliwa.

***56. Mheshimiwa Spika,*** ili kuboresha utendaji wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya, Wizara imewasilisha mapendekezo ya marekebisho ya sheria yanayolenga kubadilisha mfumo wa ajira wa Wenyeviti wa Mabaraza kutoka mfumo wa mkataba kuwa ajira ya kudumu na kuyafanya Mabaraza ya Kata kujikita katika usuluhishi wa migogoro ya ardhi badala ya kutoa maamuzi. Aidha, kupitia Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 1 ya mwaka 2021 ambayo iliruhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili katika uendeshaji wa mashauri na utoaji wa uamuzi, Mabaraza yameanza kutumia lugha hiyo katika kuendesha mashauri na kutoa uamuzi. Pamoja na maboresho hayo, katika mwaka wa fedha 2021/22, Wizara inakusudia kuongeza idadi ya Mabaraza, ajira za Wenyeviti, watumishi wa kada saidizi na kuanza kutumia mfumo wa kieletroniki katika utoaji wa huduma za Mabaraza.

### *Usimamizi wa Visiwa Vidogo Nchini*

***57. Mheshimiwa Spika,*** Tanzania imejaliwa kuwa na rasilimali nyingi ikiwemo visiwa vikubwa na vidogo. Katika mwaka wa fedha 2020/21, Wizara kwa kushirikiana na wizara za kisekta ilifanya vikao na kupitia taarifa ya usimamizi na uendelezaji wa visiwa ambayo imebainisha uwepo wa jumla ya visiwa **289** vyenye ukubwa na matumizi tofauti na

vinasimamiwa na mamlaka mbalimbali. Tathmini inaonyesha visiwa hivyo vina changamoto mbalimbali ikiwemo uratibu hafifu, uharibifu wa mazingira, kuwa maficho ya waharifu, njia za kupitisha bidhaa za magendo na uhamiaji haramu. Mamlaka zilizobainishwa kusimamia visiwa hivyo zinajumuisha Hifadhi za Taifa (TANAPA), Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu (MPRU), Wizara ya Ulinzi, Wakala wa Misitu na Serikali za Mitaa. Vilevile, tathmini inaonesha kuwepo kwa changamoto katika mfumo wa kisheria na kitaasisi wa usimamizi na uendelezaji wa visiwa nchini. Hivyo, ili kukabiliana na changamoto hizo, katika mwaka wa fedha 2020/21 Wizara kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta imeandaa mpango mkakati wa kuimarisha mfumo wa usimamizi na uendelezaji wa visiwa ili kuwa na matumizi endelevu kwa manufaa ya sasa na vizazi vijavyo.

***Kamati ya Ugawaji wa Ardhi***

***58. Mheshimiwa Spika,*** ugawaji wa ardhi nchini hutekelezwa na kamati ambazo zimeanzishwa chini ya Sheria ya Ardhi, Sura ya 113. Sheria hii, imenipa mamlaka ya kuteua Kamati za Kugawa Ardhi za Wilaya kwa kuzingatia uwiano wa jinsia. Katika mwaka wa fedha 2020/21 Wizara yangu imeteua Kamati za Kugawa Ardhi za Wilaya **127** kati ya Halmashauri **184** zilizopo nchini. **Naziagiza Halmashauri 57 zilizobaki kuwasilisha mapendekezo ya majina ya wajumbe wa kamati, kwa kuzingatia uwiano wa jinsia kama sheria inavyoelekeza.**

***Usimamizi wa Ardhi ya Uwekezaji Nchini***

***59. Mheshimiwa Spika,*** Sheria ya Uwekezaji Na. 7 ya mwaka 1997 na Sheria ya Ardhi Na.4 ya mwaka 1999 zinatoa fursa kwa mwekezaji wa kigeni kupewa ardhi baada ya kukidhi vigezo kupitia Kituo cha Uwekezaji (TIC) au Mamlaka ya Ukanda Maalum wa Uwekezaji (EPZA). Jukumu la ugawaji ardhi kwa ajili ya uwekezaji linafanywa na Wizara kupitia Kamati ya Taifa ya Ugawaji. Katika mwaka wa fedha 2020/ 21, Wizara iliahidi kuendelea kuiwezesha Kamati ya Kitaifa ya Ugawaji Ardhi kutimiza majukumu yake. Hadi kufikia tarehe

15 Mei, 2021 kamati imeidhinisha maombi ya ardhi **130** yenye ukubwa wa hekta **110, 084.6** kati ya maombi **131** yaliyowasilishwa (**Jedwali Na. 5**).

***60. Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Wizara ina wajibu wa kuhakikisha kwamba ardhi inayogawiwa inatumika kwa kuzingatia masharti yaliyowekwa. Katika mwaka wa fedha 2020/21 Wizara kwa kushirikiana na TIC pamoja na EPZA imefanya uhakiki katika maeneo **374** kati ya maeneo **784** yaliyomilikishwa kwa wawekezaji na kubaini maeneo **112** hayajaendelezwa na baadhi hayajalipiwa kodi ya pango la ardhi. Maeneo **15** yenye ukubwa wa hekta **13,850.73** (**Jedwali Na. 6**) yaliyotolewa kwa wawekezaji, milki zake zimefutwa na ardhi hiyo kwa sasa ni sehemu ya hazina ya ardhi na inaweza kutolewa kwa wawekezaji wengine. **Natoa rai kwa wawekezaji wote waliogawiwa mashamba au viwanja kuhakikisha wanaendeleza ardhi kwa mujibu wa masharti ya uendelezaji na kulipa kodi zote stahiki kwa wakati, ili kuepuka kufutiwa milki zao.**

***Bodi za Usajili wa Wataalam wa Fani za Ardhi***

***61. Mheshimiwa Spika,*** Wizara inasimamia shughuli za bodi mbalimbali za Wataalam wa Sekta ya Ardhi. Bodi hizo ni; Bodi ya Usajili wa Wataalam wa Mipangomiji, Bodi ya Usajili wa Wathamini na Bodi ya Usajili wa Wapima Ardhi. Majukumu ya Bodi hizi ni kusajili wataalam wa sekta na kampuni za kitaalam, kusimamia weledi wa wataalam na kutoa adhabu kwa ukiukwaji wa maadili ya kitaaluma. Katika mwaka wa fedha 2020/21 Bodi ya Usajili wa Wataalam wa Mipangomiji imesajili Kampuni za Upangaji **7** na kufanya jumla ya kampuni za Upangaji na Upimaji zilizosajiliwa kuwa **159** ambapo kati ya hizo, kampuni **79** ni za upangaji na Kampuni **80** ni za upimaji. Aidha, Wataalam wa Mipangomiji **30** wamesajiliwa na kufanya jumla ya wataalam wa mipangomiji waliosajiliwa nchini kuwa **413**. Kwa sasa kuna Wapima Ardhi **311** na Wathamini **862** waliosajiliwa na bodi za taaluma zao**.** Uwepo wa wataalam na kampuni binafsi

za upangaji na upimaji zilizosajiliwa na bodi umechangia kuongeza kasi ya upangaji, upimaji ardhi na urasimishaji makazi.

***62. Mheshimiwa Spika,*** katika kulinda maadili ya kitaaluma na kuwezesha kutoa huduma stahiki za ardhi kwa wananchi bodi zimechukua hatua mbalimbali za kinidhamu dhidi ya baadhi ya kampuni za upangaji na upimaji zilizokiuka maadili na masharti ya kitaaluma. Hatua hizo zinajumuisha kutoa onyo kwa kampuni **35**, kufutiwa leseni kampuni mbili (**2**) na kampuni saba (**7**) zimesimamishwa kufanya shughuli zake kwa muda. Vilevile Wizara inafanya mapitio ya sheria ili kuondoa mgongano wa maslahi kwa watumishi wa sekta ya ardhi.

## 5.2 HUDUMA ZA TEHAMA

### *Mifumo ya Utoaji Huduma na Utunzaji wa Taarifa za Ardhi*

***63. Mheshimiwa Spika,*** katika kuboresha utoaji wa huduma na utunzaji wa taarifa za ardhi, Wizara kwa nyakati tofauti imeunda mifumo mbalimbali ya TEHAMA kwa ajili ya kurahisisha utendaji kazi katika Sekta ya Ardhi. Mifumo hiyo ni pamoja na Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa za Ardhi pamoja na Usajili wa hati (MOLIS), Mfumo wa Usimamizi wa Kodi ya Pango la Ardhi (LRMS), Mfumo wa Uidhinishaji wa kazi za Upimaji na Ramani (SRS), Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Majalada (FMS) na Mfumo wa Taarifa za mashamba (LIMS). Pamoja na kurahisisha utoaji wa huduma za ardhi, mifumo hii haisomani mfano, taarifa zake haziingiliani na hivyo kusababisha ugumu wa kupata taarifa sahihi na kwa wakati.

***64. Mheshimiwa Spika,*** katika kukabiliana na changamoto za kimfumo, Wizara ilisanifu na kujenga Mfumo Unganishi wa Taarifa za Ardhi (ILMIS). Mfumo huu unaunganisha taarifa za umiliki pamoja na taarifa za kijiografia ambazo zinahusisha ramani za msingi, michoro ya mipangomiji na ramani za upimaji. Mfumo huu unasaidia kutoa huduma kwa uwazi, kuondoa umilikishaji wa kiwanja kimoja kwa zaidi ya mtu mmoja na kutoa huduma kwa haraka na kwa usahihi.

***65. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2020/21 Wizara iliahidi kuendelea kuboresha mfumo kwa kujenga miundombinu, kuchambua, kupiga picha (scanning) na kuhifadhi michoro, ramani na hati katika ofisi za ardhi za mikoa na halmashauri mbalimbali nchini. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa usimikaji wa Mfumo Unganishi wa Taarifa za Ardhi (ILMIS) pamoja na miundombinu wezeshi ya TEHAMA umekamilika katika Halmashauri zote za Mkoa wa Dar es Salaam. Wizara imekamilisha maboresho ya mfumo katika miamala msingi ambapo kwa sasa ipo katika hatua za majaribio kwa kutumia taarifa za Jiji la Dodoma kabla ya kuanza kutoa hati ya kielektroniki. Aidha, zoezi la kuchambua, kupiga picha (scanning) na kuhifadhi michoro na ramani za Ardhi za Mipangomiji na Ramani za Upimaji limetekelezwa katika Jiji la Dodoma. Jumla ya michoro **900** ya mipangomiji na michoro **4,700** ya upimaji na ramani yenye jumla ya viwanja **250,000** imebadilishwa kutoka mfumo wa analogia kwenda mfumo wa digitali ili itumike katika mfumo unganishi wa Taarifa za Ardhi ulioboreshwa. Wizara itaendelea na uboreshaji na usambazaji wa mfumo huo katika mikoa mingine kwa kutumia wataalam wa ndani.

***66. Mheshimiwa Spika,*** vilevile, kituo cha Taifa cha Taarifa za Ardhi kimeimarishwa kwa kuongezewa uwezo wa kutunza taarifa ikiwa ni matayarisho ya kupokea, kuchakata na kutunza taarifa za kidigitali kutoka mikoa mbali mbali. Katika kuimarisha miundombinu ya TEHAMA katika Ofisi za Ardhi za mikoa, Wizara imejenga na kukarabati mtandao kiambo (*Local Area Network*) katika 0fisi za Ardhi za mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Dodoma; na kuunganisha ofisi hizi na kituo cha Taifa cha Taarifa za Ardhi – NLIC. Vilevile, mikoa iliyobaki imeunganishwa katika kituo cha NLIC kwa kujengewa mtandao wa muda kwa kutumia vifaa wezeshi vya mitandao (Wireless Routers and Modems).

***67. Mheshimiwa Spika,*** katika kuboresha huduma kwa wateja, Wizara imeanza ujenzi wa kituo cha mawasiliano kwa wateja (*Call Centre*) katika Ofisi ya Makao Makuu ya Wizara Jijini Dodoma. Lengo ni kuwezesha mawasiliano ya moja kwa moja na wateja popote walipo kwa simu na kutatua

changamoto zinazowakabili bila kulazimika kufika katika ofisi za ardhi. Utaratibu huo unatarajiwa kuwapunguzia wananchi kero, gharama za usafiri na muda wa kupata huduma. Wizara pia imeboresha ukadiriaji wa kodi ya pango la ardhi mtandaoni ambapo mwananchi anaweza kulipa kodi ya pango la ardhi anayodaiwa kupitia simu za mkononi.

*Namna ya kukadiria na kulipa kodi ya pango la ardhi kwa kutumia simu ya mkononi.*

***68. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, Wizara itaendelea kuimarisha na kusimamia Kituo cha Taifa cha Taarifa za Ardhi– NLIC kilichopo Mkoani Dar es Salaam na kuunganisha kituo hiki na Ofisi za Ardhi za Mikoa. Vilevile, miundombinu ya TEHAMA na miundombinu wezeshi itaendelea kujengwa na kusimikwa kwa awamu katika ofisi za Ardhi za Mikoa yote nchini. Pia, Wizara itaendelea kuchambua, kufanya nakishi ya michoro (*scanning*) na kuihifadhi, ramani na kumbukumbu za ardhi katika Ofisi za ardhi za mikoa na Halmashauri mbalimbali nchini kwa awamu.

***69. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha wa 2021/22 Wizara itaendelea kuboresha huduma kwa wateja kwa kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano. Uboreshaji utahusisha kusimika vifaa vipya vya TEHAMA katika kituo cha huduma kwa wateja kilichopo katika Ofisi ya Ardhi ya Mkoa wa Dar es Salaam pamoja na kuimarisha kituo cha mawasiliano kwa wateja (*Call Centre*) kilichopo Makao Makuu ya Wizara Dodoma.

## 5.3 UPIMAJI ARDHI NA UTAYARISHAJI WA RAMANI

***70. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kusimamia na kuratibu shughuli za upimaji ardhi na utayarishaji wa ramani za msingi na za kiutawala kwa ajili ya kutekeleza mipango mbalimbali ya Serikali. Vilevile, Wizara imeendelea kutoa miongozo ya upimaji ardhi ili kuendana na mabadiliko ya teknolojia.

***Utayarishaji wa Ramani za Msingi***

***71. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2020/21, Wizara iliahidi kuendelea kuhuisha ramani za msingi **66** za uwiano mdogo wa **1:50,000** pamoja na ramani nyingine za kiutawala katika wilaya mbalimbali nchini. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2021 ramani za msingi za mikoa **26** zimehuishwa. Ramani hizo zitasaidia kuongeza kasi ya upangaji na upimaji ardhi nchini. Aidha, ramani ya Tanzania imehuishwa na kuonesha Mikoa na Wilaya mpya pamoja na Jiji la Dodoma ambalo ndio Makao Makuu ya nchi.

***72. Mheshimiwa Spika,*** katika kuongeza kasi na kurahisisha kazi ya upimaji ardhi nchini, Wizara inatarajia kununua ndege ndogo isiyo na rubani (drone) kwa ajili ya kupiga picha za anga zitakazowezesha uandaaji wa ramani za msingi. Picha zitakazozalishwa zitatumiwa pia katika mfumo unganishi wa kumbukumbu za ardhi. Lengo la Wizara ni kuwa na ndege kubwa ya kuwezesha upigaji wa picha za anga kwa nchi nzima.

***73. Mheshimiwa Spika,*** Wizara pia ina jukumu la kutafsiri ardhini maelezo ya Matangazo ya Serikali (GN) yanayohusu maeneo ya utawala, Hifadhi za Misitu na Wanyamapori. Jukumu hili linatekelezwa kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta, Ofisi ya Rais – TAMISEMI na Mamlaka mbalimbali baada ya kujitokeza migogoro ya ardhi. Tafsiri zinazofanyika zimewezesha kutatua migogoro ya mipaka baina ya vijiji, wilaya na mikoa na kati ya vijiji na hifadhi. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2021 jumla ya Matangazo ya Serikali Ishirini (**20**) ya maeneo ya utawala na Hifadhi ya Saadani, Msitu wa Kuni Korogwe, Hifadhi ya Taifa ya Mikumi, Msitu wa Hifadhi Chang'andu na Hifadhi ya Mwalimu Nyerere, Hifadhi ya Taifa ya Tarangire na Mapori Tengefu ya Ziwa Natron, Longido, Bulunge, Mto wa Mbu, Lol Kisare, Simanjiro, Kitwai, Handeni, Ruvu Masai, Same, Mto Umba, Loliondo na Kalimawe yamebainishwa mipaka. **Natoa rai kwa Wizara na Mamlaka mbalimbali nchini zenye migogoro inayotokana na mwingiliano wa mipaka ya ardhi na wanaohitaji kutafsiriwa GN wawasiliane na Wizara yangu ili kuweza kutafsiri ardhini maelezo ya Matangazo ya Serikali (GN). Ni marufuku kwa**

**idara au taasisi yenye migogoro kwenda yenyewe uwandani kutafsiri GN zao bila uwepo wa Mkurugenzi wa Upimaji na Ramani ambaye ndiye mhusika mkuu. Aidha, viongozi wa mikoa/wilaya lazima washirikishwe wakati wote mipaka inapohakikiwa.**

**Upimaji wa ardhi nchi kavu**

***74. Mheshimiwa Spika*,** Wizara ina jukumu la kuandaa na kuweka miundombinu ya upimaji wa ardhi ikiwemo alama za msingi za upimaji. Upimaji nchi kavu unajumuisha upimaji wa viwanja, mashamba, mipaka ya ndani ya nchi na mipaka ya kimataifa. Katika kuwezesha na kurahisisha upimaji kufanyika kwa ufanisi alama za msingi husimikwa ardhini. Katika mwaka wa fedha 2020/21 Wizara iliahidi kusimika alama za msingi mpya **150** nchini. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2021 alama za msingi za upimaji **36** katika mikoa ya Kigoma (4), Dodoma (6), Shinyanga (3) Morogoro (2), Arusha (6), Mbeya (10) na Mwanza (5) na kufanya jumla ya alama za upimaji nchini kuwa **867**. Alama hizi zinarahisisha kazi za upimaji na kupunguza muda na gharama za upimaji ardhi. Wizara itaendelea kusimika alama za msingi mpya **80** katika mwaka wa fedha 2021/22 ili kuwezesha upimaji ardhi kufanyika kwa ufanisi zaidi.

***75. Mheshimiwa Spika*,** maendeleo ya mifumo ya upimaji nchini imepitia hatua mbalimbali. Awali alama za upimaji zilisimikwa kwa kutumia mfumo wa *Arc* 1960 ambapo alama za mwanzo zilisimikwa mwaka 1830. Baada ya uhuru alama hizo ziliendelea kuwekwa na hadi kufikia mwaka 2008 kulikuwa na alama **540** nchini. Alama hizi zilijengwa juu ya milima mirefu kuwezesha kuona umbali mrefu kutoka mlima mmoja hadi mwingine. Mtandao wa alama hizo umeanzia nchini Afrika Kusini na kusambazwa kupitia Zimbabwe hadi Tanzania katika milima ya Usambara hadi nchini Misri.

***76. Mheshimiwa Spika*,** kutokana na mabadiliko makubwa ya teknolojia katika nyanja za vifaa vya upimaji kuanzia mwaka 2000, mfumo wa zamani wa upimaji umebadilishwa kwa kujenga mtandao mpya wa upimaji ardhi kwa kufuata uwiano wa mfumo wa kimataifa (International Terrestrial

Reference frame- ITRF) na kujenga mfumo wa upimaji unaoitwa Tanzania Reference Frame- TAREF 11. Aidha, kwa upande wa Tanzania usimikaji wa mfumo huo ulikamilika mwaka 2010 na kutambuliwa kisheria mwaka 2019 baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali Namba 201 la tarehe 13 Machi, 2019.

***77. Mheshimiwa Spika*****,** mtandao wa *TAREF 11* una jumla ya alama **831** ambazo zimewekwa katika mikoa yote nchini kwa umbali wa kilometa arobaini kutoka alama moja hadi nyingine. Idadi ya alama za msingi za upimaji kimkoa ni kama ifuatavyo:-

**Jedwali la Idadi ya Alama za Msingi Kimkoa**

### *Upimaji wa Viwanja na Mashamba*

***78.*** ***Mheshimiwa Spika***, kama nilivyokwishaeleza kwamba jukumu la msingi la upangaji na upimaji ardhi ni la Mamlaka za Upangaji ambazo ni halmashauri zote nchini. Wizara ina jukumu la kuratibu na kusimamia upimaji wa viwanja na mashamba unaofanywa na Mamlaka za Upangaji pamoja na sekta binafsi. Katika mwaka wa fedha 2020/21 Wizara ilipanga kuidhinisha ramani za upimaji wa viwanja na mashamba **200,000** pamoja na kutatua migogoro **25** ya mipaka ya vijiji, hifadhi na Wilaya. Hadi tarehe 15 Mei, 2021, ramani za upimaji zenye jumla ya viwanja **409,150** na mashamba **442** ziliidhinishwa (**Jedwali Na. 7**). Aidha, migogoro **50** ya mipaka ya vijiji, hifadhi na Wilaya ilitatuliwa kwa kutafsiri matangazo ya Serikali na kurejesha alama za mipaka. Katika mwaka wa fedha 2021/22 Wizara inatarajia kuidhinisha ramani za upimaji zenye jumla ya viwanja na mashamba **500,000** kutoka Mamlaka za Upangaji.

### *Upimaji wa Mipaka ya Maeneo ya Hifadhi*

***79.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta imeendelea kuhakiki na kupima mipaka ya maeneo ya hifadhi. Katika mwaka wa fedha 2020/21, Wizara iliahidi kuendelea kuhakiki na kupima mipaka ya maeneo ya Hifadhi za Taifa, Mapori Tengefu, Mapori ya Akiba na Misitu ya Hifadhi. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2021 mipaka ya maeneo yafuatayo ilihakikiwa na migogoro kutatuliwa: Ranchi ya Taifa ya Mzeri na Msitu wa Hifadhi Chang'andu katika Wilaya ya Handeni; Shamba la miti la Korogwe na Ranchi ya Taifa ya Mzeri; Hifadhi ya Taifa ya Mikumi na Mji mdogo wa Mikumi katika eneo la Kikwaraza Mkoani Morogoro; Hifadhi ya Taifa ya Saadani; shamba la miwa Bagamoyo; eneo la chumvi na vijiji vinavyozunguka Hifadhi hiyo pamoja na Bandari ya Tanga eneo la Chongoleani.

### *Uimarishaji wa Mipaka ya Kimataifa*

***80.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Tanzania inapakana na nchi **10** kwa mpaka wenye urefu wa kilomita **1,841** nchi kavu na

kilometa **2,086** ndani ya maji. Jukumu la Wizara ni kuimarisha alama za mipaka hiyo kwa kushirikiana na mamlaka mbalimbali na nchi jirani. Katika mwaka wa fedha 2020/21 Wizara iliahidi kuhakiki na kuimarisha mipaka ya nchi kati ya Tanzania na Kenya pamoja na Tanzania na Burundi. Makubaliano ya kuimarisha kilomita **100** za mpaka wa Tanzania na Burundi yamefikiwa kupitia kikao cha Kamati ya Pamoja ya Tanzania na Burundi ambapo kazi hiyo inatarajiwa kuanza kabla ya kuisha kwa mwaka wa fedha 2020/21. Aidha, kwa upande wa mpaka wa Tanzania na Kenya, kazi iliyopangwa haikufanyika kutokana na kukosekana kwa utayari wa serikali ya nchi hiyo na mlipuko wa ugonjwa wa Corona. Katika mwaka wa fedha 2021/22 Wizara itaendelea kuimarisha mpaka kati ya Tanzania na Burundi kwa urefu wa kilomita **100** na mpaka kati ya Tanzania na Kenya kwa urefu wa kilomita **128** kwa kuzingatia makubaliano yaliyofikiwa kupitia Kamati za Pamoja kwa niaba ya Serikali za Nchi zetu.

## 5.4 UPANGAJI MIJI NA MAENDELEO YA MAKAZI

***81. Mheshimiwa Spika,*** mojawapo ya majukumu ya Wizara ni kusimamia upangaji miji na uendelezaji wa makazi ikiwemo uandaaji wa mipango ya jumla (Mipango Kabambe), mipangokina, utangazaji wa maeneo yaliyoiva kwa upangaji, udhibiti wa uendelezaji miji na vijiji na urasimishaji makazi. Aidha, jukumu lingine ni usimamizi na uratibu wa uendelezaji nyumba.

### Upangaji na Usanifu wa Miji

#### *Utangazaji wa maeneo ya upangaji miji*

***82. Mheshimiwa Spika,*** kwa mujibu wa Sheria ya Mipango Miji Na. 8 ya mwaka 2007, Wizara ina jukumu la kutangaza maeneo ya vijiji yanayokua na kufikia sifa ya kupangwa na kuendelezwa kimji. Eneo lolote la kijiji ili liweze kuendelezwa kimji, ni sharti litangazwe kama eneo la upangaji. Baadhi ya vigezo muhimu vya kutangaza maeneo hayo ni idadi ya watu wasiopungua **10,000**, uwepo wa huduma za msingi za kijamii kama vile zahanati au kituo cha afya, shule ya msingi,

soko na maduka yasiyopungua matano **(5)**. Wizara hutangaza maeneo yenye sifa hizi baada ya kupokea mapendekezo kutoka kwenye mamlaka za upangaji. **Mamlaka za upangaji zina wajibu wa kuandaa mipango ya jumla na mipangokina kwa kushirikiana na wadau mbalimbali.**

***83. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2020/21, Wizara iliahidi kuendelea kushirikiana na mamlaka za upangaji kutambua, kupokea mapendekezo na kutangaza maeneo yaliyoiva kimipango miji. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2021 jumla ya maeneo **117** ya upangaji yaliyoiva kimipangomiji yamepokelewa kutoka mamlaka za upangaji **19** na kuandaliwa Rasimu za Matangazo ya Serikali (GN) **(Jedwali Na. 8 linaonesha maeneo yaliyoiva kimipangomiji)**. Katika mwaka wa fedha 2021/22 Wizara itaendelea kushirikiana na mamlaka za upangaji katika kutambua, kupokea na kutangaza maeneo yaliyoiva kimipango miji ili kudhibiti ukuaji holela wa vijiji na miji ya kibiashara nchini. **Natoa rai kwa mamlaka za upangaji kuendelea kutambua na kuwasilisha mapendekezo ya vijiji na miji ya kibiashara inayokua na kukidhi vigezo vya kutangazwa kuwa maeneo ya upangaji kwa ajili ya kuyaendeleza kimji.**

***Uandaaji wa Mipango Kabambe***

***84. Mheshimiwa Spika,*** maendeleo endelevu ya miji huwezeshwa kwa kuandaliwa mipango ya jumla inayotoa dira ya ukuaji wa miji, utoaji wa huduma mbalimbali za kiuchumi na kijamii na usalama wa miji na watu wake. Katika mwaka wa fedha 2020/21, Wizara iliahidi kuidhinisha na kutangaza Mipango Kabambe **12.** Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2021 Mipango Kabambe mitano (**5**) ya Majiji ya Mbeya na Tanga na Halmashauri za Manispaa za Mpanda, Lindi na Morogoro iliandaliwa na kuidhinishwa. Aidha, Mipango Kabambe ya miji mitano (5) ya Manispaa za Moshi na Kahama, Halmashauri za miji ya Mafinga na Makambako na Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo iko katika hatua mbalimbali za uandaaji. Katika mwaka wa fedha 2021/22, Wizara itaendelea kushirikiana na mamlaka za upangaji

kufuatilia utekelezaji wa Mipango Kabambe kwa mujibu wa sera, sheria, kanuni na miongozo iliyopo. **Natoa rai kwa mamlaka za upangaji nchini kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya uandaaji, utekelezaji na udhibiti uendelezaji miji ili kuwezesha miji yetu kusanifiwa na kuendelezwa kwa kuzingatia Mipango Kabambe.**

***Ardhi ya Uwekezaji***

***85. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuwezesha upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya uwekezaji katika maeneo mbalimbali nchini ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa azma ya Serikali ya kujenga uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu. Katika kutekeleza jukumu hili Wizara inaendelea kuzisimamia mamlaka za upangaji kutenga maeneo na fedha kwa ajili ya kulipa fidia kwa ajili ya uwekezaji wakati wa kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi mijini na vijijini.

***86. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kufanya ukaguzi na uhakiki wa mashamba makubwa ili kubaini utekelezaji wa masharti yaliyomo kwenye mikataba ya umilikishwaji ardhi ya uwekezaji. Milki za mashamba ambayo wamiliki wamekiuka masharti ya umiliki hubatilishwa na ardhi ya mashamba husika kupangwa na kupimwa upya ili kupata ardhi kwa ajili ya matumizi mbalimbali. Hadi tarehe 15 Mei, 2021 jumla ya hekta **147,967.1** zimetengwa kwa ajili ya uwekezaji katika maeneo mbalimbali nchini **(Jedwali Na. 9- ardhi iliyotengwa kwa ajili ya uwekezaji wilaya kwa wilaya).**

***87. Mheshimiwa Spika,*** kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi Sura ya 113, ardhi ya uwekezaji kutoka ardhi ya kijiji au hifadhi huhitaji kuhaulishwa kuwa ardhi ya kawaida kwa manufaa ya umma. Hatua za uhaulishaji huanzia katika ngazi ya kijiji, wilaya, Wizara na hatimaye kuwasilisha mapendekezo kwa Mheshimiwa Rais kwa ajili ya idhini. Katika mwaka wa fedha 2020/21 ardhi yenye ukubwa wa hekta **36,011.3** imehaulishwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa (Hekta **31,605.3**) na Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro (Hekta **4,406**). Ardhi hii iliyohaulishwa itamilikishwa kwa wawekezaji kupitia Kituo cha

Uwekezaji Tanzania (TIC) na Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Uwekezaji (EPZA).

***88. Mheshimiwa Spika,*** katika kushughulikia masuala yanayohusu uhaulishaji, kumekuwa na changamoto ya usahihi wa baadhi ya taarifa zinazowasilishwa kutoka katika ngazi za chini na hivyo kusababisha malalamiko ya wananchi kutohusishwa katika vikao vya maamuzi ya kutwaa ardhi husika kutoka kwa wamiliki wa asili. Wizara imechukua hatua katika kuhakikisha kwamba inahakiki kwa makini taarifa zote zinazohusu ardhi inayopendekezwa kuhaulishwa kutoka mamlaka za Serikali za Mitaa kabla ya kuwasilisha mapendekezo kwa Mheshimiwa Rais.

***Uandaaji wa Michoro ya Mipangomiji***

***89. Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa Mipango Kabambe hufanyika kwa kuandaliwa michoro ya mipangomiji katika Mamlaka za Upangaji kwa lengo la kuelekeza ukuaji na uboreshaji wa makazi, kuhifadhi mazingira, kuondoa ukinzani wa matumizi ya ardhi na kutoa uhakika wa upatikanaji wa maeneo yenye matumizi mbalimbali ikiwemo ya uwekezaji. Katika mwaka wa fedha 2020/21, Wizara ilipanga kukagua na kuidhinisha michoro ya mipangomiji **2,000** kutoka katika Mamlaka za Upangaji nchini. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2021, michoro ya mipangomiji **1,588** yenye jumla ya viwanja **408,918** kwa maeneo mapya **(Jedwali Na.10)** ilipokelewa na kuidhinishwa. Katika mwaka wa fedha 2021/22, Wizara inatarajia kukagua na kuidhinisha michoro ya mipangomiji **2,000** kutoka katika Mamlaka za Upangaji.

***Urasimishaji Makazi***

***90. Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea kutekeleza Programu ya Kurasimisha Makazi na Kuzuia Makazi Yasiyopangwa Mijini (2013 -2023). Lengo la Programu ni kuhakikisha usalama wa milki na kuwezesha upatikanaji wa maeneo kwa ajili ya huduma za kijamii na miundombinu muhimu kwa njia shirikishi kwa kuzingatia sera, sheria, kanuni na miongozo ya Sekta ya Ardhi.

***91. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2020/21, Wizara iliahidi kuendelea kuratibu shughuli za urasimishaji makazi zitakazotekelezwa na mamlaka za upangaji nchini. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2021, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka za Upangaji iliandaa michoro ya urasimishaji **2,279** yenye jumla ya viwanja **760,092** katika halmashauri mbalimbali nchini **(Jedwali Na. 11)** na taratibu za kuwapatia wananchi hati miliki zipo katika hatua mbalimbali.

***Ushiriki wa Sekta Binafsi katika Urasimishaji***

***92. Mheshimiwa Spika,*** ili kukabiliana na changamoto ya ongezeko kubwa la makazi yasiyopangwa mijini, mwaka 2015 Serikali ilipanua wigo wa ushiriki wa sekta binafsi katika kufanya kazi za urasimishaji. Pamoja na sekta binafsi kuharakisha kazi za urasimishaji, tathmini iliyofanywa na Wizara mwezi Agosti, 2020 ilibaini kuwepo kwa changamoto mbalimbali ambazo zimekuwa ni kikwazo katika ufanisi wa kazi za urasimishaji. Changamoto hizo ni pamoja na baadhi ya kampuni za upangaji na upimaji kushindwa kukamilisha kazi kwa muda uliokubalika; baadhi ya kampuni kupokea fedha bila kufanya kazi; ukiukwaji wa taratibu na maadili ya kitaaluma; na baadhi ya kampuni kutokuwa na usajili katika bodi za udhibiti.

***93. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuchukua hatua katika kutatua changamoto zinazotokana na ushiriki wa sekta binafsi na kuweka mfumo thabiti wa kuratibu ushiriki wake katika utekelezaji wa miradi ya urasimishaji makazi nchini. Hatua zilizochukuliwa na Wizara ni pamoja na kufanya maboresho ya Mwongozo wa Urasimishaji kwa lengo la kuimarisha mfumo wa usimamizi wa urasimishaji nchini; na kuchukua hatua za kinidhamu kupitia Wizara na Bodi za wataalam wa mipangomiji na upimaji ardhi. Hatua zilizochukuliwa ni kuzifutia leseni kampuni tatu (**3**); kuzisimamisha kwa muda kampuni tisa (**9**); kuzipa onyo kampuni **41**; na kampuni **15** zimesimamishwa kufanya kazi za urasimishaji ikiwa ni pamoja na kufikishwa kwenye vyombo vya uchunguzi kwa hatua stahiki.

***94. Mheshimiwa Spika,*** pamoja na hatua zilizochukuliwa na Wizara dhidi ya kampuni za upangaji na upimaji, nazipongeza kampuni zilizofuata misingi ya taaluma, weledi na uadilifu katika kutekeleza kazi za urasimishaji. Katika mwaka wa fedha 2021/22 Wizara kwa kushirikiana na mamlaka za upangaji na kampuni binafsi itaendelea kuratibu shughuli za urasimishaji makazi **300,000** nchini.

***95. Mheshimiwa Spika***, dhamira ya Serikali ni kuhakikisha kwamba ifikapo mwaka 2023 maeneo yote yaliyoendelezwa bila kufuata taratibu za ujenzi mijini yawe yametambuliwa na kurasimishwa. Hivyo, **natoa rai kwa Mamlaka za Upangaji nchini kuongeza kasi ya usanifu wa maeneo ambayo hayajaendelezwa na kuyapima ili kuzuia ujenzi holela.**

**Udhibiti na Uendelezaji wa Miji**

***96. Mheshimiwa Spika,*** kwa mujibu wa Sheria ya Mipangomiji, Sura ya 355, upangaji na uendelezaji wa miji ni suala mtambuka ambalo hushirikisha wadau mbalimbali wakiwemo wamiliki wa ardhi, taasisi zisizo za kiserikali, sekta binafsi, asasi za kijamii na taasisi zinazotoa huduma za miundombinu kama vile barabara, umeme, maji na mawasiliano.

***97. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2020/21 Wizara iliahidi kuendelea kuratibu uidhinishaji wa maombi **300** ya mabadiliko ya matumizi ya ardhi nchini. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2021, jumla ya maombi **417** ya mabadiliko ya matumizi ya ardhi yaliidhinishwa kutoka mamlaka mbalimbali za upangaji nchini kwa kuzingatia Sheria ya Mipangomiji Na.8 ya mwaka 2007.

***Usimamizi na uratibu wa uendelezaji nyumba***

***98. Mheshimiwa Spika,*** Sekta ya Nyumba ni miongoni mwa sekta muhimu katika kukuza pato la Taifa, kuongeza ajira na kuboresha maisha ya watanzania. Wadau wanaoshiriki katika ujenzi wa nyumba na majengo ya biashara ni pamoja na Wizara kupitia Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), Wakala wa

Taifa wa Majengo (TBA), *Watumishi Housing Company*, taasisi za umma na sekta binafsi. Pamoja na juhudi zinazofanywa za ujenzi wa nyumba mijini, bado kuna uhaba wa nyumba bora za makazi kwa wastani wa mahitaji ya nyumba **200,000** kwa mwaka.

***99. Mheshimiwa Spika*,** Wizara kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali imeendelea kuweka mazingira wezeshi ya upatikanaji wa huduma za uendelezaji nyumba nchini. Huduma hizo ni pamoja na upatikanaji wa mikopo ya masharti nafuu kwa ajili ya ujenzi wa nyumba; ubunifu wa nyumba za gharama nafuu ambapo Wizara imeandaa ramani za mfano za nyumba za gharama nafuu zikiambatana na makadirio ya vifaa vya ujenzi ambazo zimesambazwa kwenye Halmashauri zote nchini. Ramani hizo zitasaidia kupunguza gharama kwa wananchi wenye kipato cha chini pamoja na kurahisisha upatikanaji wa vibali vya ujenzi. Aidha, Wizara imeandaa Mwongozo wa Upangaji na Ujenzi wa Nyumba Bora Vijijini ambao unaelekeza namna ya kupanga makazi vjijini kwa kuzingatia vigezo vilivyoainishwa.

***Mikopo ya ujenzi wa nyumba***

***100. Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka wa fedha 2020/21 Wizara ilipanga kuwezesha kuboreshwa kwa mazingira ya upatikanaji wa mikopo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba kwa kushirikiana na wadau mbalimbali. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2021, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imewezesha utoaji wa mikopo ya ujenzi wa nyumba kutoka taasisi za fedha kiasi cha shilingi billioni **134.7** kwa wananchi **1,300.**

***Mfuko wa Mikopo ya Nyumba kwa Watumishi wa Serikali***

***101. Mheshimiwa Spika,*** Serikali ilianzisha Mfuko wa Mikopo ya Nyumba kwa Watumishi wa Serikali kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa nyumba kupitia Waraka wa Utumishi Na. 8 wa mwaka 1992. Lengo la mfuko huo ni kukabiliana na changamoto ya uhaba wa nyumba kwa Watumishi wa

Serikali. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2021 jumla ya watumishi **1,567** walinufaika na mikopo yenye jumla ya shilingi bilioni **9.09.** Aidha, kiasi cha shilingi **288,000,000** kimerejeshwa kwenye akaunti ya mfuko. Hata hivyo, mfuko huu umekuwa ukikabiliwa na changamoto ya kukosa uendelevu wa mtaji kutokana na mfumo uliopo wa utoaji na urejeshwaji wa mikopo. Kwa kuzingatia changamoto zilizopo, Wizara inakusudia kufanya mapitio ya utekelezaji wa mfuko huu kwa kushirikiana na wadau ili kuwezesha utoaji wa mikopo kwa watumishi kwa utaratibu endelevu.

***102.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2020/21, Wizara iliahidi kuendelea kuboresha taarifa za Nyumba katika kanzidata ikiwa ni pamoja na kuhamasisha uundwaji wa vyama vya ushirika wa nyumba. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2021, taarifa za waendelezaji na wasimamiaji milki **207** ambao wamejenga jumla ya nyumba **25,239** zimeingizwa katika kanzidata ya nyumba. Aidha, katika kanzidata kuna vyama vya Ushirika wa Nyumba **38** vyenye wanachama **2,247** na ambavyo vimejenga jumla ya nyumba **1,056** katika Mikoa ya Dar es salaam, Dodoma, Iringa, Kagera, Musoma, Morogoro, Mwanza, na Shinyanga. Katika mwaka wa fedha 2021/22 Wizara itaendelea kuhamasisha ujenzi wa nyumba kupitia vyama vya ushirika wa nyumba na kuvijengea mazingira ya kupata mikopo yenye masharti nafuu kutoka taasisi za fedha kwa kushirikiana na Tume ya Maendeleo ya Vyama vya Ushirika.

***Ushirikiano na Taasisi za kimataifa Katika Uendelezaji wa Makazi***

***103.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inao wajibu wa kushirikiana na taasisi mbalimbali za kimataifa zinazojishughulisha na uendelezaji miji na makazi duniani. Taasisi hizo ni pamoja na Shirika la Makazi Duniani (UN-Habitant); Shirika la Maendeleo (UNDP) na Taasisi ya kifedha ya Afrika inayowezesha utoaji wa mikopo kwa ajili ya uendelezaji na ujenzi wa nyumba za gharama nafuu (Shelter Afrique). Katika mwaka wa fedha 2020/21, Wizara iliahidi kusimamia na kuratibu ushirikiano wa Taasisi hizo katika

uendelezaji wa miji na makazi nchini. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2021 Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania katika mkutano wa Kimataifa wa *Shelter Afrique* kwa njia ya mtandao pamoja na maadhimisho ya Siku ya Makazi Duniani. Katika mwaka wa fedha 2021/22, Wizara itaendelea kusimamia na kuratibu ushirikiano na taasisi mbalimbali za kimataifa kwa azma ya kutekeleza malengo na mikakati itakayokubaliwa.

***Mapitio ya Sera na Sheria***

***104.*** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kuzingatia mabadiliko ya kiuchumi na kijamii, Wizara kwa kushirikiana na wadau inakamilisha mapitio ya Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995 ili iweze kukidhi mahitaji ya sasa. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau imeandaa rasimu ya Marekebisho ya Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya Mwaka 2000 na ipo katika hatua za kukamilisha ukusanyaji wa maoni ya wadau. Sawia na hatua hiyo, Wizara imeandaa rasimu ya Sera ya Taifa ya Nyumba ambayo pia ipo katika hatua ya kukamilisha uchambuzi wa maoni ya wadau.

***105.*** ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya marekebisho ya sera hizo kufanyika, baadhi ya sheria zitafanyiwa marekebisho ili kukidhi matakwa ya sera zilizorekebishwa. Aidha, Wizara imeandaa mapendekezo ya kutunga Sheria ya Kusimamia na Kuendeleza Sekta ya Milki (Real Estate Sector) kwa kuzingatia maoni ya wadau. Pia, Wizara imeandaa mapendekezo ya marekebisho madogo katika Sheria saba (7) zinazohusiana na Sekta ya Ardhi. Sheria hizo ni Sheria ya Usajili wa Wataalam wa Upimaji Ardhi Sura 270, Sheria ya Ardhi ya Vijiji Sura 114, Sheria ya Mipangomiji Sura 355, Sheria ya Usajili wa Wataalam wa Mipangomiji Sura 426, Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini Sura 138, Sheria ya Upangaji wa Matumizi ya Ardhi Sura 116 na Sheria ya Upimaji Ardhi Sura 324.

## 5.5 MIRADI YA MAENDELEO

***106.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha usalama w a milki, kuongeza ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali, kutatua na kudhibiti migogoro ya matumizi ya ardhi na

kuwawezesha wananchi kiuchumi na kuimarisha mipaka ya Kimataifa, Wizara inatekeleza miradi ifuatayo:

***Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi***

***107. Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha usalama wa milki, kupunguza migogoro ya ardhi nchini, kuifanya ardhi kuwa mtaji hai na kuiwezesha Serikali kuongeza wigo wa mapato yanayotokana na Sekta ya Ardhi; Wizara inaendelea kutekeleza programu ya kupanga, kupima na kumilikisha kila kipande cha ardhi nchini.

***108. Mheshimiwa Spika,*** Programu hii inatekelezwa kwa kushirikiana na Mamlaka za Upangaji ambazo ni Halmashauri za Miji, Manispaa na Majiji. Katika mwaka wa fedha 2018/19 Wizara iliziwezesha Halmashauri **24** kiasi cha shilingi bilioni **6.2** kutekeleza majukumu hayo ambapo jumla ya viwanja **41,733** vilipimwa na kumilikishwa. Aidha, jumla ya shilingi bilioni **4.1** zimerejeshwa Serikalini kutokana na mauzo ya viwanja na Halmashauri nyingine zinaendelea kumilikisha ardhi. Nazipongeza Halmashauri saba (7) zilizokamilisha marejesho ya fedha kwa asilimia 100. Halmashauri hizo ni Jiji la Mbeya, Manispaa za Ilemela, Kahama na Shinyanga, Mji wa Bariadi na Wilaya za Misungwi na Geita (**Jedwali Na.12A**). **Natoa rai kwa Halmashauri zilizopatiwa fedha za upimaji na umilikishaji ardhi kurejesha fedha ili Halmashauri nyingine ziweze kupatiwa fedha za kutekeleza kazi za upangaji miji.**

***109. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2020/21 Wizara iliahidi kuendelea kuzijengea uwezo na kuziwezesha Halmashauri kupanga, kupima na kumilikisha ardhi. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2021 Wizara ilizipatia Ofisi za Ardhi za Mikoa **17** jumla ya shilingi bilioni **3.5** kwa ajili ya kupanga na kupima ardhi katika halmashauri **22** ambapo jumla ya viwanja **64,227** vimepimwa na hatua za umilikishaji zinaendelea ikilinganishwa na lengo la kupima viwanja **95,756** (**Jedwali Na.12B**). Programu hii imeonesha mafanikio kwa kuziwezesha Mamlaka za upangaji kuongeza kasi ya kupanga, kupima na kumilikisha kila kipande cha ardhi nchini. Katika mwaka wa fedha 2021/22, Wizara itaendelea na

utekelezaji wa programu hii kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais – TAMISEMI ambapo vitawekwa vigezo vya kuzingatia katika kuziongezea Halmashauri uwezo wa kifedha kutekeleza majukumu yao. Aidha, Wizara itaunda Timu Jumuishi ya Ufuatiliaji na Tathmini kwa ajili ya kuimarisha usimamizi wa fedha zinazotolewa.

***Utambuzi wa vipande vya ardhi***

***110.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kupata suluhisho la kujenga na kuendeleza mifumo ya utawala wa ardhi ambayo inalenga kukidhi mahitaji yaliyopo, Wizara imebuni mbinu mpya ya upimaji ambayo ni shirikishi na inayotumia teknolojia rahisi kwa kutumia simu za kiganjani. Mbinu hii mpya imeongeza usahihi kwa kuimarisha majira ya nukta kwa kutumia GPS ya Mkono badala ya kutegemea mifumo ya kitaalam inayofuata kanuni zenye viwango vya juu vya vipimo ambavyo ni vya gharama kubwa na huchukua muda mrefu kukamilisha upimaji. Aidha, vifaa vya kisasa vya upimaji hutumika kuboresha usahihi wa mipaka ya mitaa husika na mipangomiji hususan wakati wa kuainisha mipaka ya barabara, njia za umeme na matumizi ya Umma.

***111.*** ***Mheshimiwa Spika,*** zoezi la utambuzi wa vipande vya ardhi kwa kutumia teknolojia rahisi limeiwezesha Wizara kuwatambua wamiliki wa vipande vya ardhi na taarifa za wamiliki kuingizwa katika Mfumo wa ILMIS. Tangu kuanza kwa zoezi hili mwezi Januari, 2021, jumla vipande vya ardhi **16,138** vilitambuliwa katika majiji ya Arusha na Mwanza na leseni za makazi **2,653** ziliandaliwa na kutolewa kwa wananchi katika jiji la Mwanza na Arusha. Kupitia zoezi hilo migogoro ya ardhi **83** imetatuliwa. Katika mwaka wa fedha 2021/22 wizara imepanga kutambua vipande vya ardhi **700,000** nchini ili kuwawezesha wananchi kuwa na nyaraka za umiliki wa ardhi.

***Mradi wa Uboreshaji wa Milki za Ardhi***

***112.*** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi wa kuboresha milki za ardhi unalenga kuimarisha usalama wa milki na mifumo ya

taarifa za ardhi ambao unatarajiwa kutekelezwa kwa kushirikiana na Benki ya Dunia. Kwa sasa Serikali inaendelea kukamilisha majadiliano ya mwisho kuwezesha upatikanaji wa mkopo wa dola za kimarekani milioni **150** kutekeleza maeneo ya kipaumbele ya Wizara. Kupitia mradi huu, katika mwaka wa fedha wa 2021/22, Wizara kwa kutumia fedha za ndani inatarajia kutekeleza shughuli zifuatazo; kujenga Mtandao Kiambo (LAN) kwa kuanza na mikoa minne (4) ya Lindi, Mbeya, Mwanza na Iringa yenye uhitaji mkubwa na kuunganishwa katika Kituo cha Taifa cha Kutunza Taarifa za Ardhi, kukamilisha ujenzi wa kituo cha mawasiliano kwa wateja katika makao makuu ya Wizara, kufanya matengenezo ya mfumo wa huduma kwa wateja katika ofisi za mkoa wa Dar es Salaam na kusimika vifaa vya kudhibiti majanga na vihatarishi kwa ajili ya mifumo ya taarifa za ardhi katika *Data Center* ya Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA). Vifaa hivi vitaijengea Wizara uwezo wa kuwa na utayari wa kurudisha huduma kwa haraka pindi majanga yanapotokea.

***113.*** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, katika mwaka wa fedha 2021/22, Wizara imepanga kujenga mfumo utakaorahisisha utekelezaji wa kazi katika Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya. Mfumo huo pamoja na mambo mengine, utawezesha utunzaji wa kumbukumbu za mashauri yanayohusu ardhi, ufunguaji wa mashauri mapya, ufuatiliaji wa mashauri na upatikanaji wa nakala za hukumu kwa njia ya mtandao.

***Mradi wa Upimaji Mipaka ya Kimataifa***

***114.*** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika kuimarisha usalama na ushirikiano miongoni mwa nchi za bara la Afrika, Umoja wa Afrika kupitia **Azimio Na.17** lililofikiwa na Wakuu wa Nchi za Afrika huko Durban, Afrika Kusini, ulizitaka nchi zote za Afrika kuhakiki mipaka yake ifikapo mwaka 2022.

***115.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza azimio hilo, Wizara iliahidi kuhakiki na kuimarisha mpaka wenye jumla ya kilometa **2,086** kabla ya mwaka 2022 kwa kushirikiana na nchi jirani. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2021 jumla ya kilometa **369** za

mpaka kati ya Tanzania na nchi jirani zimehakikiwa. Aidha, Kamisheni ya Pamoja ya Ushirikiano baina ya Tanzania na Burundi katika kikao chake cha tarehe 3 hadi 5 Machi, 2021 kilichofanyika mkoani Kigoma nchini Tanzania kilielekeza nchi wanachama kupitia Timu ya Pamoja ya Wataalam kuendelea na hatua za kuimarisha mpaka. Katika mwaka wa fedha 2021/22 Wizara itaendelea na uimarishaji wa mipaka ya nchi kavu km 100 kati ya Tanzania na Burundi na km 128 kati ya Tanzania na Kenya kwa kushirikiana na nchi hizo.

***Mradi wa Uimarishaji wa Miundombinu ya Upimaji na Ramani (NSDI)***

***116.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka ujao wa fedha 2021/22, Wizara inatarajia kuanza utekelezaji wa Mradi mpya wa kuimarisha Miundombinu ya Upimaji na Ramani kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Korea Kusini kupitia Benki ya Exim. Mradi huu utawezesha kununua vifaa vya kisasa vya upimaji, ununuzi wa ndege zisizo na rubani (drones) kwa ajili ya kupiga picha za anga na kutoa mafunzo kwa watumishi. Utekelezaji wa mradi huu unatarajiwa kuongeza kasi ya upangaji na upimaji wa ardhi, kuongeza uwezo wa kuandaa ramani za msingi kwa nchi nzima ambazo zinahitajika kwa matumizi mengine hususan ujenzi wa miundombinu kama vile barabara, reli, njia za mawasiliano na pia katika ulinzi na udhibiti wa maliasili, madini, mazingira n.k. Pia itaongeza alama za kielekroniki na alama za msingi za upimaji ardhi ambazo huwezesha upimaji ardhi kufanyika kwa muda mfupi na kwa gharama nafuu zaidi kwa kuwa teknolojia hii huitaji vifaa vichache na idadi ndogo ya wapima na wasanifu ramani.

***117.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, Wizara itanunua vifaa vya kisasa kwa ajili ya uandaaji wa ramani za msingi; kujenga vituo **30** vya upimaji ardhi katika makao makuu ya mikoa yote na kuongeza alama **150** za upimaji nchini; kuandaa ramani za msingi zenye uwiano mdogo na uwiano mkubwa katika mikoa ya Dodoma na Arusha; kujenga kanzidata ya kitaifa ya taarifa za kijiografia

pamoja na mifumo ya kulinda na kusambaza taarifa kwa watumiaji; na kuwajengea uwezo wataalam **30** katika nyanja a upimaji na ramani.

***Miradi ya Kimkakati ya Kitaifa***

***118.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kushiriki katika utekelezaji wa Miradi ya Kimkakati ya Kitaifa kwa kupanga, kupima na kufanya uthamini wa ardhi na mali katika maeneo ya miradi hiyo. Miradi hiyo ni pamoja na Mradi wa Ujenzi wa Bwawa la Kuzalisha Umeme la Julius Nyerere, Bomba la Mafuta kutoka Hoima nchini Uganda hadi Chongoleani jijini Tanga nchini Tanzania na ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR).

***Mradi wa uzalishaji umeme wa Julius Nyerere***

***119.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika uendelezaji wa eneo la mradi, Wizara inaendelea kuandaa mpango wa uendelezaji wa ukanda wa mradi (Corridor Development Plan) utakaowezesha mamlaka za upangaji kuandaa mipangokina katika miji midogo na mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji katika ukanda huu. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2021 mipangokina **19** yenye viwanja **4,309** iliandaliwa katika Mji Mdogo wa Kisaki na usanifu wa michoro ya mipangomiji katika Mji wa Ikwiriri umekamilika ambapo jumla ya viwanja **601** vimesanifiwa na upimaji unaendelea. Aidha, katika eneo linapojengwa Bwawa la Julius Nyerere Wizara ilipima zaidi ya hekta **4,000** katika sehemu ya ujenzi wa mtambo wa kufua umeme na hekta **12,000** zilipimwa katika eneo inapojengwa karakana na makazi ya watumishi watakaoendesha mitambo hiyo.

***120.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika eneo la dakio la Bwawa hilo jumla ya vijiji **829** vimeandaliwa mipango ya matumizi ya ardhi katika Mikoa ya Morogoro (**310**), Pwani (**69**), Lindi (**145**), Ruvuma (**90**), Dodoma (**26**), Njombe (**44)** na Iringa (**145**). Kadhalika, upimaji wa kina (Detail Survey) ulifanyika kwa ajili ya kuwezesha uwekaji wa njia ya umeme wa msongo mkubwa wa kilovoti **400** kutoka kwenye chanzo cha kuzalisha umeme hadi Chalinze (km**160**).

***Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa***

***121.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara pia inashiriki kutekeleza mradi wa ujenzi wa Reli ya kisasa kutoka Dar es Salaam hadi Makutupora kwa awamu ya kwanza ambapo jumla ya vituo **15** vinajengwa. Usanifu wa michoro ya mipangomiji na upimaji katika vituo vitatu (**3**) vya Dar es Salaam, Morogoro na Dodoma umekamilika. Aidha, usanifu wa michoro ya mipangomiji na upimaji katika maeneo ya vituo vingine **11** unaendelea.

***122.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na taasisi nyingine za Serikali inaendelea kufanya uchambuzi wa maandalizi ya Mpango maalum wa uendelezaji kiuchumi ukanda wa Reli ya Kisasa. Mpango huu utawezesha mamlaka za upangaji kuandaa mipangokina katika maeneo ya miji na mipango ya matumizi ya ardhi katika maeneo ya vijiji vilivyo katika ukanda wa Reli ya Kisasa.

***Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Mafuta***

***123.*** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kuzingatia hatua ya kusainiwa kwa mkataba wa uwekezaji baina ya Serikali ya Tanzania na Wawekezaji kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Bomba la Mafuta kutoka Hoima nchini Uganda hadi Chongoleani jijini Tanga, Wizara inaendelea kutekeleza majukumu ya sekta ya ardhi yaliyoainishwa kwenye mkataba. Katika maandalizi ya ujenzi wa bomba la mafuta, Wizara imepima kilomita **650** za njia ya bomba na kazi itakamilika kabla ya tarehe 30 Juni 2021. Aidha, Wizara imeandaa mpango wa uendelezaji wa ukanda wa mradi wa Bomba la Mafuta kwa kuandaa mipangokina katika maeneo ya miji na mipango ya matumizi ya ardhi katika maeneo ya vijiji vinavyopakana na bomba hilo ili wananchi waweze kunufaika kiuchumi na kijamii kupitia ardhi. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2021, Wizara imeshiriki katika vikao mbalimbali vya kujadili namna bora ya kutekeleza mradi, kufanya uthamini na utwaaji wa maeneo **14** yatakayotumika kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya kusukuma mafuta ghafi.

***124. Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka za Upangaji imeandaa mipangokina **21** yenye jumla ya viwanja **11,631** katika maeneo ya vijiji vinavyopakana na mkuza wa bomba la mafuta (**Jedwali Na. 13)**. Jumla ya vijiji **104** vimeandaliwa mipango ya matumizi ya ardhi katika mikoa ifuatayo; Kagera (**24**), Geita (**22**), Tabora (**9**), Singida (**19**), Dodoma (**8**), Manyara (**6**) na Tanga (**16**). Aidha, Wizara imeshiriki kupima alama za picha za anga ardhini, kuweka alama za upimaji, kuainisha njia ya mkuza wa bomba na kuanza upimaji, kupima maeneo ya vipaumbele vya mradi kwa ajili ya karakana ya kuunganishia mabomba ya mafuta na kushiriki kazi ya utafiti wa udongo katika mkuza wa bomba la mafuta. Katika mwaka wa fedha 2021/22 Wizara itaendelea kushirikiana na Mamlaka za Upangaji katika kukamilisha shughuli zinazohusiana na upimaji, upangaji na uthamini wa ardhi na mali katika maeneo ya vijiji vinavyopakana na mkuza wa bomba hilo.

## 5.6 USIMAMIZI WA TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA

***125. Mheshimiwa Spika,*** katika utekelezaji wa majukumu, Wizara imeendelea kuratibu na kusimamia shughuli za taasisi zilizo chini yake. Taasisi hizo ni Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi; Shirika la Nyumba la Taifa; na Vyuo vya Ardhi vya Tabora na Morogoro.

### Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi

***126. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi imeendelea kusimamia na kuratibu uandaaji, na utekelezaji wa mipango ya matumizi ya ardhi nchini, kutoa miongozo na elimu kwa umma na kwa mamlaka za upangaji, kushiriki katika utatuzi wa migogoro ya matumizi ya ardhi, kuimarisha na kusimamia mfumo wa utunzaji wa kumbukumbu ya mipango ya matumizi ya ardhi, kufanya tafiti na kuratibu ushiriki wa wadau mbalimbali wa kimkakati wanaochangia na kuwezesha upangaji wa matumizi ya ardhi nchini. Vilevile, Tume imeendelea kushiriki katika utekelezaji wa miradi ya Taifa ya kimkakati.

***127.*** ***Mheshimiwa Spika,*** mipango ya matumizi ya ardhi inajumuisha mipango ya Ukanda, Wilaya na Vijiji ikiwa ni utekelezaji wa Mpango wa Matumizi ya Ardhi wa Taifa (2013-2033) na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (2020-2025). Mipango hii husaidia katika kutenga maeneo ya uwekezaji, uhifadhi, makazi, uzalishaji (Kilimo na ufugaji), ardhi ya akiba, mapito ya wanyamapori, kutatua migogoro ya matumizi ya ardhi na kuongeza tija katika uzalishaji mali na hivyo kuboresha maisha ya jamii kiuchumi.

***128.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2020/21, Wizara kupitia Tume ilipanga kuendelea kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi katika maeneo mbalimbali nchini kwa kushirikiana na wadau pamoja na kufanya tathmini ya utekelezaji wa mipango hiyo. Aidha, Wizara kupitia Tume iliahidi kuwezesha upangaji matumizi ya ardhi ya vijiji **100** katika wilaya zinazopitiwa na njia ya bomba la mafuta (EACOP) na wilaya zilizo mipakani mwa nchi. Hadi kufikia 15 Mei, 2021 Tume imeratibu na kusimamia uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi ya Vijiji **77** katika Wilaya **21** kwa kushirikiana na wadau ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa, Wakala wa Misitu Tanzania (TFS), *FORVAC*, *Frankfurt Zoological Society* (FZS), Shirika la *PELUM* na Taasisi ya *Jane Goodall*, *Tanzania Forest Conservation Group* (TFCG) (**Jedwali Na. 14**). Katika mwaka wa fedha 2021/2022 Tume kwa kushirikiana na wadau mbalimbali itaandaa mipango ya matumizi ya ardhi kwa wilaya moja (**1**), vijiji **98** na kanda mbili (**2**) kupitia miradi ya kimkakati. Aidha, ili kuongeza kasi ya uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi na utekelezaji wake **natoa wito kwa Halmashauri zote nchini kutenga bajeti za uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi angalau kwa vijiji 6 kwa mwaka.**

***129.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2020/2021 Wizara kupitia Tume imeendelea kutoa miongozo na elimu kwa umma na mamlaka za upangaji juu ya sheria, kanuni na taratibu za uandaaji na usimamizi wa mipango ya matumizi ya ardhi na utatuzi wa migogoro. Hadi kufikia 15 Mei, 2021 jumla ya wajumbe **160** wa Timu Shirikishi ya Matumizi ya Ardhi ya Wilaya (PLUM), wajumbe **1,742** wa Halmashauri za vijiji na

wajumbe **536** wa Kamati za Usimamizi wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Vijiji (VLUM) walipatiwa elimu katika Halmashauri za Wilaya **20** na Vijiji **77**. Vile vile, Tume imeweza kufanya marejeo ya *Mwongozo Shirikishi wa Uandaaji na Usimamizi wa Mipango ya Matumizi Ardhi ya Vijiji wa mwaka 2013* na inaendelea na taratibu za uchapishaji ili kuusambaza kwa Halmashauri na Vijiji mbalimbali nchini. Aidha, watumishi **24** wa Tume na Halmashauri za Simanjiro na Monduli walipatiwa mafunzo kuhusu namna ya kuingiza taarifa za matumizi ya ardhi katika Mfumo wa Taifa wa Taarifa za Matumizi ya Ardhi (NLUIS). Katika mwaka wa fedha 2021/22, Wizara kupitia Tume itaendelea kutoa Miongozo na elimu ili kujenga uelewa kwa umma na kuwezesha mamlaka za upangaji kuandaa, kusimamia na kutekeleza Mipango ya Matumizi ya Ardhi.

***130.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22 Wizara kupitia Tume, itaendelea kuratibu na kushirikiana na wadau mbalimbali katika kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi katika kanda za maeneo ya kilimo, malisho ya mifugo, shoroba za wanyamapori, hifadhi za misitu na wanyamapori, miradi ya kimkakati ya Reli ya Kisasa (SGR), vyanzo vya maji kwa ajili ya mradi wa uzalishaji wa umeme (*Julius Nyerere Hydro Electric Dam Project*) na Vijiji vinavyopakana na mkuza wa bomba la mafuta (EACOP).

***131.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Tume imeendelea kuunda, kuboresha na kusimamia mfumo wa Taifa wa Taarifa za Matumizi ya ardhi (NLUIS). Mfumo huu umefanyiwa majaribio katika hatua za awali na jumla ya ramani **56** za mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji na taarifa mbalimbali za Wilaya ya Simanjiro na Monduli zimeandaliwa na kuingizwa kwenye mfumo. Katika mwaka wa fedha 2021/22, mfumo huu utaendelea kuboreshwa na kusambazwa ili kuongeza wigo wa kusajili na kuhifadhi kumbukumbu za taarifa za mipango ya matumizi ya ardhi nchini.

***132.*** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Tume imeendelea kufanya tafiti ili kubaini changamoto na kujenga uelewa kuhusu masuala mbalimbali ya kisekta, rasilimali ardhi na

mipango ya matumizi yake. Hadi kufikia 15 Mei, 2021, Tume imefanya utafiti kuhusu mabadiliko ya tabianchi, matumizi ya ardhi na uoto wa asili katika Jiji la Dodoma kwa kutumia picha za anga pamoja na uchambuzi wa taarifa kwa kutumia Mifumo ya Taarifa za
**109.** Kijiografia (*GIS analysis*). Utafiti huu umebaini uwepo wa mabadiliko makubwa katika uoto wa asili na matumizi ya ardhi kutokana na mabadiliko ya tabianchi. Katika mwaka wa fedha 2021/22, Tume itaendelea kufanya tafiti na kusambaza matokeo ya tafiti kwa wadau.

***133.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Tume imeendelea kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji mbalimbali nchini. Hadi kufikia 15 Mei, 2021 jumla ya vijiji **86** katika wilaya **7** vimefanyiwa ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa mipango ya matumizi ya ardhi (**Jedwali Na.15).** Tathmini hiyo imebaini takriban asilimia **80** ya vijiji vilivyofanyiwa tathmini mipango yao inatekelezwa kama ilivyopangwa. Katika mwaka 2021/22, Tume itaendelea kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji **200** na Wilaya **2.**

### Shirika la Nyumba la Taifa

***134.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inalo jukumu la kusimamia Shirika la Nyumba la Taifa ambalo linahusika na ujenzi wa nyumba za makazi na majengo mbalimbali kwa ajili ya matumizi ya ofisi na biashara. Shirika linaendelea kutekeleza Mpango Mkakati wa Miaka 10 (2015/16 – 2024/25) ambao umegawanywa katika kipindi cha muda mfupi, wa kati, na mrefu. Katika muda mfupi, Shirika limelenga kuboresha hali ya ukwasi (*liquidity position*) ili kuwa na fedha za kutosha kujiendesha. Mikakati hiyo ni pamoja na:-

(i) Kubana matumizi kwa kuondokana na baadhi ya matumizi yasiyo ya lazima;

(ii) Kupunguza gharama za ukarabati wa nyumba bila kuathiri ubora;

(iii) Kutekeleza mpango wa kupanga upya baadhi ya mikopo yake (loans restructuring plan) ili kupunguza kiasi cha malipo ya mikopo kwa mwezi;

(iv) Kupangisha nyumba zote za gharama nafuu ambazo zilikuwa zimekamilika na bado hazijapata wanunuzi ili kuongeza kipato cha Shirika kutokana na kodi ya pango;

(v) Kukamilisha ujenzi wa baadhi ya miradi midogo na ya kati (ya nyumba za makazi na biashara) ambayo ilikuwa imesimama na kuipangisha na/au kuiuza ili kuongeza kipato cha Shirika; na

(vi) Kuchukua hatua mbalimbali za kukusanya madeni sugu ya wapangaji wa zamani na wa sasa na kuimarisha makusanyo ya kodi ya pango kwa wapangaji waliopo. Hadi kufikia tarehe 15 Mei 2021, Shirika lilifanikiwa kukusanya madeni ya zaidi ya shilingi bilioni **3**.

***135.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika muda wa kati, Shirika linalenga kumalizia miradi mikubwa ambayo imekwama pamoja na kuimarisha njia mbadala za mapato ili kuongeza kasi ya ukuaji wa Shirika. Mikakati hiyo ni pamoja na:-

(i) Kumalizia miradi mikubwa ambayo imekwama ikiwemo *Morocco Square*, *Kawe 711*, *Golden Premier Residence* na Mradi wa Kiwanja Na. 300 *Regent Estate* katika Jiji la Dar es Salaam. Ujenzi wa *Morocco Square* unaendelea kuanzia mwezi Novemba 2020 baada ya kusimama kwa muda. Hadi kufikia tarehe 15 Mei 2021, ujenzi umekamilika kwa 90%. Ujenzi wa Kawe 711, *Golden Premier Residence* na Mradi wa Kiwanja Na. 300 *Regent Estate* umesimama kwa muda, wakati jitihada za kutafuta fedha kutoka vyanzo mbalimbali zinaendelea. Kwa mwaka wa fedha 2021/22, Shirika limepanga kukamilisha mradi wa *Morocco Square*;

(ii) Kupitia upya mikataba ya wapangaji na kufanya maboresho ya vipengele ili kuhakikisha kwamba Shirika linakusanya kodi na madeni. Pia, wapangaji

ambao wanakiuka masharti ya ulipaji wa kodi ya pango wanachukuliwa hatua za kisheria; na

(iii) Kufanya ukaguzi wa hali ya majengo yote ya Shirika (conditional assessment) ili kuweka mpango wa kuzifanyia maboresho na matengenezo ya kudumu nyumba zake ili kuziongeza thamani. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2021, Shirika limekamilisha mpango wa ukarabati utakaotekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2020/21 hadi 2025/26 wenye lengo la kuboresha nyumba za Shirika. Majaribio ya mpango huu yalifanyika katika Mradi wa Medeli Jijini Dodoma ambapo nyumba zote zinazomilikiwa na Shirika zimekarabatiwa. Utekelezaji wa mpango huu unaendelea katika Mikoa ya Dar es Salaam (Temeke), Kilimanjaro na Mtwara. Katika mwaka wa fedha 2021/22, Shirika litaendelea kukarabati na kufanya matengenezo ya nyumba katika mikoa mbalimbali nchini.

***136.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mikakati ya muda mrefu, Shirika linajielekeza katika utekelezaji wa lengo lake kuu la kuwapatia wananchi makazi bora kwa kutanua wigo wa uwekezaji wake kama ifuatavyo:-

(i) Kubadilisha malengo ya nyumba mpya zitakazojengwa kutoka kuwa za kuuza **70%** na kupangisha **30%** na kuwa za kuuza **20%** na kupangisha **80%**; na

(ii) Kuwekeza katika viwanda vya utengenezaji wa vifaa vya ujenzi kama vile kokoto, matofali na mabati kuanzia mwaka wa fedha 2021/22 ili kuwapunguzia wananchi gharama za ujenzi wa nyumba.

***137.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2020/21, Wizara kupitia Shirika la Nyumba la Taifa ilitekeleza miradi mbalimbali ya ujenzi wa nyumba za gharama nafuu nchini. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2021 Shirika liliendelea na ujenzi wa nyumba za gharama nafuu katika maeneo mbalimbali ya Halmashauri za Miji na Wilaya zifuatazo;

i) Njombe, Makete, nyumba **50** zimekamilika kwa 70%;

ii) Iyumbu, Dodoma, nyumba **300**; Nyumba **232** zimekamilika kwa 100% na ujenzi wa nyumba **68** umeanza;

iii) Inyonga, Katavi, nyumba **24** zimekamilika kwa 85%;

iv) Jangwani, Sumbawanga, nyumba **20** zimekamilika kwa 100% ambapo nyumba **18** zimepangishwa na nyumba **2** zimeuzwa; na

v) Masasi, Mtwara, nyumba **54** zimekamilika kwa 100% na upangishaji unaendelea.

***138.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, Shirika litaendelea na ujenzi wa nyumba za gharama nafuu katika maeneo mbalimbali ya Halmashauri za Miji na Wilaya. Aidha, Shirika pia litaanzisha miradi mipya ya nyumba za gharama nafuu, katika Halmashauri za Sumbawanga na Ubungo (Luguruni).Vilevile, Shirika linaendelea kutekeleza miradi ya uendelezaji Miji ya Pembezoni *(Satellite Towns)* katika maeneo linayoyamiliki ambayo ni Luguruni - Ubungo, Uvumba - Kigamboni na Kawe - Kinondoni, Burka/Matevesi- Arusha Jiji na eneo la Usa River - Meru.

***139.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2020/21, Shirika la Nyumba la Taifa lilitekeleza miradi ya ujenzi wa majengo ya biashara katika maeneo mbalimbali nchini ikiwemo:-

i) Mutukula Commercial Complex, Kagera – umekamilika kwa 90%;

ii) Singida shops, Singida – umekamilika kwa 100%; na

iii) Mwanza Commercial Shops, Mwanza – umekamilika kwa 50%.

Katika mwaka wa fedha 2021/22, Shirika litaendelea na ujenzi wa majengo ya biashara katika Halmashauri za Manispaa za Lindi na Bukoba pamoja na kuanza ujenzi wa majengo ya biashara katika Halmashauri za Manispaa za Kahama na Morogoro na Halmashauri za Wilaya za Masasi na Kilwa. Sambamba na utekelezaji wa miradi hiyo, Shirika litafanya upembuzi yakinifu wa miradi ya ujenzi wa makazi na biashara katika Mikoa ya Songwe, Ruvuma, Njombe, Geita na Simiyu.

***140.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2020/21, Shirika la Nyumba la Taifa liliahidi kuanza utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa nyumba **400** za gharama nafuu kati ya nyumba **1,000** jijini Dodoma. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2021, awamu ya kwanza ya mradi huu imeanza kutekelezwa ambapo nyumba **404** zinaendelea kujengwa baada ya kupata idhini ya Wizara ya Fedha na Mipango kukopa shilingi bilioni **20** kutoka Mfuko wa Mradi wa Nyumba. Kati ya hizo, nyumba **101** zinajengwa Chamwino na nyumba **303** zinajengwa Iyumbu. Katika mwaka wa fedha 2021/22, Shirika litaendelea na utekelezaji wa mradi huu ambapo nyumba za gharama nafuu zitajengwa na kuuzwa au kupangisha kwa wananchi na watumishi wa umma. Mnunuzi wa nyumba hizo, atasaidiwa kupata mkopo wenye riba nafuu na atakabidhiwa hati na funguo siku anapolipia nyumba.

***141.*** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2020/21 Shirika limeendelea kutekeleza miradi ya ukandarasi kwa kusanifu, kusanifu na kujenga, kumalizia ujenzi, kukarabati au kusimamia ujenzi wa nyumba za watumishi wa umma pamoja na ofisi za taasisi mbalimbali za Serikali nchini ikijumuisha:-

i) Ujenzi wa jengo la ofisi ya EWURA Medeli, Jijini Dodoma;

ii) Ujenzi wa jengo la ofisi ya Chuo Kikuu cha Mwalimu Nyerere, Musoma;

iii) Ujenzi wa Machinjio ya Kisasa Vingunguti, Dar es Salaam;

iv) Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Kumbukumbu ya Mwl. J.K. Nyerere iliyopo Kwangwa, Musoma;

v) Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kusini Mtwara;

vi) Ujenzi wa Ukumbi wa Mikutano wa Halmashauri ya Mji wa Mpanda, Katavi;

vii) Ujenzi wa Majengo 44 ya Ofisi na Makazi kwa ajili ya Wakala wa Misitu Tanzania katika maeneo 17 nchini;

viii) Ujenzi wa Shule ya Mfano Mbuye, Geita;

ix) Ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Benki ya CRDB, Dar es Salaam; na

x) Usanifu na usimamizi wa jengo la Makao Makuu ya Wizara ya Fedha na Mipango katika eneo la Mtumba, Dodoma.

***142.*** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka wa fedha 2021/22, Shirika litaendelea kutekeleza miradi ya ukandarasi ikiwemo Hospitali ya Rufaa Mwalimu Nyerere (Mara) na Soko la Kimataifa la Mifugo la Buzirayombo (Geita). Vilevile, Shirika litaanza utekelezaji wa miradi ya ukandarasi ikiwemo ujenzi wa Maabara ya Kufundishia ya Chuo cha Sayansi na Hesabu ya Chuo Kikuu cha Dodoma, ujenzi wa Jengo la Shule ya Uchumi ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na usanifu na ujenzi wa nyumba za Watumishi wa Reli ya Kisasa (SGR). Shirika pia litaendelea na usanifu na usimamizi wa ujenzi wa majengo ya Wizara ya Fedha na Mipango na Uwanja wa Ndani wa Michezo wa Magufuli (Magufuli Arena) Jijini Dodoma.

***143.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2020/21, Shirika liliahidi kuandaa Mipango ya uendelezaji wa maeneo ya Kwala (Ruvu) na mji mpya wa Kisarawe (institutional master plan). Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2021, Shirika limekamilisha majadiliano na Halmashauri za Wilaya za Kibaha na Kisarawe kuhusu mipango kazi ya upangaji wa

maeneo hayo. Utekelezaji wa mipango hiyo utafanyika katika mwaka wa fedha 2021/22.

Vilevile, Shirika liitaandaa mipango ya uendelezaji wa maeneo ya Iwambi na Mwashiwawala, mkoani Mbeya

***144. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2020/21, Shirika liliahidi kukusanya kodi ya pango kiasi cha shilingi bilioni **96.6**. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2021, Shirika limekusanya shilingi bilioni **79.7** sawa na asilimia **82%** ya lengo. Aidha, katika mwaka wa fedha 2021/22, Shirika limepanga kukusanya kodi ya pango kiasi cha shilingi bilioni **105.6. Natoa wito kwa wapangaji wote wa nyumba za Shirika la Nyumba la Taifa nchini kutimiza wajibu wao kwa kulipa kodi na malimbikizo yote wanayodaiwa.**

***145. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, Shirika litaanza utekelezaji wa mradi wa Mpango wa uendelezaji wa maeneo ya Chuo Kikuu cha Dodoma (institutional master plan) pamoja na kuendelea na utekelezaji wa Muundo Jumuishi (Integrated System) wa TEHAMA, ambao unatarajiwa kuimarisha ufanisi na utendaji kazi wa Shirika.

**Vyuo vya Ardhi Tabora na Morogoro**

***146. Mheshimiwa Spika,*** Wizara ina jukumu la kusimamia Chuo cha Ardhi Tabora (ARITA) na Chuo cha Ardhi Morogoro (ARIMO) ambavyo vinatoa mafunzo ya fani mbalimbali za ardhi katika ngazi ya Astashahada (*Certificate*) na Stashahada (*Diploma*). Fani zinazotolewa ni upangaji wa miji na vijiji; upimaji wa ardhi; usimamizi wa ardhi; uthamini na usajili; urasimu ramani; na sanaa, ubunifu na uchapishaji. Wizara imeendelea kuviimarisha vyuo hivi kwa kuboresha mitaala, kuvipatia vitendea kazi muhimu, kuwezesha ujenzi wa madarasa ili viweze kutoa ujuzi unaokidhi viwango vya taaluma zinazohitajika.

***147. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2020/21, Vyuo hivi vimedahili jumla ya wanafunzi **1,970** (ARITA - **1,446**

na ARIMO - **524**) wa fani mbalimbali ngazi ya cheti na Stashahada. Katika mwaka wa fedha 2021/22 Vyuo hivi vitaendelea kuboresha miundombinu ya kufundishia na kuongeza udahili kufikia wanafunzi **2,200** ambapo ARITA kinatarajia kudahili wanafunzi **1,600** na ARIMO wanafunzi **600**. Aidha, Wizara itaendelea kufanya mapitio ya sheria na miundo iliyoanzisha vyuo hivi kwa lengo la kuboresha usimamizi na utendaji kazi.

## 5.7 UTAWALA NA RASILIMALI WATU

***148. Mheshimiwa Spika,*** Utawala na Rasilimali Watu ni sehemu muhimu katika usimamizi na utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Katika mwaka wa fedha 2020/21, Wizara ilipanga kuajiri watumishi wapya **270** kadri vibali vya ajira vitakavyokuwa vinatolewa ikiwa ni pamoja na kujaza nafasi zilizokuwa wazi kutokana na sababu mbalimbali. Kwa sasa Wizara ina jumla ya watumishi **2,378**, kati ya watumishi hao watumishi wa kada za sekta ya ardhi ni **1,733**. Ili Wizara iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo, inapaswa kuwa na watumishi wa kada za sekta ya ardhi wapatao **4,847**. Hivyo, Wizara ina upungufu wa watumishi **3,114** wa kada za sekta ya ardhi. Tayari jumla ya vibali vya watumishi **206** wameidhinishwa katika Ikama za miaka ya fedha 2018/19, 2019/20 na 2020/21 ambao ajira zao zinasubiri vibali vya utekelezaji, na watumishi **711** wameombewa vibali vya ajira katika mwaka wa fedha 2021/22, kati ya hao watumishi **397** ni wa sekta ya ardhi. Aidha, hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2021 Wizara imepata kibali cha kuajiri watumishi **36** wa ajira mbadala wa kada mbalimbali.

### Utawala Bora na Uwajibikaji

***149. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2020/21 Wizara iliahidi kukamilisha Mkataba wa Huduma kwa Mteja na kusambaza nakala katika Ofisi zote za Ardhi za Mikoa pamoja na wadau wengine. Lengo likiwa ni kuongeza uwazi katika utoaji wa huduma za Sekta ya Ardhi. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Wizara imekamilisha Mkataba wa Huduma kwa Mteja ambao ni mwongozo wa utoaji wa

huduma. Mkataba huo unapatikana kupitia tovuti ya Wizara (*www.lands.go.tz*). Katika mwaka 2021/22 Wizara itachapisha nakala za ziada za Mkataba wa Huduma kwa Mteja na kuzisambaza kwa wadau.

***150.*** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2020/21 Wizara iliahidi kuendelea kutekeleza mkakati wa kupambana na viashiria vya rushwa katika Sekta ya Ardhi kama sehemu ya mikakati ya kuboresha huduma zinazotolewa kwa umma. Hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2021, mafunzo kuhusu maadili ya utumishi wa umma na mapambano dhidi ya rushwa yametolewa kwa Kamati ya Kudhibiti Uadilifu na Menejimenti ya Wizara. Katika mwaka wa fedha 2021/22 Wizara itaendelea na utekelezaji wa mkakati wa kupambana na viashiria vya rushwa katika Sekta ya Ardhi.

***Mafunzo kwa Watumishi***

***151.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2020/21, Wizara iliahidi kutoa mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa watumishi **700** kwa kuzingatia mahitaji na Mpango wa Mafunzo wa Wizara. Hadi kufikia 15 Mei, 2021, Wizara imewezesha utoaji wa mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa watumishi **137.** Aidha, katika mwaka wa fedha 2021/22, Wizara itaendelea kuwezesha utoaji wa mafunzo kwa watumishi **700** kwa kuzingatia mahitaji na Mpango wa Mafunzo wa Wizara.

***Habari na Elimu kwa Umma***

***152.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2020/21 Wizara iliahidi kuendelea na utaratibu wa upashanaji habari na elimu kwa umma kuhusu masuala yanayohusu Sekta ya Ardhi. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Wizara iliandaa na kusambaza nakala **23,830** za Machapisho na vipeperushi vyenye jumbe kuhusu sekta ya ardhi. Wizara pia imeshiriki katika Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya **44** (Sabasaba) jijini Dar es Salaam, Maonesho ya Wakulima ya Nanenane mkoani Simiyu na Dodoma, Maonesho ya Uwezeshaji wananchi kiuchumi jijini Arusha na Maadhimisho ya Wiki ya Sheria jijini Dodoma.

***153.*** ***Mheshimiwa Spika*****,** vilevile, vipindi na matangazo **121** ya luninga na **134** ya redio yametolewa kwa umma kuhusu utekelezaji wa masuala mbalimbali ya Sekta ya Ardhi, makala **98** za magazeti kuhusu masuala ya Sekta ya Ardhi zimeandaliwa na kuchapishwa kwenye magazeti mbalimbali nchini. Aidha, taarifa **246** zimetolewa katika mitandao ya kijamii ya *facebook, instagram, youtube*, *twitter* na tovuti ya Wizara kuhusu masuala ya Sekta ya Ardhi. Katika mwaka wa fedha 2021/22, Wizara inatarajia kuandaa na kutekeleza Mkakati wa Mawasiliano utakaowezesha kuwa na utaratibu maalum wa kuhabarisha na kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala muhimu ya Sekta ya Ardhi na hivyo, kuongeza uelewa wa wananchi na wadau kuhusu huduma zinazotolewa.

## 6.0 SHUKRANI

***154.*** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kumalizia hotuba yangu kwa kumshukuru Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa maelekezo kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara yangu na Serikali kwa ujumla. Aidha, namshukuru Makamu wa Rais Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango kwa maelekezo aliyotoa kuhusu namna ya kuongeza ufanisi katika usimamizi wa shughuli za Serikali. Vilevile, namshukuru Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa miongozo na maelekezo yaliyowezesha kuboresha utendaji wa Wizara yangu.

***155.*** ***Mheshimiwa Spika****,* kipekee nakushukuru wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi thabiti katika kusimamia shughuli za Bunge. Kadhalika, naishukuru sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii inayoongozwa na Mhe. Aloyce Andrew Kwezi, Mbunge wa Kaliua, kwa maoni na ushauri wanaotoa katika kuboresha utekelezaji wa majukumu ya Wizara yangu. Aidha, nawashukuru kwa dhati Waheshimiwa Mawaziri, Naibu Mawaziri na Makatibu Wakuu kutoka katika Wizara mbalimbali tulioshirikiana katika utekelezaji wa majukumu ya Serikali. Napenda pia

kuwashukuru Wenyeviti wa Kamati mbalimbali za Bunge na Wabunge wote kwa michango, maoni na ushauri wenu tangu kuzinduliwa kwa Bunge hili la 12.

***156.*** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kutambua mchango mkubwa wa viongozi wenzangu katika kutekeleza majukumu ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Kipekee namshukuru Naibu Waziri, Mhe. Dkt. Angeline Sylvester Lubala Mabula, Mbunge wa Jimbo la Ilemela kwa kunisaidia katika kutekeleza majukumu ya Wizara hii. Aidha, natoa shukrani zangu za dhati kwa Katibu Mkuu Bibi Mary G. Makondo, Naibu Katibu Mkuu Bw. Nicholas M. Mkapa, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, Prof. Wakuru Magigi, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Nyumba la Taifa Dkt. Maulid Banyani na Kamishna wa Ardhi Bw. Nathaniel Nhonge, Mkuu wa Chuo cha Ardhi Tabora Bw. Biseko Musiba na Mkuu wa Chuo cha Ardhi Morogoro Bw. Huruma Lugalla kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara na Taasisi zake. Vilevile, napenda kuwashukuru Wakuu wa Idara na Vitengo pamoja na watumishi wote wa Wizara, kwa kuendelea kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii.

***157.*** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, napenda kuwashukuru wadau wote wa Sekta ya Ardhi wanaojumuisha Mamlaka za Upangaji, sekta binafsi na washirika wa maendeleo wa ndani na nje kwa michango yao katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Tunatambua na kuthamini michango inayotolewa na wadau hawa katika kuwezesha utekelezaji wa majukumu yetu kwa maslahi ya Watanzania.

***158.*** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda pia, kutoa shukrani za dhati kwa Wakuu wa Mikoa kwa kuendelea kutoa ushirikiano katika kuimarisha Ofisi za Ardhi za Mikoa. Aidha, napenda kuwashukuru wadau wote ikiwemo Taasisi za Fedha zilizowezesha upatikanaji wa mikopo ya ujenzi wa nyumba. Pia, nazishukuru taasisi binafsi na mamlaka mbalimbali tulizoshirikiana nazo katika kutekeleza majukumu ya Wizara zikiwemo Bodi za Kitaaluma za Wataalam wa Mipangomiji, Wathamini na Wapima Ardhi pamoja na wamiliki wa

kampuni za Upangaji na Upimaji. Vilevile, ninawashukuru wajumbe wa Kamati ya Ugawaji Ardhi, Baraza la Kitaifa la Ushauri wa Ardhi pamoja na Wenyeviti na Wajumbe wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya kwa ushirikiano wao katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

## 7.0 HITIMISHO

***159.*** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kuhitimisha kwa kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa katika mwaka wa fedha 2021/22, Wizara itaendelea kufanya mageuzi kwa kuboresha huduma zinazotolewa katika Sekta ya Ardhi kwa kuwekeza zaidi katika matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika utoaji wa huduma za ardhi na pia kuongeza kasi ya upangaji, upimaji na umilikishaji ardhi na udhibiti wa migogoro ya matumizi ya ardhi. **Mageuzi yanayokusudiwa yanalenga kupunguza gharama kwa wananchi, kuimarisha usalama wa milki za ardhi pamoja na kuongeza thamani ya ardhi na hivyo kukuza kipato kwa mwananchi mmoja mmoja na Pato la Taifa kwa ujumla.**

## 8.0 MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2021/22

### *Makadirio ya Mapato*

***160.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/22, Wizara inatarajia kukusanya shilingi **bilioni 260** kutokana na kodi, tozo na ada mbalimbali zinazotokana na shughuli za Sekta ya Ardhi kwa kutekeleza mikakati ambayo imeainishwa katika hotuba hii.

### *Makadirio ya Matumizi*

***161.*** ***Mheshimiwa Spika,*** ili Wizara yangu iweze kutekeleza majukumu niliyoyaeleza kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2021/22, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi (Fungu **48)** na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Fungu **03)** kama ifuatavyo:-

***Fungu 48: Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi***

| AINA | MAPATO | SHILINGI |
|---|---|---|
| A | Mapato ya Serikali | **260,000,000,000** |
| | **AINA YA MATUMIZI** | **FEDHA** |
| B | Matumizi ya Kawaida: | |
| | Mishahara | 34,079,748,000 |
| | Matumizi Mengineyo | 33,918,651,000 |
| | **Jumla Ndogo** | **67,998,399,000** |
| C | Matumizi ya Maendeleo: | |
| | Fedha za Ndani<br>Fedha za Nje | 18,300,000,000<br>11,250,299,000 |
| | **Jumla Ndogo** | **29,550,299,000** |
| | **JUMLA KUU (B+C)** | **97,548,698,000** |

Jumla ya matumizi ya kawaida na maendeleo shilingi **97,548,698,000/=**.

***Fungu 03: Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi***

| AINA | MAPATO | SHILINGI |
|---|---|---|
| A | Mapato | **706,000,000** |
| | **AINA YA MATUMIZI** | **FEDHA** |
| B | Matumizi ya Kawaida: | |
| | Mishahara | 1,497,066,000 |
| | Matumizi Mengineyo | 979,822,000 |
| | **Jumla Ndogo** | **2,476,888,000** |
| C | Matumizi ya Maendeleo: | |
| | Fedha za Ndani | 1,500,000,000 |
| | **Jumla Ndogo** | **1,500,000,000** |
| | **JUMLA KUU (B+C)** | **3,976,888,000** |

Jumla ya matumizi ya kawaida na maendeleo ni shilingi **3,976,888,000/=**.

***109.*** ***Mheshimiwa Spika,*** jumla kuu ya fedha zinazoombwa kwa Wizara (Fungu **48** na Fungu **03**) ili muweze kujadili na kuidhinisha ni shilingi
**101,525,586,000/=**.

***110.*** ***Mheshimiwa Spika,*** mwisho natoa shukrani zangu za dhati kwako binafsi na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Pamoja na hotuba hii yameambatishwa majedwali ambayo yameainisha kwa kina takwimu pamoja na shughuli zilizotekelezwa. Hotuba hii pia inapatikana kwenye tovuti ya Wizara ambayo ni ***www.lands.go.tz*****.**

***111.*** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Tutaendelea na utaratibu wetu.

Nikushukuru Mheshimiwa Waziri kwa hotuba hiyo. Nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii; namwona Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Dkt. Pius Chaya. *(Makofi)*

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii, napenda kuwasilisha Taarifa kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Fungu Namba 48 na Fungu Na.3, Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, kwa mwaka 2020/2021 pamoja na Maoni Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa afya na uhai alionijalia mimi pamoja na Wabunge wote wanaofuatilia wasilisho hili katika Mkutano huu wa Tatu wa Bunge la Kumi naMbili. Kabla ya kuendelea kutoa maoni nitangulie kuomba kuwa Taarifa yote iingizwe katika Kumbukumbu Rasmi za Bunge, kama ilivyowasilishwa Mezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni 2020, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Fungu 48 pamoja na Utekelezaji wa Majukumu ya Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, Fungu Na.3, kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Fungu 48 na Na.3 kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa msingi wa Taarifa hii ni majukumu ya Kamati kwa mujibu wa Kifungu cha 7A, cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, pamoja na Masharti ya Kanuni ya 118(4) ya Kanuni za Bunge. Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa uchambuzi huo ulifanyika baada ya ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotekelezwa na kusimamiwa na Wizara ya Ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 20 naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, kuhusu Utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa hii ina Sehemu kuu Tatu. Sehemu ya Kwanza ni utangulizi; Sehemu ya Pili inabainisha uchambuzi wa namna bajeti ya Wizara ya Ardhi,

Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka 2020/2021 ilivyotekelezwa na uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara kwa mwaka wa Fedha 2021/2022; na Sehemu ya Tatu inahusu mapendekezo ya Kamati na Hitimisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 137(1)(2) na Fasili ya 6(6)(a) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni 2020, Kamati hii ina jukumu la kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Katika kusimamia masuala ya kibajeti, Kamati imechambua Fungu 48 - Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Fungu 03 – ambalo ni Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi. Aidha, uchambuzi huu ulitanguliwa na ziara za ukaguzi wa miradi mbalimbali ya maendeleo chini ya mafungu yaliyotajwa hapo juu. Lengo lilikuwa ni kujiridhisha na ufanisi uliopo katika kutekeleza bajeti ya mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uchambuzi kuhusu Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka 2020/2021; katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, Fungu 48 - Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi iliidhinishiwa na Bunge bajeti ya shilingi bilioni 129.5 na baadaye kupata nyongeza ya Shilingi bilioni 1.9 na kufanya bajeti ya Wizara kuongezeka kuwa na jumla ya shilingi bilioni 131.5. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 47.4 ilitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 84 kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Katika bajeti ya maendeleo, shilingi bilioni 17.8 zilikuwa ni fedha za ndani na shilingi bilioni 66 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Machi, 2021 Wizara ilikuwa imepokea jumla ya shilingi bilioni 44.6 ikiwa ni sawa na asilimia 33.9 ya bajeti iliyoidhinishwa kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021. Kati ya fedha zilizopokelewa, shilingi bilioni 39 ni kwa ajili ya Matumizi ya kawaida sawa na asilimia 79 ya bajeti iliyotengwa kwa shughuli hiyo na shilingi bilioni tano sawa na 30.2% zilikuwa ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Katika Bajeti ya Maendeleo iliyopokelewa, shilingi bilioni tano sawa na 30.2% zilikuwa ni fedha za ndani.

Aidha, shilingi bilioni 66 ambazo zilikuwa ni fedha za nje na hazikupokelewa kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchanganuo wa uchambuzi kuhusu utekelezaji wa bajeti kwa kwa mwaka 2021 unapatikana katika jedwali Na.1 katika Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, Fungu Na.3 - Tume ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 4.6 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Hadi kufikia tarehe 15 Machi, 2021 Tume ilikuwa imepokea jumla ya shilingi bilioni mbili sawa na 43% ya fedha iliyoidhinishwa. Kwa upande wa bajeti ya maendeleo, Tume iliidhinishiwa shilingi bilioni 1.5 na hadi kufikia tarehe 15 Machi, 2021, Tume ilikuwa bado haijapokea fedha za maendeleo kwa ajili ya kuendelea na utekelezaji wa miradi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ina maoni kuwa mwenendo huu wa upatikanaji wa fedha unakwamisha kasi na viwango vya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ukusanyaji wa Maduhuli; katika mwaka wa Fedha 2020/2021, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ilijiwekea malengo ya kukusanya jumla ya shilingi bilioni 200. Hadi kufikia Machi, 2021, Wizara ilikuwa imekusanya shilingi bilioni 84 sawa na 42% ya malengo hayo. Kwa maelezo ya Wizara, kasi ndogo ya ukusanyaji wa maduhuli ilichangiwa na mwamko mdogo wa wananchi katika kulipa kodi ya pango la ardhi kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati haikuridhishwa na sababu zilizotolewa na Wizara kuhusu mwamko mdogo wa wananchi uliosababisha makusanyo kuwa hafifu. Hivyo, ni maoni ya Kamati kwamba Wizara haikujipanga vema kusimamia utekelezaji wa mikakati iliyojiwekea. Hii ni pamoja na kuhakikisha kuwa mfumo wa malipo kwa njia za kielektroniki unatumiwa vema kurahisisha malipo ya pango la ardhi na kodi ya majengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu Na.3 - Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi ilikuwa na lengo la kukusanya jumla ya shilingi milioni 906 katika Mwaka wa Fedha 2020/2021. Hadi kufikia tarehe 15 Machi, 2021, Tume ilikuwa imekusanya kiasi cha shilingi milioni 254 tu sawa na 28.1% ya malengo waliyojiwekea. Hali kadhalika Kamati haikuridhishwa na juhudi za Tume katika kukusanya mapato. Bila shaka upangaji wa malengo ya kiasi cha kukusanya hayakuakisi uhalisia wa vyanzo vya mapato vilivyopo. Uchambuzi wa mwenendo wa ukusanyaji wa mapato ya Wizara unapatikana katika Jedwali Na.2 la Taarifa ya Kamati hii.

*Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo; Kamati ilifanya ziara ya ukaguzi wa miradi hiyo katika Mikoa ya Iringa, Mbeya na Songwe kati ya tarehe 12 – 17 Machi, 2021. Miradi iliyofanyiwa ukaguzi wa utekelezaji wake ni kama ifuatavyo:-*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi Na. 2326 – Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi – Mbeya; Wizara iliipatia Halmashauri ya Jiji la Mbeya Sh.639,000,000 kwa ajili ya utekelezaji wa Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi. Jiji liliweka lengo la kupima viwanja 564 katika eneo la Mbeya *Peak*, mpaka sasa takribani viwanja 515 vimeuzwa kwa jumla ya Shilingi Bilioni 1.4. Aidha, kwa kutumia mkopo huu, Halmashauri ya Jiji la Mbeya imeweza kutekeleza Mradi mwingine wa kupanga, kupima na kumilikisha ardhi katika eneo la Iduda Mbeya, Mbeya Mjini. Kutokana na Mradi huu, Halmashauri inatarajia kupima jumla ya viwanja 522 vyenye thamani ya Shilingi Bilioni 2.5.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imeridhishwa na inaipongeza Halmashauri ya Jiji la Mbeya kwa kutumia mkopo huo kwa ufanisi katika kupanga, kupima na kumilikisha ardhi na kuweza kurejesha mkopo. Ni maoni ya Kamati kwamba halmashauri zingine zitaiga mfano huu na kuiweka miji yao katika mipango na umiliki ulio bora zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi Na.2 ni upangaji, upimaji na umilikaji ardhi Iringa. Halmashauri ya Manispaa ya Iringa ilipata kiasi cha Sh.418,000,000 kwa ajili ya kupima viwanja 375. Halmashauri ilipima na kuuza viwanja hivyo na kupata jumla ya Sh.765,000,000. Mauzo ya viwanja hivyo yameiwezesha halmashauri kufanya marejesho ya kiasi cha Sh.50,000,000/=tu kinyume na matarajio na makubaliano ya mkataba, ambapo Halmashauri ilipaswa kurejesha fedha zote za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa mradi huu katika Halmashauri ya Manispaa ya Iringa ni wa kusuasua kwa sababu maeneo mapya yaliyopimwa na halmashauri hayajawekea vivutio vya huduma za jamii. Hali kadhalika urejeshwaji wa mikopo Wizarani ni wa kusuasua kiasi cha kuathiri halmashauri nyingine zinazotaka kukopa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi Na.3 ni mradi wa kuimarisha mipaka ya Kimataifa. Mradi wa kuimarisha mipaka ya Kimataifa katika Wizara ya Ardhi unajielekeza katika kuimarisha mpaka wa Taifa kati ya Tanzania na Zambia, lakini Tunduma katika Mkoa wa Songwe. Mpaka huu una urefu wa kilometa 286 za nchi kavu na una urefu wa kilometa 56 ndani ya maji kwenye Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia mwezi Machi 2021, jumla ya alama za kati 78 ziliwekwa kwenye mpaka wenye urefu wa kilomita 11.9. Alama za kutenga eneo la hifadhi ya mpaka yaani *buffer zone* bado hazijawekwa kwa sababu ya athari za mlipuko wa *COVID-19* na kutokufanyika kwa vikao vya makubaliano ya pamoja kuhusu ukubwa wa eneo hili yaani *buffer zone* kati ya Maafisa wa Tanzania na Zambia kwa ajili ya kuandaa ramani za msingi na andiko la mpaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Ujenzi wa Nyumba za Gharama Nafuu kwa Shirika la Nyumba la Taifa *(NHC)*

Momba; Kamati ilipata fursa ya kutembelea Ujenzi wa nyumba za gharama nafuu Mkoa wa Songwe, Wilaya ya Momba. Kamati ina taarifa kwamba, Halmashauri ya Momba iliingia mkataba na Shirika la Nyumba la Taifa wa kujenga nyumba za gharama nafuu kwa kiasi cha shilingi Bilioni 2.1. Nyumba hizo zimekamilika na kukabidhiwa kwa halmashauri. Mpaka ukaguzi wa mradi huu ulipofanyika kiasi cha shilingi bilioni 1.7 kilikuwa kimerejeshwa. Mpaka sasa halmashauri inadaiwa na Shirika kiasi cha Sh.384,000,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kazi nzuri iliyofanywa na Shirika la Nyumba la Taifa ya ujenzi wa nyumba za gharama nafuu katika Halmashauri ya Momba na Halmashauri zingine pamoja na Taasisi mbalimbali za Serikali, bado shirika linapata changamoto ya kutolipwa fedha kwa wakati kutokana na Halmashauri na Taasisi hizo za Serikali kushindwa kurejesha madeni baada ya ukamilishwaji wa ujenzi na wapangaji kushindwa kulipa pango la nyumba za shirika. Shirika linadai jumla ya shilingi bilioni 2.1 kutoka katika halmashauri mbalimbali nchini na shilingi bilioni 6.0 kutoka taasisi mbalimbali za Serikali. Orodha ya Halmashauri na Taasisi za Kiserikali zinazodaiwa na Shirika zinapatikana katika kiambatisho Na.2 na Na.3 cha taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati wakati wa kuchambua Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021, Kamati ilishauri masuala mbalimbali yazingatiwe na Serikali. Kwa mfano:-

(a) Kamati ilishauri Serikali ifanye Mikakati ya kuitangaza Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi ili ijulikane na kutumiwa na taasisi mbalimbali nchini.

(b) Tume ya Matumizi Bora ya Ardhi iweke mikakati ya kuhakikisha kuwa vijiji vyote nchini vinapimwa;(c) Serikali iandae Mpango wa Miaka Minne ya awamu ya tano

iliyobaki na *program* hiyo iwasilishwe kwenye Kamati ili kuonesha mweleko wa matumizi bora ya ardhi nchini; na

(d) Serikali iharakishe mchakato wa kukamilisha Sera ya Taifa ya Nyumba itakayotoa mwongozo wa kusimamia sekta ya nyumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imeridhishwa na namna Serikali ilivyozingatia ushauri wake katika maeneo hayo. Ni maoni yetu kwamba juhudi na uwekezaji zaidi vitafanyika ili kuhakikisha kuwa ushauri wa Kamati unatekelezwa kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka 2021/2022; Makusanyo ya Maduhuli; katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, Fungu namba 48 - Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imepanga kukusanya jumla ya Sh.260,000,000,000. Kiwango hiki ni ongezeko la asilimia 26 ya makadirio ya makusanyo Mwaka wa Fedha unaoisha ambapo Wizara ilikadiria kukusanya Sh.200,000,000,000. Kamati imeridhishwa na sababu za ongezeko hili kuwa ni kutokana na kodi ya pango la ardhi, ada na tozo mbalimbali zinazohusiana na shughuli za Sekta ya Ardhi sanjari na juhudi za kuboresha Mfumo wa Malipo wa Kieletroniki zinazofanywa na Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande mwingine, Fungu Na.3 – Tume ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, imepanga kukusanya jumla ya Sh.706,000,000 pungufu ya asilimia 22 ya bajeti iliyopangwa kukusanywa mwaka 2020/2021. Kamati imeridhika na sababu zilizotolewa kuhusu upungufu huu kwamba ni baada ya kutathmini hali halisi ya vyanzo vya mapato vilivyopo na namna vinavyoweza kutozwa. Kamati inaamini kwamba, sekta ya ardhi ikisimamiwa ipasavyo, itachangia kwa sehemu kubwa katika kuongeza wigo wa kodi, kusaidia wananchi kupata dhamana za mikopo na kukuza pato la Taifa. Kwa mfano,

endapo mikakati iliyowekwa kwa mwaka 2021/2022, itasimamiwa ipasavyo inaweza kuinua mapato kwa kiasi kikubwa. Mikakati hiyo inajumuisha:-

(a) Kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa wamiliki wa ardhi kulipa kodi kwa wakati;

(b) Kuimarisha miundombinu ya TEHAMA na kusambaza mfumo wa kielektroniki katika Ofisi za Ardhi za Mikoa na Halmashauri; na

(c) Kusambaza hati za madai na kufuatilia malipo ya madeni kutoka kwa wadaiwa sugu na kuwafikisha mahakamani wale watakaokaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jedwali namba 2 kwenye taarifa ya kamati linaonesha mwenendo wa makusanyo ya Maduhuli ya Wizara kwa kipindi cha miaka miwili ya fedha, yaani 2020/2021 na 2021/2022. Hivyo basi, Wizara inapaswa kuhakikisha kwamba inatekeleza malengo yake ya ukusanyaji wa mapato ipasavyo na kuhakikisha kuwa inajiwekea malengo halisi na yanayotekelezeka kulingana na hali ya uchumi pamoja na mahitaji halisi ya matumizi ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Matumizi ya Kawaida; katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, Fungu 48 – Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi inaomba kuidhinishiwa shilingi bilioni 67.9 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ukilinganisha na shilingi bilioni 47.4 zilizopangwa katika Mwaka wa Fedha unaoisha. Ongezeko la kiasi cha Shilingi Milioni 505 ni kutokana na Watumishi wa Sekta ya Ardhi ambao awali walikuwa chini ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI ambao kwa sasa wamehamishiwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya Fedha inayoombwa, shilingi bilioni 34.0 ni kwa ajili ya mishahara ambayo imeongezeka kwa takriban asilimia 74.8 ukilinganisha na bajeti ya mishahara ya mwaka unaoisha, shilingi bilioni 33.9 inaombwa kwa ajili ya matumizi mengine yaani *OC* ikiwa ni

ongezeko la takribani asilimia 21.52. Sababu za ongezeko hili ni mahitaji halisi ya Wizara kwa sasa katika usimamizi wa Sekta ya Ardhi na Watumishi wa Sekta ya Ardhi ambao awali walikuwa chini ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI ambao kwa sasa wamehamishiwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu Na.3 – Tume ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi; kwa mwaka wa fedha 2021/2022 inaomba kuidhinishiwa shilingi bilioni 2.4 kwa ajili ya matumizi ya kawaida ikilinganishwa na kiasi cha shilingi bilioni 2.48 zilizotengwa kwa mwaka 2020/2021. Kati ya fedha za matumizi ya kawaida zinazoombwa kuidhinishwa, shilingi bilioni 1.49 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi milioni 979,000,000 ni kwa ajili ya matumizi mengine yaani *OC*. Jedwali Na.3 kwenye taarifa ya Kamati linaonesha mwenendo wa bajeti kwa Fungu 48 Kwa Mwaka 2020/2021 Na 2021/2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti ya Maendeleo, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, Fungu 48 – Wizara ya Ardhi, Nyumba na Makazi inaomba kuidhinishiwa shilingi bilioni 29.5 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ukilinganisha na shilingi bilioni 84.0 zilizoidihinishwa Mwaka wa Fedha 2020/2021. Hii ni sawa na pungufu la asilimia 64.2. Kati ya fedha inayoombwa, shilingi bilioni 18.3 ni fedha za ndani, ukilinganisha na shilingi bilioni 17.7 zilizoidhinishwa katika Mwaka wa Fedha unaoisha na shilingi bilioni 11.2 ni fedha za nje ukilinganisha na shilingi bilioni 66.3 zilizoidhinishwa katika Mwaka wa Fedha unaoisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maelezo ya Wizara, punguzo la bajeti ya Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 limesababishwa na kukosekana kwa fedha za miradi ya maendeleo kutoka nje kwa asilimia 100. Wizara imejikita na kuzingatia ushauri wa Kamati wa kutenga fedha zaidi za ndani kuliko za nje katika kukamilisha miradi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande mwingine, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, Fungu Na.3 Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi inaomba kuidhinishiwa kiasi cha shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya kutekeleza kazi za Mradi wa Upangaji wa Matumizi ya Ardhi. Kiasi hiki ni sawa na fedha zilizotengwa katika Mwaka wa Fedha unaoisha ambazo hazikutolewa ingawa majukumu yanayotarajiwa kutekelezwa bado ya umuhimu mkubwa. Majukumu hayo yanahusu kuratibu, kushauri, kuandaa, kukagua na kusambaza programu za mipango ya matumizi bora ya ardhi kwa uwiano baina ya Sekta kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Upangaji Matumizi ya Ardhi, Sura ya 116. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa niwasilishe maoni na ushauri wa Kamati. Kutokana na uchambuzi uliofanywa na Kamati, naomba kuwasilisha Maoni na Mapendekezo ya Kamati katika maeneo yafuatayo:-

(i) Mwenendo wa upatikanaji wa fedha zinazotengwa;

(ii) Ufanisi wa Wizara katika kukusanya Maduhuli;

(iii) Ufanisi wa mfumo wa kupanga, kupima na kumilikisha ardhi;

(iv) Ufanisi wa Mabaraza ya Ardhi ya Wilaya;

(v) Ufanisi wa Tume ya Taifa ya Mipango ya Ardhi;

(vi) Alama za Mipaka ya Nchi;

(vii) Sera ya Taifa ya Nyumba;

(viii) Sera ya Taifa ya Ardhi;

(ix) Mamlaka ya Kusimamia Sekta ya Ardhi;

(x) Ufanisi wa Shirika la Nyumba la Taifa; na

(xi) Madeni Sugu ya Wizara na Shirika la Nyumba la Taifa na eneo la mwisho utoaji wa vibali vya ardhi kwa wawekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maoni na Mapendekezo ya Kamati yanakusudia kuongeza ufanisi wa Wizara katika kutekeleza majukumu iliyojipangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muundo wa Bajeti na hali ya upatikanaji wa fedha; kwa kuwa kwa muda mrefu pamekuwapo na changamoto ya ucheleweshaji wa fedha za maendeleo kutoka Hazina kwenda Wizarani na mara nyingine kiasi kinachotolewa hakikidhi haja ya kukamilisha miradi iliyokusudiwa kutekelezwa; na kwa kuwa mwenendo huo unachangia kwa kiasi kikubwa udhaifu katika utekelezaji wa mipango ya Wizara. Kwa hiyo Kamati inaishauri Serikali kubuni mfumo endelevu ambao utahakikisha fedha kutoka Serikali kuu zinatoka kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili makusanyo ya Maduhuli; kwa kuwa Kodi ya Ardhi *(Land Rent)* ni miongoni mwa vyanzo madhubuti vya mapato ya Wizara; na kwa kuwa Halmashauri ndio Wakala anayetumika kukusanya kodi hiyo; kwa hiyo basi Kamati inaishauri Wizara ifanye yafuatayo ili kuchochea Halmashauri ziweze kukusanya kodi hiyo kikamilifu. Kamati inashauri kwamba:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iwaelimishe wananchi kuhusu umuhimu na ulazima wa kulipia pango la ardhi kwa wakati. Hatua hii iende pamoja na kuimarisha Ofisi za Ardhi za Mikoa na za Wilaya ili kwamba Wasajili walioko mikoani wawajibike kutoa hati katika wilaya zote nchini ili kuboresha na kupeleka huduma karibu na wananchi.

(b) Wizara ikamilishe kuingiza wateja wote kwenye mfumo wa kieletroniki sanjari na kuimarisha mfumo wa kutuma ankara za wadaiwa wa pango la ardhi na kodi ya majengo. Hatua hii itasaidia wananchi wengi kuweza kulipa pango la ardhi na kodi ya majengo kwa wakati, pasipo kuwa na usumbufu na itaongeza makusanyo ya maduhuli.

(c) Wizara iweke mikakati madhubuti ya kusimamia maafisa ardhi katika Halmashauri nchini na kuwawekea malengo yaani *targets* za makusanyo ambayo yatakuwa sehemu ya kipimo cha utendaji kazi wao.

(d) Gawio stahiki liwe linatolewa kwa wakati katika Mamlaka za Serikali za mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa Maendeleo, kwa kuwa kumekuwa na mwenendo usioridhisha wa kutotolewa fedha za maendeleo kwa wakati; na kwa kuwa hali hiyo inaathiri utekelezaji wa miradi ya maendeleo; Kamati inashauri kwamba, Wizara ya Fedha itoe kwa wakati na kwa ukamilifu ili Wizara iweze kutekeleza kwa ukamilifu Mpango wa Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mikopo kwa ajili ya kupanga, kupima na kumilikisha ardhi kwa Halmashauri; Kamati imebaini kwamba ingawa mfumo wa kukopesha halmashauri fedha kwa ajili ya kupanga, kupima na kumilikisha ardhi umekuwa na changamoto kadhaa, lakini bado Kamati inaona ni mfumo sahihi na endelevu wa kuongeza kasi ya kupanga maeneo ya nchi. Hivyo, kamati inashauri yafuatayo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kuongeza Idadi ya halmashauri zinazopaswa kukopeshwa mfano kutoka halmashauri 24 mpaka 50 kwa mwaka na kuweka utaratibu wa kutathmini sifa za halmashauri zinazopaswa kukopeshwa.

(b) Kuelekeza Halmashauri zote nchini kupitia Wizara ya TAMISEMI kutenga bajeti za kuandaa angalau mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji sita kila mwaka. Hii itaongeza kasi ya uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi kufikia vijiji 810 kwa mwaka katika halmashauri angalau135 zilizoko nchini.

(c) Kuzijengea uwezo Halmashauri za Wilaya zote Nchini katika upimaji, uandaaji, utekelezaji na usimamizi wa mipango ya matumizi ya ardhi.

(d) Kutoa elimu kwa mamlaka za upangaji nchini kutumia teknolojia za kisasa na rahisi katika uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi mfano utumiaji wa picha za angani.

(e) Mheshimiwa Naibu Spika, kukamilisha na kusimika mfumo wa Kielekroniki yaani *Intergrated Land Management Information Systems* kwa utunzaji wa kumbukumbu za taarifa za mipango ya matumizi ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupanga na Kupima Vijiji Miji yaani *Emerging Towns;* kwa kuwa mpaka sasa ni asilimia 25 tu ya ardhi ya Tanzania imepimwa na kuna wimbi kubwa la ukuaji wa vijiji kuwa miji yaani *Emerging Towns* kutokana na ongezeko la miundombinu mfano barabara za lami, umeme na kadhalika; na kwa kuwa, ongezeko hilo limepelekea ongezeko la makazi bora kwenye makao makuu ya kata hapa nchini; na kwa kuwa, Kamati haikuridhishwa na kasi ya uandaaji mipango ya upangaji wa matumizi ya ardhi ya vijiji 169 kwa mwaka. Kamati inashauri yafuatayo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri ili kuhakikisha vijiji vyote vimepimwa Tume iongeze kasi ya utendaji kazi kwa kuongeza idadi ya vijiji vinavyotakiwa kupimwa kwa mwaka. Kutekelezwa kwa ushauri huu kutasaidia kuondoa migogoro ya ardhi inayoendelea nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia Ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020, maelekezo ya Serikali na utekelezaji wa miradi ya kimkakati, wastani wa vijiji 826 vinapaswa kuandaliwa mipango ya matumizi ya ardhi kwa mwaka. Kwa idadi hiyo ya vijiji 826 kwa mwaka itachukua takribani miaka 12 kukamilisha zoezi la kupima na kupanga matumizi ya ardhi ya vijiji vyote nchini. Hivyo Kamati inaishauri Serikali kuja na Mikakati Madhubuti ili kuweza kuendana na kasi na kufikia lengo lililopo kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi, ukurasa119.

(b) Wizara kuelekeza nguvu kubwa kwenye kupanga, kupima na kurasimisha Vijiji-Miji ili kupunguza migogoro ya ardhi, kuongeza wigo wa kodi na kuwapatia fursa wananchi wa kuwa na hati miliki za makazi. Kwa kufanya hivyo, kutapelekea ongezeko la eneo kubwa la nchi hii kupimwa na kutoka asilimia zilizopo sasa 25 angalau kufikia asilimia 50.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mabaraza ya Ardhi ya Wilaya; Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto kubwa za kiuendeshaji wa mabaraza ya ardhi na nyumba ya Wilaya na yale ya Kata kwa kuwa yanasimamiwa na mamlaka mbili tofauti. Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya yanasimamiwa na Wizara ya Ardhi wakati yale ya kata yanasimamiwa na Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Hali hii inachangia kuzorotesha utoaji wa haki katika mashauri ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kwa kuwa Wenyeviti wa Mabaraza ya Wilaya ni wataalam wa sheria wakati wale wa Mabaraza ya Kata ni watu wasio na taaluma ya sheria, hali hiyo inasababisha mashauri mengi yaliyosuluhishwa katika Mabaraza ya Kata kukatiwa rufaa kwenda kwenye Mabaraza ya Wilaya kutokana na taratibu nyingi kukiukwa. Kamati inashauri:-

(a) Serikali kuyahamishia Mabaraza yote ya Ardhi chini ya usimamizi wa mamlaka moja, mfano, Wizara ya Ardhi ili kuboresha utendaji wake;

(b) Serikali iweke utaratibu maalum wa kuzingatia weledi na uzoefu zaidi wa kuwapata Wajumbe wa Mabaraza ya Kata kuliko utaratibu uliopo sasa;

(c) Wenyeviti wa Mabaraza ya Wilaya wapewe mikataba ya ajira za kudumu kuliko utaratibu wa sasa wa ajira za mkataba ili waweze kuwa na ari ya kufanya kazi na kutenda haki;

(d) Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya yaanzishwe katika kila wilaya nchini. Vile vile, Wizara ya Ardhi iwekeze zaidi katika Mabaraza yanayotembea yaani *mobile tribunals* ili kuwafikia wananchi wengi kwenye Vijiji na Kata; na

(e) Kuweka mifumo mizuri ya uendeshaji wa Mabaraza ya Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi ili kupunguza na kuondoa rushwa inayoathiri haki za wananchi hususani wanawake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi; Kamati inatambua Tume ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi ipo kwa mujibu wa Sheria ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi Na.6 ya mwaka 2007, Sura 116. Hata hivyo, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa bado Tume hii haijulikani sana utendaji wake hapa Tanzania. Kulingana na hili Kamati inashauri mambo yafuatayo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ihuishe upya muundo wa Tume ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi ikiwa sanjari na kuipa nguvu ya Kuwa Mfuko wa Upangaji Ardhi Tanzania wa kutafuta fedha ili iongeze kasi ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi na kufikia malengo ya Mpango wa tatu wa Maendeleo ya Taifa na yale ya Maendeleo Endelevu ya Kidunia *(SDGs)*;

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti ya Tume ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi iongezwe na fedha inayoidhinishwa itolewe kwa wakati;

(c) Tume hii iongezewe wafanyakazi na vitendea kazi ili kukidhi mahitaji ya majukumu waliyonayo; na

(d) Tume iboreshe utekelezaji wa majukumu yake hususani kwenye uratibu yaani *coordination* ya wadau wote wanaoandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi ili kulinda ubora na ufanisi wa mipango ya matumizi ya ardhi inayotekelezwa na wadau.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Uimarishaji wa Mipaka Tanzania; suala la uimarishaji wa mipaka ya nchi yetu ni suala muhimu sana kwa mustakabali wa ulinzi na usalama na diplomasia ya kimataifa. Suala hili ni mtambuka na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imepewa jukumu la kiutendaji katika masuala yanayohusu miundombinu. Hata hivyo, Kamati imebaini kwamba utekelezaji wa mradi huu una changamoto nyingi ambapo Wizara hii peke yake haiwezi kuzimaliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri kwamba, Wizara ya Ardhi kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, pamoja na vyombo vya ulinzi na usalama, ifanye jitihada za kutatua changamoto zilizopo kwa sababu ya uhusiano mzuri baina ya nchi yetu na Mataifa ambayo tunapakana nayo unahitajika. Bila kuwa na makubaliano katika ngazi za juu, Wizara hii haitaweza kuwa na uwezo wa kuimarisha mipaka ya nchi yetu kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera ya Nyumba ya Taifa *(National Housing Policy)*, Kamati ina taarifa kuwa Sera ya Taifa ya Nyumba ipo kwenye mchakato kwa kipindi kirefu. Hata hivyo, bado Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Ardhi iharakishe uanzishwaji wa Sera ya Taifa ya Nyumba ili kusaidia kuweka bei elekezi kwa uuzwaji na ujenzi wa nyumba kwa ngazi ya kila Mkoa, Wilaya, kwa kuwa bei elekezi za ujenzi, kwa kuwa bei elekezi za ujenzi hutofautiana kwa kila wilaya na eneo. Sanjari na hilo Kamati inaona kuwa Sera hii itasaidia Wizara kuwa na bei elekezi kwenye ujenzi wa nyumba na hata kuleta tija kwa wananchi na wanunuzi

wa nyumba hizo kwa kuwa kutakuwa na Mwongozo unaongoza Wizara kwenye masuala ya nyumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera ya Taifa ya Ardhi; kwa kuwa Wizara imekuwa kwenye mchakato wa muda mrefu kupitia Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995; na kwa kuwa Sera hiyo ina umuhimu mkubwa sana katika suala zima la usimamizi wa maendeleo ya ardhi na makazi; Kamati inashauri Serikali kukamilisha haraka mapitio ya Sera hiyo. Kwa kufanya hivyo kutasaidia kutoa miongozo sahihi na yenye tija katika eneo la kupanga, kupima na kumilikisha ardhi kuendana na mahitaji ya sasa ya ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Madeni Sugu na Wadaiwa Sugu, Kamati imebaini kuwepo kwa taasisi na halmashauri mbalimbali zinazodaiwa na Shirika la Nyumba la Taifa, mfano, Halmashauri ya Momba, Halmashauri ya Monduli, Halmashauri ya Mbarali, Halmashauri ya Mvomero, Halmashauri ya Uyui na Halmashauri ya Muheza. Kwa kuwa Shirika la Nyumba la Taifa linajiendesha kibiashara kwa kufanya kandarasi mbalimbali na kupangisha nyumba kwa wananchi, Halmashauri na Taasisi mbalimbali nchini; na kwa kuwa mpaka sasa Shirika limekuwa na likipata changamoto ya kutolipwa madeni kwa wakati katika Halmashauri na Taasisi mbalimbali zilivyoorodheshwa katika viambatisho Na.2 na Na.3, jambo ambalo linapekelea kukwamisha maendeleo ya shirika. Kamati inashauri kuwa Halmashauri na taasisi zote zinazodaiwa na Shirika la Nyumba kulipa madeni hayo ili kuliwezesha Shirika kujiendesha kibiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Wizara ya Ardhi imekuwa ikitoa mikopo isiyokuwa na riba kwa halmashauri mbalimbali ili kuongeza kasi ya kupima ardhi, pia Wizara imekuwa ikidai taasisi mbalimbali za Serikali kodi ya pango la ardhi; na kwa kuwa hadi sasa kuna baadhi ya Halmashauri na Taasisi za Serikali zimeshindwa kurejesha mikopo na kodi hizo kwa wakati zikiwemo Halmashauri za Mji Mdogo wa Nzega, Wilaya ya Nzega, Halmashauri ya Sumbawanga, Halmashauri ya Wilaya ya Gairo, Halmashauri ya Wilaya ya

Sengerema, Mji Mdogo wa Kondoa na Manispaa ya Iringa. Kiambatanisho Na.1 na Na.4.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Serikali kusimamia halmashauri zote kurejesha mikopo kulingana na makubaliano waliyojiwekea kwenye kikao cha Kamati ya pamoja ya Ardhi, Maliasili na Utalii pamoja na Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, maboresho ya Shirika la Nyumba la Taifa; kwa kuwa Shirika la Nyumba la Taifa limejikita kujenga nyumba kwa mfumo wa ama kuuza au kupangisha katika maeneo mbalimbali hapa nchini; na kwa kuwa kumekuwa na malalamiko juu ya bei za nyumba kuwa juu na baadhi ya nyumba kujengwa maeneo ambayo hayavutii wapangaji na wanunuzi na baadhi ya nyumba kuwa na ukubwa usioridhisha; Kamati inapendekeza yafuatayo:-

(a) Shirika kushirikiana na taasisi mbalimbali zikiwemo za maji, umeme na barabara ili kupunguza gharama za ujenzi wa kujenga nyumba kwenye maeneo ambayo huduma hizo zimepelekwa;

(b) Serikali kuangalia uwezekano wa kulipunguzia Shirika la Nyumba mzigo wa kodi kwenye vifaa vya ujenzi. Hatua hii itasaidia Shirika kujenga nyumba za bei nafuu (*affordable houses*);

(c) Nyumba za gharama nafuu (*affordable houses*) za shirika zinazojengwa katika halmashauri mbalimbali nchini zijengwe kwenye maeneo ambayo ni rahisi kuuzika na kupangishwa kwa wananchi; na

(d) Kwa kuwa Shirika limeonesha ufanisi mkubwa katika kutekeleza miradi mbalimbali ya ujenzi wa nyumba, Serikali iendelee kulipatia kandarasi za ujenzi wa nyumba nchini ili kuliwezesha shirika kujiendesha kibiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Kusimamia Sekta ya Ardhi (*Real Estate Regulatory Authority - RERA*); kwa kuwa kumekuwa na wimbi kubwa na ulaghai kwenye sekta ya soko la ardhi na nyumba kutokana na kukosekana kwa mamlaka ya kutoa miongozo ya bei ya viwanja nyumba na viwango mbalimbali; na kwa kuwa hali hii imeleta taharuki kwenye soko la ardhi na nyumba hususan kwenye biashara ya upangishaji wa nyumba inayosababishwa na utitiri wa madalali ambao hawana usimamizi na hawalipi kodi; Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha mamlaka ya usimamizi wa sekta ya ardhi na nyumba hususan kwenye biashara (*Real Estate Regulatory Authority – RERA*) nchini inaundwa haraka ili kusaidia katika kusimamia viwango vya sekta ya ardhi na nyumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, utoaji wa vibali vya kumiliki ardhi kwa wawekezaji; Kamati imebaini kuwa bado mfumo wa kutoa ardhi kwa wawekezaji wa ndani na nje unapitia changamoto nyingi zikiwemo za mlolongo mrefu wa taratibu za kupata ardhi na huduma ambazo hazipatikani katika ofisi moja. Kwa kuwa azma ya Serikali ya Awamu ya Sita kwa sasa ni kufungua wigo na fursa za uwekezaji kwa wazawa na wageni; hivyo Kamati inaishauri Wizara ihuishe na kuweka utaratibu rafiki wa upatikanaji wa ardhi kwa wawekezaji sanjari na kuondoa milolongo na urasimu usio wa lazima. Lengo ni kuifanya nchi yetu kuwa rafiki kwa wawekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho; napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi kwa ajili ya kuwasilisha taarifa hii. Kwa niaba ya Kamati napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao yaliyoorodheshwa kwenye taarifa hii yaingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard).*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kutumia fursa hii kumshukuru Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi, Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Angeline Sylvester Lubala Mabula, Katibu Mkuu Ndugu Mary Gasper

Makondo, Naibu Katibu Mkuu Ndugu Nicholas Mkapa pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano na mchango wao katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya kikanuni ya Kamati.

**NAIBU SPIKA:** Makamu Mwenyekiti kwa kuwa kengele ya pili imeshagonga, unga mkono hoja.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu lipokee taarifa hii ili lijadili na kukubali na kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

## TAARIFA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

### SEHEMU YA KWANZA

### 1.0 UTANGULIZI

#### 1.1 *Maelezo ya Awali*

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni 2020, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa fedha 2020/2021, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu makadirio ya mapato

na matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

1.2 ***Muundo wa Taarifa***

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa hii ina sehemu kuu Tatu. Sehemu ya kwanza ni utangulizi, sehemu ya pili inabainisha uchambuzi wa namna bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka 2020/2021 ilivyotekelezwa na, uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara kwa mwaka wa Fedha 2021/2022. Sehemu ya Tatu inahusu mapendekezo ya Kamati na Hitimisho.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 137(1) (2) na Fasili ya 6 (6) (a) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni 2020, Kamati hii ina jukumu la kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Katika kusimamia masuala ya kibajeti, Kamati imechambua **Fungu 48** - Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na **Fungu 03** – ambalo ni Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi. Aidha, uchambuzi huu ulitanguliwa na ziara za ukaguzi wa miradi mbalimbali ya maendeleo chini ya mafungu yaliyotajwa hapo juu. Lengo lilikuwa ni kujiridhisha na ufanisi uliopo katika kutekeleza bajeti ya mwaka 2020/ 2021.

**SEHEMU YA PILI**

**2.0 UCHAMBUZI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA 2020/2021**

2.1 ***Hali ya Upatikanaji wa Fedha***

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2020/ 2021, **Fungu 48 -** Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi iliidhinishiwa na Bunge bajeti ya **shilingi bilioni 129,579,479,000** na badae kupata nyongeza ya **Shilingi bilioni 1,917,662,031.85** na kufanya bajeti ya Wizara kuongezeka kuwa na jumla ya **shlingi bilioni 131,497,141,031.85**. Kati ya fedha hizo, **shilingi bilioni 47,408,779,999** ilitengwa kwa ajili ya

matumizi ya kawaida na **shilingi bilioni 84,088,361,032** kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Katika bajeti ya maendeleo, **shilingi bilioni 17,787,522,032** zilikuwa ni fedha za ndani na shilingi **bilioni 66,300,839,000** ni fedha za nje.

Hadi kufikia Machi, 2021 Wizara ilipokea jumla ya **shilingi bilioni 44,642,406,211** ikiwa ni sawa na **asilimia 33.9** ya bajeti iliyoidhinishwa kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021. Kati ya fedha zilizopokelewa, **shilingi bilioni 39,266,711,047** ni kwa ajili ya Matumizi ya kawaida sawa na **asilimia 76.65** ya bajeti iliyotengwa kwa shughuli hiyo na shilingi **bilioni 5,375,695,164** sawa na **30.2%** zilikuwa ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Katika Bajeti ya Maendeleo iliyopokelewa, **shilingi bilioni 5,375,695,164** sawa na 30.2% zilikuwa ni fedha za ndani. Aidha, shilingi **bilioni 66,300,839,000** ambazo zilikuwa ni fedha za nje na hazikupokelewa kabisa.

Jedwali lifuatalo linaonesha mwenendo wa upatikanaji wa fedha wa Fungu 48 kwa Mwaka 2020/ 2021.

**Jedwali Na.1: Mwenendo wa Upatikanaji wa Fedha**

| UPATIKANAJI WA FEDHA FUNGU 48 KWA MWAKA 2020/2021 | | | |
|---|---|---|---|
| MATUMIZI | KILICHOIDHINISHWA PAMOJA NA NYONGEZA | KILICHOPOKELEWA | ONGEZEKO/PUNGUFU ASILIMIA |
| MISHAHARA | 19,496,335,000.00 | 20,416,369,380.84 | 4.7 |
| OC | 27,912,444,999.85 | 18,850,341,666.64 | 32.4 |
| MAENDELEO NDANI | 17,787,522,032.00 | 5,375,695,164.00 | 30.2 |
| MAENDELEO NJE | 66,300,839,000.00 | 0.00 | 0 |
| **JUMLA** | **131,497,141,031.85** | **44,642,406,211.48** | **33.9** |

**Chanzo**: Randama za Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2020/21 na 2021/22

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, **Fungu 03 - Tume ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi** iliidhinishiwa jumla ya **shilingi bilioni 4,664,768,000** kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Hadi kufikia tarehe 15 Machi, 2021 Tume ilipokea jumla ya **shilingi bilioni 2,011,950,150** sawa na **43%** ya fedha iliyoidhinishwa. Kwa upande wa bajeti ya maendeleo, Tume iliidhinishiwa **shilingi bilioni 1,500,000,000** na hadi kufikia tarehe 15 Machi, 2021 Tume ilikuwa bado haijapokea fedha za maendeleo kwa ajili ya kuendelea na utekelezaji wa miradi yake.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ina maoni kuwa mwenendo huu wa upatikanaji wa fedha unakwamisha kasi na viwango vya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Upungufu huu wa kibajeti unaifanya Tume ishindwe kutekeleza majukumu yake ya msingi. Kwa mfano, kuhuisha Mpango wa Taifa wa Matumizi ya Ardhi wa mwaka 2013 – 2033. Vilevile, kuandaa Mipango ya Kanda ya Matumizi ya Ardhi, Mipango ya Ardhi ya Wilaya na kuratibu uandaaji wa mipango ya ardhi ya vijiji katika vijiji vyote nchini.

1.1 ***Ukusanyaji wa Maduhuli***

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa Fedha 2020/2021 Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ilijiwekea malengo ya kukusanya jumla ya **shilingi bilioni 200,000,000,000**. Hadi kufikia Machi, 2021 Wizara ilikuwa imekusanya **shilingi bilioni 84,000,000,000** sawa na **42%** ya malengo hayo. Kwa maelezo ya Wizara, kasi ndogo ya ukusanyaji wa maduhuli ilichangiwa na mwamko mdogo wa wananchi kulipa kodi ya pango la ardhi kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati haikuridhishwa na sababu zilizotolewa na Wizara kuhusu mwamko mdogo wa Wananchi uliosababisha makusanyo kuwa hafifu. Hivyo, ni maoni ya Kamati kwamba Wizara haikujipanga vema kusimamia utekelezaji wa

mikakati iliyojiwekea. Hii ni pamoja na kuhakikisha kuwa mfumo wa malipo kwa njia za kielektroniki unatumiwa vema kurahisisha malipo ya pango la ardhi na kodi ya majengo.

**Msheshimiwa Spika, Fungu 03 - Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi** ilikuwa na lengo la kukusanya jumla ya **shilingi milioni 906,000,000,** katika Mwaka wa Fedha 2020/2021. Hadi kufikia tarehe 15 Machi, 2021, Tume ilikuwa imekusanya kiasi cha **shilingi milioni 254,652,874.96** sawa na **28.1%** ya malengo waliyojiwekea. Hali kadhalika Kamati haikuridhishwa na juhudi za Tume katika kukusanya mapato. Bila shaka upangaji wa malengo ya kiasi cha kukusanya hayakuakisi uhalisia wa vyanzo vya mapato vilivyopo.

### 1.2 *Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo*

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya ziara ya ukaguzi wa miradi hiyo katika mikoa ya Iringa, Mbeya na Songwe kati ya tarehe 12 – 17 Machi, 2020. Miradi iliyofanyiwa ukaguzi wa utekelezaji wake ni hii ifuatayo:-

#### 1.2.1 Mradi Na. 2326 – Kupanga, kupima na Kumilikisha Ardhi (KKK) Mkoa wa Mbeya

**Mheshimiwa Spika**, Wizara iliipatia Halmashauri ya Jiji la Mbeya shilingi 639,973,000 kwa ajili ya utekelezaji wa Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi. Jiji liliweka lengo la kupima viwanja 564 katika eneo la Mbeya Peak. Mpaka sasa takribani viwanja 515 vimeuzwa kwa jumla ya Shilingi 1,453,683,813.62. Aidha, kwa kutumia mkopo huu, Halmashauri ya Jiji la Mbeya imeanza kutekeleza Mradi mwingine wa kupanga, kupima na kumilikisha ardhi katika eneo la Iduda Mbeya mjini. Kutokana na Mradi huu, Halmashauri inatarajia kupima Jumla ya Viwanja 522 vyenye thamani ya Shilingi 2,500,000,000.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imeridhishwa na inaipongeza Halmashauri ya Jiji la mbeya kwa kutumia mkopo huo kwa ufanisi katika Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi na kuweza kurejesha mkopo. Ni maoni ya Kamati kwamba Halmashauri zingine zitaiga mfano huu na kuiweka miji yao katika mipango na umiliki ulio bora zaidi na kwa kufanya hivyo kutapekelea Halmashauri kutatua migogoro ya ardhi kwa wananchi, wananchi kuwa na dhamana ya mikopo na upatikanaji wa huduma za jamii.

### 1.2.2 Mradi Na. 2326 – Upangaji, Upimaji na Umilikaji Ardhi Iringa

**Mheshimiwa Spika**, Halmashauri ya Manispaa ya Iringa ilipata kiasi cha Shilingi **418,100,000** kwa ajili ya kupima viwanja 375. Halmashauri ilipima na kuuza viwanja hivyo na kupata jumla ya Tshs 765,631,000 mauzo ya viwanja hivyo yameiwezesha Halmashauri kufanya marejesho ya kiasi cha shilingi 100,000,000/=tu Kwa Wizara, kinyume na matarajio na makubaliano ya mkataba.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kwamba, Halmashauri ya Manispaa ya Iringa baada ya kuuza na kupata faida ya mradi huu ilitumia fedha hizi katika kupanga, kupima na kumilikisha ardhi maeneo mengine mkoani humo ambayo hayakuweza kuuzika kwa haraka. Hivyo basi, Kamati inazishauri Halmashauri zote kupima na kumilikisha ardhi maeneo ambayo yanauzika kwa haraka zaidi (Hotspots) ili kuharakisha zoezi na kasi ya umilikishaji.

**Mheshimiwa Spika,** Aidha, kamati ina taarifa kuwa ya kati ya Halmashauri 24 zilikopeshwa fedha na Wizara kwaajili ya kupanga, kupima na kumilikisha ardhi (KKK) ni Halmashauri 7 tu ndizo zilizoweza kurejesha fedha zote kwa Wizara na Halmashauri 17 kati ya hizo Halmashauri 13 zilirejesha kidogo na 4 hazikurejesha kabisa, sababu zilizotolewa ni pamoja

na halmashauri hizo kutumia fedha hizo kupima maeneo yasiyouzika kwa uharaka hivyo kupekelea kushindwa kurejesha fedha kwa Wizara. Kamati inaona ucheleweshwaji wa marejesho hayo unapelekea halmashauri zingine zinazohitaji mkopo huo na zipo tayari kurejesha kushindwa kupatiwa fedha hizo. **Kiambatisho Na.1** ni orodha ya Halmashauri zilizokopeshwa na mwenendo wa marejesho.

### 1.2.3 Mradi Na. 2324 – Kuimarisha Mipaka ya Kimataifa

**Mheshimiwa Spika**, Mradi Na. 2324 unajielekeza katika Kuimarisha Mpaka wa Kimataifa wa Tanzania na Zambia, Tunduma katika Mkoa wa Songwe. Mpaka huu una urefu wa kilometa 286 za nchi kavu na una urefu wa kilometa 56 ndani ya maji kwenye Ziwa Tanganyika.

Hadi kufikia Mwezi Machi 2021, jumla ya alama za kati 78 ziliwekwa kwenye mpaka wenye urefu wa kilomita 11.9. Alama za kutenga eneo la hifadhi ya mpaka (buffer zone) bado hazijawekwa kwa sababu ya athari za Mlipuko wa COVID-19 na kutokufanyika kwa vikao vya makubaliano ya pamoja kuhusu ukubwa wa eneo huru (Buffer Zone) kati ya Maafisa wa Tanzania na Zambia kwa ajili ya kuandaa ramani za msingi na andiko la mpaka.

### 1.2.4 Mradi wa Ujenzi wa nyumba za Gharama Nafuu wa Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), Momba.

**Mheshimiwa Spika,** Shirika la Nyumba la Taifa limekuwa likitekeleza kandarasi za ujenzi wa majengo mbalimbali nchini. Miradi yote inayotekelezwa na inayoendelea kutekelezwa sehemu mbalimbali nchini imekuwa na viwango vizuri na vyenye ubora. Baadhi ya miradi inayoendelea kutekelezwa ni kama ujenzi

wa jengo la TMDA-Dodoma, ujenzi wa jengo la makao makuu ya Wizara ya Fedha na mipango- Dodoma na Mradi wa mpango kabambe wa Matumizi ya Ardhi ya chuo Kikuu cha Dodoma.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipata fursa ya kutembelea Ujenzi wa nyumba za gharama nafuu Mkoa wa Songwe, Wilaya ya Momba. Kamati inataarifa kwamba, Halmshauri ya Momba iliingia mkataba na Shirika la Nyumba la Taifa wa kujengea nyumba za Gharama nafuu kwa shilingi Bilioni 2,175,813,800.Nyumba hizo zimekamilika na kukabidhiwa kwa halmashauri. Mpaka ukaguzi wa mradi huu ulipofanyika kiasi cha shilingi 1,790,934,870 kilikuwa kimerejeshwa. Mpaka sasa Halmashauri inadaiwa na Shirika kiasi cha shilingi 384,878,929.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na kazi nzuri iliyofanywa na Shirika la Nyumba la Taifa ya ujenzi wa Nyumba za gharama nafuu katika Halmashauri ya Momba na Halmashauri zingine pamoja na Taasisi mbalimbali za Serikali. Shirika linapata changamoto ya kutolipwa fedha kwa wakati kutokana na Halmashauri na Taasisi hizo za Serikali kushindwa kurejesha madeni baada ya ukamilishwaji wa ujenzi na wapangaji kushindwa kulipa pango la nyumba za shirika. Shirika linadai jumla ya shilingi bilioni **2,111,127,875** kutoka Halmashauri mbalimbali nchini na shilingi bilioni **6,093,517,041.45** kutoka Taasisi mbalimbali za Serikali. **Kiambatisho Na.2,3** ni taarifa ya Halmashauri na Taasisi Mbalimbali zinazodaiwa na shirika la Nyumba.

### 1.2.5 Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kuchambua Mpango wa Maendeleo na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Kamati ilishauri masuala mbalimbali ili yazingatiwe na Serikali. Kwa mfano:-

a) Kamati ilishauri Serikali ifanye Mikakati ya kuitangaza Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi ili ijulikane na kutumiwa na taasisi mbalimbali nchini.

b) Tume ya Taifa Matumizi ya Ardhi iweke mikakati ya kuhakikisha kuwa Vijiji vyote nchini vinapimwa.

c) Serikali iandae Mpango wa Miaka Minne ya awamu ya tano iliyobaki na program hiyo iwasilishwe kwenye Kamati ili kuonesha mweleko wa matumizi bora ya ardhi nchini.

d) Serikali iharakishe mchakato wa kukamilisha Sera ya Taifa ya Nyumba itakayotoa mwongozo wa kusimamia Sekta ya Nyumba.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imeridhishwa na namna Serikali ilivyozingatia Ushauri wake katika maeneo hayo. Ni maoni yetu kwamba juhudi na utekelezaji zaidi vitafanyika ili kuhakikisha kuwa ushauri wa Kamati inatekelezwa kikamilifu.

## 1.3 *Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara 2021/2022.*

### 1.3.1 Makusanyo ya Maduhuli

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 Fungu 48 - Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imepanga kukusanya jumla ya **shilingi bilioni 260,000,000,000**. Kiwango hiki ni ongezeko la **26%** ya makadirio ya makusanyo Mwaka wa Fedha unaoisha ambapo Wizara ilikadiria kukusanya **shilingi bilioni 200,000,000,000**. Kamati imeridhishwa na sababu za ongezeko hili kuwa ni

kutokana na kodi ya pango la ardhi, ada na tozo mbalimbali zinazohusiana na shughuli za Sekta ya Ardhi pamoja na juhudi za kuboresha mfumo wa malipo wa kieletroniki zinazofanywa na Wizara.

Kwa upande mwingine, **Fungu 03 – Tume ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi** imepanga kukusanya jumla ya **shilingi milioni 706,000,000** pungufu ya **22%** ya bajeti iliyopangwa kukusanywa kwa mwaka 2020/2021. Kamati imeridhika na sababu zilizotolewa na Wizara kuhusu upungufu huu kwamba ni baada ya kutathmini hali halisi ya vyanzo vya mapato vilivyopo na namna vinavyoweza kutozwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaamini kwamba, sekta ya ardhi ikisimamiwa ipasavyo, itachangia kwa sehemu kubwa katika kuongeza wigo wa kodi, kusaidia wananchi kupata dhamana za mikopo na kukuza pato la taifa. Kwa mfano endapo mikakati iliyowekwa kwa mwaka 2021/22 itasimamiwa ipasavyo inaweza kuinua mapato kwa kiasi kikubwa. Mikakati hiyo inajumuisha:

a) Kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa wamiliki wa ardhi kulipa kodi kwa wakati;

b) Kuimarisha miundombinu ya TEHAMA na kusambaza mfumo wa kielektroniki katika Ofisi za ardhi za mikoa na halmashauri; na

c) Kusambaza hati za madai na kufuatilia malipo ya madeni kutoka kwa wadaiwa sugu na kuwafikisha mahakamani kwa wale watakaokaidi.

Jedwali lifuatalo linaonesha mwenendo wa Makusanyo ya Maduhuli ya Wizara kwa kipindi cha miaka miwili ya fedha; yaani 2020/21 na 2021/22

**Jedwali Na. 2 MWENENDO WA MAKUSANYO YA MADUHULI**

| CHANZO | 2020/2021 | 2021/2022 | Nyongeza/ Pungufu% | Nyongeza/ Pungufu% |
|---|---|---|---|---|
| Utawala na Rasilimali Watu | 2,000.00 | 2,000.00 | - | - |
| Idara ya Utawala wa Ardhi | 186,859,996,000 | 232,512,496,000 | 45,652,500,000 | 24.4 |
| Idara ya Upimaji na Ramani | 940,000,000 | 1,175,000,000 | 235,000,000 | 25 |
| Kitengo cha Usajili wa Hati | 6,700,000,000 | 8,375,000,000 | 1,675,000,000 | 25 |
| Kitengo cha Uthamini wa Mali | 5,500,000,000 | 6,875,000,000 | 1,375,000,000 | 25 |
| Maendeleo ya Makazi | 0 | 125,000,000 | - | |
| Mabaraza ya Ardhi na Nyumba za Wilaya | 0 | 937,500,000 | - | |
| **Jumla Kuu** | **200,000,000,000** | **260,000,000,000** | **60,000,000,000** | **26** |

**Chanzo**: Randama za Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2020/21 na 2021/22

Hivyo basi, Wizara inapaswa kuhakikisha kwamba inatekeleza malengo yake ya ukusanyaji wa mapato ipasavyo na kuhakikisha kuwa inajiwekea malengo halisi na yanayotekelezeka kulingana na hali ya uchumi pamoja na mahitaji halisi ya matumizi ya ardhi.

### 1.1.1 Matumizi ya Kawaida

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2021/ 2022 **Fungu 48 – Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi** inaomba kuidhinishiwa **shilingi bilioni 67,998,399,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ukilinganisha na **shilingi bilioni 47,408,779,999** zilizopangwa katika Mwaka wa Fedha unaoisha. Ongezeko la kiasi cha **Shilingi milioni 20,589,619,001** ni sawa na **asilimia 43.43** limetokana ongezeko la Watumishi wa Sekta ya Ardhi ambao awali walikuwa

chini ya ofisi ya Rais TAMISEMI ambao kwa sasa wamehamishiwa Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Kati ya Fedha inayo ombwa, **shilingi bilioni 34,079,748,000** ni kwa ajili ya mishahara ambayo imeongezeka kwa takriban **asilimia 74.8** ukilinganisha na bajeti ya mishahara ya mwaka unaoisha, na **shilingi bilioni 33,918,651,000** inaombwa kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC) ikiwa imeongezeka kwa takribani **asilimia 21.52.** Sababu za ongezeko hili ni mahitaji halisi ya Wizara kwa sasa katika usimamizi wa Sekta ya Ardhi na Watumishi wa Sekta ya Ardhi ambao awali walikuwa chini ya ofisi ya Rais TAMISEMI ambao kwa sasa wamehamishiwa Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

**Jedwali Na.3 MWENENDO WA BAJETI FUNGU 48 KWA MWAKA 2020/2021 NA 2021/2022**

| MATUMIZI | 2020/2021 | 2021/2022 | ONGEZEKO/ PUNGUFU | ONGEZEKO/ PUNGUFU% |
|---|---|---|---|---|
| Mishahara | 19,496,335,000.00 | 34,079,748,000.00 | 14,583,413,000 | 74.8 |
| OC | 27,912,444,999.85 | 33,918,651,000.00 | 6,006,206,000.15 | 21.5 |
| Maendeleo Ndani | 17,787,522,032.00 | 18,300,000,000.00 | 512,477,968.00 | 2.9 |
| Maendeleo Nje | 66,300,839,000.00 | 11,250,299,000.00 | -55,050,540,000.00 | -83 |
| Reallocation | 1,920,000,000.00 | - | - | |
| **Jumla ya ulinganifu** | 131,497,141,031.85 | 97,548,698,000.00 | 33,948,443,031.85 | -24 |

**Mheshimiwa Spika**, **Fungu 03 – Tume ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi**, kwa mwaka wa fedha 2021/2022 inaomba kuidhinishiwa **shilingi bilioni 2,476,888,000** kwa ajili ya matumizi ya kawaida ikilinganishwa na kiasi cha **shilingi bilioni 2,489,290,000** zilizotengwa kwa mwaka 2020/2021. Kati ya fedha za matumizi ya kawaida zinazoombwa kuidhinishwa, **shilingi bilioni 1,497,066,000** kwa ajili ya mishahara na **shilingi milioni 979,822,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC).

### 1.1.1 Bajeti ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, **Fungu 48 – Wizara ya Ardhi, Nyumba na Makazi** inaomba kuidhinishiwa **shilingi bilioni 29,550,299,000** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ukilinganisha na **shilingi bilioni 84,088,361,032.00** zilizoidihinishwa Mwaka wa Fedha 2020/2021. Hii ni sawa na pungufu la **asilimia 64.2**. Kati ya fedha inayoombwa, **shilingi bilioni 18,300,000,000** ni fedha za ndani ukilinganisha na **shilingi bilioni 17,787,522,032** zilizoidhinishwa katika Mwaka wa Fedha unaoisha, na **shilingi bilioni 11,250,299,000** ni fedha za nje ukilinganisha na **shilingi bilioni 66,300,839,000** zilizoidhinishwa katika Mwaka wa Fedha unaoisha.

**Mheshimiwa Spika,** kwa maelezo ya Wizara, punguzo la bajeti ya Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 limesababishwa na kukosekana kwa fedha za miradi ya maendeleo kutoka nje kwa **asilimia 100**. Wizara imejikita na kuzingatia ushauri wa kamati wa kutenga fedha zaidi za ndani kuliko za nje katika kukamilisha mradi iliyopo. Hata hivyo, ni maoni ya kamati kwamba, Serikali iandelee kutafuta wadau wa Maendeleo ili kuchochea mahusiano na kusaidia kufikia lengo la kibajeti pamoja na Wizara kuendelea kutafuta ahadi zote za fedha za nje ili ziweze kuziba pengo la kibajeti.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande mwingine, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, **Fungu – 03 Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi** inaomba kuidhinishiwa kiasi cha **shilingi bilioni 1,500,000,000** kwa ajili ya kutekeleza kazi za Mradi wa Upangaji wa Matumizi ya Ardhi. Kiasi hiki ni sawa na fedha zilizotengwa katika Mwaka wa Fedha unaoisha ambazo hazikutolewa ingawa majukumu yanayotarajiwa kutekelezwa bado ya umuhimu mkubwa. Majukumu hayo yanahusu kuratibu,

kushauri, kuandaa, kukagua na kusambaza programu za mipango ya matumizi bora ya ardhi kwa uwiano baina ya Sekta kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Upangaji Matumizi ya Ardhi, Sura ya 116.

## SEHEMU YA TATU

## 2.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na uchambuzi uliofanywa na Kamati, ninaomba kuwasilisha Maoni na Mapendekezo ya Kamati katika Maeneo yafuatayo:-

1) Mwenendo wa upatikanaji wa fedha zinazotengwa;

2) Ufanisi wa Wizara katika kukusanya Maduhuli;

3) Ufanisi wa Mfumo wa Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi;

4) Ufanisi wa Mabaraza ya Ardhi ya Wilaya;

5) Ufanisi wa Tume ya Taifa ya Mipango ya Ardhi;

6) Alama za Mipaka ya Nchi;

7) Sera ya Taifa ya Nyumba;

8) Sera ya Taifa ya Ardhi

9) Mamlaka ya Kusimamia Sekta ya Ardhi; na

10) Ufanisi wa Shirika la Nyumba la Taifa.

11) Madeni Sugu ya Wizara na Shirika la Nyumba la Taifa

12) Utoaji wa Vibali vya Ardhi kwa Wawekezaji.

**Mheshimiwa Spika**, Maoni na Mapendekezo ya Kamati yanakusudia kuongeza ufanisi wa Wizara katika kutekeleza Majukumu iliyopangiwa.

2.1 ***Muundo wa Bajeti na Hali ya Upatikanaji wa Fedha***

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa kwa muda mrefu pamekuwapo na changamoto ya ucheleweshaji wa fedha za maendeleo kutoka Hazina kwenda Wizarani na mara nyingine kiasi kinachotolewa hakikidhi haja ya kukamilisha miradi iliyokusudiwa kutekelezwa, na Kwakuwa mwenendo huo unachangia kwa kiasi kikubwa udhaifu katika utekelezaji wa mipango ya Wizara, Kwahiyo Kamati inaishauri Serikali kubuni mfumo endelevu ambao utahakikisha fedha kutoka Serikali kuu zinatoka kwa wakati.

2.2 ***Makusanyo ya Maduhuli***

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuwa kodi ya Ardhi (land rent) ni miongoni mwa vyanzo madhubuti vya mapato ya Wizara na kwakuwa Halmashauri ndio Wakala anaetumika kukusanya kodi hiyo, Kwahiyo basi Kamati inaishauri Wizara ifanye yafuatayo ili kuzichochea Halmashauri ziweze kukusanya kodi hiyo kikamilifu. Kamati inashauri kwamba:-

(a) Wizara iwaelimishe wananchi kuhusu umuhimu na ulazima wa kulipia pango la ardhi kwa wakati. Hatua hii iende pamoja na kuimarisha Ofisi za Ardhi za Mikoa na za Wilaya ili kwamba Wasajili walioko mikoani wawajibike kutoa hati katika wilaya zote nchini ili kuboresha na kupeleka huduma karibu na wananchi.

(b) Wizara ikamilishe kuingiza wateja wote kwenye mfumo wa kieletroniki sanjari na kuimarisha mfumo wa kutuma Ankara za wadaiwa wa pango la ardhi na kodi ya majengo. Hatua hii itasaidia wananchi wengi kuweza kulipa pango la ardhi na

kodi ya majengo kwa wakati, pasipo kuwa na usumbufu na itaongeza makusanyo ya maduhuli.

(c) Wizara iweke mikakati madhubuti ya kusimamia maafisa ardhi katika halmashauri nchini, na kuwawekea malengo (targets) ya makusanyo ambayo yatakuwa sehemu ya kipimo cha utendaji kazi wao.

(d) Gawio stahiki liwe linatolewa kwa wakati katika Mamlaka za Serikali za mitaa.

### 2.3 *Mpango wa Maendeleo*

**Mheshimiwa Spika**, kwakuwa kumekuwa na mwenendo usioridhisha wa kutotolewa fedha za maendeleo kwa wakati na kwakuwa hali hiyo inaathiri utekelezaji wa miradi ya maendeleo Kamati inashauri kwamba, Wizara ya Fedha itoe fedha kwa wakati na kwa ukamilifu ili Wizara iweze kutekeleza kwa ukamilifu Mpango wa Maendeleo.

### 2.4 *Mikopo kwa ajili ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi kwa Halmashauri*

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kwamba ingawa mfumo wa kukopesha halmashauri fedha kwa ajili ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi umekuwa na changamoto kadhaa , lakini bado Kamati inaona ni mfumo sahihi na endelevu wa kuongeza kasi ya kupanga maeneo ya nchi. Hivyo, kamati inashauri yafuatayo;-

a) Wizara kuongeza Idadi ya Halmashauri zinazopaswa kukopeshwa (mfano. kutoka Halmashauri 24 mpaka 50) kwa Mwaka na kuweka **utaratibu wa kutathmini sifa za Halmashauri zinazopaswa kukopeshwa.**

b) Kuelekeza Halmashauri zote nchini kupitia Wizara ya TAMISEMI **kutenga bajeti za kuandaa angalau mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji 6 kwa mwaka**, hii itaongeza kasi ya uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi kufikia Vijiji 810 kwa mwaka katika Halmashauri 135 zilizoko nchini.

c) Kuzijengea uwezo Halmashauri za Wilaya zote nchini katika upimaji, uandaaji, utekelezaji na usimamizi wa mipango ya Matumizi ya Ardhi.

d) Kutoa elimu kwa mamlaka za upangaji nchini kutumia teknolojia za kisasa na rahisi katika uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi mfano utumiaji wa picha za anga.

e) Kukamilisha na kusimika mfumo wa Kielekroniki (***Intergrated Land Management Information Systems-LMIS)*** utunzaji wa kumbukumbu za taarifa za mipango ya matumizi ya ardhi.

## 2.5 *Kupanga na Kupima Vijiji Miji (Emerging Towns)*

**Mheshimiwa Spika**, Kwakuwa mpaka sasa ni asilimia 25 tu ya ardhi ya Tanzania imepimwa na kuna wimbi kubwa la ukuaji wa vijiji kuwa miji (*Emerging Towns*) kutokana na ongezeko la miundombinu mfano barabara za lami, umeme nk. na kwakuwa, ongezeko hilo limepelekea ongezeko la makazi bora kwenye makao makuu mengi ya kata hapa nchini. Na kwa kuwa, Kamati haikuridhishwa na kasi ya uandaaji mipango ya upangaji wa matumizi ya ardhi ya vijiji 169 kwa mwaka. Kamati inashauri yafuatayo;-

a) Serikali ifanye jitihada za makusudi za kuzitaka Halmashauri zote nchini ambazo ndio mamlaka ya upangaji miji kutenga bajeti ya Kupanga matumizi ya ardhi kwa kila mwaka.

b) Kamati ilishauri ili kuhakikisha Vijiji vyote vimepimwa Tume iongeze kasi ya utendaji kazi kwa kuongeza idadi ya vijiji vinavyotakiwa kupimwa kwa mwaka, kutekelezwa kwa ushauri huu kutasaidia kuondoa migogoro ya ardhi inayoendelea nchini. Kwa kuzingatia Ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020, maelekezo ya serikali na utekelezaji wa miradi ya Kimkakati, wastani wa vijiji 826 vinapaswa kuandaliwa mipango ya matumizi ya ardhi kwa mwaka. Kwa idadi hiyo ya vijiji 826 kwa mwaka itachukua takribani miaka 12 kukamilisha zoezi la kupima na kupanga matumizi ya ardhi ya vijiji vyote nchini. Hivyo kamati inaishauri Serikali Kuja na Mikakati Madhubuti ili kuweza kuendana na kasi na kufikia lengo lililopo kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi (uk.119).

c) Wizara kuelekeza nguvu kubwa kwenye Kupanga, Kupima na Kurasimisha Vijiji Miji ili kupunguza migogoro ya ardhi, kuongeza wigo wa kodi na kuwapatia fursa wananchi wa kuwa na hati miliki za makazi yao. Kwa kufanya hivyo, kutapelekea ongezeko la eneo kubwa la nchi hii kupangwa na kupimwa kutoka asilimia zilizopo sasa 25 hadi kufikia asilimia 50.

### 2.6 *Mabaraza ya Ardhi ya Wilaya*

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto kubwa za kiuendeshaji wa mabaraza ya ardhi na nyumba ya wilaya na yale ya Kata kwa kuwa yanasimamiwa na mamlaka mbili tofauti. Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya yanasimamiwa na Wizara ya Ardhi wakati yale ya kata yanasimamiwa na Ofisi ya Rais TAMISEMI. Hali hii inachangia kuzorotesha utoaji wa haki katika mashauri ya ardhi. Aidha, kwakuwa wenyeviti wa mabaraza ya wilaya ni wataalam wa sheria wakati wale wa mabaraza ya kata ni watu wasio na taaluma ya sheria hali inayosababisha mashauri

mengi yaliyosuluhishwa katika mabaraza ya kata kukatiwa rufaa kwenda kwenye mabaraza ya Wilaya kutokana na taratibu nyingi kukiukwa. Kamati inashauri:

(a) Serikali kuyahamishia mabaraza yote ya ardhi chini ya usimamizi wa mamlaka moja (Wizara ya Ardhi) ili kuboresha utendaji wake.

(b) Serikali iweke utaratibu maalum wa kuzingatia weredi na uzoefu zaidi wa kuwapata wajumbe wa mabaraza ya kata kuliko utaratibu uliopo sasa.

(c) Wenyeviti wa mabaraza ya wilaya wapewe mikataba ya ajira za kudumu kuliko utaratibu wa sasa wa ajira za mkataba ili waweze kuwa na ari ya kufanya kazi na kutenda haki.

(d) Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya yaanzishwe katika kila Wilaya nchini. Vile vile, Wizara ya Ardhi iwekeze zaidi katika Mabaraza yanayotembea (mobile tribunals/court) ili kuwafikia wananchi wengi kwenye Vijiji na Kata.

(e) Kuweka mifumo mizuri ya uendeshaji wa Mabaraza ya Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi ili kupunguza na kuondoa rushwa inayoathiri haki za wananchi hususani wanawake.

### 2.7 *Tume ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi*

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua Tume ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi ipo kwa mujibu wa Sheria ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi namba 6 ya mwaka 2007 (Sura 116) Lakini uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa bado Tume hii haijulikani sana utendaji wake hapa Tanzania. Kulingana na hili Kamati inashauri mambo yafuatayo:-

a) Serikali ihuishe upya muundo wa Tume ya **Mipango ya Matumizi ya Ardhi** ikiwa sanjari na kuipa nguvu ya Kuwa **Mfuko wa Upangaji Ardhi Tanzania** wa kutafuta fedha ili iongeze kasi ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi na kufikia malengo ya Mpango wa tatu wa Maendeleo ya Taifa na yale ya Maendeleo Endelevu ya Kidunia (SDGs).

b) Bajeti ya Tume ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi iongezwe na fedha inayoidhinishwa itolewe kwa wakati.

c) Tume hii iongezewe wafanyakazi na vitendea kazi ili kukidhi mahitaji ya majukumu waliyonayo.

d) Tume iboreshe utekelezaji wa majukumu yake hususani kwenye URATIBU/COORDINATION ya wadau wote wanaoandaa mipango ya matumizi ya ardhi ili kulinda UBORAna UFANISI wa mipango ya matumizi ya ardhi inayotekelezwa na wadau.

2.8 ***Mradi wa Uimarishaji wa Mipaka Tanzania***

**Mheshimiwa Spika**, suala la uimarishaji wa mipaka ya nchi yetu ni suala muhimu sana kwa mustakabali wa ulinzi na usalama na diplomasia ya kimataifa. Suala hili ni mtambuka, na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imepewa jukumu la kiutendaji katika masuala yanayohusu miundombinu. Hata hivyo, Kamati imebaini kwamba utekelezaji wa mradi huu una changamoto nyingi ambazo Wizara hii peke yake haiwezi kuzimaliza.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inashauri kwamba, Wizara ya Ardhi ikishikirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, pamoja na vyombo vya ulinzi na usalama, ifanye jitihada za kutatua changamoto zilizopo kwa sababu ya uhusiano mzuri ambao upo baina ya nchi yetu na mataifa ambayo tunapakana nayo. Bila kuwa na makubaliano katika

ngazi za juu, Wizara hii haitaweza kuwa na uwezo wa kuimarisha mipaka ya nchi yetu kwa wakati.

2.9 ***Sera ya Nyumba ya Taifa (National Housing Policy)***

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inataarifa kuwa Sera ya Taifa ya Nyumba ipo kwenye mchakato kwa kipindi kirefu. Hata hivyo, bado Kamati inashauri Serikali kupitia Wizara ya Ardhi iharakishe uanzishwaji wa Sera ya Taifa ya Nyumba ili kusaidia kuweka bei elekezi kwa uuzwaji na ujenzi wa nyumba kwa ngazi ya kila Mkoa, Wilaya, kwa kuwa bei za ujenzi (construction cost) hutofautiana kwa kila wilaya na eneo husika. Sanjari na hilo Kamati inaona kuwa Sera hii itasaidia Wizara kuwa na bei elekezi kwenye ujenzi wa nyumba na hata kuleta tija kwa wananchi na wanunuzi wa nyumba hizo kwa kuwa kutakuwa na Mwongozo unaongoza Wizara kwenye masuala ya nyumba.

2.10 ***Sera ya Taifa ya Ardhi***.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa Wizara imekuwa kwenye mchakato wa muda mrefu kupitia Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995. Na kwakuwa Sera hiyo inaumuhumu mkubwa katika suala zima la usimamizi wa maendeleo ya ardhi na makazi, kamati inashauri Serikali kukamilisha haraka mapitio ya Sera hiyo kwa kufanya hivyo kutasaidia kutoa miongozo sahihi na yenye tija katika eneo la kupanga, kupima na kumilikisha ardhi kuendana na mahitaji ya sasa ya ndani na nje ya nchi.

2.11 ***Madeni Sugu na Wadaiwa Sugu na Shirika la Nyumba la Taifa and Wizara ya Ardhi***

**Mheshimiwa spika,** Kamati imebaini kuwepo kwa taasisi na halmashauri mbalimbali zinazodaiwa na Shirika la Nyumba la Taifa mfano; **Halmashauri ya Momba, Monduli, Mbarali, Mvomero, Uyui, Kongwa na Muheza**. Kwa kuwa Shirika la Nyumba la Taifa

linajiendesha kibiashara kwa kufanya kandarasi mbalimbali na kupangisha nyumba kwa Wananchi, Halmashauri na Taasisi mbalimbali nchini, na kwa kuwa mpaka sasa Shirika limekuwa na likipata changamoto ya kutolipwa madeni kwa wakati katika Halmashauri na Taasisi mbalimbali kama zilivyoorodheshwa katika viambatisho na **2,3**, jambo ambalo linapekelea kukwamisha maendeleo ya shirika. Kamati inashauri kuwa Halmashauri na Taasisi zote zinazodaiwa na shirika la nyumba kulipa madeni hayo ili kuliwezesha shirika kujiendesha kibiashara.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa Wizara ya Ardhi imekuwa ikitoa mikopo isiyokuwa na riba kwa halmashauri mbalimbali ili kuongeza kasi ya kupima ardhi pia Wizara imekua ikidai Taasisi mbalimbali za Serikali kodi ya pango la ardhi. Na kwa kuwa hadi sasa kuna baadhi ya Halmashauri na taasisi za Serikali zimeshindwa kurejesha mikopo na kodi hizo kwa wakati zikiwemo Halmashauri za mji mdogo wa Nzega, Wilaya ya Nzega, Manispaa ya Sumbawanga, Wilaya ya Gairo, Wilaya ya Sengerema na Mji mdogo wa Kondoa **(kimbatisho.1, 4)**; Kamati inashauri Serikali, kusimamia Halmashauri zote kurejesha mikopo kulingana na makubaliano waliyoweka kwenye kikao Kamati ya pamoja ya Ardhi, Mali Asili na Utalii pamoja Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa.

### 2.12 *Maboresho ya Shirika la Nyumba la Taifa*

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuwa Shirika la Nyumba la Taifa limejikita kujenga nyumba kwa mfumo wa ama kuuza au kupangisha katika maeneo mbalimbali hapa nchini; na kwa kuwa kumekuwa na malalamiko juu ya bei za nyumba kuwa juu na badhi ya nyumba kujengwa maeneo ambayo hayavutii wapangaji na wanunuzi; na baadhi ya nyumba kuwa na ukubwa usioridhisha, Kamati inapendekeza yafuatayo:-

a) Shirika kushirikiana na Taasisi mbalimbali zikiwemo za maji, umeme na barabara ili kupunguza gharama za ujenzi kwa kujenga nyumba kwenye maeneo ambayo huduma hizo zimepelekwa.

b) Serikali kuangalia uwezekano wa kulipunguzia Shirika la Nyumba mzigo wa kodi (**VAT Exemption**) kwenye vifaa vya ujenzi. Hatua hii itasaidia Shirika kujenga nyumba za bei nafuu (**Affordable Houses**).

c) Nyumba za gharama nafuu (**Affordable Houses**) za Shirika zinazojengwa katika Halmashauri mbalimbali nchini zijengwe maeneo ambayo ni rahisi kuuzika na kupangishwa kwa wananchi.

d) Kwakuwa shirika limeonesha ufanisi mkubwa katika kutekeleza miradi mbalimbali ya ujenzi wa nyumba, Serikali iendelee kulipatia kandarasi za ujenzi wa nyumba nchini ili kuliwezesha shirika kujiendesha kibiashara.

### 2.13 *Mamlaka ya Kusimamia Sekta ya Ardhi (Real Estate Regulatory Authority-RERA)*

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuwa kumekuwa na wimbi kubwa na ulaghai kwenye sekta ya soko la ardhi na nyumba kutokana na kukosekana kwa mamlaka ya kutoa miongozo ya bei za viwanja na viwango mbalimbali, na kwa kuwa hali hii imeleta taharuki kwenye soko la ardhi na nyumba hususani kwenye biashara ya upangishaji wa nyumba inayosababishwa na utitiri wa madalali ambao hawana usimamizi na hawalipi kodi. Kamati inashauri Serikali, kuhakikisha Mamlaka ya Usimamizi wa Sekta ya Ardhi **(Real Estate Regulatory Authority)** nchini inaundwa haraka ili kusaidia katika kusimamia viwango vya sekta ya ardhi na nyumba.

### 2.14 *Utoaji wa Vibali vya Kumiliki Ardhi kwa Wawekezaji*

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwa bado mfumo wa kutoa vibali kwa wawekezaji wa ndani na nje unapitia changamoto nyingi zikiwemo za mlolongo mrefu wa taratibu wa kupata ardhi na huduma ambazo hazipatikani ofisi moja. Kwa kuwa azma ya Serikali kwa sasa ni kufungua wigo na fursa za uwekezaji kwa wazawa na wageni, hivyo Kamati inaishauri Wizara ihuishe na kuweka utaratibu rafiki wa upatikanaji wa ardhi kwa wawekezaji sanjari na kuondoa milolongo na urasimu usio wa lazima. Lengo ni kuifanya nchi yetu kuwa rafiki kwa wawekezaji.

## 3.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi kwa ajili ya kuwasilisha taarifa hii. Kwa niaba ya kamati napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao kama yalivyo orodheshwa katika taarifa hii yaingie kwenye taarifa rasmi za Bunge *(Hansard)* :-

1. Mhe. Aloyce Andrew Kwezi, Mb – Mwenyekiti
2. Mhe. Dkt. Pius Chaya, Mb – Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Jafari Wambura Chege, Mb
4. Mhe. Soud Mahammed Jumah, Mb
5. Mhe. Phillipo Augustino Mulugo, Mb
6. Mhe. Ally Juma Makoa, Mb
7. Mhe. Khalifa Salum Suleiman, Mb
8. Mhe. Maida Hamadi Abdallah, Mb
9. Mhe. Mohamed Lujuo Monni, Mb
10. Mhe. Shabani Omari Shekilindi, Mb
11. Mhe. Neema William Mgaya, Mb
12. Mhe. Hawa Subira Mwaifunga, Mb
13. Mhe. Flatei Gregory Massay, Mb
14. Mhe. Mwanakhamis Kassim Said, Mb

15. Mhe. Hassan Seleman Mtenga, Mb
16. Mhe. Asia Abdulkarimu Halamga, Mb
17. Mhe. Juliana Daniel Shonza, Mb
18. Mhe. Taska Restituta Mbogo, Mb
19. Mhe. Suleiman Haroub Suleiman, Mb
20. Mhe. Oliver Daniel Semuguruka, Mb
21. Mhe. Lucy Thomas Mayenga, Mb
22. Mhe. Vedastus Manyinyi Mathayo,Mb
23. Mhe. Asya Mwadini Mohammed, Mb
24. Mhe. Agnes Mathew Marwa, Mb
25. Mhe. Munira Mustafa Khatib, Mb

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kutumia fursa hii kumshukuru Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mhe. William Vangimembe Lukuvi (Mb), Naibu Waziri, Mhe. Dkt. Angeline Sylvester Lubala Mabula (Mb), Katibu Mkuu Ndg. Mary Gasper Makondo, Naibu Katibu Mkuu Ndg. Nicholas N. Mkapa pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano na mchango wao katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya kikanuni ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** mwisho lakini si kwa umuhimu, napenda kumshukuru aliyekuwa Katibu wa Bunge Ndugu Stephen Kagaigai kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na Bunge. Aidha, nampongeza Ndugu Nenelwa Mwihambi kwa kuteuliwa kuwa Mwanamke wa kwanza kuwa Katibu wa Bunge la Jamhuri la Muungano wa Tanzania, namshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Huseni, Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Gerald Magili na katibu wa Kamati hii Ndg. Monica Mwamunyange wakisaidiwa na Ndg. Mwimbe John, kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na kuhakikisha taarifa hii inakamilika kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako tukufu lipokee taarifa hii ili lijadili na kukubali kuidhinisha makadirio ya Mapato na

Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

Aloyce Andrew Kwezi, Mb
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII**

**Mei, 2021**

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge hayo ndiyo yalikuwa maoni ya Kamati ambayo wanafanyakazi kwa niaba yetu sisi sote.

Sasa tutaanza na uchangiaji; tutaanza na Mheshimiwa Jerry William Silaa na Mheshimiwa Flatei Gregory Massay, ajiandae.

**MHE. JERRY W. SILAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kufungua dimba katika uchangiaji wa hotuba ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Naomba kuchukua fursa hii kwanza kumpongeza Waziri, Mheshimiwa William Vangimembe Mwalukuvi. Nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri, Dkt Angelina Mabula na wataalam wao wa Wizara. Nimpongeze pia Katibu Mkuu wa Wizara hii, dada yetu Mary Makondo, ambaye pamoja na sifa za kiutendaji lakini ana sifa ya unyenyekevu ambayo ni sifa muhimu sana kwa utendaji wa kazi za Serikali. Vile vile nimpongeze Naibu Katibu Mkuu Nico Mkapa na watendaji wote wa Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitachangia kwenye maeneo matatu, eneo la kwanza ardhi ni rasilimali ambayo kama itapangwa na kutumika vizuri ina uwezo mkubwa wa

kuwa chanzo kikubwa cha mapato kwenye Taifa letu. Utaona kwenye mwaka wa fedha uliopita Wizara ilikadiria kukusanya bilioni 200 na mpaka hivi tunavyozungumza zaidi ya shilingi bilioni 110 zimekusanywa kwenye halmashauri zote za nchi nzima, tunawapongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala kubwa hapa ni fedha hizi zinavyokusanywa, uwekezaji wake unaorudi kwenye Wizara kuwekeza katika upimaji wa ardhi ni mdogo sana. Ukisoma bajeti ya mwaka wa fedha uliopita pamoja na fedha za nje, kwenye fedha za ndani Wizara ilitengewa shilingi bilioni 16 kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hata hivyo, mpaka Waziri anawasilisha hotuba yake ya bajeti ni shilingi bilioni tano tu ndiyo zimepelekwa kwenye Wizara kwa ajili ya miradi ya maendeleo sawa na asilimia 30.9.

Mheshimiwa Naibu Spika, wewe ni Mwalimu na moja kati ya wanafunzi wako umemtambulisha hapa asubuhi asilimia 30.9 kule shuleni ukiipata kwenye mtihani nadhani tutakubaliana *supplementary*. Ninachoomba kusema, lazima Serikali itenge fedha za kutosha kwenye Wizara hii ili Wizara iweze kutekeleza wajibu wake wa kupanga matumizi ya ardhi na kupima ardhi. Mpango huu na upimaji huu utakuja baadaye kuwa mapato makubwa kwa Serikali kwa mapato ya *land rent*. Kwenye Jiji la Dar es Salaam mpaka hivi tunavyozungumza tayari bilioni 5.6 zimekusanywa kati ya malengo ya bilioni, 11 ni kazi kubwa, lakini zitakusanywa zaidi kama maeneo mengi zaidi yatapimwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe Mheshimiwa Waziri, mimi nilikuwa Meya pale Ilala kabla halijawa Jiji la Dar es Salaam. Nilikaa miaka mitano nakaimu Mkuu wa Idara Mipango Miji. Nimeondoka miaka mitano kuna Kaimu Mkuu wa Idara hivi nimerudi kwenye Ubunge bado kuna Kaimu Mkuu wa Idara. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, hebu am-*confirm* mtendaji yule aweze kufanya kazi hizi akiwa tayari amethibitishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ninalotaka kuchangia, ni eneo la urasimishaji. Kutokana na bajeti finyu

na uwezo unaofanya Wizara iwe na uwezo mdogo wa kupima, Serikali mwaka 2015 ilianzisha zoezi la urasimishaji kwenye maeneo mengi ya mijini kwenye Mkoa wa Dar es Salaam, kwenye Jiji la Dar es Salaam, kwenye Jimbo la Ukonga inafanyika kazi ya urasimishaji. Pale Jimbo la Ukonga yako makampuni 24 kwenye mitaa 64 kwenye Kata zote 13 za Jimbo la Ukonga, kuanzia Kitunda, Mzinga, Kivule, Kipunguni, Ukonga, Gongolamboto, Pugu, Pugu *Station*, Buyuni, Zingiziwa, Chanika na mpaka Kata ya Msongola. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, zoezi hili linasuasua. Ukisikiliza hotuba ya Waziri ziko hatua wameanza kuzifanya. Nimpongeze Waziri, Waziri wetu wa Ardhi ni mtu mwepesi na anajituma sana katika kazi ya ardhi, maana kazi yenyewe hii haitaki sana kukaa ofisini. Tulipata tatizo pale Kata ya Kivule na upimaji wa kile Chuo cha Ardhi Morogoro nilimwambia Waziri na alifika kutatua tatizo lile.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile juzi Naibu Waziri amekwenda Chanika kutatua matatizo haya ya urasimishaji. Nimeona kwenye hotuba ya Waziri wanachukua hatua, lakini tukumbuke kampuni hizi zimechukua pesa za watu, hatua za kuzisimamisha, hatua ya kuzifungia upimaji, hazitasaidia Mtanzania aliyechanga fedha zake kwenye Jimbo la Ukonga na maeneo mengine kupata upimaji wa eneo lake. Nimwombe Mheshimiwa Waziri katika kuhitimisha aje atueleze nini mpango sasa wa kusimamia kampuni hizi ili Watanzania waweze kupimiwa ardhi zao, wapate hati milki, waweze kumiliki maeneo yao kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la tatu ninaloomba kuchangia ni migogoro ya ardhi; migogoro ya mipaka katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu. Naomba nijikite kwenye eneo moja tu la migogoro ya mipaka baina ya hifadhi mbalimbali na vijiji na maeneo yetu tunayotoka. Kule Ukonga uko mgogoro wa kudumu baina ya Msitu wa Kazimzumbwi na wananchi wa Jimbo la Ukonga wa Kata za Buyuni, Chanika na Zingiziwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, maana leo nilikuwa nimeshapanga kabisa jioni hapa, siyo kwa kuwa jana alisikia wachangiaji wachache angedhani bajeti ingepita kirahisi. Nilipanga leo jioni niwaombe Wabunge tushike shilingi kwenye eneo hili, lakini nimpongeze Waziri kwenye hotuba yake ameelezea vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, *The Land Survey Act,* Sura ya 324, inampa Mkurugenzi wa upimaji na Ramani mamlaka ya kusimamia upimaji na kutatua migogoro yote ya mipaka. Mheshimiwa Waziri kwenye ukurasa wa 68 ameeleza vizuri na kwenye ukurasa wa 69, naona amelimaliza tatizo hili na naomba nimnukuu Waziri anasema:

*"Ni marufuku kwa Idara au Taasisi yenye migogoro kwenda yenyewe uwandani kutafsiri GN zao bila uwepo wa Mkurugenzi wa Upimaji na Ramani ambaye ndiye mhusika mkuu. Aidha Viongozi wa Mikoa, Wilaya lazima washirikishwe wakati wote mipaka inapohakikiwa"*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni marufuku kwa idara yoyote ama taasisi kwenda kunyanyasa wananchi na kujitafsiria *GN* zao wenyewe. Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Dkt Ndumbaro marufuku, Mheshimiwa Naibu Waziri Mary Masanja marufuku, siyo maneno yangu, maneno ya Waziri mwenye dhamana ya ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye maelezo yake Waziri ametoa wito kwa Viongozi wa Mikoa na Wilaya Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, maana wengine ni mabingwa kuweka watu ndani, sasa hawa ndiyo wa kuwaweka ndani, hawa wanaokuja kutafsiri *GN* zao wenyewe na migogoro ya mipaka na kunyanyasa wananchi wetu.

## TAARIFA

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jerry Silaa, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Charles Mwijage

**MHE. CHARLES J. MWIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimpe taarifa mzungumzaji MCC mstaafu kwamba unapotoa taarifa, wale unaowapa taarifa hawapo, tatizo la maliasili hifadhi ndilo tatizo la mifugo ninalolipata kwangu kule, lakini unaowaambia hawapo hawawezi kuelewa unavyopata uchungu, hawapo hapa.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge nimeshasisitiza mara kadhaa, Serikali ipo Bungeni na ndiyo maana mnazungumza na mimi, yaani kama kuna mtu yeyote wa Serikali ambaye jambo linamhusu limezungumzwa hajaelewa vizuri hata kama yupo humu ndani ataelezwa vizuri, ni jambo gani limezungumzwa kuhusu yeye. Kwa hiyo msiwe na wasiwasi na michango yenu mnayoitoa, Serikali iko Bungeni.

Mheshimiwa Jerry Silaa, malizia mchango wako.

**MHE. JERRY W. SILAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Mwijage, kaka yangu, mtaalam wa propaganda, sisi wataalam wa sheria hapa tuna *address the chair,* tunaongea na kiti na ujumbe utafika.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la mwisho ni eneo la uthamini. Niseme tu kwamba, Wizara ya Ardhi inafanya kazi yake ya uthamini vizuri sana chini ya Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali, mama yetu Evelyn Mugasha. Nafasi hizi zenye mambo ya hela hela ama za uadilifu uadilifu, wanapokaa akinamama wanazifanya vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachoweza kusema ni kitu kimoja, naiomba Wizara ambayo ndiyo wataalam wa masuala haya, waishauri vizuri Serikali. Kulikuwa kuna wakati tunatumia *sport valuation* kuweza kupata bajeti ili idara ama taasisi inayotaka kufanyiwa uthamini iweze kutenga fedha, lakini tumeona mara nyingi uthamini unafanyika lakini kumbe hata hiyo taasisi inayoagiza uthamini hata fedha kwenye bajeti haijatengewa. Matokeo yake uthamini unafanyika, fidia zinachelewa na wananchi wetu wanapata shida sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe Serikali iweke utaratibu mzuri wa kufanya uthamini na kulipa wananchi kwa wakati. Ili hili lifanikiwe lazima wakati uthamini unafanyika tayari bajeti iwepo na fedha ziwe zimeshatengwa. Maeneo mengine wawe wanaaminiana, hawawezi wakafanya uthamini ukaidhinishwa, wakaanza uhakiki, ukakamilika, ukaja uhakiki mwingine wakati wananchi wanasubiri fidia zao, ile miezi sita ya kisheria inapita, hela za riba hazipo, tunaanza tena kurudi nyuma na wananchi wanapata shida kwenye maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nirudie tena kuipongeza Wizara, inafanya kazi nzuri hasa katika kujikita kuingia kwenye mifumo ya TEHAMA. Tukienda hivi nchi yetu itapata tija kubwa kwenye sekta ya ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na nakushukuru sana kwa nafasi hii. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Flatei Gregory Massay, atafuatiwa na Mheshimiwa Halima James Mdee na Mheshimiwa Taska Restuta Mbogo ajiandae.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza nianze kumshukuru Mungu kunipatia nafasi ya pumzi na kuniwezesha kuchangia mchango kwenye Wizara hii ya Ardhi nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze watumishi hawa kwenye Wizara ya Ardhi, nikianza na mwenyewe Waziri Mheshimiwa Lukuvi, Mheshimiwa Angelina Mabula dada yangu Mary, Stella, Nico na wengine kwa kweli kwenye Wizara hii. Napongeza kwa sababu moja kubwa sana, Wizara wamejitahidi sana katika eneo hili la ardhi wana eneo kubwa sana. Migogoro ilikuwa mingi sana na mimi nimeishuhudia katika maeneo yangu mengi na niwashukuru sana kwanza kwa kulinda, kwa sababu gani nasema hivi?

Ni kwa sababu ardhi imebaki kama rasilimali pekee ya Mtanzania aliyobaki nayo na urithi mmojawapo ni ardhi katika eneo letu hasa la kule vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo niwapongeze sana watumishi hawa kwa huku juu kama Wizara yenyewe kwa sababu wamejitahidi sana. Yuko mtangulizi amezungumza habari ya haya makampuni, nimsihi Mheshimiwa Waziri, yako mengi ambayo ameyafanya na Wizara yake, lakini machache yanaleta shida. Kwanza niliweke wazi hili kabla sijamiminika vizuri, haya makampuni ambayo kwa kweli yanakwenda kurasimisha, mara nyingi hayatumii sheria kwa jinsi Wizara ilizoziweka na hayafuati taratibu na hayasubiri miongozo ambayo wameweka Wizara kama Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mifano michache, ukiangalia wanavyokwenda kwenye halmashauri zetu, wakifika kule, kwa mfano halmashauri kama ya kwangu ina watumishi wachache wa Idara ya Ardhi na pengine hakuna kabisa. Kwa hiyo, baadaye nitampa Waziri ombi lakini aangalie haya makampuni, ushauri wangu kwake na kwa Serikali waunde Kamati ya Kisekta ambayo itasaidia kusimamia hawa warasimishaji ili walau waweze kupanga maeneo yetu vizuri. Nasema hivyo kwa sababu gani? Tanzania kama nchi lazima sasa nchi ipimwe yote na ikipimwa yote migogoro hii itaondoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, migogoro mingi inasababishwa kutokana na kwamba maeneo mengi hayajapimwa, lakini siyo hiyo tu maeneo mengi yakipimwa na yakapimwa kwa uhakika, maana yake ni kwamba hata Serikali itajipatia pesa kwa kutoza kodi ya maeneo yote yaliyopimwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia sasa hivi kila kampuni ina-*charge* kadiri inavyoona, iko nyingine ina-*charge* 150,000, nyingine 200,000 nyingine 100,000, lakini sasa basi Serikali ione namna gani ya kufanya, iwawekee utaratibu haya makampuni yanayopima ili utaratibu ule uonekane na

sisi wawakilishi tujue kabisa kwamba wanapima kwa kiasi hiki na iwe kama *formality* ili hata mwananchi anapotakiwa kupima eneo lake ajue kipande chake anapimiwa kwa namna gani na kama ni kiwanja au chochote.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine niwapongeze sasa Wizara kweli kweli, kwa sababu wametoa mikopo kwenye halmashauri kadhaa na Mheshimiwa Waziri amesema sita zimefanya vizuri na zimerejesha hela. Nimwombe Waziri waendelee kuzikopesha halmashauri ili maeneo mengi yaendelee kupimwa, wasije wakakata tamaa kwa sababu halmashauri zingine hazikulipa. Niombe Wakurugenzi wale anmbao wamekopeshwa hizi hela na maeneo yao yamepimwa na wamepata faida kutokana na kupimwa kwa ardhi hii, basi nao warudishe hizo fedha ili halmashauri zingine zipate mikopo ambayo haina riba, wakapime maeneo yao. Ikiwa hivi basi ni wazi Serikali itapata mapato, lakini siyo hiyo tu migogoro itakuwa imepungua na miji yetu mingi itakuwa imepimwa. Siyo hilo tu, unapopima miji hakuna tena sababu ya kwenda kufanya urasimishaji kwa sababu miji ile imekwishapimwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine naomba nitoe mchango wangu katika Mabaraza ya Ardhi. Niishukuru kwanza Serikali imeanzisha baraza katika jimbo langu na Wilaya ya Mbulu. Bbaraza linafanya vizuri sana na linasaidia kutatua kero hii ya ardhi, lakini wana changamoto chache; ya kwanza baraza halina namna ya kwenda kutembea.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe Mheshimiwa Waziri ikimpendeza aone namna gani ya kuanzisha haya Mabaraza yatembee yawe *mobile* zile mahakama zao zitembee, zikaone, maana wakati mwingine hazina namna ya kwenda kwenye maeneo zikaona, ni kweli kwamba hii ardhi ni ya fulani, hii ardhi ikoje kabla ya kutoa hukumu? Niombe pia wasitumie *technicality* za kisheria kabisa kutoa haki, waangalie vizuri namna ya kuhukumu kwamba haki iko wapi zaidi kuliko kutumia *technicality.* Niishukuru sana Wizara imeanza kutoa hukumu Kiswahili, kesi inasikilizwa Kiswahili na hili niwapongeze sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana leo napongeza Wizara hii kwa sababu wananchi wetu kule wanapotoa hukumu wanasikiliza na wanakuwa wanajitetea bila kuwatumia hawa Wanasheria ambao mara nyingi walikuwa wakiwadanganya. Kubwa zaidi sasa katika maeneo haya, muwasaidie hao Wazee wa Baraza wawe na posho za kutosha...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Flatei, Mawakili wanawadanganya wale wanaowawakilisha ama? Maana umesema walikuwa wanatumia Wanasheria ambao walikuwa wanawadanganya, kwani sasa hivi wakitumia Kiswahili wanajisimamia wao wenyewe unataka kumaanisha hivyo?

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Ndiyo ukweli.

**NAIBU SPIKA:** Kwa hiyo Mawakili ni waongo?

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, sitaki kusema Mawakili wote ni waongo hapana, kwenye mahakama hasa hizi za Baraza la Ardhi wako wengine wanajifanya *ma-bush lawyer,* hawana hata hizo taaluma.

**NAIBU SPIKA:** Sasa ngoja, tufafanue vizuri, kuna tofauti ya mtu ambaye ameamua kukupa wewe ushauri ambaye siyo Wakili, wala siyo Mwanasheria. Sasa ukisema walikuwa wanadanganywa na Wanasheria yaani hapo maana yake ni kwamba kimsingi sheria... *(Kicheko)*

Wanasheria humu ndani wataandamana isipokuwa mimi, sasa hiyo kauli hiyo iweke vizuri kidogo.

**MHE. EDWARD K. OLELEKAITA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, basi niifute kabisa, najua wewe ni Mwanasheria na naelewa *angle* unayozungumzia.

**NAIBU SPIKA:** Ngoja ngoja unampa taarifa Mheshimiwa Flatei Massay au mimi?

**MHE. EDWARD K. OLELEKAITA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampa anayezungumza.

**NAIBU SPIKA:** Basi ngoja tulimalize kwanza hili halafu nitakupa nafasi. Mheshimiwa Flatei ulikuwa unataka kusema *point* moja hivi sijakuelewa, hii ya pili uliyokuwa unasema kwa kuwa mimi ni Mwanasheria...

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, najua nini maana ya Mwanasheria, haya nilikuwa nataka kupongeza Wizara hii ielewe kwamba kwa sababu wananchi wetu kule hata kuweka hao Wanasheria zile gharama zinakuwa kazi kubwa sana, kwa hiyo kumtafuta mwanasheria *proper* kama wewe ni kazi sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Nadhani hoja imeeleweka, hoja ya gharama ni tofauti na hoja ya wale watumiaji wa hizo huduma za Wanasheria kudanganywa.

Mheshimiwa Olelekaita.

**TAARIFA**

**MHE. EDWARD K. OLELEKAITA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana nataka tu nimpe mzungumzaji taarifa kwamba, mawakili hatuendi kwenye Mabaraza hayo anayozungumza, kwa hivyo kama wananchi wamedanganywa huko basi watakuwa ni watu wengine lakini siyo Mawakili.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Flatei Massay.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naipokea taarifa kwa sababu ni rafiki yangu na isitoshe ni Mbunge mwenzangu na tunatoka Manyara wote, naipokea sana taarifa hii wala asiwe na wasiwasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuipongeza Wizara hii naomba niendele na mchango wangu. Kwa hiyo, Wizara inajitahidi sana na kwa kuwa sasa nimeomba kwa Mheshimiwa Waziri, wale Wazee wa Mabaraza, Wenyeviti wa Mabaraza wawasaidie basi wawapatie ajira za kudumu, ili mtu awe na hakika na ajira yake. Mtu anapokwenda kufanya kazi ile kubwa ya kutoa haki mahali fulani pia anatakiwa awe na *security* ya kutosha. Wakati mwingine anajua kabisa ajira yake inakwisha baada ya muda fulani au kwa miaka mitatu, kwa hiyo haimpi ile hali ya kujiona yeye ni mfanyakazi katika eneo hili la kutoa haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo niombe Serikali iwape hawa Wenyeviti ajira ya kudumu kwa sababu sasa hivi nadhani ajira zao siyo za kudumu. Pia niombe pia hawa Wazee wa Baraza, nao pia waangaliwe kwa namna Fulani, waletewe bajeti hapa na katika hiyo bajeti wapewe fedha ambazo zitaonyesha kabisa kwamba kweli fedha hii inaweza ikawa kama posho ya kawaida kabisa kulikoni sasa hivi ilivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kubwa, niwashukuru pia kwasababu wamefanya kazi nzuri, Mheshimiwa Waziri na Naibu wake na Stella huyu ambaye kwa kweli amekuwa akisimamia Mabaraza haya ya Kata.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine kama ushauri tu niombe Mheshimiwa Waziri aangalie kanuni katika Mabaraza haya, pawepo na namna rahisi ya kusaidia, kesi zinapoanza pawe na utaratibu ikiwezekana kesi zianze kwenye Kijiji, iende kwenye kata, lakini baadaye iende kwenye Mabaraza ya Wilaya. Kwa nini ninasema hivyo? Mtu mwingine anaweza kuwa na uhuru, akaenda kufungua kesi kwenye Baraza la Wilaya ambako anajua kabisa yule Hakimu au Mwenyekiti hawezi kuja kwenye eneo ilipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo utoaji wa haki ule mtiririko na kesi ilivyoendeshwa inakuwa hawezi kujua kwa sababu yule Mwenyekiti hawezi kwenda *site* kuona hali hii ilivyo. Kesi ikianzia kwenye kijiji ni rahisi kujua kwamba kijijini

wameamuaje, Baraza la Kata limeamuaje. Kwa hiyo ni rahisi kwa Mwenyekiti kuamua namna gani ya kutatua mgogoro huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, niombe Mheshimiwa Lukuvi, iko migogoro ambayo Mheshimiwa Waziri anaweza kuitatua, migogoro iko Manyara mingi hasa ya Mkoa kwa Mkoa, Mkoa wa Arusha na Mkoa wa Manyara...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Muda wako umekwisha Mheshimiwa kengele ya pili imeshangonga.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge Stella aliyetajwa siyo Mheshimiwa Stella Fyao, ametajwa Stella mtaalam ambaye ni Stella Tulo, yeye ni Msajili wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya, ndiye aliyekuwa anatajwa hapo.

Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Halima James Mdee, atafuatiwa na Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, Mheshimiwa Ali Juma Makoa, ajiandae.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Kiukweli mimi kama mkongwe kwenye Bunge hili Wizara hii ilikuwa kati ya Wizara moto sana kipindi hicho palikuwa hapakaliki, lakini sasa hivi naona moto umepoa sana. Kwa hiyo hicho ni kiashiria kwamba Mheshimiwa Lukuvi na timu yake wamekuwa wakifanya kazi kwa viwango vyema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, mwaka 2010 mpaka 2015 mimi nilikuwa Waziri kivuli wa Ardhi na nilitumia muda huo kufanya utafiti mkubwa sana wa migogoro ya ardhi na

sikuwa mchoyo *nika-share* na Mheshimiwa Lukuvi *ma-book* yangu yale, akayafanyia kazi na anapata kiki kutokana na kazi ambayo nilitumia *brain* yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Mheshimiwa Bashiru yuko hapa, aliyekuwa Katibu Mkuu wa CCM na yeye nilikuwa namsaidia tafiti nilizokuwa nikifanya na yeye wakati huo akiwa ni Mhadhiri akifanya maandiko yake huko na atakubali kama hatakuwa mchoyo wa fadhila. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa leo nitakuwa *local* kidogo, nitakuwa Jimbo la Kawe, kwa sababu inaonekana kama vile kumepoa Kawe kidogo. Mheshimiwa Lukuvi, mimi na yeye wakati niko Mbunge wa lile Jimbo tulifanikiwa kutatua migogoro mingi sana na nimshukuru kwa hilo. Tulitatua Nyakasangwe, tukatatua Kunduchi, tukatatua Bunju kwa Somji, tukatatua kile kimgogoro cha miaka kumi na tano Basihaya pale, kuna Mtaa wa Chatembo, cha Chui na cha Simba. Hayo majina yenyewe yanaashiria watu gani wanakaa kule. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lile eneo lina wakazi 4,000, lile eneo tarehe 13 Juni, 2015, tulienda pale kumaliza mgogoro, alikuwepo Waziri, alikuwepo Katibu Mkuu wakati huo Kidata ambaye sasa hivi ni Kamishina wa *TRA*, alikuwepo Naibu Waziri kipindi hicho, Anjella Kairuki, Wakurugenzi na timu yake yote walikuwepo. Tukatatua mgogoro husika na wananchi wa eneo lile na alikuwepo pia aliyekuwa Mkurugenzi wa kile kiwanda anaitwa bwana Alfonso Rodriguez kwa niaba ya kiwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu tuna roho nzuri siku 60 ambazo wataalam wa Wizara walikaa pale, wananchi walijigharamia, wakahakikisha wanakaa sehemu nzuri hili upimaji ufanyike. Nini tulikubaliana kwenye kikao na nasema haya Mheshimiwa Lukuvi anajua yeye ni rafiki yangu, tumefanya mengi pamoja, lakini akiona nimeamua kuja kufunguka hapa nataka arekodiwe na *Hansard* sasa akijigeuka mwenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maazimio tulikubaliana nini? Kikao cha wananchi kilikuwa na maazimio saba, nitayasoma kwa ufupi:-

(i) Eneo ambalo limekaliwa na wananchi kwa muda mrefu libadilishwe matumizi kuanzia leo tarehe 13 Juni, 2015, kutoka matumizi ya uchimbaji wa madini na kuwa eneo la makazi;

(ii) Wananchi waliotambuliwa wakati wa zoezi la uthamini ndiyo watakaohusika na zoezi zima, wananchi ambao hawakuwepo na walikuja baada ya zoezi hawatatambulika;

(iii) Wakati wa umilikishaji Wizara itatoza tozo ya mbele *premium* kwa kila kiwanja itakachomilikisha. *(Makofi)*

(iv) Wizara imekubali sehemu ya malipo ya *premium* yataenda katika kiwanda na kitasaidia kujenga miundombinu na huduma za jamii kwa zahanati;

(v) Wananchi kwa kushirikiana na Serikali ya Mtaa wataunda Kamati ya Utekelezaji na Usimamizi wa Mpango huo;

(vi) Kazi za uchimbaji mchanga na kokoto hazitaruhusiwa na atakayefanya hivyo atakamatwa; na

(vii) Kazi ifanyike haraka mwezi Oktoba, 2015, mambo yatakamilika, wananchi watakabidhiwa maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri akafunga kikao, akadondoka *signature* hapa, Mheshimiwa Lukuvi pembeni, Mheshimiwa Kidata pembeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazungumza Mheshimiwa Jerry hapa, sisi Wanasheria katika nyaraka ukishadondoka *ukaji-commit* huwezi kuja *uka-change* kote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nini kimetokea na majina haya *signature* za wananchi waliohudhuria kikao. Ameondoka Mtendaji Mkuu wa Twiga, akaja Mtendaji Mkuu mwingine, anaanza kuivimbia Serikali, anakuja na *terms* nyingine, wakati tulikubaliana hapa wananchi watachangia *premium, premium* kidogo itaenda kwenye kiwanda na nyingine itakuja kurekebisha miundombinu. Mheshimiwa Waziri aliendа juzi, Mheshimiwa Tibaijuka aliendа akaondoka akasahau kiatu, nashukuru Mheshimiwa Waziri walimstahi, anawaambia wananchi kutoka *premium* ambayo kawaida ni *one percent* kama ikiwa Serikali imesimamia mpaka *three percent* haiwezi kuzidi hapo ya thamani ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo wanaenda wanawaambia wananchi watoe *35 percent* ya thamani ya ardhi. Kwa sababu, wamethaminisha wakasema *square* mita pale ni Sh.20,000/=, wakasema wananchi walipe Sh.6,500/= kwenda Sh.7,000/= mwanzoni ilikuwa Sh.8,000/= wakapunguza kidogo kwamba walipe Sh.6,500/= hii nyingine watafidiwa na mwekezaji. *Square* mita moja Sh.7,000/= wakati tulikubaliana tunalipa *premium* ambayo ni asilimia moja ya thamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, kile alichokifanya ni kutaka wananchi wanunue ardhi *almost* upya. Wananchi wanaokaa eneo lile ni wananchi wa kipato cha chini, wananchi maskini, inakuwaje leo Mheshimiwa Waziri anageuza maneno yake na nimwambie tu kama hafahamu, wananchi wamesema hivi nikufikishie ujumbe, hawatatoka ila wako tayari kulipa *premium* tuliyokubaliana. Hilo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini Mheshimiwa Waziri ana burasa ya kuamua kulimaliza hili kwa sababu tuliendа vizuri tukagota.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Nyumba la Taifa; juzi niliuliza swali hapa, Mheshimiwa Naibu Waziri akajibu, akasema mradi huu utakuwepo kwenye bajeti mwaka huu wa fedha tunaoanza kuutekeleza. Sasa mwaka wa fedha Wizara si lazima kwenye maandishi huku nione. Waziri alisema utekelezaji wa Mradi 7111 ambayo thamani yake ni shilingi bilioni 142; na Mradi 7112 shilingi milioni 103, miradi yote miwili ina thamani ya shilingi bilioni 245 ambazo Shirika la Nyumba la Taifa liliingia mikataba na wakandarasi wawili toka mwaka 2014. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo mradi mmoja umetekelezwa kwa asilimia 20 na mwingine asilimia 30. Mkataba wa kwanza ulikuwa 2014 mpaka 2017 waka-*extend* mpaka 2019, leo kazi imelala. Mheshimiwa Naibu Waziri atakwambia tulihamishia Makao Makuu Dodoma tukagota. Waziri akasema kulikuwa kuna mikataba haijakaa vizuri tunaifanyia kazi toka mwaka jana hawajajibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na watu wa *PAC* wako hapa ni mashahidi, anasema ule mkataba na sababu ya nini kukwama, Shirika hivi linavyojiendesha kibiashara limegota limeshindwa kupewa fedha kwa sababu, wamekopa, mwisho wa ukomo wao shilingi milioni 300, wakaenda kuomba kibali Wizara ya Fedha toka 2017. Kwa sababu mradi huu ni *viable,* unakaa eneo ambalo ni *prime,* tunaomba mtupe kibali mradi huu utalipa. Toka mwaka 2017 mpaka leo hakuna ambacho kimetokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wananchi wamewekeza zaidi ya shilingi bilioni tatu pale wameshanunua nyumba kabla hazijajengwa, Waziri anatuambia kuna *process,* ni kweli? Tafiti zinaonyesha tuna upungufu wa nyumba kwenye majiji zaidi ya milioni tatu na kila mwaka nyumba laki mbili zinahitajika, halafu wanakaa hapa wanasema hatuna mapato, yaani hatuna mapato wakati pale Kawe *New City* iliyokuwa inatarajiwa kuwa na wakazi 50,000, wangeingiza *property tax* mpaka Mheshimiwa Waziri angekimbia. Hivi kwa nini tunafikiria kimaskini *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie; tusipotekeleza huu mkataba Wizara inaenda kulipa bilioni 100, wakati wamekataa kuipa ruhusu Shirika la Nyumba yaani shilingi bilioni 100 unaenda kumpa mkandarasi bure kwa kuvunja mkataba jamani hii ni akili ama nini? *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Halima kengele ya pili imeshagonga.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimwombe Waziri anipe majibu yenye mantiki kwa maslahi mapana ya nchi na Jimbo la Kawe. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo.

## MWONGOZO WA SPIKA

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kuchauka.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba mwongozo wako kwa Kanuni ya 76, sipingani na maelekezo yako ambayo umekuwa ukiyatoa zaidi ya mara mbili, lakini utaratibu huu ukiendelea, naona kama una tofauti kidogo. Sasa hivi Bunge hili limekuwa likijadili bajeti, lakini Mawaziri wenye dhamana tu ndiyo wanakuwepo mezani na mambo mengine yanahusu Wizara nyingine na mwisho hata kwenye uchangiaji wa mwisho wanaokuja *ku-windup* ni Mawaziri wale wale tu wawili. Mambo mengine yanahusu Wizara zingine, hatuoni wengine wakiingilia kujibu na hatuwaoni kwa sababu hawako Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, jana ulikataza pale Wabunge kwenda kwa Waziri Mkuu Waziri Mkuu kwa anatakiwa kusikiliza Wabunge wanaochangia. Utaratibu huu unapoendelea sasa kwamba tunaongea tu na Waziri

mwenye dhamana tu wengine wanakuwa hawahusiki sijui kama ni sawa sawa naomba mwongozo wako. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge amesimama Mheshimiwa Zuberi Kuchauka hapa akiomba Mwongozo hasa kuhusu kuwepo au kutokuwepo kwa Mawaziri wengine na Naibu Mawaziri humu Bungeni wakati hoja zikizungumzwa. Ameeleza kwa kirefu sitaki kurejea hayo, lakini ameeleza kwamba hata wakati wa michango anachangia Naibu Waziri halafu anahitimisha hoja mwenye hoja yake.

Waheshimiwa Wabunge ninyi mnafahamu Bunge linapokuwa linaendelea, Serikali haisimami na watu wanaotoa huduma ni hawa hawa, likizungumzwa jambo hapa kuna daraja limekatika mahali lazima mtu aende huko lilikokatika hilo daraja. Ukiambiwa kuna watu wamefariki sehemu fulani imetokea changamoto fulani ni hawa hawa lazima waende huko.

Waheshimiwa Wabunge, mwelewe vizuri hivi ninavyosema ndio hivyo hivyo kwa maana ya kwamba Serikali ipo Bungeni. Sasa hivi tunajadili bajeti za kisekta; Waziri na Naibu Waziri wa kisekta yupo hapa na watendaji kazi wake wapo pale na mnawaona wamejaa. Maana yake ni nini? Kanuni zetu mtakumbuka Waheshimiwa Wabunge uwa zinataka Mbunge ajadili hoja iliyoko mezani na kwa sasa hoja iliyoko mezani wasimamizi wake ni Mheshimiwa Lukuvi na Naibu wake Mheshimiwa Mabula.

Ukijadili hoja iliyoko mezani wasimamizi wake wako hapa na hawa ambao hamuwaoni Mheshimiwa Waziri Mkuu hamumwoni humu ndani, akiwa hayupo tungeshawatangazia nani anakaa pale. Hii maana yake yupo lakini yupo kwenye majukumu mengine, kwa hivyo hawa ambao hamuwaoni humu ndani wako wanazungumza kule hoja zenu Waheshimiwa Wabunge. Hapa mmechangia sana, nitoe mfano, mmechangia sana kuhusu *sulphur* labda kwenye korosho, watu wamechangia hapa mambo mengi kwenye kilimo, wameleeza kwa uzito mambo ya stakabadhi ghalani.

Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka jana Mheshimiwa Spika alisema bajeti zinazokuja kule mbele, kuna Bajeti Kuu ya Serikali itasomwa tarehe 10, hoja mlizozizungumza Waheshimiwa Wabunge kipindi hiki tunachojadili bajeti za kisekta, mtazisikia wakati huo. Majibu hayo Serikali itatoaje ikiwa yote imekaa humu ndani? Haiwezekani, lazima watoke kule nje, wakakae vikao, wakajadili, waone hoja za Wabunge zitakuja na majibu gani kwenye bajeti ile ya jumla.

Sasa yale yasiporekebisha tutarudi tena hapa ndani kwamba tulitoa mawazo mnaona imerudi vilevile, hapana, ukiona Waziri hayuko humu ndani ujue kuna jambo na ninyi mnafahamu Mheshimiwa Rais wetu, Samia Suluhu Hassan alishasema Wabunge wote waweko Bungeni hasa wa Chama Cha Mapinduzi. Ukiona viti viko wazi maana yake kuna wajumbe wako kwenye Kamati. Kwa mfano kesho hapa itaingia bajeti ya Mifugo na Uvuvi, Kamati hiyo maana yake iko kwenye maandalizi ya kuja kutuambia hapa Wabunge wamekutana na nini kule?

Hao hawezi kuwepo hapa ndani, lakini pia Waziri wa Mifugo na Uvuvi na Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, mwingine atakuwa yuko kule akikamilisha bajeti mwingine atakuwa yuko kwenye Kamati kutoa ufafanuzi wa hoja mbalimbali ili humu ndani zisiletwe hoja ambazo Wabunge wenzetu kwenye Kamati wamezisemea. Kwa hiyo tuelewane kwenye hilo Waheshimiwa Wabunge, ukiona viti viko wazi humu ndani haimaanishi kuna Mbunge basi kaenda zake sijui wapi kufanya shughuli gani, hapana. Vivyo hivyo, hata Serikali usipomwona Waziri humu ndani ujue kuna jambo.

Waheshimiwa Wabunge, niwape mfano mwingine, sasa hivi kinaendelea kikao cha *SADC,* sawa jamani? Kile kikao lazima na sisi Tanzania tuhudhurie, kwa mtandao, sasa tutahudhuria tukiwa humu ndani. Kwa hiyo tunavyoyasema haya sio kwamba kuna mtu labda anatetewa mahali, Waziri kaenda kunywa chai wapi hapana Waheshimiwa Wabunge, Mawaziri wapo kazini na Serikali iko hapa Bungeni. Mkiamini kiti kinavyosema Serikali iko Bungeni, wewe subiri hoja

uliyoisema itapata majibu au haitapata majibu. Wakati huo utaweza kuwa na hoja zaidi kwamba pengine kwa kuwa hukuwepo, kwa hiyo nataka kusema hili na lile. Kwa hiyo tuamini hivyo kwamba Serikali kama huwaoni humu ndani, wako kazini na wanashughulika na matatizo ya wananchi wetu sisi wenyewe. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, naamini hilo limeeleweka vizuri. Kwa namna hiyo hiyo hata viti vikionekana vya Wabunge hawapo humu ndani, wako kwenye vyumba vya Kamati wakikamilisha kazi. Humu ndani Wajumbe wa Kamati ya Bajeti wengine walishaenda hamuoni hapa Mheshimiwa Matiko atakuwa yuko kwenye Kamati. Sasa mtu asipomwona hapa atasema huyu Mbunge yuko wapi? Mheshimiwa Halima hapa ananyanyuka sasa hivi kuelekea kwenye Kamati. Kwa hiyo mwamini kila mtu yuko kwenye kazi, sawa Waheshimiwa Wabunge?

Nimalizie, hoja ile ambayo huwa ni ya bajeti ya jumla baada ya tarehe 10 huwa nyinyi mnaona, wakati wanachangia ile bajeti ndio wanachangia Mawaziri wote, kwa sababu pale unachangia chochote. Sasa siwezi kutarajia siku ya leo tumalize muda wa Wabunge tukiwapa Mawaziri ambao watapata fursa kule baadaye. Sasa tuchangie hoja iliyoko mezani, wasimamizi wa hoja iliyoko mezani wako hapa nasi humu ndani.

Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, atafuatiwa Mheshimiwa Ali Makoa na Mheshimiwa Jafari Wambura Chege ajiandae.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Napenda kwanza kumpongeza Mheshimiwa Lukuvi, Mheshimiwa Angeline Mabula kwa kazi yao nzuri sana waliyoifanya, kwenye Wizara ya Ardhi na kwa kweli wananchi wanawashukuru na mimi binafsi nawashukuru. Pia nawashukuru watendaji wote wa Wizara ya Ardhi, namshukuru Kamishna Mary Makondo na Naibu wake Nicholas Mkapa na watendaji wote kwa kazi nzuri wanazozifanya kwenye Wizara ya Ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakwenda kuchangia kuhusu ardhi yetu yetu ya Tanzania. Ardhi ya Tanzania iliyopimwa ni asilimia 25, ardhi nyingine iliyobaki haijapimwa. Ardhi ni mali, lakini ardhi hii pia ikipimwa mwananchi wa kawaida inamsaidia kupata mkopo benki. Pia ardhi hii ikipimwa inamsaidia huyo huyo mwananchi wa kawaida kwenda kulima mazao yake ya biashara, lakini pia na mazao ya chakula. Sasa basi ardhi yetu ya Tanzania na ukubwa wa eneo letu la nchi ni asilimia 25 tu ndio imepimwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali, iongeze nguvu kwenye kupima ardhi ili mwananchi wa kawaida aweze kufaidika na ardhi hii lakini pia ili Serikali yenyewe iweze kupata mapato. Kwa sababu ardhi inapopimwa mwananchi atapata hati anapopata ile hati anailipia kila mwaka na kuna mzunguko wa kulipia zile hati kila mwaka kwa maana hiyo Serikali itaingiza pesa, lakini pia huyu mwananchi atakuwa na uhakika wa eneo lake.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi, naomba kwenye bajeti ijayo Serikali kupitia Wizara ya Ardhi iongeze pesa ili maeneo mengi yaweze kupimwa nchini kwetu Tanzania. Liko tatizo ambalo ningependa kulizungumzia tatizo lenyewe ni kuhusu upungufu wa wataalam wa ardhi kwenye halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, halmashauri nyingi nchini kwetu zina upungufu wa wataalam wa ardhi na wataalam hawa ni kuanzia Wapimaji, Wathamini na Warasimishaji. Hivyo basi inasababisha ucheleweshaji wa upimaji wa ardhi kwenye halmashauri zetu. Naomba tuweze kuwatumia wanafunzi wanaomaliza Chuo cha Ardhi cha Dar es salaam, wanafunzi wanaomaliza Chuo cha Mipango hapa Dodoma lakini pia wanafunzi wanaomaliza kile Chuo cha Morogoro pamoja na Tabora.

Mheshimiwa Naibu Spika, wote hawa wanajua kupima hizi ardhi na wote wamesoma haya masomo ya kuthamini hizi ardhi, tungeweza kuwa-*comodate* hawa wanafunzi na kuwatumia ili waweze kupima ardhi yetu. Pia

Serikali inawasomesha kwa mikopo, kwa hiyo wanapomaliza shule nafikiri Serikali ingewatumia hawa wanafunzi ili waweze kutusaidia tuweze kutatua hili tatizo la kutokupima ardhi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipenda pia halmashauri nchini kwetu Tanzania zijitambue kwamba zenyewe ndio zenye mamlaka ya kupima ardhi kwenye halmashauri zao. Hata hivyo, niliona bajeti ya halmashauri hapa wakati inapitishwa, halmashauri nyingi zilikuwa hazijatenga fedha za kupima kwenye maeneo yao. Niombe basi hizi halmashauri ziweze kujitambua na kupima maeneo yao ili wananchi waweze kufaidika na hayo maeneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kupima hayo maeneo niweze kutoa rai kwa halmashauri zetu kumekuwa na watendaji wengi ambao wanafanya kazi *let say,* mtu anafanya kazi pale kwenye Halmashauri ya Mji wa Mpanda anaweza akapima yale maeneo lakini hafikirii miaka mia ijayo hayo maeneo yatakuwaje. Naomba watendaji wa wataalam wetu wa kupima ardhi wanapopima ardhi waipime kwa kuangalia kwamba leo tupo na kesho tupo lakini tuangalie miaka 100 ile ardhi itatumikaje.

Mheshimiwa Naibu Spika, unapoharibu mji kwa sasa hivi unapima barabara ndogo, lakini labda hujaweka eneo la kuchezea watoto au eneo la kupumzika, matokeo yake tunakuwa na miji ambayo haina maeneo ya kupumzikia, lakini haina *parking* na wala haina maeneo ya kucheza Watoto. Tunakuwa na *congested town* na kurekebisha ni vigumu kwa sababu unakuta mji umeshapimwa huwezi kubomoa zile nyumba. Niombe sana wataalam wanapopima miji waliangalie hilo wasi-*focus* kuangalia sasa hivi waangalie *hundred years to come* huu mji utakuwaje.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo ningependa kuzungumzia ni suala la vile vijiji ambavyo vinakua kwenda mji. Unakuta kata inaanza kukua, kuna majumba mazuri yamejengwa pale, unakuta kuna umeme na maji yamewekwa, lakini unakuta lile eneo halijapimwa,

matokeo yake tunajaza *squatter* kwenye miji *squatter* nyingi na tunapokuja kuzirasimisha kunakuwa na matatizo ya upungufu wa pesa, lakini pia uthamini utakuta mtu amejenga nyumba yake nzuri lakini inathaminiwa kwa pesa ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba zile vijiji ambavyo vinaanza kukua kwenda kuwa miji hizi halmashauri ziwe zinaviangalia na kuvipima ili kupunguza ukaaji holela na kupunguza migogoro ya ardhi kwenye maeneo yetu na kwenye hiyo miji.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo ningependa kulizungumizia hapa ni suala la hizi halmashauri ambazo zilikopeshwa pesa lakini hazijarudisha. Kwa sababu tunataka halmashauri nyingine zipate zile pesa ili ziweze kupima ardhi zao, tunaziomba zile halmashauri ambazo zilipewa pesa na Ofisi ya Ardhi ziweze kurudisha hizo pesa ili halmashauri nyingine ziweze kupewa hizo pesa na hizo halmashauri ziweze kupima maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuupongeza sana Mkoa wa Mbeya kwa sababu wao walipewa pesa, wamezitumia vizuri, wamepima na wamerejesha na walipata faida. Nawapongeza sana, lakini sipongezi mikoa kama ya Iringa na mingine ambayo Mheshimiwa Waziri aliiorodhesha hapo. Kwa hiyo niombe tu zile halmashauri zilizingatie hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nipende kutoa ushauri wa jumla kwa akinamama wa Tanzania. Napenda kutoa ushauri kwamba akinamama wa Tanzania, waume zetu wanapokwenda kununua ardhi basi tuhakikishe na sisi majina yetu yanakuwepo pale pembeni. Natoa ushauri huu kwa sababu akinamama wengi wamekuwa wakidhulumiwa nyumba, lakini wakidhulumiwa pia mashamba, lakini unakuta huyu mama aliolewa na huyu mtu akiwa kijana, wakaanza Maisha, wakanunua kiwanja kwa pamoja, lakini sisi kina mama kwa sababu huwa tunakuwa na tabia ile ya uvuvi wa kutaka kuweka majina yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nitoe wito, mume wako kama anataka kwenda kununua kiwanja basi mwambie na yeye aweke jina lako pale ili iondoe matatizo pale mmoja wenu anapoondoka duniani ili usiweze kufukuzwa. Naomba nitoe wito kwa akinamama wa kule Mkoani kwangu Katavi lakini pia kwa akinamama wa Tanzania na pia tusiwe wavivu wa kwenda kutafuta ardhi kwa sababu sheria haimkatazi mwanamke kununua ardhi wala kununua kiwanja, tusipende sana kuwatumatuma akinababa kaninunulie kiwanja halafu akifika pale haweki jina lako, matokeo yake unakaa pale *after 40 years* unaonekana kama wewe ni mpangaji kwenye nyumba ambayo mmejenga pamoja.

**TAARIFA**

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Taska Mbogo, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Sofia Mwakagenda.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa taarifa kwa mzungumzaji kwamba ni kweli anachosema kwamba sisi akinamama tujitahidi kuwaambia waume zetu watuandike majina. Hata hivyo, waume hawa Mheshimiwa Taska Mbogo wanapoenda kununua viwanja hawatuagi na wakati mwingine wananunua akiwa bahati mbaya amefariki unashangaa kumbe mko sita wakati wewe unajua uko peke yako. *(Makofi/ Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Sasa Waheshimiwa Wabunge huu mchango, hakuna akinamama wanaotumwa na waume zao kwenda kununua ardhi. Mheshimiwa Taska Mbogo sekunde kumi kwa sababu kengele ya pili ilikuwa imeshagonga.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Labda nipende kusema tu kwamba naupokea vizuri sana mchango wa Mheshimiwa Mwakagenda, ni mchango wenye tija lakini na mimi pia niendelee kutoa wito kwa akinababa ili kuondoa matatizo unapotoka duniani na mke

wako kupata shida kutoka kwa ndugu zako kumfukuza kwenye nyumba basi muweke mke wako kwenye hati ya nyumba. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia, wito wangu kwa akina mama ni huu.

**MBUNGE FULANI:** Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana namwona Mheshimiwa Mpembenwe ambaye ana mpango wa kuwa nao wanne, baada ya kusikia hapa kuna watu wana sita anashangaa kwa nini yeye ameambiwa wanne tu hawafiki sita.

Mheshimiwa Ally Juma Makoa atafuatiwa na Mheshimiwa Jafari Wambura Chege na Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi ajiandae.

**MHE. ALLY J. MAKOA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu lakini niwapongeze Waziri wa Ardhi, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na hata Kamishna Mkuu wa Ardhi kwa kazi kubwa wanazozifanya. Pia nisiwe mchoyo wa fadhila kumpongeza Kamishna wa Mkoa ndugu yangu Kabonge kwa majukumu makubwa anayohudumia Mkoa wa Dodoma, katika kuhakikisha wananchi wanapata hati.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo, niendelee na mchango wangu kwamba ardhi ni bidhaa pekee ambayo kama tutaitumia vizuri Taifa letu litaendelea kupata kipato endelevu. Ni kipato ambacho hakiyumbi kwa sababu hatutegemei kwamba kuna mwaka mapato yanayotokana na ardhi yatapungua kwa sababu kila mwaka tunapima ardhi na watu wanaendelea kulipa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ni chanzo pekee cha uhakika cha mapato ya Taifa letu ni lazima sasa kuiwekea miundombinu rafiki Wizara hii ili kuhakikisha mapato yanayotokana na ardhi kila mwaka yanaendelea kupanda. Nyenzo mojawapo ni kusaidia Wizara hii kupata watumishi wa kutosha katika zoezi la kuhakikisha kwamba upimaji wa ardhi unafanyika kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, halmashauri nyingi hazina Maafisa wa Ardhi. Unakuta halmashauri ina afisa mmoja huyo ndio apime, huyo ndio aandae ramani, maana yake utagundua kwamba hatuwezi kufikia malengo ya upimaji wa ardhi kama tunavyohitaji. Kwa hiyo Serikali iangalie, katika ajira ni vyema kuipa kipaumbele Wizara ya Ardhi kuajiri watendaji wa ardhi ili kuhakikisha kwamba zoezi hili la upimaji linakwenda kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja iliyo Mezani ni ardhi. Watanzania wengi vipato vyao ni vya chini sana. Mifumo ambayo inatumika kumilikisha ardhi ni mifumo ambayo si rafiki kwa Watanzania wengi ambao vipato vyao ni vya chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano, naweza nikasema kwamba, ardhi inaweza ikawa inauzwa milioni nne kwa kima cha chini na mnunuzi anatakiwa alipe kwa muda mfupi sana; miezi mitatu. Unajiuliza, ni Mtanzania wa aina gani huyu ambaye amelengwa kununua ardhi kwa bei kubwa kiasi hicho, hali ya kuwa kipato chao ni kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa nashauri sasa Wizara ya Ardhi ikishirikiana na TAMISEMI, kwa maana ya halmashauri, watafute miundombinu, watafute njia rahisi za kuhakikisha kwamba kila Mtanzania anamiliki ardhi kutokana na kipato chake alichonacho. Wanaweza wakaenda kupata wawekezaji. Mfano, wanaweza kuingia kwenye mabenki wakawa wanatoa hati, hati zinakwenda benki, Watanzania wenye kipato cha chini kidogo wakawa wanagomboa hati zao mabenki kwa kipindi hata cha miaka mitatu mpaka mitano, lakini kwa miezi mitatu Watanzania wachache sana wataweza kumiliki ardhi. Nina ushahidi; vijana wengi

wamerudisha ardhi baada ya kushindwa kukamilisha malipo kwa sababu wameshindwa kutekeleza mkataba walioingia wa kulipa ardhi kwa kipindi cha miezi mitatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, zoezi hilo la wananchi wengi kushindwa kununua ardhi linakwamisha mapato ya ardhi kwa sababu kama ardhi hainunuliwi maana yake hati hazitaandaliwa. Kama hati hazitaandaliwa maana yake Serikali itapoteza fedha nyingi kutokana na hati, lakini kama hati nyingi zitanunuliwa, Serikali itapata fedha nyingi sana. Kwa hiyo tuweke mfumo rahisi wa wananchi kupata hati mapema. Ikiwezekana, wananchi wauziwe hati na siyo wauziwe maeneo. Maandalizi ya hati yatangulie halafu ndipo watu watangaziwe kuuziwa viwanja ambavyo tayari vimekamilika hati. Hapo Ardhi itaendelea kupata fedha kupitia hati zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na migogoro; nawapongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, wanashughulika kikamilifu sana kutatua migogoro ya ardhi. Sasa pale kwetu, nilizungumza na Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri, kuna migogoro mitatu ambayo inawasubiri wao tu ili iweze kukamilika. Hapa nimekubaliana na usemi wake wa kusema kwamba, maeneo yote ya wananchi yaliyochukuliwa hayakulipwa fidia, warejeshewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tuna mgogoro ambao upo baina ya wananchi na halmashauri na wamiliki. Halmashauri imechukua maeneo ya mtu, ya wananchi, haikulipa fidia. Lakini imeyapima yale maeneo na maeneo yamekwishauzwa kwa wananchi na wananchi wamekwishalipa fedha zao. Sasa wananchi wenye maeneo hawakulipwa fidia, wamezuia shughuli yoyote ya maendeleo kama matamko ya Mheshimiwa Waziri. Kwa hiyo namwomba ile nia yake ya kwenda Kondoa kwa ajili ya kusaidia kutatua huu mgogoro kila mmoja apate haki yake, aendelee kuwa nao. Naomba baada ya zoezi hili tufuatane naye kwa ajili ya kwenda kutatua mgogoro huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, upo mgogoro mwingine wa ardhi wa wananchi, kijiji pamoja na Hifadhi ya Swagaswaga. Wananchi wa Mongoroma na maeneo yanayopitiwa na hifadhi ile wao wanalalamikia mipaka. Najua siku atakayokuja Waziri, tutakwenda kutembea na kuwasikiliza wale wananchi. Zoezi hili la migogoro ya ardhi inayohusiana na mipaka ni matumaini yangu kwamba tutakwenda kulimaliza kama tutafika kwa wananchi kuwasikiliza halafu sisi wenye mamlaka, Mheshimiwa Waziri, viongozi pamoja na wananchi na mimi Mwakilishi wao, tukae tuone namna gani tunakwenda kuitatua hii migogoro ili wananchi waendelee na shughuli za maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mgogoro namba tatu upo kati ya wananchi wa Iyoli na maeneo yanayohusiana na mgogoro Kata ya Kingale kati ya wananchi na Magereza. Waliotoa viwanja kukaribisha Gereza la King'ang'a wapo. Wenye kumiliki gereza hilo wapo. Viongozi tupo na sisi wawakilishi pia tupo; tunashindwaje kwenda kumaliza mgogoro huu ili wananchi waendelee na shughuli za kilimo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nina matumaini makubwa sana. Ahadi ya Waziri ya kwenda Kondoa kumaliza migogoro hii ikikamilika wananchi watakwenda kufanya shughuli zao za kujiongezea kipato na migogoro hii ambayo inaendelea itakuwa imekwisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Jafari Wambura Chege, atafuatiwa na Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi na Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu ajiandae.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwanza kwa kunipa nafasi. Nianze tu kusema kwa kuchangia Wizara ambayo binafsi nimeitumikia kwa zaidi ya miaka kumi. Naweza nikasema tu kwa wepesi

kwamba nimepata nafasi ya kuchangia Wizara ambayo imenilea kabla ya kuwa mwanasiasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nitumie nafasi hii kuwashukuru; wa kwanza kabisa Mheshimiwa Waziri, ndugu yangu, mzee wangu, Mheshimiwa William Lukuvi; Naibu Waziri, mama yangu, Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula. Pia nitumie nafasi hii kumshukuru Katibu Mkuu wa Wizara hii, dada yangu Mary Makondo na Naibu wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitawashukuru wafanyakazi na watendaji wote wa Wizara hii walioko ndani ya Wizara na wale ambao wanafanya shughuli kama wadau, kwa maana ya *private sector.* Haya mafanikio ambayo tunayaona ya Wizara hii, mimi kwa sababu nimekuwa kule natambua mchango mkubwa wa watu wote kwa ushiriki wao kwa pamoja ili kuhakikisha angalau tunaisukuma Wizara yetu hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa na maeneo matatu, nafasi ikiniruhusu nitakuwa na eneo la nne la kuchangia kwenye Wizara hii. La kwanza niombe nichangie kwenye ushiriki wa *private sector* kwenye Wizara hii ya Ardhi. Nianze kwa kusema kwamba ili mwananchi aweze kumilikishwa ardhi, maana yake kuna vitu vitatu au vinne vinakuwa vimefanyika; cha kwanza ni lazima ardhi iwe imepangwa; maana yake katika kupangwa ndiyo kutaainisha matumizi bora ya ardhi ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha pili, ardhi lazima iwe imepimwa. Kwenye kupimwa ndiyo tunapata ukubwa wa ardhi na maboresho mengine ili mwishoni mwananchi aweze kumilikishwa ardhi ile. Kwa haya matatu tokea Uhuru, toka mwaka 1961, ardhi ambayo imepangwa mpaka sasa tunavyozungumza ni zaidi ya viwanja milioni sita peke yake. Kati hivyo milioni sita, viwanja ambavyo vimepimwa kwa maana ya kwamba sasa vinakwenda ili viweze kupewa ardhi, ni milioni 2.5. Viwanja ambavyo mpaka sasa tunazungumza kwa maana ya umiliki wa mwananchi mmoja mmoja ni milioni 1.5.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushiriki wa *private sector* kwa mwaka 2015 kwenda 2020 ndiyo tumeanza kufanya shughuli ya urasimishaji kwenye maeneo yetu. Hawa watu, hizi *private sector* unaweza ukaona katika hiyo milioni sita ambayo ni miaka zaidi ya sitini katika kupanga matumizi ya ardhi, wao wameweza katika urasimishaji peke yake, katika milioni sita maana yake kuna viwanja milioni 1.6, hizi *private companies,* makampuni ya watu binafsi wameweza kuisaidia Serikali, kwa miaka mitano.Kwa miaka mitano wameweza kupima, kupanga ardhi viwanja zaidi ya milioni 1.6. Lakini *total* zaidi ya miaka sitini ni zaidi ya viwanja milioni 60; hilo ni la kwanza tu peke yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, katika kupima peke yake kwa miaka mitano toka 2015 hadi 2020, zaidi ya viwanja 557,000 ambavyo vimepimwa katika kazi ya urasimishaji na hizi *private companies.*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe Mheshimiwa Waziri, kwa kutambua mchango huu pamoja na kwamba amezungumza yapo makampuni ambayo hayafanyi kazi vizuri, tukae nao tuone yale makampuni katika makampuni 163, yale manne ambayo mwanzoni amekuwa akiyasema hayafanyi kazi vizuri, yale 159 twende nayo. Tukiwaweka pembeni hawa tutambue kwamba hawa ndio wana kazi kubwa sana ya kutusaidia sisi. Unaweza kuona kwa miaka mitano namna gani wmaeingia katika shughuli ya kupanga, kupima na mwishoni wakaenda kwenye kurasimisha, namna ambavyo wamefanya kazi kubwa sana. Tusiwahukumu wote kwa pamoja, twende kwenye yale makampuni mengi ambayo yamefanya kazi vizuri tuweze kwenda nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi nilikuwa namsikiliza Mheshimiwa Waziri wa Kenya, siyo vizuri kusema lakini naomba nitoe kama mfano, alikuwa anazungumza kwa miaka mitano (2015-2020) wao kwa kutumia *private sector* wameweza kupima viwanja zaidi ya milioni tano. Unaweza ukaona wao wamejikita sana kutumia *private sector* kwa miaka mitano wamepima viwanja milioni tano. Sisi toka Uhuru bado tuna milioni sita peke yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiziacha hizi *private companies* zote tukazihukumu katika mfumo huo maana yake ni kwamba Serikali peke yake ndiyo itaingia kufanya hiyo kazi. Sisi wote tunatambua Waheshimiwa Wabunge, watumishi kwenye halmashauri hawatoshi. Kwa mfano Rorya nina mtumishi mmoja tu Afisa Ardhi. Maana yake sina Mpimaji wala sina mtu wa Mipango. Maana yake tukiwaachia wao wafanye kazi hizi hatutaweza kufikisha malengo, lakini pia hatutatimiza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi katika ukurasa wa 119 ambao umesema kwa muda mchache ili twende na kasi ya kupima maeneo yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tutambue kwamba kampuni hizi zimetoa ajira kwa vijana wetu. Kampuni hizi ambazo leo hii tukiziacha pembeni zimekopa mikopo, tukiziacha pembeni zisifanye shughuli hii tutakuwa hatuwatendei haki na yawezekana tukaanzisha mgogoro mkubwa sana kwenye sekta ya ardhi huko mbeleni tunakoelekea.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni ushiriki wa halmashauri. Kwa mujibu wa sheria mwenye mamlaka ya upangaji nchi hii ni halmashauri. Hata hivyo, twende mbele turudi nyuma, kazi hii tumeona imebaki ikifanywa sana na Wizara ya Ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi wakati tunapitisha bajeti ya Wizara ya TAMISEMI tuliona ndani mle, nilikuwa naona moja ya vipaumbele vyake ni kuhakikisha ardhi yote inapimwa. Hata hivyo, ulikuwa ukienda kwenye bajeti kuona kwamba namna gani wanakwenda kufanya kazi hiyo kama Wizara ya TAMISEMI, hakuna fedha iliyotengwa kwa ajili ya kazi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tukirudisha kwamba halmashauri peke yake kwa sababu kwa mujibu wa sheria ndiyo wana mamlaka ya kupanga na kupima wafanye kazi kwa kupitia mapato yao ya ndani, mathalani mimi Rorya nakusanya milioni 800 tu kwa mwaka. Milioni 800 nichukue asilimia 40 iende kwenye shughuli za maendeleo, bado niitoe

iende kwa ajili ya kupima ardhi. Hawatakwenda na kasi tunayoizungumza ya miaka mitano ya utekelezaji wa Mpango na Ilani ya Chama chetu Cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii kumwomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha aone namna gani anaiongezea fedha Wizara ya Ardhi, hasa kwenye kipengele hiki cha upimaji ili hizi halmashauri huko chini ziingie kwenye uratibu na kutafuta namna ambayo wanaweza wakapima ardhi kuendana na kasi ya Wizara namna inavyotaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii kuomba sana kwa sababu kama kweli dhamira yetu ni ya pamoja, kwamba angalau sasa zaidi ya eneo la kilometa za mraba 883,000 tumepima asilimia 25 peke yake, tukiiachia Wizara peke yake iendelee na huo mfumo na kwa kutoa maelekezo kwa halmashauri zitafute fedha zenyewe ziende kupima, hatutakuwa tumewatendea haki hawa wananchi wetu. Lakini pia hata Serikali bado tutakuwa tunaimba wimbo uleule na inawezekana tusifikishe malengo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu ni ushiriki wa Tume ya Taifa ya Mipango na Matumizi ya Ardhi. Moja ya majukumu ya Tume hii ni kuwezesha mamlaka zote za upangaji wa matumizi ya ardhi katika kutambua mipango ya matumizi ya ardhi, zikiwemo halmashauri zote. Ukienda kwenye bajeti unaweza ukaona tume hii, ndiyo maana miaka yote watu wengine wamekuwa wakisema hatuoni tija ya tume hii, lakini inafanyaje kazi? Unaweza ukaona kwenye fedha ya maendeleo imetengewa bilioni 1.5 peke yake, namna gani itaweza kufanya kazi hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana nilikwenda mbele nikashauri kwamba kama kweli tuna mpango tumejikita kama Serikali na nchi kwa ujumla tunataka tuhakikishe tunapima ardhi kwa muda mfupi, ni lazima tutengeneze *agency. Agencies* kama ilivyo *TBA,* lazima tuwe na wakala ambaye anahusika na shughuli zote za kupanga na kupima ardhi. Ili tunapokwenda kumpangia fedha kwa

muda mfupi awe na fedha nyingi lakini utekelezaji wake utakwenda kwa kasi kama ilivyo *TBA* ambayo ni utekelezaji wa nyumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo *agencies,* wapo mawakala wengi ambao wanafanya kazi kwenye maeneo mengine. Ili tuondokane na hili na ili tuendane na mpango wa miaka mitano kwa kasi, ni lazima tutafute namna ambayo tutaiongezea fedha Tume ya Taifa ya Mipango, lakini tutengeneze *agency,* shughuli ya kupanga na kupima ardhi isibaki kwenye kurugenzi moja tu peke yake ndani ya Wizara, tujaribu namna ya kuipanua ili iendane na kasi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, naomba nizungumzie kuhusiana na makazi. Wabunge wengi tumekuwa tukitoa mawazo na michango mingi sana inajikita kwenye ardhi, lakini hatuendi sana kutafuta namna ambavyo tunaweza tukapata suluhu ya upande wa nyumba ili hiyo *concept* ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi iweze kujaa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii kushauri na pia niweze kuunga mkono maoni ya Kamati kwamba angalau kwa mwaka huu kama ikipendeza, Wizara iweze kukamilisha *Housing Policy,* Sera ambayo itaratibu shughuli za ujenzi wa nyumba. Hapa Wabunge wengi tumekuwa tukisema namna ambavyo mashirika, kwa mfano, Shirika la Nyumba na Taasisi nyingine, zinajenga nyumba kwa bei kubwa sana. Hata hivyo, leo tukiulizana humu ndani bei elekezi ya ujenzi wa nyumba, mfano Rorya, hatuitambui. Kama tukiwa na *Housing Policy* maana yake ni nini? Itakuwa na maelekezo ya ujenzi wa nyumba kuanzia ngazi ya mkoa, wilaya na maeneo yote ili hawa wanaojenga nyumba watakuwa wanajenga kwa kutambua bei elekezi iliyopangwa kwenye maeneo yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe Mheshimiwa Waziri, kwa mwaka huu angalau sasa tuwe na *policy* ambayo itatuongoza sote kama Taifa ili tukizungumza Sera ya Nyumba tuwe na Sera ya Nyumba kama zilivyo sera za

nyuki na nyingine. Hili litakuwa ni jambo zuri ambalo kimsingi naamini yale maoni mengi ambayo tumekuwa tukiyasema hapa Bungeni namna ya ku-*regulate* bei za ujenzi wa nyumba itakuwa vizuri na tutakuwa tumei-*control* vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, tumekuwa tukiongea naye mara kwa mara; kuna wananchi wangu kule walifanyiwa uthamini toka 2011 Rorya, nafikiri hili analifahamu. Niombe atakapokuwa anakuja kufanya majumuisho angalau na wao wapate jibu. Toka 2011 wamefanyiwa uthamini ili kupisha huduma za umeme, lakini mpaka leo ninavyozungumza kama ambavyo huwa nakwambia wale wananchi hawajalipwa fidia. Ni zaidi sasa ya miaka kumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, anajua kwa mujibu wa sheria baada ya miezi sita, *valuation* ile ilitakiwa ipitwe na wakati. Nitumie nafasi hii kumwomba sana Mheshimiwa Waziri atakapofanya majumuisho alizungumzie hili ili na wao waweze kusikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi, atafuatiwa na Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu na Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo ajiandae.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyeniwezesha wakati wa asubuhi najiandaa kuja kuchangia Wizara hii muhimu, nilimwomba Roho Mtakatifu anipe hekima na busara nichangie Wizara hii muhimu kwa maslahi mapana ya Taifa letu Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitajielekeza kwenye maeneo yafuatayo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la kwanza ni eneo la upangaji, upimaji na umilikishaji; Eneo la pili ni changamoto za sekta ya ardhi; Eneo la tatu ni ushiriki wa sekta binafsi; Eneo la nne ni mashamba yasiyoendelezwa; na eneo la tano muda ukiruhusu, ni Mabaraza ya Ardhi na mwisho nitahitimisha na Shirika la Nyumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la upangaji, upimaji na umilikishaji; labda nirejee historia kidogo. Mnamo mwaka 1896, kiwanja cha kwanza kilipimwa nchini wakati wa Mkoloni. Hali kadhalika, tangu Uhuru mpaka leo, upangaji ni viwanja milioni sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninavyosema upangaji, ni hesabu ya viwanja kwenye ramani za mipango miji katika mchakato wa uandaaji wa kiwanja. Ukipima hivyo milioni sita kwa mujibu wa utaalam, unaweza ukajikuta huwezi kupata milioni sita vyote vitapungua kwa sababu ya mokorongo na maeneo ambayo ni *hazardous areas.*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni upimaji wa viwanja. Viwanja vilivyopimwa tangu Uhuru ni milioni mbili na laki tano tu na viwanja vilivyotolewa umiliki ni takribani milioni moja na laki tano tu. Nilikuwa najaribu kuwasiliana na wenzetu wa Kenya, wenzetu sisi tunasema upangaji viwanja milioni sita, Kenya milioni sita ni hati miliki; mnaona kuna tofauti kidogo. Kwa hiyo nataka kujenga hoja ya namna gani hapa; hoja yangu ya msingi hapa ni kasi ndogo ya upimaji, upangaji na utoaji wa hati nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nijielekeze kwenye ushauri; nitaeleza baadaye kwenye hoja hiyo ya namna gani sasa tunaweza kuongeza uwezo wa upimaji, upangaji na upatikanaji wa hati nyingi sana kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende eneo la pili, kwa sababu ya muda naongea haraka haraka kidogo ila kuna

pointi muhimu nitaongeza kidogo maelezo. Niende kwenye eneo la changamoto za sekta ya ardhi. Changamoto za sekta ya ardhi nchini ni kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ya kwanza ni gharama za umilikishaji. Mheshimiwa Waziri atakumbuka alikuwa ukipiga simu kuwataka wananchi waje wachukue hati. Unajua changamoto kubwa inayotukuta ni nini? Kuna gharama inaitwa tozo ya *premium,* tozo ya mbele, hii gharama ni kubwa. Kwa hiyo wananchi wengi, hasa wa kipato cha chini, wanashindwa kumudu gharama hizi. Kimsingi, tukiziondoa gharama hizi za *premium,* na Waziri yupo hapa, mjamba wangu, Mheshimiwa Lukuvi, namwambia kwa dhati mwamko wa wananchi kutaka kupata hati utakuwa mkubwa sana na watajitoa kulipia kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine la changamoto ni ukosefu wa kanzidata ya uhakika ya hati miliki za viwanja. Leo hii nina uhakika mjomba wangu hapa Waziri Mheshimiwa Lukuvi nikimuuliza anieleze takwimu sahihi ya viwanja vilivyopimwa nchini kidogo kutakuwa na mtihani. Kwa hiyo nishauri Wizara, sasa tuanzishe kanzidata na zaidi teknolojia imekua, tuweke mfumo tu wa teknolojia, watu waweze kujua na mtu yeyote nchini aweze kujua na kila mtu awe na *access* ya kujua, kwa hiyo ni jambo dogo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee eneo lingine la uhaba wa watumishi; ni kweli changamoto kubwa Sekta ya Ardhi kama nitakosea *Surveyors* hawazidi 600 wa Wizara ambao ukiwachukua na wale wa kwenye halmashauri. Maafisa Ardhi hawazidi takribani labda 2,000 na kidogo. Sasa nchi nzima unaona namna gani kuna huu uhaba wa watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe Waziri na niombe Wizara ya Fedha pia, ione namna ya kuona kutatua kero hii ya watumishi. Pia, leo hii Wizara ya Ardhi imehamisha watumishi kutoka Mamlaka ya Serikali za Mitaa yaani TAMISEMI

kwenda Wizara ya Ardhi tuwatengenezee utaratibu bora watumishi wale.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii ukienda kwenye mikoa hawana vitendea kazi, utamwambia Kamishna wa Ardhi aende kwenye halmashauri hana gari ataendaje? tutawezeshe ili wafanye kazi nzuri. Pia natarajia kuona hata kwenye wilaya tupeleke vitendea kazi ili kusudi hii kazi iendelee vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende eneo lingine la uwezeshaji mdogo wa shughuli za Sekta ya Ardhi; nishukuru sana, sasa nimeona kuna mabadiliko na niseme kwa dhati kitendo cha Serikali kuanza ku-*finance* halmashauri ni wazo jema sana, lakini fedha bado ndogo, ndogo sana. Sasa nitoe tu ushauri wangu Wizara ya Fedha tuki-*finance* Wizara ya Ardhi itatusaidia kupata pato la kutosha kabisa na nitaeleza baadaye namna gani tunaweza kupata fedha hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine nijielekeze katika migogoro ya ardhi; unajua migogoro ya ardhi ikiwa mingi ni miongoni mwa *indicator za failure* ya Wizara. Kwa hiyo namwomba mjomba wangu suala hili la migogoro ajitahidi tulimalize kwa kutumia Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya hadi Wenyeviti wa Vijiji kule kwenye ngazi ya wilaya, wafanye kazi hiyo vizuri, ili awe Mamlaka ya Rufaa tu, kwenda kwenye kijiji, ataenda vijiji vingapi, kwa hiyo tuwaachie wale wafanye kazi hiyo kwa uhakika zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niende eneo lingine la ushiriki wa Sekta Binafsi; hapa naomba nijielekeze kwenye makampuni ya upimaji. Hapa nitulie kidogo, mimi nina *success story* hapa ya Dodoma, nazungumzia Mbeya na wapi, jamani mbona Dodoma hamsemi, Dodoma hata hela haikupewa imefanya maajabu hapa na sisi tunakaa hapa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana tu Manispaa ya Dodoma ilivyokabidhiwa Mamlaka ya Ustawishaji Makao

Makuu yaani *CDA,* tulikabidhiwa Mamlaka ile na deni la bilioni 12 na fedha kwenye akaunti ya milioni 400 tukapewa maelekezo na Serikali tupime watumishi wapate viwanja, hatuna fedha, mimi ndiyo nilikuwa Mtendaji Mkuu kama Mkurugenzi wa Manispaa *by then.* Tulichokifanya tukashauriana ndani ya Jiji la Dodoma tukasema tukitumia watumishi wetu hawa ambao wapo wachache hatuwezi kufanikiwa, tukaalika Sekta Binafsi, mimi nilifanya majaribio, nilitumia pale Michese viwanja 2,000 nikapeleka watumishi wangu wa halmashauri waliniletea vile viwanja baada ya miaka mitatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi fedha tunazoweka kwenye halmashauri tuwaachie wasimame wenyewe bila Sekta Binafsi tunakwenda kufeli asubuhi kweupe. Sekta Binafsi nilivyo-*engage* makampuni haya yametusaidia Dodoma tukapima viwanja 200,000; sikupata fedha Serikali Kuu, sikwenda kukopa mkopo benki, hii ni *success story* tukitaka kujifunza tusiende Ulaya mje Dodoma hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, unajua wakati mwingine huwa tunaamini ngozi nyeupe, Kunambi ningekuwa ngozi nyeupe hapa wangeamini, sasa kwa sababu ni Mtanzania huwa hatutaki, lakini tujifunze tu na sisi ni wadau, kwa sababu tuna uwezo wa kufanya maajabu ndani ya Taifa hili. Kwa hiyo Dodoma ni *success story* na nadhani Wizara ya Ardhi wachukue kama *model.*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine nimpongeze Waziri juu ya suala la mfumo *ILMIS - Integrated Land Management Information System.* Kengele?

**MBUNGE FULANI:** Bado.

**GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa mfumo ule, kwa sababu ukienda Dar es Salaam kuna mafanikio, ameuleta Dodoma na nimwambie kwa dhati, Dodoma viwanja hivi 200,000 vinaenda kupata hati kupitia ule mfumo, nampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu Mheshimiwa Waziri ule mfumo sasa aupeleke kwenye halmashauri zote nchini, kwa sababu gharama ya ule mfumo Mheshimiwa Waziri, Afisa Ardhi mmoja anaweza akatengeneza hati 300 kwa siku. Kwa hiyo kwa sababu ya uhaba wa watumishi tulionao, ukimtumia Afisa Ardhi mmoja ukampa *server,* akawa *integrated* akawa na *communication* na Kamishna na Msajili kule na ana *computer* yake, ana-*server* na *printer,* yeye kazi yake ni kubofya tu taa, hati 300 zinatoka. Leo hii tunatengeneza hati bila mchapa hati yule anachapa hati 10 kwa siku, tutafika 200,000 kweli hapa Dodoma. Kwa hiyo, niishauri Wizara kwa dhati kabisa katika eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye eneo la mashamba yasiyoendelezwa, pale jimboni kwangu Mlimba kuna Shamba la Kambenga ekari 1,000 hazijaendelezwa Serikali ipo. Pale Mlimba kuna Shamba la Serikali hekta 5,000 Kata ya Mgeta hazijaendelezwa, mwaka wa tano Serikali ipo. Kuna Shamba la Balali ekari 2,000 halijaendelezwa lipo. Waziri anapokuja kuhitimisha hapa bajeti yake anieleze mjomba wangu kwa dhati nini mpango sasa wa Wizara kwenda kuyaondoa mashamba darasa haya ili wananchi wa Mlimba wapate maeneo na mashamba walime.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine niende haraka haraka, ni eneo hili na kwa dhati kabisa juu ya Mabaraza ya Ardhi, ukienda kwenye *level* ya Mabaraza ya Kata wale siyo Wanasheria na bahati nzuri uliyekalia kiti wewe ni Mwanasheria utanisaidia kwenye eneo hili, wale hawapaswi kutoa maamuzi kwa sababu bahati mbaya zaidi maamuzi yao yale yanakuwa ni rufaa kwenye Mabaraza ya Wilaya. Ushauri wangu wawe wasuluhishi tu, wale wanaosuluhishana wakishindana basi rufaa iende kwenye Baraza la Ardhi la Nyumba na Wilaya ndiyo lifanye maamuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, kwa dhati kabisa niombe, Mungu atubariki sote. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu atafuatiwa na Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo na Mheshimiwa Benaya Kapinga ajiandae.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye Wizara hii muhimu. Kwanza ninayo kila sababu kumpongeza Mheshimiwa Waziri, baba Mkwe wangu Mheshimiwa William Lukuvi, maana nimeoa Ilula pale, Semkinywa, kwa hiyo kwangu Mheshimiwa Waziri ni baba Mkwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze pia Mheshimiwa Naibu Waziri, Dkt. Angeline Mabula, bila kuacha kuwapongeza Watendaji Wakuu wakiongozwa na Bi. Mary Makondo akisaidiwa na Naibu Katibu Mkuu Kaka yangu Nicholas Mkapa. Nawapongeza sana pamoja na wasaidizi wao kwenye Wizara, kwa kweli mnaendelea kufanya kazi vizuri katika ujumla wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, binafsi nitajielekeza katika maeneo mawili. Hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 87 hadi 89 inaeleza sana juu ya urasimishaji, kwa maana ya upangaji, upimaji na umilikishaji wa hati eneo hili, lakini eneo B nitajiekeleza kidogo kwenye mgogoro mdogo uliopo katika Hospitali yetu ya Mloganzila na sio mgogoro ni jinsi ya utatuaji wa jambo lile kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye eneo la urasimishaji baada ya kumpongeza Mheshimiwa Waziri, lakini nimpongeze kimahsusi sana baada ya kukubali maana ni mtiifu sana, kukubali maelekezo ya Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli tarehe 24 mwezi Februari pale Kibamba wakati anazindua ile Stendi ya Magufuli alitoa maelekezo ya kukabidhiwa hati wananchi wa Jimbo la Kibamba na Wilaya ya Ubungo hati ya takribani ekari 52.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima na unyenyekevu mkubwa wa Mheshimiwa Lukuvi alituletea baada ya kufufua mipaka ile hati yenye ukubwa wa ekari 75.2 nampongeza sana, sana Mheshimiwa Waziri. Aliileta

ndani ya siku mbili tarehe 26 nikiwepo pale pamoja na Wakurugenzi na Mheshimiwa *DC* tuliipokea na maelekezo yake. Tumwahidi Waziri tutatekeleza vile ambavyo wanatarajia, hakuna mtu atakula kipande kwa ajili ya kujenga nyumba yake na makazi yake na mkewe au dada yake, tunapeleka maslahi mapana ya wananchi katika eneo lile. Namshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumze juu ya urasimishaji nimekuwa nikisema hapa na juzi tu tarehe 18 nilikuwa na swali la msingi katika eneo hili na niliongea, lakini leo niseme kwa kuweka vitu sawa, hali ya upimaji ndani ya Wilaya ya Ubungo, lakini hususani Jimbo la Kibamba, ndani ya mitaa yote 43 iliyopo pale, nirudie kusema hali bado si shwari sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nia yetu ya upangaji, upimaji na umilikishaji tuone wananchi wanaenda kujiinua kiuchumi ndiyo dhamira kubwa na niliwahi kusema hapa hata kauli ya Mheshimiwa Waziri ile ya mwaka 2017 mwezi wa 10 tarehe 23 juu ya kusema jambo hili liende vizuri aone wananchi wanajiinua kiuchumi halijafikia kwenye lengo. Kama sasa tuna hali hii ambayo takribani wananchi 153,000 ambao tayari viwanja vyao vimefikia katika hatua ya upimaji tu wa awali, karibu watu 53 lakini kwa haraka juzi hapa nilijibiwa kwamba takribani viwanja 1,925 tayari vina maombi ya hati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vina maombi 1,900 tuseme 2,000 kutoka 53,000 ambao wameanza au vimeanza kupimwa kwa awali, unaitafuta asilimia hapa huioni ya utija. Taarifa ambazo ninazo kama Mbunge, hati kuandaliwa ni jambo moja, zilizoandaliwa 1,900, lakini hati ambazo zimetoka ni 845 na hii leo niirudie tena, maana *Hansard* ilikaa vizuri kwenye majibu ya msingi, lakini sio katika maswali yangu ya nyongeza. Hati 845 ndiyo zilitoka kwa wananchi katika mitaa 43 ukigawanya kawaida ukawapa tu kila mtaa hati 19 na *point* kwa sisi wahasibu tunasema hati 20 kwa kila mtaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kweli takribani mradi ambao umeanza 2013 wa miaka kumi hadi 2023 tumeambiwa leo asubuhi hapa mradi utaenda kuisha 2023, kwa Kibamba pale umeanza 2017 baada ya kauli ya Mheshimiwa Waziri mpaka 2023 tutakuwa na miaka mitano tu, leo tupo chini ya asilimia 10 ya utoaji hati, yale malengo mahsusi yatafikia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sina shaka juu ya uwajibikaji wa Mheshimiwa Waziri, lakini najua na nitamwambia anaangushwa sehemu gani. Hali hii ina changamoto nyingi sana, lakini kwenye hili ndiyo maana hawafiki ni kwa kuwa pia kuna shida moja ya mashamba limezungumzwa hapa. Yapo mashamba ambayo kama bado tunaendelea kuchelea kuyafuta hati zake maana yake tutashindwa kufanya upimaji wa jumla wa viwanja vingine ambayo yapo karibu na maeneo hayo. Kwa hiyo nimwombe Mheshimiwa Waziri na hilo pia anaweza akaja kulizungumza juu ya mkakati, kwa sababu nimeona maelezo yake yapo vizuri kabisa, nia njema ya kupima mashamba, lakini pia na kufuta mashamba ambayo yatakuwa hayana tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili eneo, tunazo changamoto karibu tatu, nne na nitazisema na nilieleza hapa. Huu mpango ni mzuri, sina shaka nao, yenyewe *program* na nia yake ni nzuri, dhamira yake kwa wananchi ni nzuri sana, lakini bado ipo shida juu ya usimamizi wake. Jukumu la Serikali, jukumu la Wizara wala siyo kupanga, wala siyo kupima, wala siyo kuthamini zile ardhi, siyo jukumu lao kimsingi au kisheria, hili ni jukumu la Mamlaka za Miji pamoja na Sekta Binafsi na wameeleza vizuri kwenye hotuba ya Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la Wizara ni kusimamia na kuratibu mambo haya yaende vizuri, lakini lao moja kwa moja ni kuona hati zinatoka ili ile dhima kuu ya jambo hili iweze kufikiwa. Tulivyoanza hili jambo maelekezo ya Wizara kwenye kuratibu yalieleza akaunti zote za urasimishaji zifunguliwe kwa ushirika baina ya mkandarasi na Kamati ya Urasimishaji, kuna shida ikatokea hapo,

alivyohusishwa mkandarasi kwenye akaunti zile ndiyo upigaji wa fedha kwenye akaunti za benki ulifanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilieleza juzi tukashindana kwenye *figure,* hela zimepigwa nyingi leo wananchi wa Jimbo la Kibamba wanalia, lakini wanalia kwa sababu wamekosa majibu. Msimamizi na mratibu akisaidiwa na halmashauri zetu kule hawezi kutoa majibu kwa wananchi waliotoa hela zao. Katika hii hatua ya awali tu, nieleze ukweli, malipo yale ni kati ya 150,000 mpaka 200,000. Ilianza 200,000, mratibu na msimamizi akaona ni nyingi akasaidia 180,000 ikaenda hadi 150,000, watu wamejitahidi kulipa, wapo wanaolipa kidogo kidogo wapo wamelipa kwa ukamilifu, lakini hizi hela zilizolipwa awamu ya kwanza zimepotea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baadaye baada ya Mheshimiwa Waziri kuliona, ndiyo maana namsifia sana, akaja akawaondoa wakandarasi akaacha timu ya Kamati ya Urasimishaji, sasa mambo yanaenda vizuri na najua hata majibu yale ya msingi ni watu 30,000 tu ambao ndiyo wamelipia ni wale baada ya utaratibu umekaa vizuri. Hoja yangu ilikuja hawa kabla wakati wamehusishwa wakandarasi na wakapiga zile hela, thamani ya fedha za wananchi wa jimbo lile zimekwenda wapi? Tunazionaje? Maana hati hamna na hela zao hawajui zilipokwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niliomba juzi hapa kama kweli yule Mtaalam wa Fedha, Mkaguzi wa Fedha na Mdhibiti wa Hesabu za Serikali kama anaweza kuingia hapa, maana nao wana taratibu zao, lakini nafikiria hizi hela ni za wananchi, wananchi wa Serikali hii na hii hapa ni Kamati yetu ya Ukaguzi, *I mean* Mdhibiti Mkuu *(CAG)* apewe nafasi kama siyo yeye nani jicho la tatu, kati ya Serikali na wananchi juu ya hela zilizopigwa, ndiyo nia yangu jicho la tatu liende. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa haraka sana hizo ni fedha, Mheshimiwa Waziri atatwambia mkakati wa Serikali juu ya jicho la tatu kwenye eneo hili. Hata hivyo, kuna makampuni yanasemekana yamefilisika, makampuni kati ya

makampuni 162 ambao walitwambia kwenye taarifa zao wameyasajili kama nchi, lakini yapo makampuni 32 yameingia kwenye mchakato huu ndani ya Jimbo la Kibamba, haya makampuni ni ukweli hayafanyi kazi, lakini yapo makampuni yasiyopungua manne, matano mengine yametamkwa yamefisilika na Mheshimiwa Waziri anajua hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimsifie Waziri amewahi kufika kwenye vikao vyake ndani ya mkoa, ndani ya wilaya na akachukua hatua. Zipo hatua amechukua, hatua mojawapo aliyochukua, nishukuru sana na taarifa yake imesema amechukua hatua, ndiyo maana amefuta leseni za kampuni tatu, lakini amechukua hatua kwa kusimamisha kwa muda makampuni tisa, amechukua hatua kwa kuyapa onyo makampuni 41, lakini amezisimamisha kampuni 15, nampongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili la ziada, hayo tu hayatoshi na mengine amewapeleka TAKUKURU wafanye kazi, hakuna majibu kwa wananchi nini mpaka leo na hapa tunaambiwa mwaka mmoja na nusu ujao mradi unaisha, tusije tukawa kama benki tuambiwe, mlango ukifungwa tunapotaka kwenda kuchukua hela ndani ya benki, je, zikiwa nje tunatolewa? Waliokuwepo ndani wamefungiwa huduma itawaishia watu wa ndani? Watuambie au huo mwaka 2023 Mheshimiwa Naibu Waziri jana amezungumza hapa ikiisha ndiyo tunarudi kwenye utaratibu wa kawaida kule kwa furaha, naomba tupate majibu hapa, huu unaishajeishaje na hela zetu hatujui zilipokwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumaliza kwa sababu siwezi kumaliza yote na hata lile la Mloganzila...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Kengele imeshagonga hata hivyo.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru, kwa haya machache niliyosema lakini

najua dhima itakuwa imeeleweka na Mheshimiwa Waziri atasema vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa kiwango kinachofaa. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo atafuatiwa na Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nitumie fursa hii kukushukuru sana kwa nafasi hii ili niweze kuchangia bajeti ya Wizara ya Ardhi. Mimi nina msemo wangu mmoja huwa nasema, mtu ukiwa mnafiki ukiwa kijana, ukizeeka lazima utakuwa mchawi, na mimi kwa sababu sina mpango wa kuwa mchawi kwenye uzee wangu, napenda nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, William Lukuvi; Naibu wake Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Makamishna wote kwa kazi kubwa wanayofanya kwenye Wizara ya Ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa changamoto za Wizara hii ukiona wachangiaji wachache maana yake changamoto nyingi zimefanyiwa kazi, tumebaki na sisi wachache ambao tunadhani pia watatusikiliza, watakwenda kuzimaliza ili huko mbeleni changamoto zisiwepo kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakwenda kwenye masuala mahsusi kwa sababu yale maswala ya kijumla jumla sijui kuna mgogoro mpaka kati ya mtaa na mtaa, sijui kata na kata hayo siwezi kuzungumza kwa sababu ule ni mipaka ya kiutawala tu, haikuzuii kununua ardhi mahali popote, haikuzuii kufanya shughuli zako. Kwa hiyo ni masuala ambayo yatamalizwa huko kwenye ngazi ya mitaa, ngazi ya kata, wilaya na mikoa, hapa tunazungumzia masuala mahsusi ambayo tunadhani yanahitaji *attention* ya Wizara ili mambo yaweze kuwa rahisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo langu la kwanza; Arusha tuna mgogoro mkubwa sana wa ardhi ni mgogoro kati ya Jeshi letu la Wananchi na Kata za Mushono, Mlangalini

na Nduruma. Ni mgogoro wa miaka mingi sana, lakini mgogoro ambao umeshika kasi mwaka 2012. Tunaishukuru sana Serikali, baada ya changamoto kuwa kubwa, Mheshimiwa Waziri Mkuu kipindi hicho alikuwa ni Mheshimiwa Mizengo Peter Kayanza Pinda, aliitisha kikao tarehe 20 Machi, 2012 kwa ajili ya kujadili mgogoro huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye kikao hicho maelekezo yaliyotoka. Katika maelekezo hayo pamoja na kuwa na maagizo kumi, lakini maelekezo ya msingi yalikuwa ni mawili. La kwanza, Jeshi irekebishe mipaka yake upya na kuacha eneo lenye mgogoro kwa wananchi; na la pili, Jeshi wapewe eneo la mlima ambapo wananchi hawana mgogoro nalo eneo hilo wapo tayari kulitoa. Maelezo haya ya Serikali yaliwasilishwa na Naibu Waziri Mheshimiwa Goodluck Ole-Medeye kipindi hicho, aliyafanya kwa wananchi tarehe 28 Machi, 2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto iliyojitokeza pale Serikali ilikwenda mwaka 2012, ikabainisha baadhi ya maeneo ambayo wanadhani wanatakiwa waondoe watu wakaenda wakafanya uthamini mwaka 2012, wakaondoka zao. Mwaka 2012, 2013, 2014, 2015 mpaka 2019 na tunafahamu kwa mujibu wa sheria uthamini ukishafanyika ikipita miezi sita kuna *interest* kidogo inalipwa, ikifika miaka miwili inabidi ule uthamini ufanywe upya, lakini uthamini wa mwaka 2012, Serikali imekuja kurudi mwaka 2019 na kuwalipa watu kwa uthamini wa siku za nyuma ambao hautambuliki kwa mujibu wa sheria kwa sababu miaka miwili tayari ilishapita.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kibaya zaidi mwaka 2015 Serikali ilikwenda pale na Mkuu wa Wilaya wa kipindi hicho na viongozi wengine wakawahakikishia wananchi kwamba, eneo hili Serikali haina *interest* nalo tena kwa hiyo, wananchi wenye maeneo yao wanao uhuru wa kufanya shughuli zozote. Wale wananchi wakaamua kuyauza yale, maeneo wakawauzia wadau wengine na wakati huo Serikali hiyo hiyo, ilishakwenda kutengeneza mchoro, kuna *approved plan*

pale *No. CAO/65/01/6* na wananchi ambao wanataka kujenga walienda kuomba vibali vya ujenzi wakapewa na halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi walikwenda kwenye mitaa na vijiji wakapitishiwa, wamejenga mpaka magorofa, leo Serikali inakuja, inataka kutumia mabavu na kutaka kwenda kuwaondoa wale wananchi. Kosa lililofanyika hapo mara baada ya Serikali kurudi mwaka 2019, ikaja na orodha yao ile ile ya mwaka 2012, wakaanza kutumia nguvu na mabavu wanawarushia watu hela kwenye *Mpesa* na kwa njia nyingine ili mradi tu zile hela zilizokuja ziweze kwenda.

Mheshimwia Naibu Spika, badala ya kumlipa mwananchi ambaye anaishi pale kwa wakati huo na ambaye amejenga, wamekwenda kumlipa mtu ambaye alishauza na alishaondoka siku nyingi. Nadhani hapa TAKUKURU wana kazi ya kufanya kuwatafuta wale watu waliolipwa, warudishe zile fedha na Serikali ifuate maelekezo haya ya Serikali ambayo yalisimamiwa na Waziri Mkuu wa nchi hii, ili wale wananchi wabaki pale wafanye shughuli zao na kama kuna maelekezo mengine yoyote basi ni vizuri Serikali ikakaa chini na wahanga wale tutafute *solution* ya kudumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu kwenye jambo hili, kwanza, nimepata taarifa kwamba Mheshimiwa Waziri huenda akawa Arusha kwenye ziara ya kikazi wiki ijayo, tulikuwa tunamwomba Mheshimiwa Waziri akutane na wahanga hawa ili apate picha pana ya jambo hili na mwisho wa siku Serikali ifanye maamuzi kwa maslahi mapana ya wananchi wa nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu la pili kwa Mheshimiwa Waziri, namwomba kwamba kama kuna mchakato wowote wa kutoa hati kwa Jeshi la Wananchi usitishwe hadi hapo mgogoro huu utakapohitimishwa na Serikali itakaporidhika na hali halisi ya mchakato mzima kwenye eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo langu la pili, shida ya hii nchi kuna *double standard,* kuna maeneo mengine maamuzi yanafanyika *very fast*, kuna maeneo mengine maamuzi yanafanyika kuangalia maslahi mapana ya nchi, kuna maeneo mengine kuna *ku-delay*. Yako mashamba ambayo hayajaendelezwa kwenye nchi hii ambayo Serikali imeyachukua, lakini kwa upande wa Jiji la Arusha kuna kigugumizi kikubwa sana, liko shamba la Bondeni *City* ambalo kwanza halijaendelezwa na mimi nina ushahidi na Mheshimiwa Waziri anafahamu kwamba halijaendelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi na yeye tuliwahi kuhudhuria kikao kikubwa kabisa kilichoongozwa na Kiongozi Mkuu wa Nchi hii yeye akiwepo, Mheshimiwa Mhagama, Waziri wa TAMISEMI na Makatibu wao Wakuu na mimi nilikuwepo, maelekezo yalishatoka pale lakini kuna kwenda mbele, kuna kurudi nyuma. Ziko baadhi ya hatua zimechukuliwa, kwanza, lilitakiwa lipatikane eneo mahususi kwa ajili ya kujenga stendi, kwenye hili Waziri nampongeza sana kwa sababu, eneo limeshapatikana na Wizara ya TAMISEMI kupitia *TACTIC imeji-commit* kutoa fedha, pale tutajenga stendi ya kisasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi letu kwa Mheshimiwa Waziri, hili jambo alipe uzito unaostahili, tunaomba hili jambo sasa aende akalihitimishe, tunaomba hili jambo ajiridhishe kwa sababu kwanza taarifa ziko kwamba mmiliki mwenyewe kwanza sio raia wa Tanzania, taarifa zipo pia mmiliki mwenyewe ameshakufa, taarifa zipo kwamba halmashauri waliingia makubaliano ya kiujanjaujanja na yule mwekezaji ya hiyo asilimia tano, eti Jiji asilimia tano yule mhusika asilimia 95.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kupigwa mkwara wakabadilisha, ikawa Jiji asilimia 10 yule asilimia 90. Sasa hivi tena wamepigwa mkwara mwingine tena wanasema Jiji asilimia 50 yule mwingine asilimia 50, huu ni utani, kwa sababu, Jiji la Arusha tuna changamoto kubwa ya ardhi, tumetenga fedha kujenga vituo vya afya, kujenga shule na maeneo mengine ya maendeleo. Tulikuwa tunaomba Serikali

ikasimamie jambo hili kwa haki na kwa mujibu wa sheria na ikiwezekana hiyo ardhi irudi Serikalini ili maeneo ambayo hakuna shule tukajenge. Maeneo hakuna vituo vya afya tukajenge na mambo mengine yaweze kuwa mazuri zaidi. Tunamwomba Waziri mwenye dhamana ya ardhi aingilie kati ili mgogoro huu uhitimishwe kwa mujibu wa sheria na tufanye masuala ya maendeleo badala ya kuanza kunung'unika na kuzua masuala mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwangu la tatu ni kuhusu urasimishaji. Tuna dhamira nzuri sana, lakini kama kuna zoezi ni kichefuchefu ni urasimishaji. Tuna Kata pale kama ya Sekei, kuna Kata ya Balaa, Kata ya Lemala na Kata nyingi za Jiji la Arusha ambazo watu wamekwenda kufanya zoezi la kurasimisha, wamechukua fedha za watu na zoezi halijakamilika, zaidi ya mwaka umeshakwenda. mambo haya hayatoi sura nzuri kwa Serikali, Mheshimiwa Waziri Lukuvi ni mtu anayefanya kazi kwa weledi sana, watendaji wake wanaendana na kasi yake vizuri sana, heshima aliyoijenga kwenye nchi hii ni kubwa sana, lakini hili la urasimishaji litampunguzia umaarufu kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ombi langu atakapokuja Arusha tukutane pia na viongozi wanaotoka kwenye Kata zote zinazofanyiwa urasimishaji, ili tumweleze changamoto halisi na yeye kama Waziri mwenye dhamana na timu yake waende wakatutafutie majawabu ya kudumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, kwa heshima na taadhima naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Waheshimiwa tumalizie na Mheshimiwa Benaya Kapinga.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kuwa mzungumzaji wa mwisho wa *session* hii ya asubuhi. Niungane na wenzangu kwa dhati kabisa, kumpongeza mtani wangu mla kale kanyama katamu, Mheshimiwa Lukuvi, hongera sana pamoja na Naibu

Waziri, lakini na wataalam kule. Kwa kweli mmefanya kazi nzuri na hii inaonesha wachangiaji wamekuwa wachache tofauti na pale nyuma Wizara hii ilikuwa na wachangiaji wengi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nachangia eneo moja eneo la migogoro. Nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri, Jimboni kwangu kumekuwa na matatizo mengi ya migogoro kwa muda mrefu kuanzia mwaka 2017, nina orodha hapa zaidi ya watu 3,000, hawa wananchi wa Kata ya Maguu, Kijiji cha Mkuwani na vijiji vingine vya Jirani. Hawa wananchi kwa miaka zaidi ya minne wanahangaika na maeneo yao ambayo yalikuwa mashamba sasa yamechukuliwa na Wilaya ya Nyasa kufanya mradi wa panda miti kibiashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu ni mzuri sana, lakini utaratibu uliotumika ni wa hovyo mno, umesababisha tumefika mahali sasa hivi wanapigana risasi pale kijijini. Tumefika mahali wananchi hawa wanachukuliwa mali zao, tumefika mahali wananchi hawa hawawezi kufanya shughuli ya kiuchumi kwenye hayo, maeneo ambayo walikuwa wanayamiliki tangu wengine walivyozaliwa na wengine sasa hivi ni wababu, wana wajukuu na vitukuu, lakini imefika mtu mmoja tu ameamua huu mradi uanzishwe na kuwafukuza hawa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2019 aliendа Waziri Mkuu, wananchi wale walishika mabango tunadhulumiwa ardhi yetu, tunadhulumiwa ardhi yetu. Waziri Mkuu alitoa maelekezo kwa viongozi ambao leo pia Mheshimiwa Waziri ametoa maelekezo hapa kwamba, viongozi waliopo huku watatue kero za wananchi. Kwa bahati mbaya sana yale maelekezo viongozi wale hawakuyafanyia kazi, wananchi hawa wamehangaika ngazi zote katika mkoa wetu hawakupata masuluhisho, mwisho wa siku waliamua kuja hapa. Namshukuru sana sana Waziri, alipiga simu na sasa hivi angalau wanapumua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe Mheshimiwa Waziri ile ahadi aliyoisema kwamba atakwenda kule kwenda

kuona naomba aitekeleze, kwa sababu bila yeye hatutapata masuluhisho, kwa nini nasema hivi? Shida kubwa hao viongozi aliowaelekeza hapa na wao wana *interest* na maeneo hayo. Nimefuatilia nimegundua kwamba, maeneo yale viongozi wa maeneo ya kule nao wameamua kujiingiza kwenye hii miradi, sasa mwananchi akilalamika eneo langu linaporwa, hana masuluhisho hawezi kutoa utatuzi wa ile shida ikiwa yeye pia ni mmiliki wa mradi ule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, inahitaji mtu mwingine kama alivyofanya Waziri. Nimesikia hapa wenzangu wanasema tuwaachie Mwenyekiti wa Kijiji, sijui na nani anayefuata na mwingine, wengine ndio wanufaika wa hii miradi sasa atatoaje masuluhisho? Kwa hiyo, mgogoro huu umeleta shida sana sana sana, leo hii ukifika Mbinga Mheshimiwa Waziri watakupa jogoo, mbuzi na ng'ombe kwa majibu aliyoyatoa hapa siku ile kwa wale wananchi wachache waliokuja kumwona. Kwa hiyo, nimpongeze sana sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri, ninachosema ule mradi ni mzuri sana, ingewezekana kabisa. Kwa sababu, kwa maneno yao wanasema kwamba wameshauriwa kimazingira kwamba sasa eneo lile linatunza maji ya Ziwa Nyasa, kwa hiyo, ni lazima liwekwe vizuri, lipandwe miti, sawa. Kwa nini hawakufikia kuwashirikisha hawa wananchi wamiliki wa yale maeneo na kuwaambia sasa jamani mmekuwa hapa kwa muda mrefu, sasa hivi imefika mahalI hapa tunataka tupaboreshe tufanye mradi wa kimazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa badala ya sisi wa eneo fulani au watu fulani kuwanyang'anya ninyi maeneo yenu, basi muwe sehemu ya huu mradi, kwani hili haliwezekani? Lingefanyika hili, pengine lisingeleta usumbufu ambao sasa hivi zaidi ya miaka minne wale watu hawana sehemu ya kulima. Kwa hiyo, ninachoshauri Mheshimiwa Waziri aje na maelekezo mazuri kuhusiana na hawa wananchi kwenye ardhi ambayo wamekuwa nayo, wamekufa nayo na wengine wanaendelea kuzeeka nayo mpaka leo hii, lakini sasa hawana haki nayo kabisa. Imefika mahali wamepigwa

risasi watu pale kabisa kabisa, sasa unampigaje mtu mwenye haki yake risasi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi ni kweli Watanzania tuko hivyo? Kilichofanyika ni kwamba, kabla ya mwaka 2012, eneo lile lilikuwa Wilaya moja, sasa hivi Wilaya ile imegawanyika iko Wilaya ya Nyasa na Wilaya hii ya Mbinga.

**TAARIFA**

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Stella Manyanya.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuwa mimi ni Mbunge ninayetoka Nyasa na kwa mchango huu unaotolewa na Mheshimiwa Mbunge, jirani yangu kuhusu mgogoro huu uliodumu kwa muda mrefu kidogo, ambao nakubaliana kwamba, mpango na mradi unaoendelea pale wa miti ni mzuri na kwa sababu mwekezaji sio lazima atoke sehemu za mbali tu na asiwe Jirani yetu. Kwa hiyo, jambo jema ni kwamba hata wao wanaweza kuendeleza katika misingi ya mradi ule lakini bila kuwa na migogoro. Kwa hiyo ninachoomba ni kwamba siku ikitokea Mheshimiwa Waziri anaenda huko, basi mimi Mbunge wa Nyasa niwepo pia, ili kuhakikisha kwamba haki zinatendeka katika pande zote mbili. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Benaya Kapinga, malizia mchango wako.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana na taarifa yake naipokea, nilikuwa nasubiri aongee vile alivyosema, ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kugawanyika kwa mipaka hakumwondolei mtu haki ya kumiliki mali, sisi wote ni Watanzania, tuna haki ya kufanya shughuli eneo lolote ili mradi hatuvunji sheria. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Waziri, sikuwa na maneno mengi nilitaka nimwambie hili ili aendelee kutusaidia kama alivyotatua maeneo mengine na sisi akatutatulie huu mgogoro wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa kipindi chetu cha kwanza, mchana tutaendelea na wachangiaji; niwataje wachache ambao tutaanza nao jioni, Mheshimiwa Aleksia Asia Kamuguna, Mheshimiwa Soud Mohamed Juma, Mheshimiwa Francis Leonard Mtega, Mheshimiwa Oliva Semguruka na tutaendelea kutaja Wabunge wengine.

Nilishawahi kusema hapa, nirudie tena, Waheshimiwa Wabunge orodha inayoletwa hapa mbele unapata fursa ya kuchangia ukiitwa jina, kwa hivyo, orodha ikiletwa hapa mbele maombi huwa yako mengi kama tunavyoona Wabunge wengine wanaelekea kwenye Kamati. Kwa hiyo, usije ukawa umeshikilia namba kwamba kwenye orodha ulikuwa namba moja halafu hujaitwa. Makatibu wa pande zote mbili mnaoleta majina hapa, ni kama vile sasa mnakuwa mmeleta sheria hapa mbele yaani kwamba umetupangia sisi wahitaji tumuite nani. *(Makofi)*

Kimsingi ni kwamba ninyi mnaleta orodha ya majina, nani anamuita nani ni Kiti kinaamua kimuite nani, nadhani hilo litakuwa limeeleweka vizuri. Vyama vinaleta orodha hapa mbele ya wachangiaji, lakini nani anapangwa wa kwanza ama wa mwisho ni vizuri mnavyokutana kwenye maeneo yenu, hili jambo lifafanuliwe vizuri ili mtu asiwe anajisikia vibaya kwamba nilikuwa wa kwanza sasa nimekuwa wa mwisho. Hakuna wa kwanza, hakuna wa mwisho Kiti ndicho kinachoita majina. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja kamili jioni leo.

*(Saa 7.15 Mchana Bunge lilisitishwa mpaka Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11 Jioni Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano ya hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Tutaanza na Mheshimiwa Oliver Semuguruka, atafuatiwa na Mheshimiwa Aleksia Asya Kamguna na Mheshimiwa Soud Mohamed Juma ajiandae.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi kwa jioni ya leo na kuwa mchangiaji wa kwanza. Nampongeza Waziri wa Ardhi na Naibu wake dada yangu Mheshimiwa Angelina kwa kazi nzuri wanazozidi kuzifanya pamoja na watendaji wote wa Wizara na Katibu Mkuu dada yangu Mary Makondo. Nawapongeza sana kwa ajili ya kazi zote wanazozifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nijielekeze moja kwa moja katika changamoto zilizopo katika ardhi. Migogoro ya ardhi imekuwepo mingi na haiishi. Sababu mojawapo ni hawa wazee wa Mabaraza ya Ardhi. Wananchi wanyonge wamekuwa ndiyo *victim* wakubwa. Hawa wazee wa Baraza la Ardhi hawapati posho yao kwa wakati. Unaweza ukakuta wamepata posho baada ya miezi mitatu, minne au mitano. Sasa hapo tunawawekea wananchi ambao ni wa hali ya chini kupata shida. Kwa sababu, ambao wanapata haki katika haya Mabaraza ya Ardhi ni wale ambao wana kitu ambao ni matajiri lakini wanyonge wanapata shida.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, mtu anaenda pale ana kesi yake, lakini yule Mzee wa Baraza la Ardhi atazungusha nenda rudi, atakayepata haki ni huyu ambaye amempa kitu kidogo na hiyo inatokana na wale wazee kutokupata posho yao kwa wakati. Kwa hiyo, niiombe sana Serikali yangu, kaka yangu Lukuvi naomba awaangalie kwa umakini hawa wazee wa Baraza la Ardhi, awalipe posho yao kwa wakati, ili hii migogoro ya kupata rushwa iweze kutoka. Rushwa haiwezi kukoma kwa *style* hiyo. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri wa Ardhi aweze kuliangalia hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee pia vijana. Vijana wengi hawana ajira. Wanazunguka na karatasi na vyeti vyao kila kukicha. Ningeshauri ardhi ya akiba inayotengwa na vijiji wangepewa hawa vijana wakalima, wangepewa hawa vijana wakapata hati, hatimiliki itakayowawezesha kupata mkopo wa pembejeo. Wakishapata ile mikopo watalima, watapata mazao. Mfano mzuri ni mimi mwenyewe nalima mpunga, nina heka na heka, naweza kupata tofauti na hii hapa ambayo ajira yangu niliyonayo ya wananchi, naweza nikapata hela kutoka huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tukiwaangalia hawa vijana au nikimtolea pia mfano Mariam Ditopile. Naye ni mkulima na anapata hela kutokana na huo ukulima. Kwa hiyo wakiwapa vijana hatimiliki wakamiliki kutoka katika hizi ardhi za vijiji vya akiba, wakafanya hata biashara ya kilimo. Wanaweza wakapata hela wakaondokana na hali duni ya maisha. Kwa hiyo naomba Mheshimiwa Waziri aangalie hali za vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ardhi ya akiba inayotengwa mara nyingi hupewa wawekezaji wenye hela zao na matajiri. Hawa watu ambao hawana uwezo wanakosa. Naomba Serikali iangalie kama kuna mwekezaji ambaye sio tajiri sana, wasiangalie wawekezaji wanaotoka nje, waweze kuwasaidia hawa wawekezaji wa ndani ya nchi ambao wanaweza wakalima vitu na wakasaidia ndugu zetu wakatoka katika hali duni ya Maisha na kuwaondolea umaskini. Kwa hiyo, naomba huu upande wa wawekezaji wasiangaliwe sana matajiri, waangaliwe pia wanyonge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Ardhi naomba ijikite sana kusafisha Maafisa Ardhi na Wapima ambao wamekuwa ni chanzo cha migogoro. Unaweza ukaenda ukakuta mpima anakuja mpima sijui binafsi, anakuja mpima wa Serikali, anakuja sijui mpima gani. Sasa inakuja kutokea unakuta kila mtu ana hati, shida inayokuja kutokea huyu ana hati na huyu ana hati. Mwingine anasema Serikali ilikuja ikapima, huyu mwingine anasema nilileta mtu binafsi alikuja

kupima, huyu ana Sekta Binafsi ya kupima. Kwa hiyo, naomba Serikali ijikite kuangalia mpima ambaye anatambulika na Serikali kuliko kuzidi kuchanganya wananchi katika ule upimaji wa ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya uwepo wa Mabaraza ya Ardhi ya Kijiji, Kata na Wilaya bado lipo ongezeko la migogoro ya ardhi. Migogoro ya mipaka kati ya kijiji na kijiji kingine, migogoro kati ya wakulima na wafugaji, hapa ndiyo balaa kabisa. Mkulima analima mazao yake, mfugaji anaenda anapeleka ng'ombe au mbuzi au *whatever,* wale wanyama anaowafuga wanaenda wanaharibu mazao ya yule mkulima. Ukiangalia, mfugaji ndiyo ana hela kuliko mkulima. Kwa hiyo anaweza kufanya chochote kile. Kwa hiyo naomba Serikali yangu iangalie haki ya hawa watu. Huu mgogoro wa mkulima na mfugaji wauangalie kwa undani sana. Waache kunyanyasa, hakuna mtu anayependa kutokuwa na kitu. Kila mtu anapenda awe na kitu lakini ukimnyanyasa yule ambaye hana kwa kweli inatia huzuni na simanzi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna migogoro kati ya vijiji na taasisi za Serikali, wenzangu wameshaongea. Unakuta kuna *beacon,* huyu anakuja anasema *beacon* yangu iko hapa, *beacon* yangu iko pale, lakini hiyo yote inatokana na wale Wapima. Ndiyo maana nilianza kumwambia Waziri wangu wa Ardhi angalia hawa Wapima kwa umakini. Sio kuangalia tu mtu huyu anapewa, wewe nenda ukapime, mara sijui nina taasisi fulani napima, wawe ni watu wanaoeleweka ili kuondoa hiyo migogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee pia migogoro hii msingi wake inasababishwa na tamaa. Rushwa kwa baadhi ya watendaji katika Mabaraza, waliopewa kusimamia migogoro ya ardhi kwa njia ya usuluhishi. Narudi kule kule kwa wale wazee wa Mabaraza. Hawa hawa ndiyo wanakuwa chanzo cha migogoro lakini migogoro yao ni kutokulipwa posho. Unakuta huyu mzee wa Baraza anadai posho yake miezi mitano, miezi minne na kuendelea. Sasa kweli, akutane na pedeshee amwambie sasa huyu hapa,

lazima ummalize mimi nakupa hela. Atashindwa kweli kama mwanadamu? Ili kumaliza rushwa, naomba tuwalipe hawa wazee kila anapodai posho yake mwezi au siku ikiisha, nafikiri wanalipwa kwa siku, wawalipe posho yao kuondoa huo mkanganyiko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujua Wizara ina mpango gani mahsusi wa kuhakikisha inasimamia na kuwajibisha watendaji hawa. Endapo mtu amejulikana kabisa huyu mtu ametoa rushwa, je, Serikali inamchukulia hatua gani. Naomba Mheshimiwa Waziri na Naibu Wake waangalie kuanzia kwenye Kata, wasiangalie wilayani wala mkoani. Huku chini ndiyo chanzo cha yote, huku vijijini. Kwa hiyo, wakitaka kupata *information* iliyo sahihi, waanziae huku chini ndiyo kuna shida. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri wa Ardhi afuatilie kwa undani sana. Tusipofuatilia, hii rushwa haitakaa iishe katika mambo ya ardhi kutokana na huo mpango unaoendelea kuwepo, ambapo hatuwasaidii hawa ambao wanatakiwa kusuluhisha ili kila mtu apate haki yake, zaidi tunazidi kuwaumiza hawa wanyonge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano kuna hawa ma-*secretary* ambao wanawasaidia hawa Wazee wa Mabaraza, unaweza kukuta wamelipwa miezi mitatu na miezi mingine hawalipi. Au wanalipwa kwa miezi mitatu mitatu. Hawana ajira, namwomba Mheshimiwa Waziri Lukuvi awasiliane na Waziri wa Utumishi ili tuweze kujua hawa watu watalipwa kwa wakati au...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Aleksia Asia Kamguna, atafuatiwa na Mheshimiwa Soud Mohamed Jumah na Mheshimiwa Francis Leonard Mtega ajiandae.

**MHE. ALEKSIA A. KAMGUNA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia. Awali ya yote hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha sote kuwa salama. Nawapongeza Wizara ya Ardhi, ukweli Wizara ya Ardhi ni kati ya Wizara ambazo zilikuwa na matatizo makubwa sana katika nchi hii lakini wamejitahidi. Hapa walipofikia si haba, wamefanya kazi kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, panapokuwa na manufaa hapakosekani changamoto. Wizara hii pamoja na kujitahidi lakini kuna changamoto hususan za mipaka. Nazungumzia mipaka iliyopo katika Bonde la Kilombero, Wilaya ya Malinyi, Ulanga, Kilombero yenyewe na Jimbo la Mlimba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hizo wilaya zina matatizo. Tumepata bahati ya kupata ardhi nzuri, tunamshukuru Mungu, lakini ardhi tuliyopata inatutesa. Kuna mwananchi ambaye amezaliwa Malinyi tangu miaka hiyo, yawezekana labda Mjerumani au Mwingereza yuko pale kwenye Bonde la Mlimba, kwenye Bonde la Ngombo. Sasa leo hii wanamwambia yule mwananchi ahame. Sasa hatujui akihama anaenda wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara ya kwanza wanasema lile eneo lilipimwa mwaka 1952, lilipimwa na *GN* ya kwanza ikawekwa 2012. Wakaja wakaweka tena *GN* ya pili 2017. Zote hizi zinam-*limit* yule mwananchi asiweze kulima, asiweze kuwa na makazi pale. Sasa tunajiuliza kwa miaka yote hiyo, huyu mwananchi ataenda kuishi wapi? Kazaliwa pale, kakulia pale na pengine hata Morogoro Mjini haijui. Leo unamwambia ahame Ngombo, ahame Mlimba, ahame Kilombero na sasa hivi Kilombero ni mji mkubwa sana wa Ifakara, wenyewe wanafahamu, lakini mnatuambia tuhame.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naiuliza hii Wizara, kama iliweza kupima mwaka 1952 wakati wananchi wale walikuwa wachache tu hawakuweza kuwaelewesha kuwa eneo limepimwa na mwondoke wakaja wakaweka *GN* 2012

na 2017. Hebu niiulize Wizara, Tanzania ni kubwa na ina ardhi nzuri hususan Morogoro na hizi wilaya ambazo nimezitaja. Sasa naiomba Serikali itoe tamko, je, kwa sasa hivi tufuate *GN* ya 2012 au wale wananchi wafuate *GN* ya 2017, kwa maana wale wananchi hawawezi wakafanya kazi zozote za kimaendeleo, wapo wamekaa. Wakienda kulima watu wa *TAWA* wanawafuata ambao ni askari wa maliasili wanasema hili ni eneo la maliasili. Wakikaa hivi hivi ina maana kwamba watu wanakaribisha umaskini. Je, hawa watu tunawafanyaje? Naomba Wizara inisaidie hilo ili wale watu waweze kujua kama wanaishi pale na kama hawataishi watupe mbadala kwamba waelekee wapi. Tanzania ni kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, nazungumzia mipaka vile vile kati ya wakulima na wafugaji. Mkoa wa Morogoro ni kati ya mikoa ambayo ina changamoto kubwa sana ya migogoro kati ya wakulima na wafugaji na hii migogoro inatokana na mipaka. Hakuna mipaka ambayo inaainisha kwamba hili ni eneo la wakulima na hili ni eneo la wafugaji. Matokeo yake watu tunasema tuna amani. Ukweli katika ule mkoa sehemu kubwa amani haipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kipindi cha kampeni tulienda kufanya kampeni tunakuta kabisa mtu anaenda analisha sio ya kuambiwa, kwa macho yangu, anaenda analisha ng'ombe wake anapeleka kwenye mashamba ya watu. Mimi mwenyewe pia lilinipata kwenye shamba langu, nawakuta vijana wanaenda, nawauliza mbona mnalisha kwenye shamba, wananiambia unaniuliza mimi, muulize ng'ombe!

Mheshimiwa Naibu Spika, niambie, hivi unamkuta mtu analisha ng'ombe kabisa kwenye shamba lako, unamuuliza, anasema unaniuliza mimi, muulize ng'ombe unamjibu nini? Unamfanyaje mtu kama huyu? Ni mateso. Yaani tunaishi kama vile sisi ni wahamiaji. Uende kwenye *GN* unaambiwa uondoke, basi ulime angalau ujikwamue mkulima mdogo, unaambiwa mashamba hayo ndiyo malisho kwao. Sasa huyu mwananchi wa Ifakara, mwananchi wa Kilombero na Kilosa

na Mvomero katika Mkoa wa Morogoro, anaishije huyu? Siku zote ukiangalia sana mkulima na mfugaji, mkulima kipato chake ni cha chini na mkulima huyu ndiyo anayegandamizwa. Naomba majibu kwa haya masuala yangu mawili. *(Makofl)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Wizara kama wanataka kuwe na amani tungechukua ile mipaka tuweke ekari kama moja yaani huku wakulima na huku wafugaji. Anayevuka kuelekea kwa mwenzake ni mgomvi, maana sasa hivi amani hakuna! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nataka kuongelea ni hizi *institution* zetu za Serikali, kwamba tuna shule na hospitali za Serikali, lakini zile hospitali zina viwanja, shule zina viwanja. Ukiangalia sana unakuta kwamba shule nyingi wanafika wakati vile viwanja vinachukuliwa na watu wenye pesa. Sasa ukiuliza kwa nini, kwa mfano kiwanja cha mpira, watu wameweka wamejenga shule ya Serikali, wana kiwanja chao cha mpira cha michezo, lakini baada ya muda mwenye pesa akiona eneo linamfaa anaenda anajenga nyumba. Sababu ni nini? Hakuna, eneo lile halina hatimiliki, lingekuwa na hatimiliki wale watu wasingevamia lile eneo. Kwa hiyo, naiomba Wizara tujitahidi kupima mali za umma. Shule zetu, hospitali zetu ili wale watu wachache wenye pesa wanaorubuni wasiweze kuingilia pale hatimaye wakachukua maeneo ya umma na baadaye tukakosa hizo sehemu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la nne na la mwisho kabisa, nashindwa kuwaelewa Wizara ya Ardhi kwamba, hivi mtu anajenga bondeni, anajenga sehemu ambayo haitakiwi mtu kujenga. Anajenga wa kwanza, mnamwangalia; anajenga wa pili, mnamwangalia, wanafika 1,000 mnasema wabomolewe waondoke. Sasa mlishindwa nini kumsimamisha yule wa kwanza badala ya kulete hasara kubwa katika Serikali? Hilo nalo naomba mnieleze, kwani kunakuwa na matatizo gani kuwasimamisha mtu ambaye amejenga kwenye sehemu ambayo ni bonde au njia ya kupita maji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimetoka kwenye maji. Watu wanakwambia, maji yanakimbia watu, sio kweli hata siku moja. Maji hata ujenge nyumba ya aina gani...

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kamguna, kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Kuchauka.

## TAARIFA

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nataka nimpe taarifa mchangiaji. Siyo tu kwamba hao watu wanaojenga wanaonekana, mpaka umeme wanaletewa na pengine hata kama huduma ya maji wanaletewa vilevile. Halafu baadaye wanakuja kuwaambiwa wabomolewe. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kamguna, unapokea taarifa hiyo?

**MHE. ALEKSIA A. KAMGUNA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimeipokea hiyo taarifa. Nakubaliana naye kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hebu angalieni na mara nyingi wanaojenga pale ni wale walalahoi. Wale watu tunawachukuliaje? Mtu amejipigapiga akajikusanyakusanya akajenga pale kwenye bonde, tunamwachia, halafu akija kubomolewa tunasema hatukulipi *compensation* kwa sababu wewe umejenga sehemu ambayo haikutakiwa. Kwani mwanzo anajenga ninyi hamkumwona? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, katika hilo, kama mtakuwa mnatuachia hivyo, basi inabidi wale muwalipe. Ni wenyewe mnataka, kwani mwanzo hayakuwepo mabonde? Mbona yalikuwa hayazibwi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache naomba kuwasilisha. Naunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Soud Mohammed Juma, atafuatiwa na Mheshimiwa Francis Leonard Mtega na Mheshimiwa Michael Kembaki ajiandae.

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nami naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwa kunipa hii nafasi kuweza kuchangia katika Wizara hii muhimu ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Pia naomba niwashukuru kwa dhati Mheshimiwa Waziri Lukuvi pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri Angelina Mabula na timu yake ya Watendaji ikiongozwa na Ndugu Mary Makondo pamoja na Ndugu Nicholous, Naibu Katibu Mkuu pamoja na timu nzima ya watendaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli, hii timu imefanya kazi nzuri sana katika kipindi cha miaka mitano iliyopita na halikadhalika wanaendelea kufanya vizuri. Napenda kuelekeza mchango wangu katika maeneo mawili na kama muda utaruhusu, basi nitaongeza na mawili madogo. Sehemu ya kwanza kabisa napenda kuelekeza mchango wangu katika masuala mazima ya upimaji na umilikaji wa ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama unavyofahamu, wenzangu wengi wamechangia hapa kuhusu umuhimu wa kufanya haraka kupima ardhi yetu ya Tanzania na kuimilikisha ili kuweza kupunguza changamoto ambazo zinakabili ardhi yetu. Kila tukichelewa basi changamoto zinaongezeka na kuna uwezekano, kwa kuwa sasa hivi tuko katika uchumi wa kati wa kiwango cha chini, basi itakuwa Tanzania ni nchi ya mfano ya kuwa na *squatters* ambao wako katika uchumi wa kati katika daraja la juu. Kwa hiyo, ni vyema tukafanya haraka kuweza kuipima ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu zinatuonesha kwamba kuanzia mwaka 2007 mpaka mwaka 2021 tumeweza kupima ardhi vijiji 2,204 tu. Katika kipindi chote

hicho, ni sawa sawa kwamba tumepima vijiji 169 kwa mwaka mmoja na kama *trend* itaendelea hivi, basi tujue kwamba tunahitaji miaka 58 ili tuweze kukamilisha kuipima ardhi yote ya Tanzania. Yaani ni mwaka 2079 ndiyo tutakuwa tumepima ardhi yote ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 imeelekeza kwamba tuhakikishe tunaongeza wigo wa upimaji wa ardhi ya Tanzania ili angalau kwa kila mwaka tuweze kupima vijiji 826 ambapo kama tutakwenda na *trend* hiyo, basi itatuchukua miaka 12 kuweza kupima ardhi yote ya Tanzania. Kwa hiyo, tutakuwa tumepiga hatua kubwa kama tutakuwa tumefanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Lukuvi amefanya kazi nzuri sana. Nami nafikiri hatuna zawadi ya kumpa zaidi ya kumsaidia kuweza kufikia lengo la kuipima ardhi ili atakapoondoka katika Wizara hii ionekane kwamba ameacha *legacy* ya kumaliza au angalau kupunguza tatizo la upimaji na umilikaji wa ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzetu wa ardhi wamefanya kazi kubwa ikiwa ni pamoja na kuwajengea uwezo wenzetu wa Halmashauri. Kuna Halmashauri 102 zimejengewa uwezo kati ya Halmashauri zote 135. Ni kazi kubwa. Halikadhalika wameweza kutenga fungu la shilingi bilioni 3.5 na hizi fedha kuzikopesha Halmashauri na Manispaa ili kuweza kuharakisha au kuchochea upimaji wa ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, jambo la kusikitisha, wenzetu wa TAMISEMI nafikiri hawakufanya kama ni *core function* yao hii ya upimaji na umilikaji wa ardhi. Sasa napenda tuwanasihi sana, tuwaombe na tuwa-*task* wenzetu wa TAMISEMI waone kwamba suala la upimaji na umilikaji wa ardhi ni *core function* yao badala ya kuiacha Wizara ya Ardhi kufanya shughuli hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, halikadhalika katika bajeti ambayo amewasilisha Mheshimiwa Waziri hapa, kuna

mpango wa kuajiri vijana ambao watakwenda kuongeza wigo wa upimaji wa ardhi. Naomba sana katika ajira hizi, basi tuzingatie sana vyuo vyetu ambavyo vipo Tanzania. Bahati nzuri, namshukuru Mheshimiwa Jafo ameniteua kuwa Balozi wa Mazingira, nashukuru sana kwa nafasi; kwa hiyo, nitumie nafasi hii katika mchango wangu kuweza kunasihi sana Wizara ya Ardhi kwamba wahakikishe kwamba katika upimaji wa ardhi, basi wazingatie masuala ya mazingira kwa sababu ni suala muhimu sana. Bila kuzingatia hilo, inawezekana upimaji huu ukaacha ombwe kubwa sana katika umilikaji na upimaji wa ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzetu wa Chuo cha Mipango hapa Dodoma wameshatusaidia kazi, kwa sababu nimeangalia ile *content* yao ya *curriculum* ya masomo ya *certificate, diploma* pamoja na *degree* na *masters degree* ya kozi ya Chuo cha Mipango wanatoa *Urban Planning and Environmental Management Course* kuanzia Cheti mpaka *Masters Degree.* Hawa vijana hawa tukiwatumia, tayari hii kozi imekuwa *well contented* kwa sababu, masuala ya mazingira yamo ndani humo; watapima, watamilikisha na watazingatia masuala ya ardhi humo ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimesikia kwamba hawa vijana wetu wa kozi ya Mipango katika ajira hizi za Wizara ya Ardhi wanaonekana wao ni kama hawahusiki sana, kwamba wao labda ni sehemu ya daraja la pili au la tatu na zaidi wanazingatia vile vyuo vya ardhi. Napenda tu kuiomba Wizara ya Ardhi, nimeangalia *course content* yao kwa makini, iko vizuri, imeshiba, mpaka *remote sensing* imo ndani. Kwa hiyo, nafikiri tutakuwa tunafanya makosa makubwa kama hatutawatumia vijana hawa wanaomaliza Chuo cha Mipango Dodoma katika ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasikia vilevile kuna tatizo la *Scheme of Service* kwamba hawakutajwa huko. Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri wa Utumishi akaliangalia hilo kwa haraka kwa sababu tutakuwa tunasomesha watoto kwa gharama kubwa, chuo kile kina

walimu zaidi ya 150, tunawalipa Serikali, tunapoteza pesa, halafu itakuwa hatujawafanyia haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haraka haraka kuna suala la wenzetu hawa wanaokwenda kupima visiwa. Naomba tu, visiwa 289 ambavyo vimepimwa, vimekuwa *identified,* basi hiyo ni *step* ya kwanza, naomba tuendelee na hatua ya pili kwa kuweza kutayarisha Mpango Kazi na vilevile kutayarisha utaratibu wa kuangalia *resource mapping* ili tuweze kuona tunaviendeleza vipi kwa sababu kuna uharibifu mwingi wa mazingira katika hivi visiwa vidogo vidogo ambavyo vimo katika maziwa na vilevile katika maeneo ya bahari.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kuzungumzia jambo moja kumalizia mchango wangu.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba kuwasilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Francis Leonard Mtega, atafuatiwa na Mheshimiwa Michael Mwita Kembaki na Mheshimiwa Nape Moses Nnauye, ajiandae.

**MHE. FRANCIS L. MTEGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika Wizara hii ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Nianze kwa kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri anayofanya, lakini nimpongeze sana Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo ningependa nichangie kuhusu migogoro ya ardhi na mipaka, hususan mipaka.

Migogoro ya ardhi imekuwa mingi kwa nchi yetu kwa ujumla, lakini Mheshimiwa Lukuvi amekuwa hodari sana na mahiri kwa kuitatua, nampongeza sana. Hata Mbarali tulikuwa na mgogoro baina ya mwekezaji wa Kapunga na wananchi, lakini mwaka ule 2015 alikuja haraka sana na kuumaliza mgogoro ule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mgogoro mkubwa sana wa mipaka kati ya *TANAPA* na vijiji 55 katika Jimbo la Mbarali. Huu mgogoro kwa kweli ni mkubwa sana na una athari nyingi. Namwomba Mheshimiwa Waziri aupe kipaumbele kuutatua mgogoro huu, vinginevyo Wana-Mbarali hawatakuwa na amani na utulivu kabisa. Mpaka huu wa *GN* Namba 28 bahati mbaya sana umepita vijijini, mawe mengine yako katikati ya vijiji. Sasa wananchi wale wanaishi kwa matamko; atakuja kiongozi huyu anasema msiwe na wasiwasi, endeleeni na shughuli zenu kama kawaida, Serikali inafanyia kazi. Anakuja kiongozi mwingine anasema mko ndani ya hifadhi hamruhusiwi kufanya kitu chochote. Sasa hii inawapa shida wananchi wale, hawajui wafanye nini, kwa sababu, shughuli nyingi wanazifanya ndani ya maeneo yao wanayoishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, kuna mashamba mazuri kule Mnazi na mashamba yale yanatoa mpunga kwa wingi na tuna viwanda vikubwa pale Ubaruku vinachakata mpunga tena wa hali ya juu. Sasa kuwaambia wasifanye shughuli yoyote, maana yake ni kuwarudisha nyuma kiuchumi na kukosesha pato la Taifa. Kwenye Ilani imeainishwa kabisa kwamba tunaenda kuboresha kilimo na kuhakikisha wananchi hawa wanakuwa na kipato cha kutosha na vilevile Taifa linakuwa na akiba ya chakula. Sasa wanapozuiwa wasifanye shughuli zao za kila siku, kwa kweli hatuwatendei haki wananchi wale wa Mbarali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna shughuli mbalimbali, kwa mfano kule Luhanga kuna ujenzi wa Shule ya Msingi na ujenzi wa Zahanati. Sasa kiongozi huyu anakuja anasema endeleeni na ujenzi msiwe na wasiwasi, kesho kiongozi mwingine anakuja kuzuia kwamba msifanye jambo

lolote la kuendeleza kwa sababu mpo ndani ya hifadhi, subirini Serikali itoe maamuzi yake kwamba wapi kutakuwa ni mpaka ndipo mtakapoendeleza ujenzi. Sasa hii inawavunja moyo wananchi wale, wamepoteza nguvu zao na sasa hawaendelei na ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamwomba Mheshimiwa Waziri, maamuzi ya Serikali yaharakishwe ili kubainisha mpaka sahihi ni upi? Yawezekana kuna vijiji vitaambiwa viondoke, yawezekana kuna vitongoji vitarekebishwa, sasa hii ingefanyika haraka ili wananchi wawe huru kufanya kazi zao za kila siku wajipatie kipato na vilevile waweze kuliongezea pato Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nije upande wa *GPS.* Zamani mipaka ilikuwa inawekwa mawe tu, kiasi kwamba wazee wanakuwepo ni mashuhuda kwamba mpaka ulikuwa hapa na viongozi wa eneo lile wanashuhudia, lakini sasa ni *GPS. GPS* hii ni wataalamu peke yao wanaoweza kutafsiri. Sasa naomba Waziri atakapojumuisha, atuambie ni nani ata-*cross check* kuona kwamba hawa wataalam wetu wanaotafsiri *coordinates* zile kuweka mawe, je, hawawezi wakawa wanaingia ndani zaidi au pengine kutoka nje zaidi? Kwa sababu, wananchi pale hawana utaalamu wowote, wao wakishaona jiwe limewekwa ni kulalamika tu kwamba, sisi mpaka tunajua ulikuwa kule, sisi mpaka haukuwa hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo tuna migogoro mingi sana kuhusu *GPS* katika tafsiri yake na mawe yanavyowekwa, wananchi hawawi na uhakika, wanakuwa na wasiwasi mkubwa sana. Kwa kweli, Mbarali tuna uhaba mkubwa sana wa ardhi, Mbarali tuna mifugo mingi, Mbarali tuna mashamba ya mpunga, Mbarali tuna hifadhi ya *TANAPA;* ile hifadhi ni kubwa mno kiasi kwamba eneo linalotumika kwa wanyama liko upande wake, lakini eneo la wananchi ambapo linaonekana ni oevu, kwa kweli ni kubwa mno na kwa sasa hivi ule u-oevu haupo. Nimezunguka sehemu nyingi ni vumbi tupu na mashamba, lakini Ihefu kwa kweli bado ni sehemu oevu na inahifadhiwa na wananchi hawaruhusiwi kwenda kule. Sehemu nyingine zote ni kavu, zina mashamba,

hakuna uoevu, hakuna maji; maji yanapita tu mtoni, yanatoka Makete, pale ni mapito ya maji, wala hakuna madhara yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri, kwa kweli aende mwenyewe kule ashuhudie, aone haya mawe yaliyopandwa vijijini yanavyoathiri wananchi na kwamba, sehemu zile kwa kweli hazihusiani kabisa na uoevu unaoongelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Michael Mwita Kembaki, atafuatiwa na Mheshimiwa Nape Moses Nnauye na Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, ajiandae.

**MHE. MICHAEL M. KEMBAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia katika Wizara hii muhimu katika ustawi wa uchumi wa nchi yetu. Nianze kwa kumpongeza Waziri na Naibu Waziri na watumishi wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya kuhakikisha kwamba, wanapunguza malalamiko na kero ambazo zinakabili Watanzania katika idara hii ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kusoma majukumu ya Wizara hii ambapo miongoni mwa majukumu hayo ni pamoja na kutatua migogoro ya ardhi na nyumba. Mengine ni kupima ardhi na kutayarisha ramani; kusimamia Shirika la Nyumba la Taifa, pamoja na mambo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeanza kwa kusema haya kwa sababu katika Jimbo letu la Tarime Mjini ipo migogoro ya ardhi ambayo imechukua muda mrefu. Miongoni mwa migogoro hii ya ardhi ni pamoja na ile ya Nyagesese, lakini pia ile ya Mlima Nkongore. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama unavyojua, mtu akitaka akuondoe utu au akufanye uwe ombaomba ushindwe kutekeleza majukumu yako ipasavyo ni pale anapokunyima uhuru wa kumiliki ardhi. Unapokuwa huna ardhi maana yake utakuwa mhamiaji, utakuwa kibarua na vilevile utakuwa ombaomba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo letu la Tarime wapo wakazi zaidi ya kaya 10 ambao sasa hivi wanaishi maisha ya hofu, hawana shughuli za kufanya, wamekuwa vibarua katika mashamba ya wengine kwa sababu ardhi yao imechukuliwa. Ningependa nitaje hizi kaya 10 ambazo ardhi yao imechukuliwa na sasa hawafanyi shughuli zozote na wamebaki ombaomba katika ardhi ambayo wamezaliwa. Wamezaliwa pale, baba zao wamezaliwa pale na wameoa pale na sasa hivi wana wajukuu, lakini sasa hivi ardhi ile hawawezi kuimiliki kwa sababu imechukuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kaya hizi ni pamoja na Kaya ya Girimu Aryuva Kisiri, Kaya ya Maro Muniko Kisiri, Mkami Marwa Mkami, Lewis Cosmas Mwita, Marwa Girima Ngendo, Marwa Kirumwa Mkirya, Nyamuhanga M. Nyasebe, Matiko Mturu, Rugumba G. Ngendo na Chacha Mukami George. Kaya hizi sasa hivi hazina sehemu ya kulima kwa sababu eneo lao limechukuliwa kwa kisingizio kwamba wanalinda Hifadhi ya Mlima Nkongole.

Mheshimiwa Naibu Spika, najiuliza, mwaka 2018 Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ilienda katika Mlima Nkongole na waling'oa bangi pale, baada ya kung'oa bangi wakaja kwamba wanalitaifisha lile eneo ili wasiendelee kulima bangi. Toka wakati huo, mwaka 2018 wananchi hawa ambao wanaishi katika Mlima Nkongole hawana sehemu ya kulima na walikuwa wanategemea kulima katika eneo lile.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile miji yao wengine wamejenga nyumba pale nyumba za kudumu, miji yao

*beacon* imewekwa kwamba sasa wanatakiwa wahame katika eneo lile.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukweli ni kwamba vitu vingine vinaumiza moyo kwa sababu watu walikuwa wanaendelea na shughuli zao za kila siku, ghafla wanasimamishwa. Ninapozungumza sasa hivi kuna watu wawili wako ndani wamekamatwa kwa sababu wameonekana wakipita pale; na huyu ni Lugumba G. Ngendo. Kwa sababu jukumu la Wizara hii ni kutatua migogoro ya ardhi, ninamwomba Waziri, mimi ninakuaminia sana Mheshimiwa kwa uchapa kazi wako mzuri, naomba utatue tatizo hili la mlima Nkongole ili watu wale wapate haki waendelee kufanya shughuli zao za kila siku kama walivyokuwa wanaendelea hapo mwanzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliuliza swali hili siku chache zilizopita na majibu niliyopewa hayakuridhisha kwa sababu niliambiwa kwamba Serikali ichukue eneo lile ili kulinda mazingira, lakini kigezo cha kulinda mazingira wananchi wale walikuwa wanalima, lakini waliopewa kulinda eneo lile, vile vile wanalima. Sasa najiuliza, kama walionyang'anywa eneo walikuwa wanalima na hawa waliopewa wanaendelea kulima: Je, ni nani sasa anatunza mazingira hapa?

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia katika maeneo mengi, kwa mfano ukienda Milima ya Uluguru utakuta watu wanaishi pale na ile milima kwanza ni chanzo cha maji lakini watu wanaendelea kuishi na wanaendelea kufanya shughuli zao kama kawaida; lakini ukija katika Mlima Nkongole, hata panya ukimtafuta humpati kwa sababu hakuna chochote ambacho unachoweza kuhifadhi pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana sana Mheshimiwa Waziri anaposimama kumalizia, tafadhali aje na majibu ya namna gani wananchi wa Nkongole watapata haki yako ya kuendelea kufanya shughuli zao za kila siku ili maisha yaendelee, wasiwe watumwa na wasiwe wahamiaji katika ardhi ya baba zao ambao wamezaliwa pale siku zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile napenda kuzungumzia nyumba za *National Housing* ambazo zipo katika Jimbo letu la Tarime Mjini. Kwa sababu majukumu ya Wizara ni kusimamia Shirika la Nyumba, ukienda katika nyumba zile za *National Housing* ni aibu sana, watu wanaziba mpaka na makaratasi ya *nylon* juu ili wasinyeshewe, wengine wanaweka mawe ili vile vigae visidondoke. Naomba Waziri tafadhali sana macho yako yafike pale katika nyumba zile za *National Housing* ili watu wale wapate kuishi mazingira rafiki kama ilivyo, lakini pia mapato ya Serikali yasipotee hivi hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya nakushukuru kwa kunipa nafasi, Mungu akubariki sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Nape Moses Nnauye atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga na Mheshimiwa Nicodemas Henry Maganga ajiandae.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami nichangie kidogo kwenye hotuba hii ya bajeti ya Wizara ya Ardhi na nianze kwa kumpongeza Waziri na Naibu Waziri na timu yake nzima kwa kazi nzuri wanayoifanya kwenye Wizara hii. Kama wenzangu waliotangulia wavyolisema, Wizara hii mwanzoni ilikuwa na kelele nyingi sana, lakini Mheshimiwa Lukuvi kwa uzoefu wake nadhani ameweza kuituliza, kelele zimepungua, hata kama bado yapo mambo machache lakini kwa kweli mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni, amefanya kazi nzuri sana. Hongera sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Bunge la Kumi na Moja mimi kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mtama tulileta mapendekezo Serikalini ya kufuta shamba Na. 37ambalo lipo Maumbika Jimboni Mtama ambalo lilikuwa na hati Na. 5,438; shamba hili tuliliomba kwa muda mwanzoni, hati yake ikafutwa, baada ya muda ikabatilishwa ufuataji wake, sasa kwa niaba ya wananchi wa Mtama nimesimama kumshukuru

Mheshimiwa Waziri Lukuvi kwa sababu baada ya mjadala naye Serikali imechukua uamuzi wa kulichukua hili shamba na kuwakabidhi Halmashauri ya Mtama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri na Serikali nawashukuru sana na usikivu wenu na wananchi wa Mtama wanashukuru kwa uamuzi huu wa kulirudisha shamba hili sasa lisimamiwe na Halmashauri mpya ya Mtama. Nikuhakikishe kwamba tumeanza utaratibu wa kupanga matumizi bora ya eneo hili na hivi karibuni tutakamilisha utaratibu wa mapendekezo yetu na tutayaleta Wizarani kwa ajili ya kuidhinishwa. Ni matumaini yangu kwamba kelele za watu wachache hazitawarudisha nyuma tena. Mmeshatukabidhi, msirudi nyuma. Mwanzoni mlirudi nyuma, ikatusumbua sana.

Mheshimiwa Niabu Spika, safari hii msirudi nyuma tena, tupo katika mchakato wa kupanga matumizi na tupo katika hatua ya mwisho kabisa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri nakuomba ulinde uamuzi wako ili tupate kupaendeleza mahali hapa kwa matumizi ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza pia Wizara hii kwa kuhamisha huduma zilizokuwa zinatolewa kwenye kanda kuzipeleka mkoani. Jambo hili limetupunguzia sana gharama wananchi, lakini naomba nitoe mapendekezo, kama mmeweza kutoka kwenye kanda kwenda mkoani, mnaweza pia kutoka mkoani kwenda wilayani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, umefika wakati baada ya kufanya kazi kwenye kanda na mkaona usumbufu ambao ulikuwepo na bila shaka mtaona tija iliyopatikana baada ya kuzitoa huduma za kwenye kanda kuzipeleka kwenye mkoa. Sasa Mheshimiwa Waziri nadhani twende zaidi, tuzitoe hata kama kwa kuanzia baadhi ya huduma na hasa huduma kama za upatikanaji wa hati hizi. Upatikanaji wa baadhi ya vitu tuutoe kwenye mkoa tuupeleke kwenye wilaya. Tutakuwa tumewasogelea sana watu na tutapunguza sana gharama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa kama wa Lindi bado ni mbali sana mtu kutoka Liwale kuja Lindi Mjini kuchukua huduma. Kwa hiyo, ni mapendekezo yangu kwamba kwa kuwa tumefanikiwa kupeleka kwenye Mkoa na umeona inafanya vizuri; na katika dunia hii ambayo Sayansi na Teknolojia imekua sana, tunaweza bado tuka-*control* kutoka mkoani lakini bado huduma fulani wasilazimike kusafiri kuzifuata mkoani, bali waende wakazichukue Wilayani. Hayo ni mapendekezo yangu, nami naamini kwa uzoefu wenu na uwezo wenu mnaweza mkalifanya hilo na tukasogeza huduma karibu na wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mwisho nililotaka kulizungumzia ni suala la upimaji na upangaji wa miji yetu. Nimeona kwenye Kamati na nichukue nafasi hii kuipongeza iliyokuwa Kamati yangu ya zamani ya Ardhi wameliona hili jambo la utengaji wa fedha na kuzikopesha Halmashauri zetu zipime zenyewe. Jambo zuri lililofanyika hapa, mnawapa kwa *zero interest,* nadhani hili jambo ni zuri sana na bila shaka Serikali wameona, kwamba hii fedha wakipeleka, hata kwa hizi chache walizoanza nazo, wakifanikiwa kupima na kumilikisha, tayari ni mradi mzuri wa kuiingizia Serikali mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mapendekezo yangu; la kwanza, naiomba Serikali iongeze fedha, hizi Wilaya ni kidogo sana, ikiwezekana tu- *roll* hata nchi nzima kwa sababu itaongeza mapato kwa kiwango kikubwa sana. Kwa hiyo, eneo la kwanza fedha iongezwe. Eneo la pili Mheshimiwa Waziri nilikuwa napendekeza, kwa kuwa kasi ya ukuaji wa miji ni mkubwa, badala ya kwenda kwenye urasimishaji na bila shaka Waziri wa Fedha yupo na amenisikia, hili ni eneo zuri litatupatia fedha ya bure sana. Wape fedha ya kutosha waongeze Wilaya. Sasa pendekezo la pili miji inakua kwa kasi kuna mradi wa kurasimisha urasimishaji una matatizo yake kwa sababu unakuta watu wameshajipanga mnaanza kurasimisha inachukua muda na ni gharama.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo yangu ilikuwa kipaumbele cha hizi fedha pelekeni kwenye Halmashauri mpya ambazo miji yake ndiyo inaanza kukua na hapa naomba upendeleo mkubwa kwa Halmashauri yangu ya Mtama. Naomba tuletewe fedha, Halmashauri bado ni mpya, hatujatawanyika sana. Tukiletewa fedha, tutapima na kupanga vizuri bila gharama na tutajikuta tuna miji mizuri ya kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa namwomba Mheshimiwa Waziri jambo mahsusi, Mji wa Mtama wakati Mheshimiwa Hayati Dkt. Rais Magufuli anaamua kutupa Halmashauri, ule mji umepanuka. Bahati mbaya wakati wa kupanuka kuna mahali wakapanuka mji ukaenda ukachukua eneo la Tandahimba, nasi tukadhani ni eneo la Mtama. Wakati wa kupima sasa vipimo kuleta kutangaza *GN* ya Mji wa Mtama, tukakuta lile eneo ambalo wananchi wanapata huduma Mtama, tunajua ni wananchi wa Mtama miaka yote, tukajikuta wanawekwa nje. Karibia theluthi moja ya Mji wa Mtama ipo nje ya Mtama na ipo nje ya Mkoa wa Lindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri ikiwezekana basi tuma watu wako waje waliangalie tatizo hili na kwa sababu limevuka suala la Jimbo, limevuka Wilaya, limeenda Mkoa, kwa hiyo, likotokea Wizarani itakuwa rahisi kulitatua. Watume watu wako waje waangalie, ikiwezekana tuone namna ya ku-*accommodate.* Kwa sababu wenzatu wa Tandahimba wala hawana shida, kwa sababu hili eneo wala hawakujua kama ni lao, isipokuwa *GN* ya miaka mingi inaonesha hili eneo lipo Tandahimba. Kwa hiyo, ombi langu Mheshimiwa Waziri tuma watu wako waje watusaidie.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nashukuru kwa kazi nzuri iliyofanywa, lakini nawapongeza kwa kusogeza huduma mkoani, sasa zipelekeni wilayani. Napongeza kwa kutenga fedha za upimaji na kuwakopesha Halmashauri na ninawaomba wale wanaokopeshwa wasimamie fedha zirudi ili na wengine tukope. Hata hivyo Mheshimiwa Waziri

nakuomba ukisimama, basi iingize Mtama nipate fedha kwa ajili ya kupima mji wangu mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Naunga Mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga atafutatiwa na Mheshimiwa Nicodemas Henry Maganga na Mheshimiwa Samweli Xaday Hhayuma, ajiandae.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hotuba hii ya Wizara nyeti ambayo inawagusa wananchi moja kwa moja. Nianze kwa kumpongeza sana Waziri, Mheshimiwa William Lukuvi, kimsingi huyu ni mlezi wangu, kwa sababu miaka 10 ambayo nimefanya kazi kwenye sekta hii, amenitumia vizuri sana na nimejifunza mambo mengi sana. Kwa hiyo, namshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile namshukuru Mheshimiwa Angeline Mabula, naye amekuwa kama mzazi na mlezi wa karibu, kwa kweli niwapongeze, mnafanya kazi nzuri sana. Nampongeza Katibu Mkuu, Mary Gasper Makondo, bosi wangu wa zamani, naye anafanya kazi nzuri sana. Naweza kusema ni Katibu Mkuu wa kwanza ambaye ame-*practice* kwenye sekta hii kwa muda mrefu. Kwa hiyo, anaisimamia vizuri na anaifahamu sana. Kamishna Mathew na Makamishna wenzangu wote, maana mimi niliachia hicho cheo cha Ukamishna Mkoa wa Dodoma. Kwa hiyo, nawashukuru sana, tupo pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi, naomba Serikali iangalie Wizara hii kwa jicho la karibu sana, kwa sababu ardhi ni rasilimali namba moja. Mheshimiwa Waziri wa Fedha anajua, ni mchumi mzuri kwamba *number one resource* ni ardhi. Migogoro mingi siyo wakati wote inatokana labda na matatizo yaliyomo kwa wataalam, wakati mwingine ni kutokana na ardhi yenyewe kuwa ni kitu cha thamani. Kitu cha thamani lazima kigombaniwe.

Changamoto za wataalam zipo, lakini na ardhi yenyewe nayo ni tatizo kwa sababu ni kitu cha thamani, kwa hiyo, inahitaji umakini zaidi na bajeti ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, ukiangalia wakati huu; nampongeza Mheshimiwa Waziri na Serikali wameanzisha Ofisi za Mikoa, maana yake huduma zimesogea jirani na wananchi. Kwa hiyo, wananchi wanapata hati kwa gharama nafuu zaidi na gharama ya muda, gharama ya fedha tumeweza kumwondolea mwananchi wa hali ya chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naipongeza sana Serikali, lakini niombe sasa Serikali iweze kuongeza fedha kwenye hii Wizara kwasababu nayo itakuwa na fursa yakukusanya zaidi iwapo itapewa vitendea kazi. Nitatoa mfano mmoja, pale Ofisi ya Kamishna wa Ardhi Mkoa, nina maana ya Ofisi ya Ardhi Mkoa, ina vitengo vinne ambavyo vinafanya kazi tofauti kabisa. Kuna watu wa Mipango Miji, kuna Kamishna wa Ardhi, kuna Wathamini na kuna wale Wapima. Sasa kila mmoja unakuta anahitaji aweze kusafiri kwenda kusimamia kazi, kuna miji mipya huko inakua, inatakiwa itangazwe kwenye magazeti ya Serikali ili ipangwe, lakini wanashindwa kutokana na vitendea kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba sana Wizara hii iweze kuongezewa fedha ili ofisi zile za mikoa ziweze kuboreshwa na kuwa na vitendea kazi vya kutosha; kama vyombo vya usafiri na vifaa vya kupimia ardhi, maana sasa hivi teknolojia imekuwa kubwa. Vile vile wakiongezewa fedha za kutosha wataweza kuboresha hii mifumo ya ardhi; Kuna mfumo unaitwa *ILMIS,* kuna mfumo unaitwa *Land Rent Management System* na mifumo mingine ambayo inahitaji uwekezaji mkubwa wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mifumo hii itawezesha Wizara kupunguza muda ambao mwananchi anapata huduma, kwa sababu kila kitu kikiwa kwenye *computer* ni *mouse click* mwananchi anahudumiwa. Kwa sababu kitu ambacho kinawakwaza sana wananchi kwenye hii sekta ni

upotevu wa muda, kwa sababu sekta hii ina mambo mengi. Kuna mtu anaandaa michoro ya mipangomiji, kuna mtu mwingine anaenda kupima na kuweka *beacon,* kuna mtu anafanya uthamini kwa ajili ya fidia na mtu mwingine anamilikisha. Kwa hiyo, kuna milolongo mingi ambapo hakuna mlolongo ambao unaweza ukauacha kisheria na kila kitu kipo kwa nia njema. Kwa hiyo, wakiongezewa fedha, waweze kuboresha mifumo hii ya umilikishaji ardhi na utunzaji wa kumbukumbu tutaongeza sana tija kwenye sekta hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Wizara hii ina upungufu sana wa watumishi, kwa hiyo, naomba Serikali iweze kuangalia namna ya kutoa kibali ili watumishi waweze kuajiriwa. Kwa mfano, mahitaji ya watumishi kwenye sekta hii; nilikuwa nasoma hotuba ya bajeti, inaonekana ni 4,847 lakini watumishi waliopo ni 2,378. Upufungu ni watumishi 3,114, lakini wenzetu wa Utumishi wa Umma wametoa kibali cha kuajiri watumishi 36 tu. Kwa kweli hapa tutaendelea kulaumu Wizara hii kwa sababu hatuwawezeshi kuajiri watumishi wa kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri tuna vyuo vikuu; tuna chuo kinafundisha pale Morogoro, ni chuo kizuri, kinatoa wataalam wa ngazi ya Cheti na Diploma ya Upimaji, kuna chuo Tabora nacho kinatoa mpaka ngazi ya Diploma, kuna Chuo Kikuu cha Ardhi, kuna Chuo Kikuu cha Dodoma, kuna Chuo cha Mipango na vyuo vingine, vinatoa wahitimu hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mtakumbuka pale Jiji la Dodoma tulikuwa na watoto wanakuja ku-*volunteer* wakati mwingine wanafika mpaka 50, 60 na wengine tumewafundisha kazi, ni wazuri. Kwa hiyo, kuendelea kuwatumia wakiwa wanajitolea ni *risk* sana kwa Serikali. Kwa hiyo, napenda kutoa ushauri kwa Serikali, iweze kuwaajiri hawa na wengine ambao wapo mtaani ili waweze kusaidia kuongeza kasi ya upangaji ardhi, upimaji na utoaji hati za umiliki wa ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile napenda kuzungumzia kipengele cha upimaji, upimaji shirikishi na urasimishaji. Wabunge wengi wameonekana hawajaridhika sana na kipengele cha urasimishaji. Hii kurasimisha maana yake ni kufanya makazi ambayo hayakuwa rasmi yawe rasmi. Sasa mazoezi haya huwa yanakuwa na migogoro na malalamiko mengi sana kwa sababu wananchi tayari wameshaendeleza maeneo yao, namna ya kuwapanga kwa kweli ni lazima itokee migogoro mingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ile ya upimaji shirikishi ni njia ambayo inasaidia sana kuepusha matatizo ambayo yanatokana na uhitaji mkubwa wa fedha kwa ajili ya fidia. Kwa hiyo, kama fedha hamna, maana yake wataalam watakubaliana na wananchi, wanawapimia viwanja, halafu wanagawana viwanja. Viwanja vingine vinakuwa vya wenye ardhi na vingine vinakuwa vya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kinachotakiwa tu, wale wananchi kwa sababu tunawapa viwanja vingi, tuweke tu utaratibu wa kuwasaidia kuuza ili wapate kipato ambacho kinaendana na bei ya soko. Vinginevyo wananchi hawa watakuwa na viwanja vingi na hawana cha kufanyia. Kwa hiyo, tungeweka utaratibu mzuri wa kuwasaidia kuuza ili wapate fedha halali ya haki ambayo inaendana na bei ya soko.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile naipongeza Wizara kwa kuanzisha huu mfuko wa kukopesha fedha kwenye Halmashauri. Sasa Wizara iende mbali zaidi, iangalie pia na haya makampuni binafsi ambayo yanatambulika na Bodi za Mipango Miji na Upimaji. Kama nao wanaweza kuwakopesha hata kwa *interest* kidogo ili wabadilishe mfumo wa utendaji wao wa kazi, kwa sababu inaonekana hawana mitaji na ni Watanzania, wamesajiliwa na vyombo vinavyokubalika, kwa hiyo, wakipewa mikopo hii hata kwa riba kidogo, tutakuwa tunatengeneza ajira ndani ya nchi yetu na vile vile tunaongeza kasi ya upimaji na sasa hivi upimaji wao kwa kiasi kikubwa unategemea fedha za wananchi. Ndiyo maana utakuta takwimu zinaonesha

makampuni binafsi yanawadai wananchi zaidi ya shilingi bilioni 70. Sasa kwenda kupima kutegemea hela ya wananchi ni changamoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile naomba kule kwangu Ludewa, nami nina miji midogo mitano ambayo imetangazwa tokea mwaka 2001 ila bado haijapimwa; na wananchi wa Ludewa wanaamini kwamba Mbunge wao ni mtaalam mbobevu kwenye Sekta ya Ardhi. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri na wataalam wako mniondoe aibu hapa ili tuweze kuwapimia wananchi. Kuna Kijiji cha Lugarawa, Mawengi, kuna Manda pale, kuna *Beach Plots*, kuna Kijiji cha Amani ambako miradi ya Mchuchuma na Liganga inakwenda, kuna Kijiji cha Mavanga na Mawengi. Kwa hiyo, maeneo haya bila kusahau Kata ya Mlangali pale, ni maeneo ambayo yameshaiva kimji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Nashukuru sana Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu aliwapokea Madiwani wangu, walikwenda pale Wizarani wakapata mafunzo. Kwa hiyo, wana ari ya kupokea hii huduma ya mipango miji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache, naunga mkono hoja, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Nicodemas Henry Maganga, atafuatiwa na Mheshimiwa Samweli Xaday Hhayuma na Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga Bananga ajiandae.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Awali ya yote napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa siku ya leo tena kuweza kupata fursa hii ya kuweza kuchangia Wizara hii ya Ardhi. Mimi ni Mbunge wa Mbogwe. Jimbo la Mbogwe ni Wilaya mpya. Nitumie nafasi hii kumshauri mtani wangu, Mheshimiwa Waziri Lukuvi pamoja na Naibu Waziri, dada yangu Mheshimiwa Angeline Mabula.

Mheshimiwa Naibu Spika, michango mingi wenzangu wameigusia, mimi naomba kutumia muda vizuri ku-*focus* kwenye nafasi ambazo ni za muhimu zinazowakabili wananchi wa Tanzania hasa wa Mbogwe. Lipo jambo moja Mheshimiwa Waziri kwenye upande wa hizi taasisi, kwa maana ya Makanisa pamoja na Misikiti, pale ninapotokea Mbogwe, kuna migogoro mingi sana maeneo yale ya taasisi. Nianze kwa kukueleza Mheshimiwa Waziri, kwa kuwa Jimbo la Mbogwe ni Wilaya mpya kwanza sina Baraza la Wilaya. Naomba unisaidie sana jambo hilo na uiweke kwenye kumbukumbu zako ili usisahau mtani wangu, itakuwa hakuna nilichokifanya katika mchango wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikusikiliza wakati unatoa hotuba Mheshimiwa Waziri, kiukweli bila unafiki, nimeridhishwa na maelezo yako. Japokuwa sasa nami nimepata hii nafasi ya kukushauri leo mbele ya Bunge hili Tukufu, uniruhusu tu nigusie kidogo ili kusudi pale panapowezekana nawe uweze kujipanga ili kusudi Taifa letu tuweze kusafiri vizuri na tuweze kufika salama safari yetu ya kuelekea 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nasikitika kwa kuanza kumpa Mheshimiwa Waziri shutuma ya sekta yake. Toka niapishwe kuwa Mbunge, kwenye ofisi zangu migogoro mingi ni ya ardhi. Nilipomaliza kuapishwa tu pale, niliporudi nyumbani, nilikutana na watu hawa wa Msikiti wa Masumbwe Mjini, walikuwa na kesi, tayari ilikuwa Mahakamani na baadaye hiyo kesi ikahukumiwa kwamba walipe shilingi milioni 70. Wazee wangu hawa wamekuwa wakilalamika sana, maana Serikali ni moja tunayoiongoza na mpaka sasa hivi hawana uwezo wa kulipa hiyo hela.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nitumie nafasi hii kuiomba tu Serikali iangalie upya hilo suala, pamoja na kwamba kesi zilishafika Mahakamani, lakini hawa watu hawana uwezo wa kulipa hayo madeni ya nyuma. Kwa hiyo, nakuomba wewe pamoja na Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Sita, mwone namna gani mnaweza kuwasaidia watu wenye misikiti na makanisa ili kusudi waendelee kumwabudu

Mungu katika roho na kweli pasipo na *pressure* za madeni. Maana kila Kanisa ukiingia sasa hivi, michango mingi utaambiwa Serikali inatudai na ukiangalia kiuhalisia, hawana uwezo wa kuyalipa hayo madeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri, likiisha hili Bunge, afike Mbogwe; maana kwa kuwa Mbogwe kwanza haina Baraza, halafu ni Wilaya mpya ambayo *GN* yake ilitoka mwaka 2019; kwanza kuna uhaba wa watumishi kwenye sekta yake. Nafahamu Serikali ya Awamu ya Tano tulikuwa tukipigania kuhusu maendeleo na kiukweli huwezi ukapata maendeleo bila kuwa na hati *(document)* ya kuweza kukufanya ukakopa hata benki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mbogwe sasa inakuwa kwa kasi na ni Wilaya inayojitambua ina Mbunge kijana halafu makini, anazijua biashara vizuri, namwomba Waziri pamoja na Naibu Waziri wa Ardhi dada yangu, wafike Mbogwe waangalie Mji wa Mbogwe jinsi ulivyo, ni mzuri. Mbogwe sisi tuna madini lakini pia sisi ni wafugaji, kumekuwa na migogoro kati ya wafugaji na wakulima; wewe Waziri mtani wangu ndio mwenye kutoa maamuzi hayo ukifika. Kwanza ukifika tu wakakuona, wataona kama vile ameshuka Yesu hapa, watakuwa na imani hata wale watumishi wa shetani walioko kwenye Wizara yako ambao wanatumia utapeli kuwatapeli wananchi na kuwapora ardhi yao watakuogopa na wananchi wale watapata haki zao za msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, upo mgogoro mwingine ambao nimekuwa nikiuzungumza kwenye mikutano yangu karibia kote. Kuna mashamba haya ya dhahabu, Wilaya yangu ina migodi karibia 22, lakini ukiangalia kila palipo na dhahabu kuna migogoro ya ardhi na kiuhalisia migogoro ya ardhi ya mashamba ya dhahabu haiwezi kutatuliwa na sekta ya madini, maana kila sekta inajitosheleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, japokuwa yale maeneo hayajapimwa, kwa busara ya Mheshimiwa Waziri na heshima ambayo umenipa kwanza toka unipokee hapa Bungeni,

ukifika utaona jinsi gani unaweza kuitatua hiyo migogoro ili watu waweze kupata zile asilimia na haki zao wenye mashamba yale yaliyojaliwa na Mwenyezi Mungu kupata dhahabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri wa Ardhi pamoja na Naibu, jambo lingine kuna Kata moja inaitwa Bukandwe Kijiji cha Kanegele Kambarage, pale na penyewe kuna mgogoro wa mbuga nzuri ambayo ina rutuba na inatoa mpunga mzuri sana. Ukifika na penyewe utaona jinsi gani uweze kunisaidia, kuna heka karibia 145 ambazo wamekuwa wananchi wakizigombania pamoja na kampuni moja ambayo jina nimelisahau, nitakwambia nikitoka hapa Bungeni ili kusudi uweze kunisaidia Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo changamoto nyingine. Kuna Sekondari ya Kata yangu ya Burugala, Sekondari ilijengwa, lakini wananchi wanavyodai ni kwamba hawajapewa chochote na Serikali. Hivyo sasa, kwa kuwa sekta hii ni yako Mheshimiwa na mtani wangu, tukifika huko mambo hayo nina imani utayamaliza tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, Mji wa Mbogwe una kata karibia saba ambazo zimeendelea sana; ukinipa wataalamu wazuri waaminifu, maana mimi katika maisha yangu huwa napigania sana kupata watu waaminifu wa kufanya nao kazi; na ninakumbuka mchango wangu wa kwanza wakati naingia hapa Bungeni, niliishauri Serikali ya Awamu ya Tano kwamba sasa kwa kuwa Serikali imeanza upya; na sisi darasa la saba tupo na tupo wengi tunapiga sana kura, tena kwa uaminifu, huwa tunashinda kwenye misitari, msitubague. Mteue Wakurugenzi hata Darasa la Saba, maana kazi ya Ukurugenzi siyo kazi sana na hakuna kazi rahisi kama kuwa Mkurugenzi. Maana watendaji wapo tu wale Wakuu wa Idara, Wakuu unawaamrisha tu kwamba fanya hiki na hiki. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo sasa, leo hii Awamu ya Sita nitumie nafasi hii tena kurudia maneno yale niliyoyazungumza mwanzoni. Kwa kuwa najua uteuzi

unaendelea, tupewe nafasi watu wa Darasa la Saba ambao hatuna *CV* nyingi sana, ila tuna sifa ya uaminifu, ili twende tukazisimamie Halmashauri. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu iko kwenye vita ya uchumi, hatuwezi tukaweka michango kwa kukupongeza tu, lazima mzee ukae *attention.* Kwanza unatakiwa ubadilike, sura yako ni nzuri mno Mheshimiwa Waziri, wakati mwingine na watendaji wako wanakudharau. Wewe una nia nzuri, huwa nakuangalia sana mambo yako, una nia nzuri sana ya kuweza kuliletea mabadiliko hili Taifa, lakini waliomo ndani ya sekta yako hawana mapenzi mema na nchi hii na wala na wewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niko Dodoma hapa leo mwezi wa Saba. Jana niliongea na wewe Waziri, wakati naingia hapa Dodoma, mimi niliingia kwa kutafuta maeneo yale *hot cake,* kuna maeneo mengi tu yenye uwazi ambayo yalikuwa yanaonekana, kama unavyofahamu Mheshimiwa Waziri sisi Wasukuma kwa kuwa tuna roho nzuri sana, ni wepesi wa kuwaamini watu. Baada ya kujaribu kuchukua yale maeneo, tumeingia migogoro ambayo yaani haiwezi ikaisha leo wala kesho. Ufafanuzi ulionipa, nami kwa kuwa ni mwelewa halafu ni *senior,* nimeshaelewa ni nini cha kufanya ili kusudi hela yangu isipotee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri nikuombe sana, kwa kuwa tuko kwenye vita ya uchumi, badilika uwe mkali kidogo pamoja na Naibu Waziri ili kusudi wakuogope wale watendaji wako, watu waweze kupata haki zao kwa wakati muafaka. Leo Mheshimiwa Waziri utaona watu wengi wanakupongeza, kila mtu anasimama anakupongeza, lakini siku ukikosa haya madaraka, utakuja kuniambia, siku moja Maganga uliongea Bungeni. Hao hao ambao walikuwa wanakupongeza, watakugeuka na kukuona yaani hufai na hukutumia vizuri mamlaka yako wakati ukiwa Waziri. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo, Mheshimiwa Waziri nakuomba sana utembelee kwenye Jimbo langu la Mbogwe maana wewe ardhi zote ni za kwako; na kuna mapori mengi ambayo yalishamaliza kwanza kuwa na sifa ya kuwa mapori...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa kengele ya pili imegonga, nikawa nasubiri umalizie sentensi, naona mambo mazito unaendelea kumwaga hapo. Ahsante sana.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, haya nakushukuru. Basi mchango wangu mwingine nitamwandikia Waziri ili auone, maana nimeshauandaa hapa ninao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, nashukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Samweli Xaday Hhayuma atafuatiwa na Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga na Mheshimiwa Askofu Josephat Mathias Gwajima ajiandae.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Awali ya yote nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na wataalamu wote wa Wizara ya Ardhi kwa kazi nzuri wanayoifanya. Kwa kweli Mheshimiwa Waziri toka amepewa jukumu la kuiongoza Wizara ya Ardhi, Wizara ya Ardhi imekuwa na utulivu mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya nitaongelea mambo kama matatu kama muda utaniruhusu. La kwanza ni suala la upimaji wa ardhi ambao wenzangu pia wameongelea kwa kina kwenye eneo hili, hasa kwa maeneo yetu ya vijijini unakuta miji yetu inaanza kuwa vijiji baadaye inaanza kuwa miji na kwenye maeneo hayo unakuta watu wamepimiwa maeneo makubwa kiasi cha ekari moja. Wanapoanza sasa kwenye kuzipima, unaambiwa kwamba ikipimwa ekari moja kuwa eneo la makazi inakuwa

ni ngumu, mpaka ugawe maeneo kadhaa ili viwanja viweze kutambulika kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachoomba tu, wananchi hao wapewe elimu ya kutosha wakati wa upimaji huu ili waweze kuelewa na kweli wananchi wetu wa vijijini wana changamoto kubwa ya hofu ya Maafisa wanaotoka wilayani. Washirikishwe vizuri, waelezwe wanapata manufaa gani baada ya kufanya upimaji huo? Unaambiwa kwamba ukipima eneo moja, ni kiasi fulani cha fedha, lakini viwanja vile vinavyoongezeka gharama pia inaongezeka. Sasa wananchi wanapaswa kuelezwa kwamba gharama zile zinapoongezeka, wao wanapata manufaa gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati mwingine kwa sababu ya uhaba wa wataalam, Wizara imekuja na ubunifu ambao ni mzuri sana wa kushirikisha kampuni binafsi. Hizi kampuni binafsi zina mtazamo wa kunufaika. Sasa ukiangalia mahitaji ya wananchi wa vijijini; hawana fedha. Tuangalie namna ya kuwezesha ili hawa wananchi waweze kupimiwa ardhi yao bila gharama kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyowahi kuchangia kwenye Bunge hili, eneo la ardhi tukipima ardhi yote kwa kasi, tunaweza kupata mapato kwenye eneo la ardhi. Ninaomba sana Wizara iwekeze kwenye eneo la kupeleka wataalamu wa kutosha wa ardhi kwenye wilaya zetu. Wapeleke pia na vifaa vya kutosha. Kuna changamoto kubwa ya kwenye eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna upungufu mkubwa wa wataalam hasa baada ya kuanzishwa kwenye Ofisi hizi za Kanda, Ofisi za Mikoa; za mikoa zimewezeshwa vizuri na kama Mheshimiwa Nape alivyosema, wilaya nazo ziwezeshwe ili ardhi iweze kupimwa. Hii itasaidia kuondoa migogoro ya ardhi inayojitokeza mara kwa mara. Wataalam wapewe vifaa kwa sababu kwa sasa hivi vifaa viko mikoani. Ili tuweze kupata huduma, maana yake tuzunguke kwenye wilaya zote za mkoa, mpaka afanye *booking* sisi huku kuna migogoro vijiji na vijiji kwenda kuitatua, ni kalenda ndefu.

Mtusaidie tupate vifaa vya kutosha vya upimaji wa ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee pia eneo la Mabaraza ya Ardhi, wenzangu wameongelea sana, nami nikazie hapo. Kwenye Mabaraza ya Ardhi yale ya Kata, tujaribu kuona namna ya kuyaboresha, yana changamoto kubwa ya kiutendaji kwa sababu hayawezeshwi vizuri. Mabaraza haya pia wale wanaofanya maamuzi wanapaswa wapewe elimu nzuri ili angalau waamue kwa mujibu wa taratibu na sheria. Kwenye taratibu hizi za kuamua kesi kwenye Mabaraza ya Kata, linapofika suala la kwenda kutembelea eneo, hapo sasa zinaanza dalili ya kuanza kupata changamoto, kwa sababu unatakiwa kila upande uchangie kiasi ili waweze kufika kwenye *site*. Maana yake yule ambaye ana nguvu, ndiye atakayeangaliwa na yule ambaye hana uwezo, maana yake hataweza kuchangia hizo gharama za kwenda kwenye *site*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hili eneo tuliangalie vizuri namna ya kuratibu haya mabaraza kwa sababu wakiamua, ndiyo maamuzi yao; kama kuna rufaa, yanaenda kwenye Mabaraza ya Ardhi ya Wilaya. Ukija kwenye Baraza la Ardhi, Mabaraza haya ya Wilaya ambayo yako chini ya Wizara yako Mheshimiwa Waziri, hapa tuna changamoto kubwa, Wabunge wengi wanalalamika kwenye maeneo yao, hakuna Mabaraza ya Ardhi. Mfano tu mimi Jimbo langu la Hanang; Wilaya ya Hanang hatuna Baraza la Ardhi, tunategemea Baraza la Ardhi la Babati, nalo kwa muda mrefu halina Mwenyekiti. Jinsi Wilaya ya Hanang ilivyo, kuna wananchi wanatoka kilometa zaidi ya 100 kufika tu Makao Makuu ya Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutoka Katesh Mjini ambayo ni Makao Makuu ya Wilaya, kilometa 70 mpaka Babati. Ukienda babati unakuta Mwenyekiti hayupo, wala udhuru huo haujatolewa kabla. Yawezekana ni siku ambapo kesi hiyo inatakiwa itolewe Ushahidi, anakuja na watu wanne au watano ambao ni mashahidi, kilometa zaidi ya 170. Gharama za kuwaleta hao watu, nauli tu ni zaidi ya shilingi

75,000/=. Anafika na watu hao anaambiwa kesi imeahirishwa kwa sababu Mwenyekiti hayupo. Baada ya hapo, itaahirishwa tena na wala hataambiwa kwamba Mwenyekiti atapatikana wakati gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, huo ni usumbufu mkubwa kwa wananchi, tuwe na Baraza la Ardhi la Wilaya ya Hanang. Tulishatoa majengo, tupate Mwenyekiti na lile baraza lianzishwe ili kuondoa kero ambayo tunaipata kwa sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nigusie kidogo kwenye haya mashamba makubwa ambayo tumewapa wawekezaji. Sisi tuna mashamba tumempa mwekezaji ambayo zamani yalikuwa ya *NAFCO,* yalilimwa na tulikuwa tunapata ngano yakutosha. Baada ya kuwa yule mwekezaji wa awali amejitoa kwenye kilimo cha ngano, mashamba yale tukampa mwekezaji mpya. Ni zaidi ya miaka 12 sasa hivi hakuna chochote kinachoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo ameenda ameona na Wizara ya Kilimo imesema kwamba wameshajadiliana naye, wamekubaliana ndani ya mwaka mmoja, kama hatakuwa na chochote anachokifanya basi yale mashamba yaweze kutwaliwa, yarudi Serikalini na tuangalie namna ya kuwapatia watu wengine ambao watazalisha kwa tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri, wakati tutakapokuja atusaidie kwenye eneo hili. Imekuwa kwa mwaka huu amelima ekari 3,000 kati ya ekari ya 47,000. Sasa hii ni kama hujuma tu kwa sababu hatuzalishi, sisi Halmashauri hatupati chochote, wananchi wetu hawapati chochote. Tunaomba ukishaileta hili utusaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya ninaamini, Mheshimiwa Waziri atakuwa na majibu ya kina juu ya taabu hii wanayopata wananchi wangu kwenye eneo la Mabaraza la Ardhi. Kama sitapata ufafanuzi wa kina,

nafakiri tumeshajaribu kuongea hili suala kwa sababu ni kero kubwa kwa wananchi wangu, nitamshikia shilingi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga, atafuatiwa na Mheshimiwa Lemburis Saputu Mollel na Mheshimiwa Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula, ajiandae.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hoja ya Wizara hii ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Kwanza napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema kwa kunijalia afya tele, nimeweza kusimama hapa tena na kuchangaia hoja ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda kumpongeza Kamshna wetu wa Mkoa wa Tabora kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuhakikisha kwamba Wana-Tabora na maeneo mengi wanaweza kufanikiwa kupima ardhi na kupata hati zao. Kamashna huyu ametoa ushirikiano mkubwa kwa Wana-UWATA, yaani Umoja wa Wana-Tabora chini ya Mwenyekiti wetu Bwana Othuman Mahango, amefanya kazi kubwa sana. Leo watu wengi sasa katika Manispaa ya Tabora wana hati zao mikononi ambazo zitawawezesha hata kwenda kupata mikopo katika taasisi mbalimbali za kifedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie kwenye zoezi la urasimishaji. Zoezi hili limekuwa na changamoto nyingi sana, pamoja na kwamba linakwenda lakini limekuwa likienda ndivyo sivyo katika maeneo mengi. Tatizo kubwa liko kwenye baadhi ya makampuni haya yaliyopewa kazi ya kufanya zoezi hili. Kwanza wengi makampuni yao hayana uwezo, hayana vifaa na pia wamekuwa hawana wataalam wa kutosha, hivyo,

kusababisha zoezi hili kuendelea kusuasua na kuwa zoezi ambalo halionyeshi manufaa kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa sababu ameliona hili jambo, lakini ameelekeza kwamba angalau haya makampuni yawe yanashirikiana na watendaji katika Halmashauri mbalimbali, lakini kwa masikitiko makubwa, huko ndiko kubaya zaidi kwa makampuni haya, hasa yanayofanya vizuri. Wamekuwa wakidaiwa *ten percent* sana. Nimwambie Mheshimiwa Waziri, hili linakuwa ni changamoto kubwa sana kwa makampuni haya, inafika mahali wanashindwa kabisa kuelewana na mwisho wa siku hii kazi inakuwa haifanyiki kwa ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuishauri Wizara, zoezi hili wanapolitoa kwenye haya makampuni angalau waweke *deadline* ili basi wakati wanaingia ile mikataba, wawaambie kwamba unapopewa hii kazi wahakikishe mpaka muda fulani kazi hii iwe imeshakamilika. Bila hivyo malalamiko yataendelea kuwa mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia wakati wa zoezi hili la urasimishaji tungeiomba sana Wizara ifanye utaratibu wa kuhakikisha wanawafikia wananchi, kuwashawishi na kuwaeleza umuhimu wa zoezi hili la urasimishaji kama ambavyo ilivyofanyika katika Jiji la Mbeya; tumefika pale sisi kama Kamati na tumekuta wamefanyiwa urasilimishaji na hakuna changamoto zozote baina ya wananchi na Wizara. Kwa hiyo, niseme tu kwamba zoezi lile limeenda vizuri; na maeneo mengine Mheshimiwa Waziri tunaomba yafanye hivyo ili kupunguza hizi kele na changamoto ambazo zinaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Tabora ni moja kati ya Mikoa ambayo imezungukwa na mapori mengi ya akiba na hifadhi nyingi. Naomba sana Wizara itusaidie katika mkoa wetu kwenda kuainisha mipaka ya maeneo haya ili kuondoa migogoro baina ya Wizara ya Maliasili na wananchi. Kwa kweli naongea kwa masikitiko makubwa kwa sababu

moja kati ya migogoro inayosikitisha ni mgogoro uliopo katika Jimbo la Kaliuwa; mgogoro baina ya Hifadhi pale Isawima na wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba sana Mheshimiwa Waziri atusaidie, twende katika Jimbo la Kaliuwa akasaidie kuainisha mipaka ili mipaka ya hifadhi ijulikane na mipaka ya mwisho ya wananchi ijulikane ili wananchi wale waweze kuwa na amani pamoja na Askari wa Hifadhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie kuhusu hizi fedha ambazo Wizara inazitoa kwa Halmashauri mbalimbali kwa ajili ya kupima, kupanga na kurasimisha. Hizi Halmashauri ambazo zimepata fedha ziko Halmshauri zimefanya vizuri na niseme kuwa nazipongeza ikiwepo Halmashauri ya Mbeya Mjini, lakini zipo Halmashauri ambazo zinafanya masihara na hizi fedha, wanadhani kwamba fedha hizi wamepewa kama bakshishi ama za kwao. Fedha hizi Halmashauri mbalimbali zimepewa ili wapime, Halmashauri nyingine zimepima, zimepata fedha na faida juu, lakini wameshindwa kurejesha fedha hizi ili ziweze kusaidia Halmashauri nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Wizara, wakati inataka kutoa fedha hii iangalie uwezo wa hizo Halmashauri husika, ili wazipe fedha Halmashauri ambazo zinaweza kupima na kuuza ili waweze kurejesha fedha na Halmashauri nyingine ziweze kupata fedha hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, huu mradi ni mzuri sana, unasaidia sana kupima maeneo mengi. Serikali kupitia Wizara ya Fedha iweze kuongeza fedha katika eneo hili ili Halmashauri nyingi ziweze kupima na kurejesha fedha na kupata fedha katika Halmashauri zao za kuendeleza upimaji wa siku hadi siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie eneo la *National Housing.* Kwa masikitiko makubwa, Halmashauri mbalimbali zimekuwa zikiomba kujengewa nyumba za

gharama nafuu kwenye maeneo yao, lakini ulipaji wa fedha hizi umekuwa ni wakusuasua na wakukatisha tamaa kabisa. Tumekwenda Momba kweli, tulijionea hali halisi ya zile nyumba, lakini niseme pamoja na kwamba mkataba wao ulikwisha, lakini bado wameendelea kulipa na tumeona bado wana moyo wa kulipa ili waendelee kuzitumia nyumba zile.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo kuna Halmashauri nyingine yaani wala hawana hata wasiwasi, kuna wengine *National Housing* wameamua kuchukua Nyumba zao, wameamua kuzipangisha na mwisho wa siku wamepata hasara tofauti na walivyotegemea, ikiwepo Halmashauri ya Uyui.

Mheshimiwa Naibu Spika, naona Mheshimiwa Naibu Waziri ananikumbusha kwamba Uyui; niseme tu ni ukweli kwamba Halmashauri ya Uyui katika Mkoa wangu wa Tabora na yenyewe ni moja kati ya Halmashauri iliyojengewa nyumba 32, lakini Halmashauri ile imeshindwa kuzilipa, mpaka sasa wamelipa shilingi milioni 200 peke yake katika shilingi bilioni 1.8.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni jambo la kusikitisha sana, lakini naomba nishauri kwenye eneo hili, *National Housing* kupitia Wizara ya Ardhi wana maeneo mazuri katika maeneo ya Miji, ikiwemo katika Jimbo la Tabora Mjini, wana eneo zuri, liko nyuma pale ya *TRA,* eneo lile lina miundombinu yote, lina barabara, kuna umeme, kuna maji, yaani hakuna shida kabisa. Waende wakawekeze pale, fedha ipo, haina matatizo yoyote. Vile vile kuna maeneo kama Kawe, Bunda Mjini, Tarime Mjini na maeneo mengine ambayo yanaweza kuuzika kwa hizi nyumba kwa haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa sana naomba nizungumzie suala zima la madeni ya Serikali katika Wizara hii. Ni aibu kuona Serikali inawadai wananchi wa kawaida, taasisi za kawaida mpaka wanafikia kuwapeleka Mahakamani watu hawa kwa sababu ya

madeni, lakini Idara, Taasisi na Wizara za Serikali zina madeni makubwa na ya aibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiiuliza Wizara wanakwambia wanashindwa kuwapeleka Mahakamani kwa sababu na hiyo ni Serikali. Ningependa kushauri kwenye eneo hili, kama Wizara inashindwa kuwadai wakiwepo wao wenyewe Wizara ya Ardhi, wanadaiwa zaidi ya shilingi milioni 324, wanatakiwa wazilipe, wanashindwa kuzilipa na wao wana deni, kwa hiyo, ningeomba sana fedha hizi kama inashindikana kwa Serikali kupelekana wenyewe kwa wenyewe Mahakamani, basi watusaidie madeni haya ili yapelekwe *CAG* na *CAG* aweze kuziita Wizara hizi na Taasisi za Serikali ili tujue hizi fedha zitaletwa lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba sana waweze kutuambia hata Waziri atakapokuja *ku-wind-up* hapa, atuambie hizi fedha za Serikali zikiwepo kwenye Wizara yake lini zitalipwa? Kwa sababu tunazihitaji hizi fedha, tunahitaji tukapimie watu wetu, tunahitaji hizi fedha kwa matumizi mbalimbali, zilipwe. Watu binafsi wanapelekwa mpaka Mahakamani kwa sababu ya madeni haya, inakuwaje? Wenyewe wa Serikali tuwafanye nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nishauri jambo la mwisho, kumekuwa na Idara ya Mipango Miji katika Wizara hii, lakini bado ujenzi holela umekuwa ukiendelea katika maeneo ya miji mbalimbali. Tungetaka kufahamu idara hii inafanya kazi gani kuzuia ujenzi holela katika maeneo mbalimbali ya miji yetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Wakati namsikiliza Mheshimiwa Hawa Mwaifunga, nikajiambia kweli mganga hajigangi. Mheshimiwa Lemburis Saputu Mollel, atafuatiwa na Mheshimiwa Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula na Mheshimiwa Eng. Stella Martin Manyanya, ajiandae.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Wizara hii ya Ardhi. Naomba nianze kumpongeza Waziri wa Ardhi pamoja na Naibu wake kwa kazi nzuri wanayoifanya; na Wizara hii kwa kweli wamejitahidi kuituliza kwa kiasi fulani.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kazi nzuri wanayoifanya Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, kuna changamoto mbalimbali ambayo sitaacha kuendelea kuwaambia ili waweze kuendelea kutatua na kuhakikisha kwamba wanazidi kung'aa. Kwanza kabisa urasimishaji wa makazi. Suala la urasimishaji wa makazi ni changamoto. Mmekuja na mpango wa kuwapa makampuni ili waweze kufanya urasimishaji wa makazi, lakini makampuni haya hayana uwezo, kwa sababu hawana wataalam mahususi wa kuhakikisha kwamba wanapima ardhi kwa manufaa ya wananchi. Wamekuwa kama ni matapeli fulani hivi ambao kule kijijini kwanza hawaeleweki, wakienda wanajifichaficha, hawana ushirikiano na viongozi vya wa vijiji, kata na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri Mheshimiwa Waziri na timu yake nzima, Wizara nzima wakaangalia eneo hili la urasimishaji wa makazi ikiwezekana waangalie yale makampuni ambayo hayana uwezo, lakini pia waongezee Halmashauri ili iweze kushirikiana kuhakikisha kwamba wananchi wanapimiwa ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni suala la wawekezaji kutumia mashamba makubwa kukopa fedha katika Taifa letu na hatimaye kuingia mtini watakapokuwa wamepata hizo fedha. Hili ni suala la kuangalia kwa makini kwa sababu wawekezaji wanakuja wakisema tunawekeza, lakini mwisho wa siku wanakopa fedha kwenye benki zetu na kwenye taasisi zetu za fedha na baadaye wanatoweka na fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe mfano mmoja. Kuna shamba moja kwenye Jimbo langu la Arumeru Magharibi *Lucy Estate.* Mwekezaji huyu alikopa fedha kutoka

Benki ya *Standard Chartered* na baadaye wakakopa *NSSF* kiasi cha shilingi zaidi ya bilioni tisa, wametoweka, hakuna uwekezaji wala chochote. Wakati huo huo, baada ya kuona *Standard Chartered* inataka kuuza hilo shamba na *NSSF* waliamua kuweka *objection* mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunaona kwamba tunapata hasara kwa sababu ya mali yetu. Shamba ni letu, fedha tumewakopesha, kwa nini tunawaachia hiyo *loophole* kiasi hicho? Naishauri Serikali kwamba ni vizuri kama mwekezaji anakuja; tuseme umekuja unataka kuwekeza Tanzania kuhusu masuala ya ardhi, basi uwe na asilimia 50 na unachotaka kuwekeza, ndiyo uweze kukopa kwenye Benki zetu na taasisi. Vinginevyo tutaendelea kupoteza ardhi na mwisho wa siku wananchi hawatakuwa na faida na Serikali yetu haitakuwa na faida yoyote. kwa hiyo, naomba Waziri atakapokuja atuambie hili eneo la wawekezaji kutumia *loophole* hiyo, hatusemi wawekezaji ni watu wabaya, ni wazuri lakini sheria zetu tutaliangalia vipi ili ziwe na manufaa?

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni mashambapori. Kwa mfano, shamba hilo la Lucy sasa ni zaidi ya miaka kama 15, liko, ni shamba zuri, lina rutuba Arusha, hakuna elimu; shamba la *Gomba Estate* liko pale, ni shamba zuri halilimwi, lakini nazungumzia kilimo. Nitazungumziaje kilimo kama tunaweza kuacha maeneo mazuri kama hayo bila kutumia kwa manufaa ya wananchi wetu ili kuongeza ajira, kukuza uchumi wa nchi yetu? Tunasema kilimo, tunatunza ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Waziri pia maeneo haya ayaangalie kwa sababu inaumiza sana, wananchi hawana ardhi, lakini ardhi inalala miaka 15, 20, 30 hailimwi na ni ardhi ambayo inalimika vizuri, inaingia kila aina ya mazao, inasikitisha na inakera.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna shamba la Aga Khan ambapo walisema wanajenga Chuo Kikuu tangu mwaka 2006. Wameng'oa kahawa na hilo shamba lilikuwa linaajiri zaidi ya watu 1,500 mpaka 2,000; wameng'oa kahawa,

wamefanya nini, wamesema wanajenga Chuo Kikuu tangu 2006, hawajajenga Chuo Kikuu mpaka leo. Je si ukiukwaji wa Sheria za Ardhi Na. 5 na Na. 4 za Ardhi na sheria nyingine za umiliki? Ni kwa nini Mheshimiwa Waziri sehemu hii usiiangalie.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili shamba wananchi wanalilalamikia ni zaidi ya ekari 4,000 kasoro limekaa; kwa sababu gani? Ni eneo ambalo linaingia aina ya mazao yote, ilikuwa inalimwa maharage, ilikuwa inalimwa ngano na mazao mengine mengi; maua na kadhalika. Wananchi walikuwa wanapata ajira; na Serikali sasa hivi haipati kodi kutokana na mazao ambayo yangelimwa pale hakuna. Tumeacha, tumenyamaza: Je, *Aga Khan* tunawaogopa, siamini kama Mheshimiwa Waziri Lukuvi anaweza kuwaogopa *Aga Khan,* kwa sababu hakuna mtu aliyeko juu ya sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi wote tuko chini ya sheria, kwa hiyo, naomba eneo hili liangaliwe hasa katika shamba la *Aga Khan.* Naomba Mheshimiwa Waziri atembelee hilo eneo akague shamba lote aone. Asione tu kwamba sisi tunaongea kwa sababu labda tuna chuki, hapana. Tunataka kueleza namna na azima ya wananchi ambao tunataka Taifa letu liende.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna shamba la *Gomba Estate* pia tumewapa JKT sawa, lakini je, wananchi ambao wako maeneo hayo, wao wanapata nini? Hili nalo tuliangalie.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende eneo lingine la Mabaraza ya Ardhi. Mabaraza ya Ardhi inaanzia kwenye ngazi ya vijiji kwa maana ya Kushauri Kata na baadaye Wilaya. Mabaraza haya hasa katika ngazi ya wilaya kuna changamoto kubwa ya ucheleweshaji wa kesi. Kesi inaweza ikakaa mwaka mzima, miaka miwili, miaka mitatu mpaka minne. Hii siyo sawa, ni kuwakosesha wananchi haki. Hili nalo liangaliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwa Mabaraza haya wanatakiwa waangalie namna ya kutoa *circular* kuwapa posho hasa watu wa kwenye ngazi ya Kata, wanateseka. Tunaepukaje rushwa? Tunasema tunaondoa rushwa kwenye mfumo wa Mahakama, kama watu hao hatujawawekea mfumo mzuri, kwa mfano ufunguzi wa kesi kwenye Baraza la Kata, hayo makatarasi wale watu wanapata wapi kama hakuna chochote ambacho wanapewa kwa ajili ya kuweza kufanya hivyo kazi na kuwaangalia pia namna ya kuwapa posho?

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la migogoro ya ardhi hasa baina ya wananchi na taasisi zetu za Umma imekidhiri. Kwa mfano, kuna mgogoro wa Kata ya Oldonyosambu, wananchi wale waliondolewa kutoka Oldonyosambu Jeshi letu likachukuwa eneo hilo. Ni vizuri sana kwa sababu ni kwa manufaa ya Taifa letu, lakini sheria inasema, mtu unapotaka kuchukuwa ardhi , mmiliki lazima apewe fidia. Tunaomba Serikali ihakikishe kwamba inapotaka kuchukuwa eneo, iwape wananchi fidia na wale wananchi wale wananchi wa Odonyosambu wakumbukwe k wa sababu hii ni haki yao ya msingi. Kuwaondoa bila kuwapa haki yao, siyo sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wananchi na Nengun'g Kata ya Musa walishinda kesi Mahakama Kuu toka mwaka 2016, lakini taasisi yetu ya *TMA* imeng'ang'ania. Ni kwa nini tusiheshimu sheria? Naomba hii migogoro itatuliwe kwa sababu wananchi wanajiona hawana haki na wakati naamini kwamba chini ya Chama cha Mapinduzi, chama chetu, kimetengeneza ilani ya kuhakikisha kwamba wananchi wanapata haki zao kikamilifu. Kwa hiyo, naamini hili litatendewa haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna shamba lingine la Mlangalini Kiserya ,nao halikadhalika ni hivyo hivyo. Wananchi wamenyang'anywa kupitia Jeshi lakini bado hawapati haki zao, kutoka kule Kiserya Kata ya Mlangalini. Nayasema haya ili Mheshimiwa Waziri aweze kuona kwamba kuna haja ya kuangalia hayo maeneo kwa kushirikiana na Wizara

nyingine kutatua hii migogoro, maana haileti picha nzuri kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ni suala la mabenki kukataa kutoa mikopo kwa kutumia hati miliki ya kimila. Benki nyingi zinakataa hiyo hati kwa sababu wanasema haina *value.* Sasa ni vizuri Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa ujumla tuangalie hati hii, tusije tukawa tunasema tuweke tu hati ya kimila lakini wananchi hawanufaiki. Mtu kuwa na hati ni kwa ajili ya kumsaidia kupata mikopo na mambo mengine mengi. Kwa hiyo, kama haina *value,* basi Serikali iseme wazi kwamba hii hati haina *value.* Kwa hiyo, wananchi wasihangaike kuiweka, lakini naamini kwa sababu Serikali ilikuwa na nia njema, hati hiyo lazima ina *value.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba baadaye pia Mheshimiwa Waziri atakapokuwa ana-*wind-up,* atueleze hiyo hati ni kwa nini mabenki hayapokei na kuna benki nyingine zinasema labda tunaweza tukawapa shilingi milioni tatu tu, mwisho wa hiyo hati. Sababu hakuna. Kwa hiyo, bado kuna changamoto katika hiyo hati.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula atafuatiwa na Mheshimiwa Eng. Stella Martin Manyanya na Mheshimiwa Angelina Malembeka ajiandae.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushuru sana nami kwa kunipa nafasi ya kuchangia jioni hii kwenye Wizara hii muhimu kabisa kwa maisha ya Watanzania wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mungu lakini kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu, pamoja na

watendaji wote wa Wizara hii ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Kiukweli Wizara hii pamoja na changamoto nyingi sana tulizonazo kwenye sekta ya ardhi, sina shaka wenzangu watakubaliana nami kazi kubwa sana imefanyika kwenye sekta zote; kupima, kupanga pamoja na kutatua migogoro mingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuishukuru sana Wizara, nawe kama Mbunge wa Mbeya utakubaliana nami kwamba moja ya majiji yenye changamoto kubwa za makazi kwa wananchi na maeneo yake, Jiji la Mwanza ni kama ilivyo kwa Jiji la Mbeya. Namshukuru sana Mheshimiwa Lukuvi, Bunge la Kumi na Moja baada ya maombi ya muda mrefu alihamua kwa dhati kukubali Leseni za Makazi baada ya Dar es Dalaam ziende Mwanza, Arusha pamoja na kwako Mbeya. Sina shaka zoezi hili litafanyika na limeshaanza na inawezekana likawasaidia sana wananchi wa Mbeya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kule Mwanza unafahamu maeneo ya Mabatini, Pamba, Isamilo, Igogo na baadhi ya maeneo ya Mkuyuni, wananchi wote waliozunguka kwenye vilima, walikuwa hawana sifa hata ya kulipa kodi ya ardhi kwa sababu maeneo yao hayatambuliki. Leo naamini Serikali kwa mpango iliyonao wa kurasimisha makazi haya na kupata Leseni za Makazi zaidi ya kaya 15,000 tutakuwa tumeisadia Serikali na Wizara kupata mapato. Hii ndiyo moja kati ya kazi kubwa zilizofanywa na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa taarifa tu, nitumie nafasi hii kuwapongeza sana watendaji wa Jiji la Mwanza wa Kitengo cha Ardhi, pamoja na changamoto, wanafanya kazi kubwa. Leo tuko zaidi ya nusu ya kazi ambayo Mheshimiwa Waziri umewaelekeza na wamekusudia kuifanya. Tayari tumeshatambua vipande vya viwanja hivi zaidi ya 9,437. Hii siyo kazi ndogo kati ya viwanja 15,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri na niendelee kumwomba asituchoke, aendelee kutusaidia kwa sababu ndilo jukumu aliloaminiwa

nalo; na bado Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano Mama Samia ameendelea kumwamini. Sina shaka anafanya vizuri kwa sababu ana timu nzuri ya watendaji ambayo imesheheni pamoja na Naibu Waziri ambaye ni msaidizi wake, kwa karibu wanafanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili, napenda kuzungumzia suala la urasilimishaji wa makazi. Ni mfano ule ule tu, tumekuwa na changamoto kubwa zinazotokana na migogoro. Hii inawezekana ni kwa sababu maeneo mengi yalipimwa na kupangwa zamani. Kwa namna moja au nyingine kutokana na kukosa fedha na changamoto mbalimbali, maeneo haya hayakuendelezwa kwa wakati na badala yake wananchi walio wengi wakaingia kwenye maeneo haya. Sasa Serikali inapoteza kodi katika maeneo yote mawili; mtu aliyemilikishwa mwanzo hajaonekana zaidi ya miaka 30, wananchi wamejenga kwenye lile eneo, wameanza maisha yao, wamejenga majumba na maisha yanaendelea. Siyo rahisi sana kuvunja zaidi ya nyumba 200, 300 au 500 kwa sababu tu eneo hili alipewa mtu mmoja hati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri amekuja Mwanza na Naibu Waziri amekuja kwa wakati tofauti, wamefanya kazi kubwa sana. Mifano iko mingi, ukienda kule Mandu Mtaa wa Sokoni, tumefanya maamuzi ambayo leo yametuweka kwenye hali nzuri ya wananchi waliokuwa wamepoteza matumaini na sasa wana imani kubwa na Serikali yao, chini ya Mheshimiwa Mama Samia wanaamini kwamba wataendelea kuijenga Serikali hii.

Mheshimiwa Naibu Spika na Mheshimiwa Waziri, bado tunayo changamoto kwenye baadhi ya maeneo. Tulikabidhi baadhi karibia maeneo saba, umeshatutatulia maeneo mawili, lakini bado yapo maeneo ya Kata za Isamilo, kuna kiwanja *Na. 359 Block D* ambayo ni ya Mtaa wa Isamilo Kaskazini A, Kaskazini B pamoja na Neshen.

Mheshimiwa NaibuSpika, pia kipo kiwanja Na. 590 cha *Block C* kule Nyegezi kati ya Mtaa wa Ibanda, Swila, Igubinya

pamoja na Punzenza. Ninaamini maeneo haya yote Mheshimiwa Waziri akitumia utaratibu ule na ikiwezekana hata kwenye ile asilimia moja kama alivyofanya akaongeza asilimia ikawa mbili itasaidia lile deni liendelee kujifidia kule na wananchi wapate uhalali wa kuishi kwenye lile eneo kama walivyojenga na hatimaye waweze kulipa kodi ili tuweze kuondokana na kelele ambazo hazina shida sana.

Mheshimiwa Naibu Spika na Mheshimiwa Waziri, ninaamini kazi hii ambayo umeianza kwa muda mrefu na sasa tukiwa kwenye Awamu ya Sita, sina shaka tutakapofika 2025 kwa timu uliyonayo, wananchi wetu kwenye majiji haya; tunafahamu, ni kweli kwamba zoezi la upimaji na upangaji mara nyingi sana linaangalia maeneo ambayo bado hayajachangamka sana, lakini ukweli ni kwamba, maeneo yaliyochangamka sana kama Jiji la Mwanza la Mbeya na maeneo mengine, yanahitaji sana zoezi hili ili yaweze kuwa bora zaidi na Serikali na Wizara yako pia iweze kuingiza fedha za kutosha kupitia kodi ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la mwisho kwa leo, napenda niizungumizie hii *premium* ambayo inalipwa kwenye masuala mazima ya upatikanaji wa ardhi. Ninafahamu miaka michache iliyopita tulikuwa na utaratibu mzuri sana, ilikuwa fedha hii inatumika kama *revolving fund.* Pale Halmashauri zinapotumia, zinapopima, kumilikisha na kupanga, zile gharama zote zinazopatikana, Wizara ilikuwa na utaratibu wa kurejesha asilimia 30.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu baadaye mambo yakabadilika fedha hizi zikawa hazirudi, lakini sasa hii Mheshimiwa Waziri naomba niilete kwako kama ombi, Halmashauri hizi ambazo tunazitegemea zilipe fidia kwenye maeneo ya masoko, shule, hospitali, kwenye maeneo mbalimbali ya viwanja na kadhalika, zinakuwa na mzigo mkubwa. Unaweza kukuta Halmashauri kama ya ndugu yangu Mheshimiwa Deo hapa labda inaingiza shilingi bilioni mbili au tatu, atawezaje kulipa fidia? Atawezaje kulipa mapato mbalimbali ili aweze kukamilisha mahitaji haya? Kwa hiyo, mliangalie hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, uzuri Mheshimiwa Waziri anao mpango, aidha aendelee kuturudishia hii asilimia 30 au aendelee kutukopesha ile mikopo ambayo ametukopesha kwa muda mrefu na mifano mizuri ya matumizi bora ya hii fedha yapo. Ukiangalia leo Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela, jirani pale kwa Mheshimiwa Mama Angelina Mabula, Mbunge na Naibu Waziri, aliwakopesha karibia shilingi 1,500,000,000/=, wamefanya vizuri hakuna mfano na ninawapongeza sana. Kwa sababu wameweza kurejesha fedha, yote na kupitia fedha hiyo wamepima na wamepata faida. Wamepima kwenya kata nyingi; kwa mfano, wamepima Kata ya Kirumba, Kata ya Shibura, Kata ya Buswelu, Sangabuye na hata Nyamongoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Mheshimiwa Waziri, fedha hizi hebu tuletee. Hata Mwanza Jiji tunazihitaji.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, mwongozo wa Spika.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo wa Spika.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda Mbeya watakuwa wanazihitaji.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo wa Spika.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, tukipata fedha hizi za kutosha, sina shaka tutazitumia vizuri na tutarejesha kama walivyofanya Ilemela. Huu naomba uwe mfano wa kuigwa kwa sababu faida iliyopatikana na kazi iliyofanyika, leo hata wakiomba tena Mheshimiwa Waziri, wape zaidi ya shilingi bilioni 1.5 uliyowapa kwa sababu wameonyesha mfano. Nasi Jiji la Mwanza tumeomba kama shilingi bilioni tatu tu, tupe hizi fedha ili tufanya kazi hiyo na

tuweze kupima na kupanga vizuri mji wako ili wananchi wako ikifika 2025 kura zote ziende kwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sina shaka na Mheshimiwa Waziri, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, Mungu aendelee kuwabariki Wizara hii kazi nzuri.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Eng. Stella Martin Manyanya atafuatiwa na Mheshimiwa Angelina Malembeka na Mheshimiwa Angelina Mabula ajiandae.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa hii nafasi ambayo kwa kweli nilikuwa nimeshakata tamaa kwa ajili ya muda, lakini nashukuru sana kwa nafasi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami pamoja na wenzangu kama walivyotangulia, nianzie kwa kumshukuru Mungu na pia niwapongeze sana Mheshimiwa Waziri Lukuvi pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Dkt. Mabula na Katibu Mkuu, Mheshimiwa Mary Matondo ambaye tulikuwa naye kwenye Bunge la Katiba, alisaidia sana katika rasimu ile ya Katiba; vilevile Naibu Katibu Mkuu, ndugu yetu Nicolaus Mkapa pamoja na timu yao yote ambayo inawasaidia katika ngazi mbalimbali za kiutendaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee zaidi kuhusu gharama za kuhaulisha ardhi. Suala hili nililizungumza pia kupitia swali langu ambalo niliuliza hapa Bungeni na likapata majibu tarehe 9 Aprili, 2021 na lilikuwa swali Na. 329. Nashukuru sana kwa majibu ambayo nilipewa wakati huo, kwa hiyo, niko katika mwendelezo wa kuendelea kutetea juu ya jambo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna changamoto kubwa sana. Pamoja na kazi kubwa inayofanywa vizuri na Wizara hii, lakini changamoto ya kodi zinazotozwa katika kuhaulisha ardhi, zinafanya kuwe na kikwazo cha watu kuhaulisha ardhi zao au mali wanazokuwa wamezipa, matokea yake wanabaki kuwa na mitaji ambayo ni mfu. Kwa sababu unapokuwa na ardhi uliyonunua, lakini iko kwenye jina la mtu na unashindwa kuihaulisha aidha kwa sababu umekosa fedha za kufanyia hivyo, basi inakufanya uwe na kitu ambacho siku yoyote yule ambaye alikuuzia akigundua pengine hujabadilisha, anaweza akaja kukudai kwamba hii bado ni mali yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye majibu nilifahamishwa kwamba kuna ada ya upekuzi 40,000, pia kuna asilimia 0.02 ambayo ni ada ya uthamini wa hiyo mali inayokuwa imepatikana. Ada ya taarifa shilingi 40,000; ada ya kibali shilingi 80,000/=; na ada ya usajili 1% ya thamani ya hiyo mali. Baada ya kulipa hizo, kuna kodi sasa ambayo inalipwa *TRA,* asilimia 10 ya thamani ya mali uliyoipata.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa haraka tunaweza tukaona ni jambo la kawaida. Ukisema kwamba unaponunua, basi tenga na fedha ya kulipa hayo yote, lakini siyo rahisi kiasi hicho. Tukumbuke kwamba wakati mwingine mtu anauza kitu chake siyo kwa sababu alitaka kuuza, bali ni kutokana na shida aliyonayo au changamoto fulani inayomkabili. Kwa hiyo, anaweza kuuza hata kwa bei ambayo ni ya chini isiyotarajiwa, sawa na minada inavyofanyika. Hata hivyo unakuta kwa yule aliyenunua, akitaka kuhaulisha, huyu mthamini au mpekuzi anapoenda atatoa thamani inayodaiwa inalingana na hali ya sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mzee mmoja nilimkuta akilalamika anasema kwamba ameambiwa thamani ya eneo kwa mfano la hapa maeneo ya *St. Gasper* ni takribani shilingi 80,000/= kwa *square* mita. Sasa unakuta katika kile kiwanja chake kidogo kilikuwa kinafikia karibu shilingi milioni 80. Mpaka akasema basi, nipeni mimi hiyo shilingi milioni 80

ili niwaachie hicho kiwanja. Kwenda kulipa asilimia 10 ya huo mtaji ambao anasema kwamba ameupata, inakuwa ni gharama ambayo mtu hawezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile siku za nyuma elimu haikutolea kiasi cha kutosha. Unakuta mtu labda pengine mstaafu alinunua kiwanja chake kutoka kwa mtu ambaye wakati huo tuseme alikinunua kwa shilingi milioni moja na baada ya kukinunua, akakaa akapata kiinua mgongo chake akajenga, anasema nikabalishe, anaambiwa ahaa, sasa pamoja na hiyo nyumba uliyojenga, pamoja na hicho kiwanja, sasa gharama imeshakuwa shilingi milioni 150, ulipe asilimia 10 ya huo mtaji uliokaa hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, unakuta ni mambo ambayo ni kweli kwa mujibu wa Sheria ya Kodi yako sawa, lakini nadhani ni vema tukayaangilia upya hasa kwa hawa wananchi wanyonge ili na wenyewe waweze kumiliki mitaji yao kihalali. Hata kwenye jibu la Mheshimiwa Waziri wakati ananijibu, alisema katika sehemu kubwa inayopewa malalamiko ni hiyo ya *capital gain,* yaani mtaji uliopatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hatusemi kwamba hatujui athari yake kimapato, tunajua, lakini sasa hayo mapato hayakusanywi vizuri, kwa sababu hawa watu wanashindwa kuweza kulipa hizo gharama na matokea yake sasa hata kama anataka kukopa, anakopa vipi ili aweze kuwekeza wakati huo mtaji uko kwa jina la mtu mwingine?

Mheshimiwa Naibu Spika, hili suala ni muhimu na kwa sababu nilijibiwa siku ile kwamba watazungumza na Wizara ya Fedha ili kuweza kupata namna bora zaidi ya kulishughulikia ikiwezekana, sasa nimeangalia kwenye taarifa yao sijaona mahali palipozungumziwa suala hili. Ndiyo maana nikaona kwamba nilikumbushe tena kwamba kuna changamoto kubwa, watu wengi wana viwanja, wana mashamba, wana majengo yako kwenye hayo mashamba, lakini yanasomeka kwa jina lingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati mbaya hiyo sasa inatokana na nini? Hata ukitaka kufuatilia, unaweza kukuta hata anuani iliyopo pale ni ya mtu mwingine matokeo yake sasa hata kufuatilia masuala ya mapato kwa ujumla wake inakuwa ni shida. Naomba kama tulivyofanya hayo katika masuala mengine, mfano magari wakati ule yalivyokuwa na kero za kodi zile tukafanikiwa, basi na hili tuliangalie hasa kwa hawa wananchi wanyonge wale ambao wanahitaji kuwekeza, wanaohitaji nao wapate mtaji ambao ni halali kupitia hizi mali za rasilimali ya ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine nilikuwa naungana na wenzangu katika suala la Mabaraza ya Ardhi. Katika baadhi ya maeneo hilo suala bado ni tatizo, kwa sababu wale wazee wanaendelea kushughulikia mabaraza hayo unakuta wengine ni ndugu zao, wengine ndio anakuwa mtu ambaye sio ndugu yake. Kuna wakati unakuta wao wenyewe wanakuwa ni sehemu ya mgogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi binafsi kwenye Kijiji cha Kata ya Kihagana, pale Tumbi na Kihagana, nina migogoro iliyodumu zaidi ya miaka nane, mtu anatoka hapo kwenye Baraza la Kata anaambiwa wewe ndio umeshinda, wakienda Wilayani huyu ndio kashinda; wanaenda Mkoani wanarudi. Mwingine anaanza tena upya kutaka rufaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaomba pia Mheshimiwa Waziri katika ziara zake za Mkoa wa Ruvuma atusaidie kumaliza pia hii changamoto ya kesi hizi; ya kwanza ni ya Bwana Mateso na Binti mmoja Nombo, pia kuna ya akina Ndiu na ya tatu niliisahau ya Mama Lambo, zimedumu muda mrefu, ni kero. Yaani ukifika pale, Mbunge kazi yako ndiyo hiyo. Ukiongea na huyu, anakwambia wewe unataka kumsaidia fulani. Naomba kwa kweli Mabaraza ya Ardhi sasa hivi wasomi ni wengi, kwa nini tusiyaweke sasa yakawa katika sura bora zaidi kuliko iliyopo sasa hivi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba pia nizungumzie suala la mgogoro wa Lipalamba, naomba pia kwenye Hifadhi ya Lipalamba ule mgogoro bado unafukuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maneno hayo, nakushukuru sana. Ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Angelina Malembeka, ajiandae Mheshimiwa Angeline Mabula na Mheshimiwa Mtoa Hoja jitayarishe.

**MHE. ANGELINA A. MALEMBEKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami kuchangia katika Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Kwanza nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri sana wanayoifanya. Hii imeonyesha jinsi gani migogoro ya ardhi ilivyopungua hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa hivi tunajua ni asilimia 25 tu ya ardhi yetu ambayo imepangwa na kupimwa. Kati ya hizo, kuna viwanja 2,337,938 ambavyo vimepangwa. Tuna miliki zilizotolewa 1,557,819; tuna vijiji vilivyopimwa 11,743,000 ambavyo vimepimwa na kuandaliwa hati ya ardhi; na pia tuna hati zilizosajiliwa 868,474. Hii ni dalili tosha kuonyesha kwamba kazi ndani ya Wizara hii inafanyika vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, asilimia 75 iliyobaki, nasema, kama Wizara imejipanga vizuri, lakini kuna watu au taasisi ambazo zinawarudisha nyuma. Kama wameweza kufanya kazi hii, naona kila mtu abebe mzigo wake mwenyewe, kwa sababu inafika sehemu mtu anafanya kazi lakini mwenzie anamrudisha nyuma. Yeye anashindwa kufanya kazi zake anamsababisha na mwingine ashindwe kufanya kazi. Hii ipo kwa baadhi ya Wakurugenzi wa Halmashauri. Wamepokea shilingi milioni 400 ili wapime hivi viwanja na kuvipanga vizuri, matokeo yake wamefanya vitu vitatu tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo kundi la kwanza ambao wamefanya vizuri, tunawapongeza. Kuna kundi la pili wamekwenda wamebadilisha matumizi kwa kuwasingizia Madiwani. Kuna kundi la tatu wamekamilisha ule mradi halafu wameanzisha mradi mwingine na pesa

hawajarusdisha wakati wanajua kuna Halmashauri nyingine zinahitaji fedha hizi ili wapange miji yao vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakurugenzi hawa ambao wamekiri, mimi nasema kwa sababu niko kwenye Kamati ya TAMISEMI, tumewaita na kuwahoji, wamekiri lakini wanatoa kisingizio cha Madiwani. Sasa naomba wasiwasingizie Madiwani. Wao ndio Watendaji Wakuu na ndio wataalam, kwa nini wasingizie Madiwani wamebadilisha matumizi? Kama kweli wanafuata utaratibu wa Madiwani, mbona Madiwani wakisema tunawafukuza Wakurugenzi, wanaanza kusoma kanuni, sheria na taratibu ili mradi wabaki? Kwa nini na huku wasitoe utaratibu? Kwa nini wasiwaongoze Madiwani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wanafika sehemu agenda nyingi zinapokuja pale, mimi najua; kuna baadhi ya ajenda ambazo zinaletwa moja kwa moja na Madiwani, lakini kuna ajenda nyingine zinatoka kwenye Kamati ya Fedha na Utawala, wanakuja nazo pale kujadili; na wale ni wataalam tunategemea kwamba wataongea na Madiwani, watawaelimisha halafu Madiwani watafanya maamuzi. Ila wakishaona hii hoja ina maslahi kwao, basi wanawadanganya wale Madiwani ili mradi tu waseme ndiyo halafu waje waharibu. Katika hili Mkurugenzi mmoja, sina haja ya kumtaja jina au Halmashauri yake, anasema kabisa nimewasomesha Madiwani wakakubali, tumebadilisha matumizi; kwa sifa tu, wala hana wasiwasi wowote. Sasa kwa nini mwasingizie Madiwani?

Mheshimiwa Naibu Spika, itafika kipindi hapa akija Mkurugenzi tunamwambia njoo na Meya wako ili tuone ukweli uko wapi? Kwa sababu wale Mameya na wale Madiwani wenyewe hawapo huko ndiyo maana Wakurugenzi wengine wanasema sivyo. Kinachotakiwa sasa hivi, wale waliochukua shilingi milioni 400 za mkopo bila riba, warudishe ili wenzao waweze kufanya kazi katika maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mnasema Serikali na Serikali mnashindwa kushitakiana, mimi nasema kwenye

hili Waziri amtafute Waziri mwenzake wa TAMISEMI awabane Wakurugenzi wake fedha zirudi. Kuna miji mizuri sasa hivi inashindwa kuendelea kwa sababu haijapangwa. Watu wanapewa fedha wanabadilisha matumizi. Kama hamzitaki, kwa nini mlizichukua? Nasema kabisa mpango huu ni kumvuta shati Waziri wa Ardhi na Naibu wake ili kazi isiendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu hii ardhi ni mali ya Halmashauri. Hawa Halmashauri ndiyo wanatakiwa wapange hapa kuna shule, hapa kuna zahanati, hapa kuna kiwanja cha michezo, hapa kuna soko, ni kazi ya Halmashauri. Cha ajabu wanapokaa kwenye bajeti zao hawapangi kwamba tunatenga kiasi hiki kwa ajili ya kupanga miji na kupima, wanasubiri mikopo ambayo hawataki kurudisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye hili naomba Wakurugenzi ambao wamechukua fedha na hawajarudisha na pia wengine wamebadilisha matumizi, hatua za nidhamu zichukuliwe dhidi yao. Kwa sababu utawala bora ni pamoja na kuheshimu matumizi ya fedha na kuwa na nidhamu ya fedha na matumizi yake. Hatuwezi tukawa tunapitisha fedha halafu watu wanabadilisha matumizi, wengine wanakosa, yeye amekaa tu ame-*relax* anasingizia Madiwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na taarifa hiyo, bado kuna suala lingine la ardhi ambalo wote mara nyingi tunalalamikia. Ndani ya Halmashauri mpangilio uko mzuri, kuanzia ngazi ya Halmashauri kwenye Kata, kwenye Vijiji mpaka kwenye Mitaa. Mtu anaanza kujenga wanamwona, anachimba msingi, anaweka tofali wanamwangalia, anapiga plasta wanamwona, anapiga bati wanamwona; akishahamia anaambiwa bomoa, hapa kuna barabara inapima. Hiyo mipango miji hamuioni? Kwa nini tuwatia hasara wananchi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama utendaji upo na Maafisa Mipango Miji wapo, wakiona msingi umechimbwa,

basi waende wakamwambie mapema hapa usijenge kuna barabara inapita, lakini siyo anamwacha amejenga mpaka mwisho, anamaliza, unamwambia abomoe, hela yenyewe ya kuungaunga, utabomoa mara ngapi? Sisi tunawajua Watanzania wenzetu. Pesa hatuna, kujenga kwenyewe kwa kudunduliza, kwa nini uningoje nipige bati ndiyo uniambie nibomoe? *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba hawa watu wa Mipango Miji huko wazunguke kwenye mitaa yao, maeneo ambayo wanaona haya kuna kitu kingine kinakuja wasiruhusu watu kujenga, wawaondoe kabisa. Hii inatokana na huo uzembe wa hizo fedha, badala ya kwenda kuwapangia watu wapate viwanja halali wanawaacha wanazagaazagaa tu wanajenga popote. *(Kicheko*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mengi ya kuongea kuhusu Wizara hii lakini kwa leo naomba niishie hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, natoa ushauri kwa Serikali kuwa itoe ajira za kudumu kwa Wenyeviti wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba Wilaya. Msingi wa hoja hii ni kuongeza uhuru wa Mabaraza haya, *(independence of the tribunals).*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni maoni yangu kuwa kitendo cha kuajiri Wenyeviti hawa kwa mikataba ya miaka mitatu, mitatu ni kumweka Mwenyekiti katika hali ya kukosa uhakika wa ajira. Kwa mfano, Majaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania wamepewa *security of tenure* ili kulinda uhuru wa Mahakama. Maisha ni ardhi, ardhi ni mali. Hatuwezi kulinda mali muhimu ya wananchi ambayo ni ardhi inayosimamiwa na kuamuliwa na mtu ambaye hana uhuru, *freedom* ya ajira yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naunga mkono hoja

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Waziri na Naibu Waziri pamoja na wataalamu wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ardhi ni hitaji muhimu la binadamu wote. Kumnyima binadamu haki ya kumiliki, kutunza na kutumia ardhi ni kuvunja haki za binaadamu.

Katika jimbo langu la Moshi Vijijini, kuna migogoro mikubwa baina ya wakulima na wafugaji katika Kata za Mabogini (Kijiji cha Mserekie) na Arusha Chini (Mikocheni na Chemchem) zilizoko maeneo ya tambarare. Migogoro hii inahusiana na matumizi ya ardhi. Migogoro hii imeshasababisha madhara makubwa ikiwemo vifo na uharibifu mkubwa wa mali. Mpaka sasa Serikali ya Wilaya na Mkoa haijaweza kupambana na changamoto hii, kwani tatizo hili linajirudia mara kwa mara. Kwa mfano, katika Kata ya Arusha Chini, Kijiji cha Mikocheni migogoro hii imesababisha shule ya sekondari isijengwe, kwani mmiliki halali wa haya maeneo hajaainishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, migogoro ya wakulima na wafugaji jimboni kwangu inasababishwa na uhaba unaoendelea kukua wa rasilimali ardhi. Vilevile, migogoro hii inakuwa kwa sababu pande hizi mbili zina maadili ya kimila yanayotofautiana sana yanayohusisha makabila ya Wamasai (wafugaji) na Wachaga na Wapare (wakulima).

Mheshimiwa Naibu Spika, migogoro hii kwa kiasi kikubwa inasababishwa na haya yafuatayo; kupanuka kwa shughuli za kilimo na makazi ya watu; kubadilika kwa tabia nchi kunakopelekea malisho kukauka na kusababisha uhaba wa chakula cha mifugo na pia Serikali haijayapima haya maeneo na kuyamilikisha kwa wahusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu kwa Serikali; kwanza kutokana na migogoro inayoendelea, kuna umuhimu wa Serikali kuingilia jambo hili na kuhakikisha kuwa maeneo husika yamepimwa na kumilikishwa rasmi kwa wahusika, ili utatuzi wa migogoro hii kupitia mifumo ya kimila na ile ya kitaifa iweze kutumika kwa usahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kutokana na mazingira ya Kitanzania, ninaishauri Serikali ipitie sera za umiliki wa ardhi zenye utata zinazoweza kuchochea migogoro ya matumizi ya ardhi kati ya wakulima na wafugaji. Sera nzuri na rafiki itasaidia kutoa haki bila malalamiko.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo yangu hapo juu, naunga mkono hoja.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze mchango wangu kwanza kwa kuwapongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa uchapakazi wake katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu unajikita mwanzo kwa Kitengo cha Upimaji wa Ardhi, naomba kuishauri Serikali kuongeza kasi ya upimaji wa ardhi kwenye Halmashauri zetu. Kitendo cha kuiachia Halmashauri jukumu la kupima ardhi bila msaada wa Serikali Kuu kutaacha Halmashauri nyingi kuwa na makazi holela kwenye Halmashauri zetu nchini, hasa zile Halmashauri zenye mapato kidogo. Hivyo basi niishauri Serikali kuongeza fedha za upimaji wa ardhi ili kupunguza utaratibu wa urasmishaji wa aridhi ambao hauna tofauti sana na makazi holela.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wilaya yangu ya Liwale yuko Afisa Ardhi ambaye ameleta huu utaratibu wa urasmishaji ambao kwa mazingira ya Wilaya yetu haina uhaba wa ardhi, hivyo nikuombe Mheshimiwa Waziri kumsimamisha mara moja mpimaji huyu ambaye anakwenda kuharibu makazi ya mji wetu wa Liwale.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine kwenye Halmashauri yetu inakabiliwa na uhaba mkubwa watumishi wa ardhi kiasi cha kulazimika kuazima wapima toka Wilaya jirani ya Nachingwea ambapo Halmashauri huingia gharama za ziada ya upimaji kwa kuwa mpima toka jirani hulipwa malipo ya ziada nje ya bejeti. Jambo hili huongeza bei za viwanja na kuwafanya wananchi wa kawaida kushindwa kumudu viwanja hivyo na hivyo kuwafanya wandelee kukaa kwenye makazi holela.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkoa wa Lindi, Liwale ndio Wilaya pekee iliyokubali kupokea wafugaji katika Vijiji vya Kimambi, Ndapata na Lilombe. Lakini hadi leo vijiji hivyo havijafanyiwa matumizi bora ya ardhi, jambo linalosababisha migogoro ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo niiombe Serikali kuja kuisaidia Halmashauri kufanya matumizi bora ya ardhi katika vijiji hivi.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza sana kwa kupunguza kiasi kikubwa cha migogoro iliyokuwa na Maafisa Ardhi wasio waaminifu ambao walikuwa wanagawa ardhi moja kwa zaidi ya watu wawili, changamoto hii ilikuwa kubwa sana katika baadhi ya maeneo ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa. Hongereni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio hayo bado kuna baadhi ya changamoto za ardhi ikiwemo moja, mgogoro wa mpaka kati ya Halmashauri ya Wilaya ya Newala na Halmashauri ya Wilaya ya Masasi kati ya eneo la Mpanyani karibu na Nangoo. Kutokana na mgogoro uliopo ambao haujapata suluhisho, msimu wa korosho unapowadia Halmshauri hizi mbili hugombania wapi kwa kwenda kuuza korosho zao, kila Wilaya huvutia kwake ili wapate mapato. Mgogoro huu umechukua muda mrefu tunaomba utatuliwe.

Pili, katika Kijiji cha Chilangala eneo la Mbwinji, watu wa Mamlaka ya Maji *(MANAWASA)* wamechukua ardhi

ambayo wanakijiji walikuwa wamelima mazao yao ya chakula na biashara bila kulipa fidia kwa wananchi husika wa Chilangala kwa ajili ya mradi wa maji. Changamoto hiyo imezua mgogoro mkubwa kwa wananchi wa Chilangala ambao hawajajua hatma ya ardhi yao iliyochukuliwa. Tunaiomba Wizara ya Ardhi iingilie kati ili wananchi wa Chilangala walipwe fidia ya ardhi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, Serikali imeanza kufanya sensa ya utambuzi wa nyumba vijijini zenye hadhi angalau ya kudumu kwa miaka 15, nyumba zilizojengwa kwa udongo, saruji na kuezekwa kwa bati ili ziweze kulipa pango la nyumba. Pamoja na lengo zuri la Serikali la kudhibiti mapato lakini malalamiko yaliyopo kwa wananchi wa kipato kidogo ni namna watakavyopata fedha za kulipia pango kwa kuwa wapo baadhi yao wamejengewa nyumba hizo na watoto wao au ndugu zao. Lakini wapo wanaolalamika kwa kuwa walijenga nyumba hizo kipindi bei ya zao la korosho ikiwa nzuri, lakini kwa hali iliyopo sasa wanapata wakati mgumu ni namna gani watakwenda kulipia pango hilo katika mazingira ya sasa ambapo bei ya mazao haijatulia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye kifungu 2011 - Ofisi ya Ardhi Mtwara ilijiwekea mpango wa kutoa elimu kwa umma kuhusu sheria mbalimbali za ardhi katika Halmashauri tisa za mkoa huo kufikia Juni, 2021. Hadi kufikia Mei 15, 2021 Ofisi ya Ardhi Mkoa imefanikiwa kutoa elimu kwa Halamshauri za Masasi, Nanyamba na Nanyumbu pekee huku muda uliobaki ni mwezi mmoja tu. Je, ni nini kimekwamisha zoezi hilo kusuasua ukizingatia kuwa muda wa mpango umebaki mwezi mmoja tu? Je, upo uwezekano wa Ofisi ya Ardhi Mkoa kumaliza zoezi la utoaji wa elimu katika mwaka huu wa fedha wa 2021/2022?

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kukushukuru wewe kwa kinipatia nafasi hii ya kutoa mchango wangu katika hotuba ya Wizara hii. Hii ni miongoni mwa Wizara muhimu sana katika nchi yetu. Wizara inawahusu wananchi wote wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa kutayarisha na hatimaye kuiwasilisha hotuba hii katika Bunge lako Tukufu kwa ufasaha na umakini mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuchangia hotuba hii napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo; nikianza na mafunzo kwa watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Wizara hii kwa mipango yake madhubuti ya kuiongoza Wizara hii. Kwa kweli wanaendeleza na kuiongoza Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, dunia sasa hivi inaendelea kwa kasi sana kwa nyanja zote za kiuchumi, kisiasa na kitekhnolojia. Hivyo basi ili kuenda sambamba na kasi hiyo hatuna budi kuwapa fursa za masomo watendaji wetu. Lazima tuwasomeshe ili waweze kufanya kazi zao kiutaalam na kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2020 Wizara hii iliahidi kutoa mafunzo kwa watendaji 700. Lakini mpaka hotuba hii inasomwa leo ni asilimia 19.5 tu ya ahadi hiyo ndio ilioweza kutekelezwa; yaani ni watendaji 137 ndio waliopata mafunzo; hii ni idadi ndogo sana. Pamoja na kwamba Wizara haikusema sababu ya kutokifika lengo hilo lakini ukweli unabaki pale pale kuwa hii ni idadi ndogo kabisa.Ushauri wangu kwenye jambo hili kwa Serikali kuweka kipaumbele cha hali ya juu kutoa mafunzo kwa watumishi wa Wizara hii ili kuenda sambamba na kasi ya ukuaji wa kiitaalam duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ni kuhusu utawala na raislimali watu. Rasilimali watu ni kitendea kazi katika Wizara. Ni lazima suala hili lifikiriwe kwa nguvu zote. Upungufu wa wafabyakazi 3,114 katika nchi ambayo kila mwaka inatoa wahitimu wengi, ni kitu ambacho hakipendezi. Ushauri wangu kwa suala hili kwa Serikali ni kutoa fursa za ajira kwa vijana ambao wapo wengi sana katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JUMANNE A. SAGINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa hatua mbalimbali zilizochukuliwa ili kuboresha maendeleo na usimamizi wa ardhi hapa nchini likiwemo suala la usimamizi wa wataalam wa sekta ya ardhi. Pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Waziri, Naibu Waziri na wataalam wakiongozwa na Katibu Mkuu, naomba kushauri kuhusu maeneo yanayohitajika kufanyiwa kazi zaidi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, mamlaka ya upangaji ni Mamlaka za Serikali za Mitaa lakini ushirikiano wao na wataalam wa Wizara kwenye baadhi ya maeneo si wa kuridhisha. Bahati mbaya wataalam wa ardhi kwa baadhi ya maeneo hawana ushirikiano miongoni mwao. *Surveyors* wanafanya kazi bila kushirikiana na wataalam wengine. Hali hii inadhoofisha uendelezaji bora wa ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ili kuondoa kuendelea kuwepo kwa makazi holela yasiyopangwa, nashauri kuwepo maamuzi ya kisera na kuandaliwe miongozo ya upangaji wa vijiji na miji midogo ambayo haijapangwa. Viongozi wa ngazi za kata na vijiji wapewe mafunzo ya namna wanavyoweza kupanga vijiji vyao na kusimamia mipango hiyo. Ikiwa wakati wa *operation* vijiji, vijiji vingi vilipangwa vizuri, hatuna sababu kuwa na vijiji visivyopangwa leo wakati wasomi wameongezeka, na vitendea kazi vimeongezeka. Vijiji hivi vinapozidi kukua vinasababisha kuwa na miji isiyopangiliwa yenye makazi holela, miji isiyokuwa na maeneo ya masoko, vituo vya mabasi, viwanja vya michezo, shule, vituo vya afya na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, Tume ya Matumizi Bora ya Ardhi inaongozwa na mtaalam kijana msomi, Profesa Magigi, lakini tume hii haijawezeshwa vya kutosha kifedha ili iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Tume hii inapaswa kuzisaidia mamlaka zote za upangaji ambazo ni Halmashauri 184. Lakini kwa bajeti iliyopo na kwa kutegemea

uhisani wa *World Bank* itakuwa vigumu kuzifikia Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ufanisi. Ushauri wangu hapa ni kwamba Tume hii itengewe fedha za ndani za kutosha ili ifanye kazi muda wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushuru na ninaunga mkono hoja.

**MHE. JONAS W. MBUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kusimamia na kutatua migogoro mingi ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza pia Waziri wa Ardhi, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa kuandaa mpango mzuri wa mapato na matumizi ya Wizara ya Ardhi kwa mwaka 2021/2022.

Katika kuzingatia utekelezaji wa mipango hiyo napendekeza kama ifuatavyo; kwanza kusimamia na kuhakikisha kuwa sehemu kubwa ya ardhi ipimwe kwa kuwa kasi ya ukuaji wa miji ni kubwa.

Pili, kuhakikisha ankara za malipo ya kodi za ardhi zinatolewa kupitia simu za wateja n atatu, kuhakikisha hati za kumiliki ardhi zinatolewa kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, Serikali kuendelea kutatua na kumaliza migogoro ya ardhi; tano, Serikali kuongeza wafanyakazi hasa katika kitengo cha mipango miji na Upimaji wa ardhi; sita, Serikali kuhakikisha vitendea kazi kama vifaa vya kupimia, magari na pikipiki vinanunuliwa na saba, Serikali ihakikishe Mabaraza ya Ardhi yanakuwepo katika kila Wilaya na kuhakikisha haki inatendeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nane, Serikali kupitia Wizara ya Ardhi kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji kuhakikisha miundombinu ya barabara, umeme na maji inafikishwa katika maeneo yaliyopimwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naunga mkono hoja.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimkumbushe Mheshimiwa Waziri alitoa maelekezo kwa barua ya tarehe 18.12.2018 kufanya marekebisho ya mpaka kati ya Wilaya ya Ubungo na Wilaya ya Kisarawe. Kazi ilianza tarehe 10.01.2019; walipitia *GN* Na. 41 ya tarehe 15.02.1974 na ramani yake Na. E1/341/254 iliyosajiliwa kwa Na. 43075 inayoonesha Hospitali ya Mloganzila.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa maelekezo umefanyika kikamilifu, aidha, mapendekezo na ushauri umetolewa ipasavyo. Taarifa hii imewasilishwa kwenye ofisi za Mheshimiwa Waziri kwa ajili ya kutoa *GN* mpya na mpaka sasa bado utekelezaji haujafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri ukifika kwenye majumuisho uweze kutuambia juu ya hitimisho ya suala hili ili wananchi wa maeneo haya waweze kupata huduma zinazostahili kwa mamlaka sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Waziri Mheshimiwa Lukuvi kwa kazi kubwa anayoifanya pamoja na timu yake kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimpongeze kwa hotuba yake iliyojaa matumaini makubwa ya kupelekea kwenda kumaliza upimaji pamoja na kupunguza kama sio kumaliza kabisa migogoro hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Lushoto imekuwa ni Wilaya ambayo ipo chini sana hasa katika suala la upimaji ardhi na sijajua hili suala la kutopima ardhi Lushoto inasababishwa na Maafsa Ardhi ambao sio waaminifu, kazi yao maafisa hawa ni kula pesa za wananchi na

kuwadanganya kuwa mtapata hati. Mpaka sasa hivi ninavyoandika ujumbe huu kuna wananchi ambao wameshalipia gharama zote za kupimia viwanja vyao, lakini mpaka sasa ni miaka saba sasa hawajapata hati zao wala kupimiwa viwanja vyao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo niombe Wizara ya Ardhi iende Lushoto kwenda kuwanasua wananchi wale waliodhulumiwa na Maafsa Ardhi wale.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na migogoro ya ardhi kwa wananchi na Serikali pamoja na mipaka ya vijiji na vijiji, kata kwa kata na hata wilaya kwa wilaya. Hivyo basi ili migogoro hii imalizike Wizara iendelee kukopesha Halmashauri ili ziweze kupima maeneo haya hasa ya wakulima na wafugaji. Jambo hili linachelewesha sana maendeleo kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niishauri Serikali ianzishe sera ya nyumba kwani sera hii itakapoanzishwa itakuwa ni sheria yenye manufaa hasa katika ukusanyaji wa kodi za nyumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hayo niendelee kuishauri Serikali yangu tukufu hasa Wizara ya Ardhi itenge bajeti kubwa zaidi ili imalize kupima ardhi yote hapa nchini, kwani ardhi itakapopimwa kwanza kabisa migogoro ya ardhi itaisha, pili, Serikali itapata pesa za kutosha ambazo pesa hizo hazipatikani kwa kutokupimwa kwa viwanja vingi hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza Waziri na Naibu wa Wizara hii kwa kazi nzuri na ubunifu mkubwa kwenye kutatua matatizo ya migogoro ya ardhi. Ninapongeza pia Katibu Mkuu pamoja na uongozi mzima wa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Wilaya ya Moshi Vijijini, hususan Mji Mdogo wa Himo, kumekuwepo na migogoro mingi inayosababishwa na Maafisa Ardhi kufanya *double allocation* kwa nia ya kujipatia rushwa. Aidha, wafanyabiashara wachache wamejirundikia maeneo makubwa na mji ni kama vile umekuwa mali ya matajiri wachache. Tunaomba Wizara iingilie kati na kugawa maeneo yaliyohodhiwa bila kuendelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo kubwa kwenye Wizara ni ucheleweshaji wa vibali vya kujenga, pamoja na utoaji wa *electronic titles* jambo ambalo tuliahidiwa lingefanyika kwa haraka, inachukua muda mrefu na ingekuwa vizuri kuchapisha kwenye vyombo vya habari *titles* ambazo ziko tayari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna umuhimu wa kutenga maeneo ya kilimo kwenye kila Halmashauri kwa wawekezaji wakubwa.

**MHE. DKT. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba riba ya kodi ya viwanja kwa wale wanao *delay* iangaliwe, ni kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa sikupata nafasi ya kuchangia hoja hii ndani ya Bunge naomba niwasilishe mchango wangu kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitangulie kwanza kumpongeza Waziri Mheshimiwa Lukuvi, Naibu Waziri Mheshimiwa Dkt. Angelina Mabula, Katibu Mkuu na watendaji wote Wizarani pamoja na taasisi zilizoko chini Wizara kwa kazi nzuri wanayofanya. Nadiriki kusema bila kumumunya maneno kwamba Waziri Lukuvi ni mmoja wa Mawaziri wenye uwezo mkubwa ndani ya Baraza la Mawaziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nimpongeze Waziri kwa kufuta hati ya shamba la Valeska kule Arumeru Mashariki na kwamba sasa yuko tayari kwenda Meru na kukabidhi shamba hilo Halmashauri na wananchi wa Meru.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huo sasa nachangia kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Naibu Spika, upimaji na umilikishaji na kupanga matumizi bora ya ardhi; nilipokuwa nahudumu kwenye Kamati ya Ardhi Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Waziri aliwahi kutuahidi kwamba kila inchi ya nchi yetu itapimwa na kuwekewa mpango bora wa matumizi. Mpaka sasa zoezi la upimaji wa ardhi linafanyika kwa kususua sana. Nashauri Wizara ije na mpango kabambe wa kuharakisha upimaji na umilikishaji wa ardhi nchini kote ili tuondokane na janga la ujenzi holela ambao unapelekea miji yetu kuwa *squatters.* Lakini si hivyo, ardhi iliyopimwa na kumilikishwa ni chanzo cha kuaminika cha mapato. Serikali iangalie eneo hili kwa jicho tofauti na kulifanyia kazi kwani zoezi hili linaweza kuwa mwarobaini wa tatizo sugu la ufinyu wa bajeti ya ujenzi wa barabara na sekta zingine ambazo ni muhimu na zinahitaji fedha nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, migogoro ya ardhi; Serikali ibadilike sasa na kuacha kunyang'anya wananchi ardhi bila ustaarabu kwa kisingizio cha kupisha miradi ya kitaifa/ uwekezaji. Nikisema hivyo siyo kwamba napingana na Serkali katika utekelezaji wa miradi muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu. Tatizo liko kwenye namna ya utekelezaji wa zoezi zima la kuwaondoa wananchi kwenye mashamba ambayo yamekuwa *earmarked* kubadilisha matumizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba wananchi washirikishwe kikamilifu kabla ya kuwaondoa kwenye mashamba husika. Mfano mzuri ni mashamba ya Malula upande wa Meru na Hai jirani na *KIA.* Wananchi walioko kwenye mashamba hayo waliambiwa siku nyingi wangeondolewa na kulipwa fidia kwa lengo la

kuwawezesha wakapate mashamba sehemu nyingine ukizingatia kwamba wamekua pale kihalaii kwa miaka zaidi ya 40. Baada ya miaka takribani kumi tangu watangaziwe kwa mara ya kwanza kwamba wangeondolewa kupisha mradi wa *industrial park* na bandari kavu hivi karibuni Serikali ilikuja kwa ukali kwamba ardhi hiyo ni mali ya Serikali. Matisho hayo si sawa kwa sababu ardhi yote nchini ni mali ya Serikali na hata pale penye nyumba yangu ya kuishi ni mali ya Serikali, lakini ninaamini Serikali ikipahitaji itaniondoa kwa utaratibu fulani. Iko mifano mingi nchi nzima lakini itoshe kusema kwamba tuondokane na migogoro ya ardhi kwa kuwatendea wananchi haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu migogoro ya mipaka; nashauri Wizara ije na mkakati wa kumaliza migogoro yote ya mipaka kati ya wananchi na hifadhi ikiwa ni pamoja na mpaka wa kitongoji cha Momella na *ANAPA* (Hifadhi ya Arusha). Pia kuna migogoro kila leo kwenye mpaka wa Arumeru na Hai na Siha. Naomba Waziri atenge muda kidogo aje Arumeru na Siha aone ni jinsi gani matatizo yaliyoko kule yataondolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya haya machache, nakushuru na naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Angeline Sylvester Mabula, atafuatiwa na Mtoa Hoja.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumshukuru Mungu kwa fursa ambayo tumeipata leo hii kuweza kushiriki vizuri katika Bajeti yetu ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Aidha, imani huzaa Imani. Napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuniamini na kuendelea kunipa ridhaa ya kuwa katika Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru sana wananchi wote wa Jimbo la Ilemela ambao pia

wameniwezesha kuingia katika Bunge lako hili kwa kipindi cha pili. Kwa uwakilishi, nawashukuru sana Waheshimiwa Madiwani ambao leo tuko nao hapa na wameshuhudia jinsi Mbunge wao anavyomenyeka hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru pia Waziri wangu kwa malezi mazuri katika Wizara, anatuelekeza na kutuongoza vyema. Sifa zote zinazosemwa hapa, zinatokana na uongozi shirikishi ndani ya Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru sana watumishi wote wa Wizara ya Ardhi kwa ushirikiano, pia nawashukuru sana Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hususan Kamati ambao wametupa ushirikiano mzuri sana katika kuhakikisha tunatenda kazi zetu vyema. Nakushukuru wewe pamoja na Spika na uongozi wote katika Bunge hili wakiwemo Wenyeviti kwa namna ambavyo tumeshirikiana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru sana viongozi wa dini ambao wameendelea kututia moyo kwa sala na dua zao, wanazidi kututia nguvu hata pale tunapokutana na magumu mengi yakiwemo ya magonjwa ya *Covid* na mengine, lakini wametuweka imara na tunaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, naishukuru familia yangu, David na Sandra, Jacqueline na James, Diana na Emmanuel pamoja na Dorothy, kwa jinsi wanavyoweza kunivumilia katika hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kushukuru, basi nianze tena kwa kuwapongeza Wabunge wote waliochangia. Jumla ya Wabunge 33 wamechangia; 24 wamechangia kwa kuongea na tisa wameleta kwa maandishi, lakini pia kuna wengine wanane nilikuwa nimewasahau hapa, walichangia wakati ule wanachangia Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano. Hoja zao tumezichukua na wote waliochangia, hata kama sitaisema

hapa na Waziri hataisema, tutazijibu kwa maandishi na tutawaletea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto nyingi zinazozungumzwa zinatokana pia na uelewa pengine mdogo wa wananchi wetu lakini pia na lile suala zima la kutojua haki zao na wajibu wao katika suala zima la sekta hii ya ardhi. Hayo yote tutakwenda kuyafanyia kazi kutokana na miongozo mbalimbali ambayo tunaendelea kuitoa, elimu kupitia vipindi mbalimbali na vijarida tunavyovitoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze sasa kwa kujibu hoja ambazo ziko nyingi, nitajitahidi kadri nitakavyoweza. Kamati imetoa hoja nyingi, zaidi ya 30 ambazo wamezileta na sisi kama Wizara tumezipokea. Ya kwanza ilikuwa inaongelea habari ya Serikali kubuni mfumo endelevu ambao utahakikisha fedha za Serikali zinaletwa kutoka Serikali Kuu. Niseme ushauri umezingatiwa na ndiyo maana Wizara inaendelea kupata fedha na kuendelea katika kuweka kwenye vipaumbele ambavyo tumejiwekea. Kwa hiyo, zinakuja japo katika utaratibu ambao upo, unaeleweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuhusu Wizara kuelimisha wananchi, katika suala zima la ulipaji kodi, naomba niseme, Sheria ya Ardhi Na. 4 katika kile kifungu cha 33(1), kila mwananchi anayemiliki ardhi anao wajibu wa kulipa kodi ya pango la ardhi, lakini watu wanasubiri kusukumwa. Naomba tu Watanzania kwa ujumla tutii sheria, tuzingatie sheria zinasemaje? Kwa sababu mapato pengine yanapungua kwa sababu watu hatutii sheria zetu, lakini ukiangalia kile kifungu kinasema, “kila anayemiliki.”

Mheshimiwa Naibu Spika, pia mwaka 2020 hapa Wabunge wametupitishia mabadiliko ya sheria. Kifungu Na. 24A na Na. 33 kifungu cha 13 na cha 14, pale ambapo tayari upimaji unakamilika na *surveys* zinapita, tayari ana siku 90 tu yule mwananchi kuomba kumilikishwa. Asipomilikishwa ardhi ile, anaanza kutozwa kodi ya pango ya ardhi. Ile ni sheria ipo ambayo tunahitaji kuendelea kuwaelewesha wananchi ili waweze kujua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hili linafanyika, lakini watu wanapuuzia sheria. Nasi tumeshaelekeza, basi kwa sababu tayari Kamati imeona kuna upungufu katika makusanyo, lakini pengine inatokana na wananchi kutozingatia sheria, tutaendelea kukaza buti ili tuendelee pia kuhakikisha kwamba madeni yote au kodi zote zinalipwa. Mheshimiwa Hawa pia kazungumzia hili, nadhani yale yote yanayodaiwa kwa Serikali, yaani hayabagui; uwe ni ardhi uwe ni nani unadaiwa, lakini tunawadai fedha nyingi sana, ndiyo maana tunasema tutazidi kuzifuatilia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wamesema pia Wizara iagize wamiliki wote wa ardhi waingizwe kwenye mfumo. Tunaendelea kwa kutumia mfumo wetu unganishi wa *ILMIS* ambao sasa hivi unatumika kwa asilimia zote Dar es Salaam na mwaka huu wa fedha tunakwenda kuanza hapa Dodoma. Kwa hiyo pia itarahisisha kuweza kuwatambua wamiliki wote na kuweza kujua.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanaongelea pia Wizara kuandaa mikakati madhubuti ya kusimamia Maafisa Ardhi katika Halmashauri zetu. Naomba tuseme tu kwamba pamoja na kwamba Serikali imehuisha muundo wa ajira kwa Watumishi wa Sekta ya Ardhi na kuwaleta katika Wizara ya Ardhi kwa maana ya ajira pamoja na nidhamu, bado majukumu yao kama watendaji wako chini ya Halmashauri zetu. Kwa hiyo, ni jukumu la Halmashauri, hasa Wakurugenzi, kuhakikisha kwamba watumishi hawa wanawatumia katika kazi za upangaji, kupima na kumilikisha ili kasi iendelee kuwa vilevile. Kwa sababu kuletwa huku wengi wamekuwa pia wakijisahau, wanafikiri kwamba sasa wametolewa majukumu yao kwenye Halmashauri na wameletwa Wizarani. Wizarani tunasimamia suala zima la ajira na nidhamu, lakini kiutendaji, *operational-wise* ni *a hundred percent* wako chini ya Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, wamezungumzia suala la gawio stahiki kwa wakati liende kwenye Mamlaka za Mitaa. Naomba niseme tu, bahati nzuri Mheshimiwa Mabula amezungumza; *retention* ya 30 *percent* ilishaondolewa, na

mliondoa hapa hapa Bungeni 2016/2017. Kwa hiyo, sasa hivi tunachofanya kama Wizara, ili kuzifanya Halmashauri zifanye kazi, ndiyo hiyo mikopo ambayo haina riba tunaipeleka na tumeendelea kutoa katika Halmashauri mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama taarifa mmeiona, tulitoa kwa Halmashauri 24. Pendekezo la Kamati linasema walau twende kwenye asilimia 50. Nasi tunasema tumelipokea kama Wizara na wenzetu wa fedha wanasikia kwa sababu tuko Serikali moja. Kwa hiyo tutaliona hili, kwa sababu tunajua huku ukiwekeza unakusanya pesa nyingi zaidi na kwa Halmashauri wanapata *own source* ya kutosha kutokana na pesa wanazopewa ambazo hazina riba, wanauza viwanja vingi na bado wanabaki na akiba ya kuweza kufanya maendelezo mengine. Kama ambavyo tumeona Mbeya, Ilemela, Kahama, Geita *DC,* Bariadi – wote haoa wamefanya. Wengine wamezitumia vizuri, baada ya kuwa wameuza viwanja wameweza kununua vitendea kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano Geita *DC* wamenunua gari; Mbeya wameongeza wigo wa kupima maeneo; Ilemela vivyo hivyo wameongeza wigo. Kwa hiyo, tutafanya kila jitihada kuhakikisha hili linatekelezeka ili tuziwezeshe kwanza Halmashauri zetu kwa kupanua wigo wa kipato cha ndani lakini pia kuhakikisha tunaongeza kasi ya upimaji. Hata hivyo, hii haiondoi wajibu au jukumu kubwa la Halmashauri la kupanga, kupima na kumilikisha. Sisi tunakwenda tu kama ku-*support,* tunafanya hizi *interventions* ili kufanya wigo wa upimaji uende kwa kasi na kupima maeneo mengi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna lingine limeongelewa kwamba Wizara ielekeze Halmashauri kupitia Ofisi ya TAMISEMI kutenga bajeti. Hatuielekezi TAMISEMI, isipokuwa tunafanya kazi kama Serikali kwa pamoja. Kwa hiyo, ni jukumu la Halmashauri kutenga bajeti zao na kuhakikisha kwamba hasa kupitia mapato ya ndani, watenge ili waweze kuongeza kasi katika suala zima hili la upimaji. Haya yote yanawezekana iwapo tutafanya kazi kwa kushirikiana ili kuongeza kasi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni Wizara kuzijengea uwezo Halmashari zetu. Kazi hii tumeshaianza. Kati ya hizo Halmashauri nadhani ni kama 184, tayari Halmashauri 102 tumeshazijengea uwezo wa kuweza kufanya kazi zake vizuri. Kwa hiyo, kazi tumeshaianza na tunaendelea, tutazifikia Halmashauri zote 184. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ya Kamati ilikuwa inasema Wizara iendelee kuwekeza nguvu kwenye kupanga na kupima. Nimeshalizungumzia, ambapo tunashirikiana nao kama Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala lingine linasema; kusimamia Halmashauri katika suala zima la marejesho ya mikopo iliyopewa. Katika hatua hii, naomba kwa dhati kabisa tushukuru Kamati zetu mbili, Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira pamoja na Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa na mikoa ambao wameweza kukaa kwa pamoja na kuweza kuyaunganisha majukumu haya na kuweza kuangalia kipi kinaweza kufanyika katika suala zima la ukusanyaji wa madeni? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ambacho tumekubaliana na tunaendelea kuweka mikakati ya pamoja ya kuweza kuona jinsi gani tutasimamia zoezi hili, ni kwamba wale wote wanaodaiwa waliitwa na walipewa taratibu za kulipa wakapewa muda, lakini bado sasa katika kuwapa Halmashauri nyingine tutaweka utaratibu kwa kushirikiana na TAMISEMI ili hata vile vigezo basi vifahamike. Siyo suala tu la kuandika labda *proposal* analeta halafu anapewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wengine wameandika *proposals* nzuri, na ndiyo hao wanadaiwa mpaka leo hawajaleta. Kwa hiyo, bado pia inahitaji kusimamiwa kwa karibu. Nami namshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati ya USEMI ambaye alizungumza kwamba hili wanalibeba na wanakwenda kulisimamia kwa nguvu zote ili waweze kwenda sambamba na hilo.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kengele imeshapiga, lakini mambo yako mengi kweli. Ngoja nijaribu kuona nita-*cover* yapi, mengine itabidi tuwaletee kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, limeongelewa suala la *National Housing* hapa, hasa kwenye ule mradi wa Kawe ambao wanasema ni Kawe *Seven Eleven,* kwamba haujakamilika na pengine *National Housing* walipewa mkopo wakafikia ukomo sasa hawapewi tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, habari njema kwa Mbunge wa Kawe pamoja na Mbunge aliyeuliza swali, Mheshimiwa Halima Mdee, ni kwamba sasa hivi Serikali inafanya utaratibu wa kuweza kuwapa pesa waweze kumalizia mradi ule wa Kawe *Seven Eleven.* Pia Jengo la *Morocco Square* limeshafikia asilimia 94 ambapo ni uwekezaji mkubwa sana. Pale kuna vyumba zaidi 100 ambavyo vyote vinaingiza pesa, lakini kuna vyumba vingine katika mahoteli viko 80, kuna *square meters* 120,000 ambavyo vitawekewa maduka. Hivi vyote ni kitega uchumi kwa *National Housing.* Kwa hiyo, wakimaliza hiyo maana yake ni kwamba wataweza kujitegemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia alizungumzia suala la kutoingizwa kwenye bajeti. Suala la *National Housing* haliingizwi kwenye bajeti ya Wizara kwa sababu ile ni taasisi inayojitegemea, ina bajeti yake na haipati ruzuku kutoka Serikalini. Kwa hiyo, haiwezi kuwa sehemu ya bajeti ya Wizara ya Ardhi, isipokuwa Wizara ya Ardhi ni wasimamizi wa *National Housing.* Kwa hiyo, shughuli zote zinaofanyika, sisi kama Wizara lazima tuzisimamie na tuziripoti hapa kwenu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Wabunge pia walitoa hoja zao kwa maandishi ambao sasa nitajibu kiasi kulingana na muda uliobaki. Wamezungumzia suala la ajira za kudumu kwa wenyeviti wa mabaraza. Ni kwamba Serikali kupitia

Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa mwaka 2021, imewasilisha Mapendekezo ya Marekebisho ya Sheria ambayo yataleta utatuzi wa migogoro katika sheria hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, marekebisho haya yatarekebisha mfumo wa ajira kwa Wenyeviti wa Mabaraza kwa mikataba yao ile ya miaka mitatu mitatu waliyokuwa wanafanya. Sasa tunataka kuwaweka wawe kwenye ajira za kudumu ili wawe na *confidence* pia hata wanapofanya kazi zao. Kwa hiyo, hili tumelichukua.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la wazee kutolipwa na nini, nadhani kipindi kilichopita walikuwa chini ya idara nyingine, walikuwa chini ya Kamishna Msaidizi wa Mkoa, lakini sasa hivi wametengewa bajeti yao zaidi ya shilingi bilioni sita. Kwa hiyo, sasa hivi wana kasma yao ambayo inakwenda kuhudumia idara hiyo. Kwa hiyo, haitakuwa na shida tena kama ambavyo ilikuwa hapo mwanzoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala zima la mabaraza, kila Mbunge aliyechangia alisema habari ya kuwa kwake baraza halipo, ni Wilaya mpya. Tuseme tu kwamba ni mabaraza 111 ambayo yapo kati ya Wilaya karibu 139 ambazo zipo. Sheria inatutaka kila wilaya iwe na baraza lake, lakini Waziri alishaandikia Ma-*RAS* katika mikoa yote kuleta majina ya Wazee wa Baraza wa kila Wilaya ili wale wachache tulionao kabla hatujapata ajira ya wengine basi waweze kuwa wanakwenda kule kwenye maeneo kusikiliza kesi kwenye wilaya husika, badala ya watu kuja pengine anatoka labda Chemba au wapi kuja Dodoma, basi itabidi Mwenyekiti wa Baraza amfuate yule wa Chemba kule kule kwa sababu kutakuwa na Wazee wa Baraza.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunachoomba katika Halmashauri zetu na wilaya, waandae ofisi ambazo zitatumika kama mabaraza, kwa sababu sisi kama Wizara hatujengi, tunatumia majengo ya Serikali yaliyopo kwenye wilaya husika. Kwa hiyo, hilo nalo tutalitekeleza kwa namna hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, wamezungumzia suala la migogoro katika Jimbo la Newala ambalo limezungumzwa. Naomba niseme migogoro hii inashughulikiwa kwa kutumia Kamati ya Usalama ya Mkoa. Ni wazi kweli viongozi wa Newala hawakushirikishwa, lakini hata hivyo Wizara inajipanga kupitia watalaam wake kwa mwaka huu 2021 watakwenda kutatua suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala ya madai ya fidia kwa Mamlaka ya Maji ya Masasi tuseme Wizara inaongea na mamlaka ile ili kuhakikisha hiyo fidia inalipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la *Property Tax* ambalo limezungumziwa ya kwamba nyumba zimejengwa ambazo pengine ni za watu masikini, lakini zinadaiwa *Property Tax.* Nataka tu niseme kwamba Wizara inafanya mawasiliano ya karibu na Ofisi zetu za TAMISEMI ambayo inaratibu kodi hiyo ya majengo ili kuona namna bora ya kushughulikia suala hili. Limeleta kelele kwa sababu hiyo kwamba watu wanaona ni kitu kipya, lakini kwa kawaida majengo yanalipiwa. Sasa ni majengo ya namna gani? Basi utaratibu unafanyika kuweza kujua ni jinsi gani tunaweza kuwafikia hawa na kuweza kuwadai wale wanaostahili.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, hoja zipo nyingi, lakini nashukuru tu. Baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Haya yote yaliyochangiwa tutayatolea maelezo kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsanteni, nashukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, nimwite sasa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa William Lukuvi, aje ahitimishe hoja yake. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kushukuru kupata nafasi ya pili ya leo angalau nihitimishe hii hoja. Kwanza nianze kwa kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kwa kusema ambao katika orodha yangu hii wapo 25 akiwepo Naibu Waziri wa Ardhi. Majina yenu nayajua kuanzia msemaji wa kwanza Mheshimiwa Silaa mpaka msemaji wa Mwisho Mheshimiwa Malembeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nawashukuru wachangiaji wengine ambao wamechangia kwa maandishi ambao wapo tisa. Maandishi yenu tunayo, tunatafakari na tumezijua hoja zenu na tutazijibu vile vile kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii baada ya maelezo ya Mheshimiwa Naibu Waziri, namshukuru sana. Nitumie muda mfupi kwanza kutoa maelezo juu ya sheria. Wengi mmezungumzia juu ya masuala ya upangaji wa miji. Kwanza kwa mujibu wa Sheria ya Mipango Miji Na. 8 ya Mwaka 2007 inatamka wazi kwamba Mamlaka za Upangaji wa Ardhi ni Halmashauri za Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge tujue kwamba sisi kama Wabunge na wenzetu Madiwani kwenye Halmashauri ndiyo Mamlaka halali ya kisheria ya kupanga ardhi ndani ya Wilaya yetu. Waziri wa Ardhi hatakuja kukupangia ardhi ya Tarime hata mahali pamoja. Sisi tunafanya tu udhibiti wa ile michoro, kuhakikisha kwamba mkishapanga, tukishakubaliana hambadilishibadilishi kila mara, lakini Mamlaka ya Upangaji ni Halmashauri. Kwa hiyo, wewe ndio mwenye kitambaa unapeleka kwa fundi ushonewe suti kwa mshono unaoutaka, haiwezi kuwa Wizara. Kwa hiyo, nataka hilo tuelewane kuhusu Mamlaka ya Upangaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ujenzi holela, mdhibiti ni Halmashauri. Baada ya kutunga sheria hii, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Kamati ya TAMISEMI bila shaka mnajua ipo kanuni za Udhibiti na Uendeshaji Miji Sura 244, ni kanuni za TAMISEMI.

TAMISEMI ndiyo anayepaswa kudhibiti. Mamlaka za Upangaji ndizo zinazopaswa kudhibiti masuala yote ya ujenzi na uendelezaji wa miji. Kwa sababu ukishapanga, kama hili ni eneo la makaburi, mtu akijenga si wewe uliyepanga ndiyo lazima umwondoe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, suala la udhibiti na suala la upangaji ni mamlaka. Yaani Jiji, Manispaa, Miji na Halmashauri, hii ni ardhi yenu. Yaani ukipewa kipande kile cha utawala, ni ardhi yenu; na vijijini kupanga matumizi bora ya ardhi ya vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa namwona kule Mheshimiwa Aleksia, amezungumzia habari ya ardhi za vijiji, pengine akapendekeza lichimbwe shimo, yaani mpaka; wakulima wawe huku na wafugaji wawe huku. Bahati mbaya kuna rafiki yangu mmoja ameondoka hapa, aliwahi kujaribu pale Mvomero, tukachimba tuta wakulima wawe huku na wafugaji kule, ilishindikana. Hivi binadamu unamwekeaje mpaka, kwamba umwekee shimo hapa asiende upande huu, asiende huko, ilishindikana kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nawaambia ndugu zangu, dawa ni kupanga matumizi bora ya ardhi ya vijiji. Kwa mujibu wa Sheria Na. 5 ya Mwaka 1999 ya Vijiji, ardhi na yenyewe kijiji ndiyo mali yao chini ya usimamizi wa Halmashauri. Wao katika mkutano wao wakiamua kwamba eneo hili ni la kufuga, eneo hili ni la makazi, eneo hili ni la kilimo, ile ni sheria tayari. Wakishaileta kwangu maana yake hawaruhusiwi kubadilisha mpaka waombe kibali kwangu. Kwa hiyo, wanaopanga matumizi bora ya ardhi ni vijiji husika, lakini chini ya usimamizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ningefurahi bajeti ijayo mwulize vijiji vimepanga bajeti kiasi gani ya kupanga matumizi bora ya ardhi? Kwa sababu ardhi ni mali yao. Halmashauri nazo lazima zijue ardhi ile waliyokasimiwa na wale viongozi waliochaguliwa kwa ardhi ile na viongozi wa

kuteuliwa walioteuliwa kusimamia ardhi, wajue kwamba Mamlaka ya Sheria ya Mipango Miji imewapa kupanga ardhi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengi wamejua hilo, wamepanga ardhi yao na imewanufaisha. Wananchi wamejenga kwenye viwanja vilivyopangwa na kupimwa na Halmashauri zimepata mapato kwa sababu wametekeleza vizuri sheria hiyo. Nilitaka nianzie hapo ili tujue.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sisi kama wasimamizi wa sera tumeona haiwezekani kuacha Mamlaka za Upangaji peke yake ndiyo maana tunashirikiana kupanga mipango mikubwa. Bajeti ile iliyopita tulikuwa tumetengewa fedha za *World Bank* nyingi, zaidi ya shilingi bilioni 60, sasa bahati mbaya mazungumzo hayajamalizika, mnajua tena mambo ya *Corona* watu wanafanyia majumbani, lakini lengo letu ilikuwa ni kushirikiana na Halmashauri ili kukamilisha zoezi la Upangaji na Upimaji nchi nzima; kwa vijijini kuweka mipango ya matumizi bora ya ardhi na kwa mijini kwa kutumia Sheria Na. 4 kupanga miji yetu kwa kushirikisha watalaam wetu. Hayo makampuni binafsi, tulitaka yashiriki kikamilifu kwa sababu tunajua kweli hayana hela, lakini tungeyashirikisha na kupeana maeneo ya kusimamia upangaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka huu tunashukuru, mmeona kwenye vitabu vya fedha, tuna fedha nyingine ambazo Serikali imetupatia kutoka Korea, bado tunaendelea. Hizi fedha zinapita kwetu tu, lakini washiriki wakubwa wa upangaji ni Mamlaka za Upangaji ambazo ni Halmashauri. Kwa hiyo, bado zikitokea hizi fedha tutashirikiana. Moja ya gharama kubwa ambayo inawapata Halmashauri katika upangaji ni ununuzi wa vifaa. Tunataka fedha hizi zitusaidie kidogo kununua vifaa, vipatikane vifaa vya kisasa vya kupima ili wasiwe wanakodisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya gharama kubwa ya upimaji, huwezi kupanga mezani, kuchora kwamba hapa nitaweka makaburi, nitajenga nyumba, lazima upige picha

juu ya ardhi, picha ya anga ili ikupe sura hapo chini unapotaka kupanga pakoje? Hiyo ni gharama kubwa sana. Wengine wanatumia hizi za kwenye mtandao, *copy, copy* hizi, lakini hazitoi taswira nzuri. Kwa hiyo, tunanunua vifaa mtaona; tunanunua *drone* na ndege kwa ajili ya kurahisisha kazi ya wapangaji Halmashauri ili tuwasaidie kuwapa picha za anga zirahisishe ununuzi na upigaji wa picha zile ambao ni gharama sana ili kupata picha zenye sura halisi ili wapangaji waweze kupanga jambo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunashirikiana na Mamlaka za Upangaji ili kurahisisha kazi hizi. Ndiyo maana katika fedha za Maendeleo tulizozipata sisi Wizara tuliona siyo vizuri kufanya ziara tu, tukafikiri tuwarudishie Halmashauri wajitahidi kupanga maeneo yao. Watatafuta maeneo mazuri ya kupanga, lakini tuwape fedha shilingi 10/=, warudishe shilingi 10/=. Ndiyo maana wengine kama Jiji la Mbeya na wengine wamechukua zaidi ya bilioni, wamepima viwanja wamerudisha bilioni, wamepata zaidi ya bilioni nao wanaendelea vilevile. Wengine wamefanya bila pesa ya Serikali, lakini wameendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tumeona hili jambo ni jema. Badala ya kuzipeleka fedha kwa miradi ambayo itasimamiwa na Wizara, sisi wataalam wa Wizara tupeleke Wilayani kule kwenye ardhi ili Mamlaka za Upangaji zifanye. Nataka kuahidi, fedha zozote nitakazopewa na Mheshimiwa Mwigulu mwaka huu, zote zitakuja Wilayani, hazitabaki Wizarani. Hazitabaki kwa sababu sisi ni Wizara ndiyo, lakini hatuwezi kwenda kufanya kazi Halmashauri wakati Halmashauri ina wataalam wenye weledi na waliosoma kama sisi na wale wanasimamiwa na mamlaka ya upangaji. Mamlaka ya Upangaji, Halmashauri ndiyo wanaojua, wanaotaka kujua na wanaotakiwa kuwaambiwa hawa wanataka kupimiwa viwanja vya namna gani; na mji wao uwe namna gani? kwa hiyo tutaendelea kushirikiana ndugu zangu Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nachotaka tu niwaambie kwamba safari hii Kamati hizi mbili za TAMISEMI na Ardhi

tumekubaliana tuunde timu ya pamoja ambayo itaweka masharti na mwongozo ili ijulikane nani mwenye sifa ya kupata na asipopata afanywe nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kila Halmashauri ina uwezo wa kuomba. Kwa hiyo, kama Mbunge hapa unatamani Halmashauri yako ingependa kuingia katika *program* hii, mwambie Mkurugenzi aombe tu. Zikifika hizi fedha, ninyi mnajua kona hii nikipanga leo viwanja vitanunulika kesho. Msianze kupanga maeneo ya makaburi, hutapata hela. Anza kwanza kupanga maeneo mazuri ili upate hela ya kurudisha, halafu baadaye ndiyo utakuja kupanga maeneo ya makaburi. Sasa wengine wameanza kupanga maeneo ya makaburi; nani atanunua makaburi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni jukumu la Halmashauri kujua fedha za mwanzo upeleke wapi ili upate mtaji, baadaye ujitegemee? Kwa hiyo, mipango hiyo mtafanya wenyewe. Kwa hiyo, waambieni Wakurugenzi waombe kwa Katibu Mkuu, vigezo vitawekwa wazi na Wizara yangu wataalam wangu, wa Katibu Mkuu wa TAMISEMI na Katibu Mkuu wangu, wataunda timu, wataweka vigezo na ikiwezekana baadaye hata Kamati ya TAMISEMI mkienda kukagua miradi, mtakagua pamoja na miradi hii inayotekelezwa katika hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nawaombeni ndugu zangu tukumbushane tu huko kwenye Halmashauri, tujitahidi angalau Halmashauri kwa mwaka iweke bajeti hata ya kupanga matumizi bora ya ardhi ya vijiji viwili, vitatu, kumi; *Inshallah* Mwenyezi Mungu akitupa hizi fedha tulizobajeti mtakuta kama tulivyofanya katika wilaya tatu za Mkoa wa Morogoro, tulipata fedha kidogo tukaenda kufanyafanya vijiji vingi zaidi. Vinginevyo kwa kweli, kazi ya msingi hii ya kupanga matumizi bora na kusimamia kwenye Halmashauri ni kazi ya Mamlaka ya Upangaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni tulikuwa tumependekeza kwamba zamani tulikuwa na ikama ya mtu anaitwa *Land Ranger* kwenye mitaa huko; kama kiherehere

hivi, akiona mtu amechimba msingi, basi ameshatoa ripoti, watu wamebomoa. Sasa hivi hawa watu hawapo. Dodoma walikuwa wengi sana. Tunafikiria namna ya kutumia Watendaji wa Mitaa, kwa sababu Watendaji wa Mitaa wapo pale, yule anaweza akamwona kila mtu anayevunja kanuni za Mipango Miji na akatoa taarifa. Kwa hiyo, tunafikiria namna ya kuwatumia hawa ili angalau wasimamie mambo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, urasimishaji limezungumzwa sana. Jambo hili ni jema, nimelipigia debe kwa nguvu tangu nimeingia. Haya makampuni nimeruhusu mimi yakasajiliwa na tumeyasimia. Ni kweli mwanzo walikuwa wanapanga bei vibaya, tukarudi na hivi, tumeenda mbele nyuma, lakini kidogo wengine wanafanya kazi nzuri, lakini kweli ni masikini, hawana fedha. Pia namna ya uendeshaji wake ulikuwa wa ovyo, ovyo siku za mwanzo. Ilikuwa wanakwenda kuomba kazi kwa Mwenyekiti wa Mtaa, wanapatana, kumi, ishirini, wanachukua fedha kwa masikini halafu hawafanyi kazi. Tumedhibiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwaambie, mpaka sasa makampuni yaliyochukua fedha za wananchi na hawajafanya kazi inafikia shilingi bilioni 45. Mmoja amesema hapa, makampuni yanadai wananchi shilingi bilioni 70, lakini kwa sababu michoro wanayo, wananchi watalipia tu; lakini makampuni yamechukua amana hizi laki moja na nusu, laki moja na nusu, karibu shilingi bilioni 45 na hawajapima hivyo viwanja. Ndiyo hao wa Kimamba tunaopambana nao. Nataka kuwahakikishia watazirudisha hizi fedha na kazi watafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sina nia kuwafukuza, najua wamegawa gawa barua humu; wameandika barua, wametia kwenye *box* za watu wanaofikiri watawasaidia, bahati nzuri wengi wao wamenirushia zile barua ninazo. Ila wengine wamezitumia kusema humu, lakini wengine wamenirudishia, haiwasaidii sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, watendaji wangu walitoa taarifa fulani, nataka wajue zile kampuni za kupima wangekuja kwangu kuniambia badala ya kuandika barua. Sasa Mtendaji wangu kasema atawafuta badala ya kuja kwa Waziri ku-*appeal,* ninyi mnaandika barua mitaani, itawasaidia nini? Mimi ndio niliyetoa fursa hii ya makampuni kufanya urasimishaji. Mimi ndio niliyepanga hata bei na ndio niliyewasha moto mpaka wakasambaa kufanya kazi zote pamoja na Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ndugu zangu wenye makampuni binafsi, njooni tuzungumze, nitawaita tena, nitakuja kila mkoa nizungumze na makampuni yanayoshiriki na kazi ya urasimishaji kila mkoa tuzungumze kulikoni? Ni kweli hatuwezi kufanya kazi hii ya urasimishaji Serikali peke yetu, hatutaweza, lazima tushirikiane na hawa jamaa, hatuwezi. Hiyo lazima niwaambie ukweli, hatuwezi. Hata tungepata ikama ya kuweka mpima mmoja mmoja kila wilaya hatutaweza. Kazi ni tushirikiane sasa na ninyi mmeshapata ufahamu, tushirikiane katika udhibiti; *win, win situation.*

Mheshimiwa Naibu Spika, watendaji wangu wasiombe rushwa kwa hawa jamaa, wapitishe michoro bila bahasha, lakini na hawa wafanye kazi kwa uadilifu. Hata mabenki wajue hapa kuna fedha, wangeweza kuwakopesha hawa, wakabaki na michoro halafu watu wakawa wanalipa benki kuchukua hati zao. Hili tunaendelea nalo, najua litakwisha, tutaenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka niwaambie urasimishaji utaendelea, tutashirikiana. Nitakuja Mkoa wa Dar es Salaam, nitapiga kambi pale mwezi mmoja tufanye kazi yote iishe. Tupite maeneo yote yenye kero tumalize hili jambo, tuzungumze tuone namna ya kuwasaidia hawa. Ni lazima wananchi wapate haki yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika na ndugu zangu wote, najua wengi katika hotuba zenu mmenipa mialiko. Mheshimiwa Jerry Silaa nakuja kumalizia kazi yangu kule;

Mheshimiwa Massay ingawa umeomba mambo mengi, lakini nilikuwa na mpango wa kuja Mbulu, nitakuja; Mheshimiwa Halima Mdee lile jambo la Chasimba, Chatembo na Chachui, wewe unalijua sana, ila leo umepiga chenga, hukusema mpaka mwisho. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaambie Waheshimiwa Wabunge, hili analolizungumza siwezi kulisema sana, ni la kimahakama. Wale watu wa Chasimba, Chatembo na Chachui ipo hukumu ya Mahakama ya Rufaa kabisa iliyowataka zile kaya 4,000 lazima waondoke. Sasa mimi kuwa Waziri wa Makazi nikaona watu 4,000 waondoke kweli nyumba zibomelewe! Ndiyo nikawa-*engage* wale wazungu wa kiwanda, ee bwana, kwani wewe unataka nini? Akasema bwana mimi nina madini hapa, lakini nina-*surface right.* Kama watu wako wataweza kunirudishia kidogo, mimi nitawaacha wakae hapo hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukaenda kutangaza na aliyekuwa Mbunge pale, watu hawatoki. Tuelewane sasa kiasi gani nikurudishie ili anunue ile *raw material* mahali pengine kiwanda kiendelee. Sasa ile naona Mheshimiwa Halima hakuisema. Hawawezi. Nataka kuwaambia hivi, hawataweza kubaki pale kwa sababu kuna hukumu ya Mahakama ya Rufaa na hakuna mtu ambaye yupo juu ya Mahakama. Ni lazima tuelewane; na ndiyo maana thamani ya ardhi pale ni *square meter* moja ni shilingi 20,000 wakati ule; hawa kiwanda wamesema wawape shilingi 6,400/= wawapimie wawabakize pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, ingawa sehemu nyingine ya pili kuna wengine wenye mashamba, wanachaji mpaka shilingi 100,000/= *per square meter.* Hawa Wazungu wana hati. Siwezi kuwapa hati hawa wananchi wa Chasimba ya mtu mmoja, mmoja juu ya hati ya kiwanda. Maana yule Mzungu lazima nimlipe hii fidia ndipo arudishe ile hati. Fursa ya kubaki, watabaki, hawaondoki, wale Wazungu wameshakubali, lakini wawalipe kidogo fidia ya ardhi. Hivi nani huyo Dar es Salaam anaweza kupata kiwanja bure kulipa

chochote? Nani? Sasa mvamizi ndio apate *privilege* ya kubaki na kiwanja bure! Ilitokea wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Halima ulisahau *element* ya fidia. Sasa hapa tusifungue mjadala, mara nyingi wewe tunakutana Dar es Salaam. Mimi nitakukumbusha yale makaratasi ya Kamati ile ya mwanzo ambayo tulikuwa tunazungumza tulikwama wapi na ndiyo maana mgogoro huu umenichukua miaka sita. Nitakukumbusha Dar es Salaam. Tusiwape faida, maana Mahakama wasije wakafiri Bunge huwa linatafsiri hukumu zao, maana hii ni hukumu; nawe ni mwanasheria, wakili. Kwa hiyo, tuzungumze Dar es Salaam, nitakupa ushirikiano, nitakupa makaratasi ili usome vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwaahidi kwamba Mheshimiwa Mtemvu, Mheshimiwa Gambo nitafika Arusha na Arumeru zote mbili, nitakuja. Pia Mheshimiwa Mbunge wa Mtama, timu ile uliyoomba ya kuja kuangalia ule mpaka itakuja ili tuone namna gani, halafu baadaye tutashirikiana na Waziri wa TAMISEMI namna ya kumshauri Mheshimiwa Rais ikibidi, tukiona kama kuna sababu juu ya mipaka hiyo. Lakini kule…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, kengele ya pili imegonga.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuwaahidi tu Wabunge wote mliozungumza hapa, mliohitaji migogoro yenu kutatuliwa kwenye *site,* mimi mmenipa mwaliko, nitafika; na ratiba hii naanza wiki ijayo. Kote huko nitakuja. Nitaenda Mtama, nitaenda Mbogwe, nitaenda Hanang, Arumeru zote, Nyamagana narudi tena na Kaliua nitakwenda. Kaliua kulikuwa na ratiba ambayo tulishaombwa na Mheshimiwa Mama Sitta na Waziri wa Utalii, tutakuja huko. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, omba fedha, kwa sababu hata mimi nitataja hapo kwamba uje na Mbeya. Orodha ni ndefu, wewe omba hela tukupe halafu uje tuonane huko.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuruni sana kwa kunisikiliza. Naomba mnipe pesa na yote haya mliyoyasema watu wote yatatimizwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu.

**NDG. MOSSI LUKUVI – KATIBU MEZANI:**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 48 – Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi**

Kif. 1001 – *Administration and HRM ......* Shs. 10,154,380,400/=

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kifungu hiki ndicho chenye mshahara wa Waziri na kuna majina hapa ya Wabunge mbalimbali ambao wanataka ufafanuzi. Sina hakika kama tutaweza kuwafikia wote, lakini kabla hatujaanza hao, naongeza nusu saa ili tuweze kukamilisha kazi tulizonazo. Tutaanza na Mheshimiwa Godwin Kunambi.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri; baada ya ufafanuzi huu mzuri kabisa wa Naibu Waziri, nawapongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri. Kimsingi Naibu Waziri ni mama mtulivu, mnyenyekevu kabisa, hata anavyoongea wote tunashuhudia; na Katibu Mkuu pamoja na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijielekeze kwenye hoja yangu ya msingi. Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli aliwahi kuteua timu ya Kamati ya Mawaziri wanane ili waende wakatafute suluhu ya migogoro hasa ya mipaka baina ya vijiji na hifadhi. Sasa ningefurahi nipate ufafanuzi kwa Mheshimiwa Waziri, kwa sababu yeye ndio alikuwa Mwenyekiti wa Kamati hiyo kuhusu utekelezaji wa Kamati hii. Yale ambayo yamekutwa huko wananchi wanawezaje kuyajua hasa wananchi wa Jimbo la Mlimba liko kwenye Bonde la Mto Kilombero? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri aliwahi kutoa hayo maelezo humu Bungeni kuhusu hiyo Kamati. Labda nimpe dakika moja aeleze; na sidhani kama utarejea tena kwenye hii, kwa sababu alieleza kwa namna ambayo wanajipanga kufanya jambo. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba tulielekezwa na Marehemu Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano na kazi ile tuliikamilisha kama kawaida na kuipitisha kwenye Baraza la Mawaziri na uamuzi ukatoka. Vijiji vilivyokuwa vimependekezwa wakati ule vilivyokuwa na migogoro ni 975 kwenye Baraza walisema vijiji 220 viendelee *ku-exist* kwa mapendekezo yale, lakini pia vijiji 55 tulikabidhiwa sisi tuendelee kuvifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miongoni mwa vijiji hivyo 55, vingine viko kwenye Bonde hili wanalozungumza Kilombero na kule Mbarali. Maeneo haya mawili ndiyo yanayofanya vijiji

55 pamoja na Bwawa la Mindu pale Morogoro. Tulielekezwa tufanye hiyo kazi na siku ile niliomba hapa kwamba tumeshakamilisha hiyo kazi, tunajua tutapewa nafasi kwenye Baraza la Mawaziri tutoe taarifa ili maelekezo yatolewe kwa vijiji hivyo 55. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka nimwambie Mheshimiwa Kunambi na wananchi wa Kilombero na maeneo yale wajue kwamba, uamuzi huu ukitolewa vijiji 55, sasa utekelezaji wa vijiji vyote 975 utafanywa kwa pamoja kwa mujibu wa bajeti hii. Wizara zetu safari hii tumetenga bajeti za kwenda kutengeneza maneno hayo. Kuna maeneo tutakwenda kurekebisha mipaka, kuna maeneo tutakwenda kurekebisha vitongoji, kuna maeneo tutakwenda kuhakiki mipaka upya. Ila yote haya yatafanyika baada ya uamuzi wa vijiji hivi 55. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nadhani tumeshaelewa, lakini tunatamani lisiendelee kuchukua miaka tena.

Mheshimiwa Issa Mtemvu. Naona umesimama Mheshimiwa Kunambi.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeridhishwa na maelezo ya Mheshimiwa Waziri. Ombi langu, baada ya Bunge hili walau tuambatane nami, twende kwa wananchi wa Jimbo la Mlimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Sasa, zima kwanza *mic* yako.

Waheshimiwa Wabunge, tuelewane vizuri. Ukishatoa hoja yako pale mwanzoni, ukisimama maana yake hujaridhika. Kwa hiyo, unataka utoe shilingi ili ijadiliwe. Nadhani tunaelewana vizuri. Ndiyo maana ukisimama mara ya pili huwa hatutoi tena muda wa kujieleza, unasema tu kama unaendelea na hoja yako ama vipi.

Mheshimiwa Issa Mtemvu.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nampongeza sana Waziri na timu yake, akiwepo na Naibu Waziri, kwa kweli kwa ufafanuzi mzuri ambao wamekuja nao hapo mbele yako. Pamoja na majibu hayo mazuri ya ufafanuzi, lakini tunatambua bado tumekuwa na huu mpango/program hii ya urasimishaji kwenye sehemu kubwa ya nchi hii, kama Mpango wa miaka kumi; 2013 - 2023 na bado mwaka mmoja kama na nusu uishe; na tunatambua pamoja na maeneo hayo mengi mahususi kabisa, Mkoa wa Dar es Salaam haujafanikiwa sana kwenye jambo hili: Je, ni upi mkakati mahususi kabisa au *commitment* ya Serikali, kwenye kuhakikisha sasa hati zinatoka kama vile dhima ya mpango huu ulivyo kabla ya mwaka 2023 kufika?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri ufafanuzi.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la urasimishaji kwa Mheshimiwa na wengine, hasa kwake, ni kwamba baadhi ya michoro iko tayari lakini Dar es Salaam ndio mkoa wa wajanja kuliko wote Tanzania. Michoro mingine imekutwa sasa watu wanataka kurasimisha, lakini chini yake kulikuwa na michoro siku nyingi. Sasa tulivyokuwa *tuna-scan* na kuingiza kwenye mfumo wa *electronic* mitambo imekataa, hawawezi kupitisha mchoro wa juu wa urasimishaji. Ndani yake kulikuwa na michoro ya upimaji wa juu. Kwa hiyo, kuna matatizo mengi yanayosababisha michoro kutokupita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hati haziwezi kuandikwa mpaka mwananchi alipe; na ili alipe hati lazima amlipe yule aliyepima. Kwa hiyo, wapima wameweka michoro kwenye kwapa mpaka walipwe shilingi 150,000/=. Sasa shilingi 150,000/= hazilipwi, hawawezi kupimiwa. Kwa hiyo, ndiyo maana nimesema nitakuja kupanga ratiba na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam tukwamue tuelewane ili michoro hii iliyoidhinishwa, iliyo tayari na kupimwa wananchi tuaminiane tuwekeane ratiba, walipie kwa mpimaji, lakini na sisi kwetu tuweke utaratibu wa wananchi kulipa hata kidogo kidogo ili hati zitolewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ndiyo maana nimeomba Mheshimiwa Mtemvu nitakuja Dar es Salaam *nita-camp* pale kwa sababu, Dar es Salaam ndiyo kitovu cha zoezi hili, tuje tufanye hiyo kazi mwezi mzima tutakamilisha hii kazi na hati zitatolewa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Samweli Hhayuma.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Kwenye maelezo ya Naibu Waziri, aligusia kidogo suala la mabaraza ya ardhi na kwamba sasa yatakuwa yanawafuata wananchi kwenye wilaya husika. Ninaomba kupata *commitment* ya Serikali. Kwa sasa hivi mazoezi haya yanafanyika pale Babati, Kiteto na maeneo mengine, lakini mahudhurio ya Wenyeviti hao ni haba sana: Je, kwenye maeneo hayo ambayo anasema kwamba Wenyeviti hao watakuwa wanaenda watatuhakikishiaje kwamba kweli watakuwa wanafika? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ufafanuzi.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mbunge kwa swali lake. Naomba nimthibitishie au niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge wote, mpango tulioupanga ni kwamba utaenda kutekelezwa. Tutakachokwenda kufanya sasa, namwagiza Msajili wa Mabaraza ya Ardhi ili aweze kuwasiliana na Wenyeviti wote waweze kuwasilisha ratiba zao za maeneo wanayoyahudumia. Kwa sababu, kama una wilaya nne maana yake kila mwezi lazima utapanga aidha wiki moja moja au kulingana na utakavyojipanga ili zile ratiba ziwe zinakaa kwenye wilaya husika na wajue wiki hii watakuwa Babati, wiki ijayo watakuwa Mbulu, kwa namna hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napenda kumhakikishia kwamba watatoa ratiba ambayo itakuwa wilayani na watatambua lini anakwenda. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya, ufafanuzi wa ziada.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nyongeza kidogo. Suluhisho la mwisho ambalo tunataka kulifanya mwaka huu, Wenyeviti hawa tulionao ni wa mkataba wa miaka mitatu mitatu na sio watumishi wa Serikali. Tuna marekebisho ya sheria tutayaleta hapa. Tunataka turuhusiwe kutumia wanasheria wabobezi, ambao tunao Serikalini wa kutosha. Tunataka kila Wilaya iwe na Mwenyekiti, sio hawa wa kuazimana. Tukisharekebisha ile sheria, tutateua wanasheria tulionao ndani ya Serikali, wabobezi ili wawe wa kudumu katika kila wilaya ili kila wilaya iwe na baraza lake la kudumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ya kwenda kutembea wilaya nne kwa Mwenyekiti mmoja ni ya dharura tuliyonayo leo, ni kwa sababu Wenyeviti hatunao wa kutosha. Tunao mpango wa kudumu Mheshimiwa Mbunge wa Hanang, tunataka tuajiri Wenyeviti kila wilaya na tunataka tubadilishe sheria itakayotuwezesha sisi kuwafanya Wenyeviti wawe Watumishi wa Umma ili tuchukue Wanasheria waliomo Serikalini wawe Wenyeviti. Kwa hiyo, hilo litakuwa suluhisho la kudumu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Halima Mdee.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amesema na Chasimba tutaenda kuzungumza huko, nami niseme bora tukazungumze huko, maana tukizungumza hapa hatutamaliza, sasa naliacha hilo tukazungumze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nije kwenye hoja ya vifaa vya ujenzi. Serikali yoyote makini inatamani wananchi wake wakae kwenye nyumba zenye staha na zenye hadhi, lakini nyumba hizo zisaidie Serikali kupata mapato. Nyie ni mashuhuda kwamba wakati tukiwa tunapitisha kodi za majengo ama *Property Tax,* kuna nyumba zinaitwa za tope

na mabati tunashindwa kuzitoza kwa sababu hazina hadhi ya kutozwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa miaka mingi sana tumekuwa tukisema, kwa nini Serikali isipunguze kodi kwenye vifaa vya majengo? Itakosa kodi wakati wananchi wananunua vifaa, lakini wananchi wakija kuwa na nyumba bora na imara, tutapanua wigo wetu wa kukusanya kodi za majengo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru leo Kamati ya Ardhi kwa mara ya tatu...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Dakika zangu bado. Kengele ya kwanza hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Ardhi imependekeza...

**MWENYEKITI:** Hamnaga kengele mbili kwenye Kamati jamani. Tuelewane vizuri, maana unaanza na mkwara wa ya kwanza. Wewe ungeomba tu umalizie hoja yako.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dakika tano. Haya ngoja nimalizie hoja yangu.

**MWENYEKITI:** Ungeomba umalizie hoja yako, usianze kengele ya kwanza. Sekunde 30, malizia.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Ardhi imependekeza mashirika yetu haya yanayojenga nyumba ili ziweze kuwa *affordable,* waweze kupata huruma ya kikodi ili wananchi wengi waweze kupata hii huduma. Kwa sababu hizi kodi nyingi, zinajengwa nyumba, lakini gharama zake zinakuwa kubwa na nyumba zinabaki magofu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nipate *commitment* yenye tija ya Serikali na tusiangalie hapa... *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya, umeshaeleweka Mheshimiwa Halima.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie *implication* ya hizi nyumba. Naomba *commitment* ya Serikali. Nisipopata majibu mazuri...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima hawezi *kuji-commit* Waziri wa Ardhi wakati kodi unayoizungumzia iko Wizara nyingine.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, si yuko pale.

**MWENYEKITI:** Aah, tuelewane vizuri, maana unasema unataka *commitment.* Waziri ambaye hoja yake iko mezani ni Waziri wa Ardhi, wewe unazungumzia kwamba Waziri atafaidika ikiwa Waziri wa Fedha ataondoa kodi kadhaa. Sasa, *commitment* hapo atatoa wa Ardhi wakati sio yeye anayehusika na kodi!

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iko hapa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwigulu, toa ufafanuzi.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Hayo ndiyo maneno.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Mbunge aridhie tu tuipokee hoja yake kwa sababu upande wa masuala ya kikodi bado tunayafanyia kazi; na jambo hilo la kikodi ni kubwa na bado linahitaji *discussion* ndani ya Serikali. Likishakamilika, basi tutakuja kuleta hoja ikiwa kamili mbele ya Bunge lako Tukufu kujadili masuala hayo yanayohusiana na kodi pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hilo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Basi vizuri. Mheshimiwa January Makamba.

**MHE. JANUARY Y. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Sijui nina muda gani?

**MWENYEKITI:** *(Aliongea nje ya microphone)*

**MHE. JANUARY Y. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, dakika mbili. Nyumba ni hitaji kubwa sana la kila mtu na watu wengi wana ndoto za kujenga nyumba, lakini wengi wanapanga na wanaopanga nyumba ni watu wa kipato cha chini na wanapanga kwa wale wamiliki wa nyumba ambao wana uwezo mkubwa kidogo wa kiuchumi. Sasa mazingira na haki za wapangaji kwa kweli hazina ulinzi wa kutosha sana. Mahali ambapo kuna mtoa huduma mwenye nguvu na mlaji ambaye ni mnyonge, Serikali inakuwepo kwa maana ya mamlaka ya udhibiti. Kwenye mafuta kuna *EWURA,* kwenye Mawasiliano kuna *TCRA*, kuna *LATRA* na kadhalika. Ziko mamlaka za udhibiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisimama hapa Bungeni mwezi wa Februari, 2012 na kuleta hoja hapa Bunge na ikapita kwamba Serikali ilete sheria ya kuwalinda wapangaji hapa nchini dhidi ya dhuluma na uonevu wa kupandishiwa kodi ya nyumba ghafla, kulazimishwa kulipa kodi ya nyumba ya mwaka mzima, uwezekano wa kuondolewa ndani ya nyumba wakati wowote bila ulinzi wowote; na hawa ndio wananchi wengi wanyonge tunaowawakilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilitoa ahadi wakati ule kwamba italeta vitu vitatu; kwanza, Sera ya Nyumba na mpaka sasa Sera ya Nyumba hakuna. Kila bajeti ya Waziri wa Ardhi kuna ahadi ya Sera ya Nyumba, hata kwenye bajeti hii kuna ahadi ya Sera ya Nyumba. Namheshimu sana kaka yangu Mheshimiwa Lukuvi na naamini kabisa hawezi kuwa Waziri wa Nyumba na anaendesha Wizara ya Nyumba bila Sera ya Nyumba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na ahadi ya kuleta *RERA (Real Estate Regulatory Authority),* Mamlaka ya Udhibiti wa Shughuli za Upangaji na Upangishaji wa Nyumba. Mpaka mwaka 2019 ahadi hiyo ilitoka, lakini mpaka sasa bado... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Malizia Mheshimiwa kengele imeshagonga.

**MHE. JANUARY Y. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba *commitment* ya Waziri leo hii kwamba ni lini Serikali itachukua hatua hizi za kuwalinda wanyonge, watu wenye kipato cha chini wanaopanga nyumba katika mazingira magumu?

**MWENYEKITI:** Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Waziri, ufafanuzi.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli alivyosema Mheshimiwa Makamba, tulikuwa na mambo matatu ya kufanya. Tulikuwa tumeagizwa ili tufikie lengo la kuandaa *Real Estate Regulatory Authority,* lazima turekebishe Sheria ya Ardhi. Tumeshaifanya na mpaka sasa tunayo, tunatafuta *slot* ili angalau marekebisho yale yarekebishwe kupitia Baraza la Mawaziri. Pia tuliambiwa hatuwezi kutengeneza hiyo mamlaka bila kuwa na Sera ya Nyumba. Wataalam elekezi wameshamaliza, tunayo, tumepeleka dodoso mahali fulani kwa watu fulani fulani, wameshaanza kujibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kukuhakikishia wewe na Mheshimiwa Makamba kwamba mwaka huu wa bajeti Sera ya Nyumba itakamilika; na *draft* ya mwisho kabisa ya Muswada huu wa *Real Estate Regulatory Authority* upo. Tumefanya utafiti wa kutosha, tumepeleka wataalam wetu kwenye nchi mbalimbali ambazo wamefanya jambo hili na limewaletea tija kubwa sana hata kimapato ya udhibiti na

kuzuia fedha haramu na pia kuwezesha wananchi kuondoka katika huo unyonge, hata kusimamia haki za wapangaji na wapangishwaji wa nyumba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, yote haya yanaenda pamoja. Sisi tungetamani sana kwa sababu zoezi la kuanzisha hii mamlaka litaongeza hata kodi ya Serikali. Kwa hiyo, hilo nataka kumpa *commitment* kwamba ni kazi ya msingi ya mwaka huu. Naamini Mungu akitujaalia, yote matatu yatapita mwaka huu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Kaa tu Mheshimiwa Waziri.

Wakati tukiwatetea hao wanyonge, hizi mamlaka nyingi, siyo zote, wanaolipa tena kuifanya mamlaka ifanye kazi ni walaji. Kwa hiyo, hayo nayo tuyatazame, tusijekuwa tunamtetea mlaji, halafu tunamwongezea tena mzigo kwa mlango mwingine. Kwa sababu, hizi mamlaka nyingine, tunaolipa ni sisi walaji. Sasa yule ambaye tunataka kumpunguzia mzigo, tuangalie kwenye huo Muswada ambao haujaja bado, namna ambavyo tunachotaka kumwondolea huyu unyonge, tusije tukamwongezea tena mzigo wa malipo.

Mheshimiwa Hamis Tabasam.

**MHE. HAMIS H. T. MWAGAO:** Naam.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tabasam.

**MHE. HAMIS H. T. MWAGAO:** Naam.

**MWENYEKITI:** Ama jina lako limeandikwa kwa makosa hapa?

**MHE. HAMIS H. T. MWAGAO:** Hapana, kuna mtu alikuwa anataka kusimama hapa, Mheshimiwa January Makamba kuhusiana na hiki...

**MWENYEKITI:** Alikuwa anataka kusimama? Sasa mimi nitajuaje alitaka kusimama? Nia yake mimi sijaiona. Lazima

nimwone, awe amesimama ndiyo nijue Mheshimiwa kasimama. Sasa wewe utasemaje ana nia ya kusimama. Sijaijua nia.

Mheshimiwa Tabasam.

**MHE. JANUARY Y. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, basi, nia yangu nadhani imejulikana sasa. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaongozwa na Kanuni. Mheshimiwa January Makamba, nimemwita Mheshimiwa Tabasam.

**MHE. HAMIS H. T. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka maelezo katika majumuisho yake Mheshimiwa Waziri wa Ardhi. Ni kwamba tunayo sera ya kuandaa na kuipima hii miji, kuiandalia *Master Plan* katika nchi hii; na miongoni mwa maeneo ambayo sasa hivi yana miradi mikubwa ya maendeleo, kwa mfano Mkoa wa Mwanza kuna mradi wa daraja la kilometa 3.3 kutokea Mji wa Kigongo kwenda Busisi *Ferry.* Kigongo ni upande wa Wilaya ya Misungwi na upande wa Sengerema, Busisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka kujua je, Serikali ina mpango gani wa kuandaa miji mipya sasa kutokana na hali ya Mwanza ilivyokuwa imejaa. Tupate kuweza kupimiwa miji ya kisasa, tuweze kutengenza Jiji Sengerema na tutengeneze Jiji Misungwi? Nini ahadi yako katika jambo hili la upimaji wa ardhi katika eneo hilo? Kwa sababu tuna maeneo ya *beach* lakini pia Sengerema hatuna Afisa Mipango Miji na tunakuja na mradi mkubwa.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwenye ngazi hii huwa unazungumza hoja ya kisera ili ipate ufafanuzi. Sasa hapa naona Mheshimiwa Tabasamu analeta hoja fulani hivi ambayo iko mahsusi kwa ajili ya eneo fulani. Sasa ananipa wakati mgumu kidogo kufanya uamuzi kama hilo jambo kweli linahitaji ufafanuzi ama vipi. Kwa sababu mwishoni

kamalizia kuhusu upimaji wa miji, basi fafanua kuhusu upimaji wa miji katika nchi hii.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa maelezo Mheshimiwa Tabasam, Mbunge wa Sengerema. Kwanza, tunao mpango wa kupanga miji midogo upande wa Misungwi na upande wa Sengerema. Upande wa ng'ambo ya daraja wa misungwi na upande mwingine wa Sengerema. Tumeshawapa fedha watu wa Misungwi, shilingi milioni 300 za kuanza kulipa fidia pale. Nadhani na wewe tumekupa hela kidogo za kuhangaika kupima. Hata hivyo, Wizara itasimamia. Nimeshaagiza wataalam wangu watoe utaalam unaotakiwa kwa ajili ya kupanga miji mipya kando kando kuzunguka lile daraja kubwa lenye thamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Manispaa ya Sengerema, *Master Plan* ya Sengerema lazima muanze wenyewe kwa sababu jukumu la kuandaa *Master Plan* ni Mamlaka ya Upangaji. Mkihitaji utaalam, tuko tayari na ndiyo maana kuna ofisi yangu ya Mkoa, ina Maafisa wabobezi wa Mipango Miji, wanaweza kushirikiana na Halmashauri yako ya Sengerema katika kuwaelekeza namna ya kupanga *Master Plan* ya Sengerema. Afisa Mipango Miji tuwasiliane. Tutakutafutia popote pale tutakuletea kama huna Afisa Mipango Miji. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Kifungu kinaafikiwa?

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, zimebaki dakika kumi. Tunaingia kwenye *guillotine*. Katibu.

**NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI:**

Kif. 1002 – *Finance and Accounts Unit…..*Shs. 1,131,894,000/=
Kif. 1003 – *Policy and Planning Unit……….*Shs. 883,511,600/=

Kif. 1004 – *Mgt Information System Unit*...Shs. 1,492,573,100/=
Kif. 1005 – *Internal Audit Unit* ..................Shs. 384,660,000/=
Kif. 1006 – *Procurement Audit Unit*............Shs. 492,592,000/=
Kif. 1007 – *Government Comm. Unit*.......... Shs. 383,068,000/=
Kif. 1008 – *Legal Services Unit* ..................Shs. 456,580,000/=
Kif. 2001 – *Land Administration Division*...Shs. 11,964,787,758/=
Kif. 2002 – *Surveys and Mapping Division*...Shs. 6,717,464,000/=
Kif. 2003 – *Registration of Titles Unit* .........Shs. 974,510,000/=
Kif. 2004 – *Valuation Unit* ......................Shs. 2,570,601,000/=
Kif. 2005 – *Dar es Salaam Land Office* ......Shs. 1,162,840,000/=
Kif. 2007 – *Dodoma Land Office* ..............Shs. 749,020,000/=
Kif. 2008 – *Tabora Land Office* .................Shs. 716,640,000/=
Kif. 2009 – Mwanza *Land Office* ................Shs. 843,840,000/=
Kif. 2010 – *Kilimanjaro Land Office* ............Shs. 731,740,000/=
Kif. 2011 – *Mtwara Land Office* ................Shs. 604,600,000/=
Kif. 2012 – *Mbeya Land Office* .................Shs. 716,520,000/=
Kif. 2013 – *Simiyu Land Office* ..................Shs. 604,760,000/=
Kif. 2014 – *Arusha Land Office* ..................Shs. 695,220,000/=
Kif. 2015 – *Geita Land Office* ...................Shs. 586,990,000/=
Kif. 2016 – *Njombe Land Office* .................Shs.568,340,000/=
Kif. 2017 – *Katavi Land Office* ..................Shs. 520,490,000/=
Kif. 2018 – *Coastal Land Office* ................Shs. 612,200,000/=
Kif. 2019 – *Iringa Land Office* ...................Shs. 594,960,000/=
Kif. 2020 – *Kigoma Land Office* ................Shs. 603,440,000/=
Kif. 2021 – *Lindi Land Office* .....................Shs. 612,520,000/=
Kif. 2022 – *Mara Land Office* ....................Shs. 674,140,000/=
Kif. 2023 – *Morogoro Land Office* ...........Shs. 826,470,000/=
Kif. 2024 – *Ruvuma Land Office* ..............Shs. 603,380,000/=
Kif. 2026 – *Singida Land Office* .................Shs. 577,840,000/=
Kif. 2027 – *Tanga Land Office* ..................Shs. 701,560,000/=
Kif. 2028 – *Kagera Land Office* .................Shs. 671,120,000/=
Kif. 2029 – *Rukwa Land Office* ..................Shs. 494,200,000/=
Kif. 2030 – *Songwe Land Office* ................Shs. 552,620,000/=
Kif. 2031 – *Manyara Land Office* ...............Shs. 603,560,000/=
Kif. 3001 – *Rural and Town Plan. Division*....Shs. 7,160,941,142/=
Kif. 3002 – *Housing Division* ..................................Shs. 0/=
Kif. 3003 – *Distr.Land & Housing Trib. Unit*..Shs.6,046,866,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 3 – Tume ya Matumizi Bora ya Ardhi**

Kif. 1002 – *Directorate of Corporate Serv*..... Shs. 928,926,000/=
Kif. 1003 – *Procurement and Mangnt Unit*....Shs. 139,680,000/=
Kif. 1004 – *Internal Audit Unit* ....................Shs. 82,360,000/=
Kif. 1005 – *Legal Services Unit* ..................Shs. 246,840,000/=
Kif. 2001 – *Directorate of Land Use Planning, MGT & Coordination* .......................Shs. 514,040,000/=
Kif. 2002 – *Directorate of Research, Compliance & Information*...........................Shs. 432,042,000/=
Kif. 2003 – *Tabora Zone Office*..................Shs. 133,000,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 48 – Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi**

Kif. 1001 – *Admin. and HR MGT*...............Shs. 1,600,000,000/=
Kif. 1003 – *Policy and Planning Unit* ........................Shs. 0/=
Kif. 2001 – *Land Administration Division*...Shs. 10,800,000,000/=
Kif. 2002 – Surveys and Mapping Div.......Shs. 17,150,299,000/=

**Fungu 3 – Tume ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi**

Kif. 1001 – *Directorate of Corporate Services* ............Shs. 0/=
Kif. 2001 – *Directorate of Land Use Planning MGT & Coordination*.......Shs. 1,300,000,000/=
Kif. 2002 – *Directorate of Research, Compliance & Inform*..................................Shs. 200,000,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tukae. Mtoa hoja taarifa.

## TAARIFA

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na shukrani nyingi kwako kwa kutuendeshea vizuri kikao cha leo, nawashukuru tena Waheshimiwa Wabunge wote kwa kazi kubwa mliyoifanya. Kama tulivyowaahidi, tutatekeleza yote tuliyokubaliana humu ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa taarifa kwako kwamba Bunge lako lilikaa kama Kamati ya Matumizi, limekamilisha kazi zake. Naomba Taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2020/2021 – Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Wote wameafiki na kwa hiyo, Makadirio ya Mapato na Matumizi kama yalivyokuwa yameombwa, yameidhinishwa na Bunge. Nachukua fursa hii kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wenu wote kwa kazi nzuri mliyoileta mbele ya Bunge na pia kwa kuwa wasikivu kwa kusikiliza maoni ya Kamati ambayo mmefanya nayo kazi muda wote na Bunge sasa limeidhinisha maombi mliyokuwa mmeleta kama mlivyoomba. Nasi tunaamini yale yote mliyoahidi mtaenda kuyatekeleza hayo na tunawatakia kila la heri kwenye utekelezaji wa yale yote ambayo mmekusudia kuyafanya. Mengine mlikuwa mmeyaeleza wazi kwenye bajeti, mengine mmeeleza kwamba mtaenda kuyafanya baada ya michango ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaamini yote ambayo

mmeyaahidi mtaenda kuyafanya na sisi tunategemea mwaka huu kutakuwa na mabadiliko mazuri zaidi kuliko yale ambayo mlikuwa mkipongezwa humu ndani.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, muda wetu umekwenda sana. Naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 2.10 Usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Alhamisi, Tarehe 27 Mei, 2021, Saa Tatu Asubuhi)*